**MPANGO WA UTAFITI NA ELIMU YA DEMOKRASIA TANZANIA**

**(REDET)**

**REDET - ASASI KIONGOZI WA TEMCO**

# UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2020

**TAARIFA YA MPANGO WA UTAFITI NA ELIMU KWA AJILI YA DEMOKRASIA TANZANIA**
**(REDET)**

**MEI 2021**

# CONTENTS

**VIFUPISHO ........ xi**

**DIBAJI ........ xv**

**SURA YA KWANZA ........ 1**

**USULI NA METHODOLOJIA ........ 1**

**1.1 UTANGULIZI ........ 1**
**1.2 USULI ........ 1**
**1.3 SABABU NA MADHUMUNI YA REDET KUTAZAMA UCHAGUZI ........ 2**
**1.4 MAWANDA YA UTAZAMAJI ........ 3**
**1.5 UTEUZI NA UTOAJI MAFUNZO KWA WATAZAMAJI ........ 4**
1.5.1 Uteuzi wa Watazamaji ........ 4
1.5.2 Utoaji Mafunzo kwa Watazamaji ........ 5
**1.6 MBINU NA METHODOLOJIA ........ 5**
1.6.1 Madodoso ya Kukusanyia Data ........ 6
1.6.2 Usambazaji wa Watazamaji wa Muda Mrefu na wa Muda Mfupi ........ 6
1.6.4 Hatua za Kukabiliana na UVIKO-19 ........ 7
**1.7 VIGEZO VYA KUTATHMINI UCHAGUZI ........ 8**
**1.8 MUUNDO WA TAARIFA HII ........ 9**
**1.9 SHUKRANI ........ 9**

**SURA YA PILI ........ 12**

**MUKTADHA WA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA WA MWAKA 2020 ........ 12**

**2.1 UTANGULIZI ........ 12**
**2.2 UTENDAJI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO (2015-2020) ........ 13**
**2.3 MIENENDO YA VYAMA VYA SIASA ........ 19**
**2.4 MKWAMO WA KISIASA ZANZIBAR ........ 23**
**2.5 MUKTADHA WA KIKANDA NA KIMATAIFA ........ 24**
**2.6 HITIMISHO ........ 26**

**SURA YA TATU ........ 27**

**MFUMO WA KISHERIA NA KITAASISI KWA AJILI YA KUENDESHA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020..........27**

**3.1 UTANGULIZI ..........27**

**3.2 MFUMO YA KISHERIA KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 ..........27**

3.2.1 Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari..........28

3.2.2 Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni)..........29

3.2.3 Sheria ya Takwimu ..........29

3.2.4 Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ..........30

3.2.5 Sheria ya Vyama vya Siasa..........31

3.2.6 Sheria ya Gharama za Uchaguzi..........33

**3.3 USIMAMIAJI WA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020..........35**

3.3.1 Uteuzi na Utoaji Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi..........35

3.3.2 Usajili wa Watazamaji Uchaguzi na Watoaji Elimu ya Mpiga Kura .38

3.3.3 Kuapishwa kwa Mawakala wa Uchaguzi..........39

3.3.4 Ugawaji wa Maeneo ya Uchaguzi..........43

3.3.5 Gharama za Uchaguzi..........44

3.3.6 Uandikishaji Wapiga Kura..........44

3.3.7 Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura..........45

**3.4 HITIMISHO ..........48**

**SURA YA NNE ..........50**

**UTEUZI WA WAGOMBEA..........50**

**4.1 UTANGULIZI ..........50**

**4.2 MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI ..........50**

4.2.1 Taratibu na Kanuni za Vyama ..........51

**4.3 UTEUZI WA WAGOMBEA URAIS ..........51**

4.3.1 Uteuzi wa Mgombea Urais katika Chama cha Mapinduzi..........52

4.3.2 Uteuzi wa Mgombea Urais wa CHADEMA ..........54

4.3.4 Uteuzi katika Vyama Vingine..........55

4.4.6 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ..........56

**4.4 UTEUZI WA TUME ..........57**

4.4.1 Uteuzi wa Wagombea Urais ..........58

4.4.2 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ..........59

**4.5 KUSHUGHULIKIA RUFAA..........60**

**4.6 WAGOMBEA WALIOPITA BILA KUPINGWA..........61**

**4:7 TATHMINI YA JUMLA YA MCHAKATO WA UTEUZI ....................62**

**4.8 HITIMISHO .......................................................................................63**

**SURA YA TANO.......................................................................................64**

**MWENENDO WA KAMPENI ZA UCHAGUZI ................................................64**

**5.1 UTANGULIZI .......................................................................................64**

**5.2 MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI INAYOSIMAMIA KAMPENI .......................................................................................64**

**5.3 KUGHARAMIA KAMPENI ZA UCHAGUZI – UTEKELEZAJI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI ....................................66**

**5.4 KANUNI NA MAADILI YA UCHAGUZI.............................................67**

**5.5 MATUMIZI YA FAIDA YA KUWA MADARAKANI ...........................70**

**5.6 MBINU NA MIKAKATI YA KAMPENI...............................................71**

**5.7 KAMPENI HASI......................................................................................74**

**5.8 MATUKIO HATARISHI WAKATI WA KAMPENI ZA UCHAGUZI .........................................................................................74**

**5.9 ILANI ZA UCHAGUZI: AJENDA NA MASUALA..............................75**

5.9.1 Kilimo .......................................................................................76

5.9.2 Rushwa .....................................................................................77

5.9.3 Elimu ........................................................................................77

5.9.4 Madini ......................................................................................78

**5:10 MIPANGO YA KIUSALAMA NA UTENDAJI WA POLISI ...........80**

**5.11 TATHMINI YA JUMLA YA KAMPENI ZA UCHAGUZI ................83**

**5.12 HITIMISHO..........................................................................................84**

**SURA YA SITA.........................................................................................85**

**VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI.....................................................85**

**6.1 UTANGULIZI .......................................................................................85**

**6.2 KANUNI ZA MAADILI KWA WANAHABARI KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020................................................85**

**6.3 MFUMO WA KISHERIA WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 ..............................87**

**6.4 MAJUKUMU YA WADHIBITI WA VYOMBO VYA HABARI .......88**

**6.5 UCHAMBUZI WA UTOAJI TAARIFA JUU YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020..............................................................90**

6.5.1 Wigo wa Magazeti .......................................................................90

6.5.2 Vyombo vya Habari vya Mtandaoni ....................................................91
6.5.3 Maudhui na Mwelekeo katika Matangazo ya Vyombo vya Habari ...92
6.5.4 Matangazo ya Redio za Kijamii ..................................................96
6.5.5 Makala za Magazetini na Vijarida ..............................................98
6.5.6 Mchango wa Mitandao ya Kijamii ..............................................98
**6.6 HITIMISHO ......................................................................................99**

**SURA YA SABA ........................................................................................100**

**USHIRIKI WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 NCHINI TANZANIA ..100**
**7.1 UTANGULIZI ....................................................................................100**
**7.2 MFUMO WA KISHERIA KWA AJILI YA MAKUNDI MAALUM...............................................................................................100**
**7.3 WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWENYE USIMAMIZI WA UCHAGUZI .......................................101**
**7.4 UANDIKISHAJI WAPIGA KURA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU..................................................................104**
**7.5 UTOAJI WA ELIMU YA MPIGA KURA KWA WATU WA MAKUNDI MAALUMU..............................................................................107**
**7.6 UZINGATIAJI WA JINSIA WAKATI WA KUTEUA WAGOMBEA...............................................................................................109**
7.6.1 Wagombea Urais Wanawake Walioteuliwa ....................................110
7.6.2 Wagombea Ubunge Wanawake Walioteuliwa ................................111
7.6.3 Uteuzi wa Wanawake wa Viti Maalumu..........................................112
**7.7 USHIRIKI KATIKA KAMPENI ZA UCHAGUZI ...........................113**
**7.7 KUHUDUMIA MAKUNDI MAALUMU SIKU YA UCHAGUZI ...115**
**7.8 MATOKEO YA UCHAGUZI YA WAGOMBEA WA KIKE.............116**
7.8.1 Ukinzani wa Suala la Wabunge wa Viti Maalumu wa CHADEMA .......................................................................................117
**7.9 HITIMISHO.......................................................................................118**

**SURA YA NANE .......................................................................................119**

**UCHAGUZI WA ZANZIBAR .................................................................119**
**8.1 UTANGULIZI.....................................................................................119**
**8.2MUKTADHA WA KISIASA KUELEKEA UCHAGUZI WA ZANZIBAR WA MWAKA 2020 ..........................................................119**

**8.3 UTEUZI WA WAGOMBEA ZANZIBAR....121**
8.3.1 Uteuzi wa Wagombea Urais Zanzibar Ndani ya CCM....121
8.3.2 Uteuzi wa Wagombea Ubunge Ndani ya CCM....122
8.3.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ACT-Wazalendo....122
8.3.4 Uteuzi wa Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi na Pingamizi....122
8.3.5 Mabadiliko na Ushirikiano baada ya Uteuzi....127
**8.4 KAMPENI ZA UCHAGUZI....129**
8.4.1 Kampeni za Uchaguzi za Mgombea Urais wa CCM....130
8.4.2. Mikakati ya Kampeni ya CCM....132
8.4.3 Kampeni za Uchaguzi za Mgombea Urais wa ACT-Wazalendo....133
8.4.4 Mikakati ya Kampeni ya Mgombea Urais wa ACT-Wazalendo....133
8.4.5 Kampeni za Wagombea Urais wa Vyama Vingine vya Siasa....135
8.4.6 Kampeni Hasi....136
8.4.7 Usafirishaji Watu Kwenda kwenye Maeneo ya Kampeni....138
8.4.8 Mienendo Mibaya katika Kampeni za Uchaguzi na Vurugu....139
**8.5 FUMBO/KIZUNGUMKUTI CHA UPIGAJI KURA WA MAPEMA....141**
**8.6 KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO....143**
8.6.1 Upigaji Kura....143
8.6.2 Kuhesabu Kura....144
8.6.3 Kutangaza Matokeo....146
**8.7 MATUKIO BAADA YA UCHAGUZI WA ZANZIBAR....149**
**8.8 TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI WA ZANZIBAR....150**
**8.9 HITIMISHO....152**

**SURA YA TISA....153**

**SIKU YA UCHAGUZI NA TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI WA MWAKA 2020....153**
**9.1. UTANGULIZI....153**
**9.2. KUFUNGUA NA KUFUNGA VITUO VYA KUPIGIA KURA NA VIFAA VYA KUPIGIA KURA....153**
2.9.1 Kuanza kwa Upigaji Kura....153
9.2.2 Utoshelevu na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura....154
9.2.3 Upangaji, Ufikikaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Namna ya Kuwahudumia Wapiga Kura....155
9.2.4 Ufungaji wa Vituo vya Kupigia Kura....158

**9.3. KUHESABU KURA, KUJUMLISHA KURA NA KUBANDIKA MATOKEO KWENYE VITUO VYA KUHESABIA KURA............159**
**9.4 MIPANGO YA KIUSALAMA ..........................................................162**
**9.5 KUTANGAZA MATOKEO ..........................................................162**
9.5.1 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais ..........................................................163
9.5.2 Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge ..........................................................163
9.5.3 Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani..........................................................166
**9.6 MWITIKIO WA WAPIGA KURA ..........................................................167**
**9.7 MATUKIO YALIYOJITOKEZA BAADA YA UCHAGUZI ............168**
9.7.1 Mlipuko wa Vurugu..........................................................168
9.7.2 Kuingiliwa na Kufungwa kwa Mitandao ya Kijamiii ......................172
9.7.3 Utafutaji Hifadhi na Madai ya Kutishiwa Uhai...............................172
**9.8 UTENDAJI NA MWENENDO WA WATENDAJI WA UCHAGUZI ..........................................................173**
**9.9 UTENDAJI NA MWENENDO WA MAWAKALA WA VYAMA VYA SIASA..........................................................174**
**9.10 TATHMINI YA MICHAKATO YA UPIGAJI NA UHESABUJI KURA..........................................................176**
9.9.1 Tathmini ya Mchakato wa Upigaji Kura ..........................................176
9.9.2 Tathmini ya Mchakato wa Kuhesabu Kura ....................................176
**9.11 TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 ..........................................................178**
**9.12 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..........................................................179**
9.12.1 Hitimisho ..........................................................179
9.12.2 Mapendekezo..........................................................180

**MAREJEO..........................................................183**

**VIAMBATISHO ..........................................................186**
**Kiambatisho 1: Watazamaji wa Muda Mrefu Waliosambazwa ............186**
**Kiambatisho 2: Barua ya Usajili kutoka Tume ......................................196**
**Appendix 3: Photo Gallery..........................................................197**

**Sekretarieti ya Programu ya TEPO ..........................................................203**

## ORODHA YA MAJEDWALI NA MAUMBO


*Jedwali Na. 2.1:* *Mgawanyo wa Viti vya Ubunge na Udiwani kwa Mwaka 2015 ....22*

*Jedwali Na. 3.2:* *Tofauti ya Idadi ya Mawakala wa Vyama katika Jimbo la Shinyanga Mjini ....43*

*Jedwali Na. 3.3:* *Utolewaji wa Elimu ya Mpiga Kura na Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi na Asasi za Kiraia ....45*

*Jedwali Na. 3.4:* *Njia Zilizotumika kutoa Elimu ya Mpiga Kura ....46*

*Jedwali Na. 4.1:* *Wagombea Urais na Wagombea Mwenza....58*

*Jedwali Na. 4.2:* *Watu Walioteuliwa Kugombea Ubunge ....60*

*Jedwali Na. 4.3:* *Wagombea Ubunge Waliopita bila Kupingwa ....61*

*Jedwali Na. 4.4:* *Tathmini ya Mchakato wa Uteuzi ....62*

*Jedwali Na. 5.1:* *Matukio Hatarishi....75*

*Jedwali Na. 5.2:* *Ilani za Uchaguzi na Kilimo ....76*

*Jedwali Na. 5.3:* *Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Rushwa....77*

*Jedwali Na. 5.4:* *Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Elimu....78*

*Jedwali Na. 5.5:* *Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Sekta ya Madini .... 79*

*Jedwali Na. 5.6:* *Kauli mbiu Zilizotumiwa na Vyama vya Siasa Kuhamasisha Wapiga Kura ....80*

*Jedwali Na. 5.7:* *Utendaji wa Polisi katika Kampeni za Uchaguzi ....81*

*Jedwali Na. 5.8:* *Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi ....83*

*Jedwali Na. 6.1:* *Matangazo katika Redio za Kijamii ....97*

*Jedwali Na. 7.1:* *Mgawanyo wa Waandikishaji Wapiga Kura kwa Jinsia....102*

*Jedwali Na. 7.2:* *Mgawanyo wa Watendaji Walioteuliwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa Umri na Jinsia ....103*

*Jedwali Na. 7.3:* *Mgawanyo wa Watu Walioandikishwa kwa Umri ....105*

*Jedwali Na. 7.4:* *Watu wenye Ulemavu Walioandikishwa Kupiga Kura .105*

*Chati Na. 7.1:* *Ufikikaji wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga kura na Watu wenye Ulemavu....106*

*Jedwali Na. 7.5:* *Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ....108*

*Jedwali Na. 7.6:* *Mgawanyo wa Wagombea wa Kiti cha Urais cha Muungano kwa Jinsia ....110*

*Jedwali Na. 7.7:* *Mgawanyo wa Wabunge wa Kuteuliwa kwa Jinsia ...... 112*

*Jedwali Na. 7.8: Usalama na Vitendo dhidi ya Wagombea Wanawake na Wafuasi wa Vyama wa Kike .................................. 114*

*Jedwali Na. 7.9: Kuhudumia Makundi Maalumu Siku ya Uchaguzi .......115*

*Jedwali Na. 7.10: Wabunge Wanawake wa Kuchaguliwa katika Uchaguzi wa Mwaka 2020 ........................................ 116*

*Jedwali Na. 8.1: Wagombea wa Baraza la Wawakilishi na wa Udiwani Walioteuliwa .............................................................124*

*Jedwali Na. 8.2: Baadhi ya Wagombea Waliooondolewa........................124*

*Jedwali Na. 8.3: Tathmini ya Teuzi ........................................................126*

*Jedwali Na. 8.4: Kauli Mbiu Zilizotumiwa na Vyama vya Siasa Zanzibar.....................................................................................136*

*Jedwali Na. 8.5: Mikakati ya Uchaguzi ya Vyama vya Siasa Zanzibar...136*

*Jedwali Na. 8.6: Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi za Zanzibar ...........140*

*Jedwali Na. 8.7: Kuanza kwa Upigaji Kura ..........................................143*

*Jedwali Na. 8.8: Utoshelevu, Mipango na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura ...............................................................144*

*Jedwali Na. 8.9: Kuanza Kuhesabu Kura...............................................144*

*Jedwali Na. 8.10: Mipango na Taratibu kwenye Vituo vya Kuhesabu Kura ......................................................................................145*

*Jedwali Na. 8.11: Ubandikaji wa Matokeo ya Uchaguzi..........................146*

*Jedwali Na. 8.12: Kukubalika kwa Matokeo ya Uchaguzi .......................147*

*Jedwali Na. 8.13: Kama Wagombea Waliyakubali Matokeo ya Uchaguzi.................................................................................147*

*Jedwali Na. 8.14: Tathmini ya Upigaji Kura, Uhesabuji Kura na Utangazaji Matokeo ...................................................148*

*Jedwali Na. 8.15: Tathmini ya Jumla ya Uchaguzi wa Zanzibar .............151*

*Jedwali Na 9.1: Ufunguzi wa Vituo vya Kupigia Kura..........................154*

*Jedwali Na. 9.2: Utoshelevu, Mpangilio wa Kituo cha Kupigia Kura na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura....................155*

*Jedwali Na. 9.3: Upangaji, Ufikikaji na Namna ya Kuwahudumia Wapiga Kura..............................................................156*

*Jedwali Na. 9.4: Wapiga kura Wakisubiri Kupiga Kura Muda wa Kufunga Vituo vya Kupigia Kura ................................158*

*Jedwali Na. 9.5: Kama Wapiga Kura Waliokuwa kwenye Mstari Waliruhusiwa Kupiga Kura ........................................158*

*Jedwali Na. 9.6: Muda ambao Mpiga Kura wa Mwisho Alipiga Kura ...159*

*Jedwali Na. 9.7: Muda wa Kuanza na Kukamilisha Uhesabuji Kura .....159*

*Jedwali Na. 9.8: Mipangilio na Taratibu kwenye Vituo vya Kuhesabia Kura ....................160*
*Jedwali Na. 9.9: Muda wa Kuhesabu Kura na Kubandika Matokeo ya Uchaguzi ....................161*
*Jedwali Na. 9.10: Hisia za Watu Kuhusu Uchaguzi Mkuu ....................161*
*Jedwali Na. 9.11: Kutumia Fedha Kushawishi Wapiga Kura, Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura au Mawakala wa Vyama ....................162*
*Jedwali Na. 9.12: Kukubali Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge ..............164*
*Jedwali Na. 9.13: Kukubalika kwa Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani .166*
*Jedwali Na. 9.14: Matukio ya Vurugu Yaliyotokea baada ya Uchaguzi....169*
*Jedwali Na. 9.15: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi katika Vituo vya Kupigia Kura....................173*
*Jedwali Na. 9.16: Utendaji wa Watendaji wa Uchaguzi....................174*
*Jedwali Na. 9.17: Mawakala wa Vyama vya Siasa....................175*
*Jedwali Na. 9.18: Tathmni ya Zoezi la Upigaji Kura ....................176*
*Jedwali Na. 9.19: Thathmini ya Mchakato wa Kuhesabu Kura ................176*
*Jedwali Na. 9.20: Tathmini ya Siku ya Kupiga Kura....................177*
*Jedwali Na. 9.21: Tathmini ya Jumla ya Michakato ya Uchaguzi.............178*

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAFP | Alliance for Tanzania Farmers' Party |
| ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency |
| ADA-TADEA | African Democratic Alliance -Tanzania Democratic Alliance |
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| AIDS | Acquired Immuno-deficiency Syndrome, |
| ASP | Afro-Shirazi Party. |
| ATCL | Air Tanzania Corporation Limited |
| BAKWATA | Baraza Kuu la Waislam Tanzania |
| BAVICHA | Baraza la Vijana CHADEMA |
| BAWACHA | Baraza la Wanawake CHADEMA |
| BBC | British Broadcasting Corporation |
| CCK | Chama cha Kijamii |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CCT | Christian Council of Tanzania |
| CDTI | Community Development Institute |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama cha Ustawi wa Umma |
| COVID-19 | Corona Virus Disease-19 |
| CSO | Civil Society Organisation |
| CUF | Civic United Front |
| CWT | Chama cha Walimu Tanzania |
| DANIDA | Danish International Development Agency |

| | |
|---|---|
| DC | District Council |
| DP | Democratic Party |
| EAC | East African Community |
| EACJ | East African Court of Justice |
| EAPCOP | East Africa Crude Oil Pipeline |
| EEA | Election Expenses Act |
| EMBs | Electoral Management Bodies |
| EO | Election Officer |
| GBV | Gender-based Violence. |
| GNU | Government of National Unity |
| ICT | Information and Communications Technology |
| LGA | Local Government Authority |
| LGAs | Local Government Authorities |
| LTOs | Long Term Observers |
| MAKINI | Chama cha Demokrasia Makini |
| MCT | Media Council of Tanzania |
| MP | Member of Parliament |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Constitutional Reform-Mageuzi |
| NEC | National Electoral Commission |
| NEMC | National Environmental Regulatory Authority |
| NGO | Non-governmental Organisation |
| NLD | National League for Democracy |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| OCD | Officer Commanding District |

| | |
|---|---|
| ODK | Open Data Kit |
| ORPP | Office of the Registrar of Political Parties |
| PCCB | Prevention and Combating of Corruption Bureau |
| PNVR | Permanent National Voter Register |
| PO | Presiding Officer |
| PPA | Political Parties Act |
| PWD | People with Disability |
| PWDs | People with Disabilities |
| REC | Regional Election Co-ordinator |
| REDET | Research and Education for Democracy in Tanzania |
| REOCs | Regional Election Observation Committees |
| RO | Returning Officer |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SAU | Sauti ya Umma |
| STAMICO | State Mining Corporation |
| STOs | Short Term Observers |
| TANESCO | Tanzania National Electricity Supply Company |
| TANU | Tanganyika African National Unity |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TCF | Tanzania Constitution Forum |
| TCRA | Tanzania Communications Regulatory Authority |
| TEC | Tanzania Episcopal Conference |
| TCF | Tanzania Communication Forum |
| TEF | Tanzania Editors' Forum |

| | |
|---|---|
| TEMCO | Tanzania Election Monitoring Committee |
| TEPO | Tanzania Electoral Processes Observation |
| THDRC | Tanzania Human Rights Defenders' Coalition |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| TLS | Tanganyika Law Society |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TTU | Tanzania Teachers' Union |
| UDP | United Democratic Party |
| UDSM | University of Dar es Salaam |
| UKAWA | Umoja wa Katiba ya Wananchi |
| UMD | Union for Multiparty Democracy |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UPDP | United People's Democratic Party |
| URT | United Republic of Tanzania |
| USAID | United States Agency for International Development |
| ZEC | Zanzibar Electoral Commission |

# DIBAJI

Uchaguzi hutoa fursa kwa wananchi kuchagua viongozi au vyama wanaohudumu katika ofisi za umma. Ni njia muhimu ya kushughulikia ushindani wa kutafuta madaraka na utawala chini ya mfumo wa uliberali. Ni kitendo rasmi cha kufanya maamuzi ya pamoja ambayo yanajumuisha hatua kadhaa za msingi. Hatua hizo zinajumuisha kukubaliana kuhusu kanuni za mchezo, zikiwamo katiba, sheria na taratibu za uchaguzi, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, uhesabuji kura, utangazaji matokeo na mwisho kukubali au kukataa matokeo. Historia inaonesha kwamba mambo yanaweza kwenda kombo katika hatua yeyote kati ya hizi au katika hatua zote kwa makusudi au vinginevyo, na hivyo kufanya utazamaji uchaguzi kuwa ni shughuli muhimu.

Siasa za demokrasia ya kiliberali zilianzishwa tena barani Afrika mwanzoni mwa miaka ya 1990 zikitegemea sana utazamaji wa uchaguzi kama sehemu muhimu ya ustawi wake kutokana na sababu kuu tatu. Kwa kuanzia, kwenye nchi nyingi demokrasia ilianzishwa kwa msukumo wa nguvu za ndani na nje ya nchi. Haikua hiari au uamuzi tu wa kufanya hivyo. Ulikuwapo na bado kuna wasiwasi kuhusu uaminifu wa dola na vyombo vya kusimamia uchaguzi kutompendelea mtu yeyote. Hali kadhalika, kupitishwa na kuendelea kutumika kwa katiba za mfumo wa chama kimoja kulichangia wasiwasi huo. Katiba nyingi za aina hii zinaanzisha dola zenye nguvu dhidi ya mihimili mengine ya serikali na vyombo vya kusimamia uchaguzi ambavyo vinaonekana kukipendelea chama au mgombea fulani. Tatu, siasa za chama kimoja zinazokataza ukosoaji na zinazoviona vyama vya upinzani kama maadui ziliendelea. Vivyo hivyo, kuendelea kwa utamaduni wa kisiasa ambao unawaona raia kama watu wasiokuwa huru badala ya raia ambao wako huru ulikuwa kikwazo cha kuanzishwa kwa taasisi imara za kidemokrasia (Almond na Verba, 1963). Kwa ujumla, watu wengi walikuwa watiifu na waoga badala ya kuwa raia mahiri wanaojiamini na wanaotaka kutoa msukumo kwenye mfumo wa siasa (Mushi, 2001).

Kutokana na sababu hizo Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania (REDET) na Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO), iliamua kuendelea na utamaduni iliouanzisha wakati wa uchaguzi wa chama kimoja uliofanyika mwaka 1965 kwa kutafiti na kutazama uchaguzi wa kwanza uliofanyika chini ya mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1995.

Je, utazamaji uchaguzi ulikuwa na umuhimu wowote miaka 25 tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi? Jibu lilikuwa ni ndiyo, hususan kwa sababu uimarishaji wa demokrasia nchini Tanzania haukuwa rahisi au mkamilifu kama ambavyo mtu mwingine angependa uwe. Katiba bado haina vipengele muhimu vya kidemokrasia. Na wakati huohuo jitihada za kuandika katiba mpya zimekwama tangu mwaka 2015 wakati Katiba Inayopendekezwa ilipopitishwa. Vyama vya siasa havijaimarika kiuendelevu. Kwa mfano, mafanikio makubwa vilivyoyapata katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika mwaka 2014 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 yalifuatiwa na mlipuko ambao umeviacha vyama hivyo vimegawanyika na dhaifu, kama taarifa hii inavyoonesha. Uhuru wa kiraia na kisiasa si wa kudumu na unabanwa na sheria na kanuni nyingi mno. Uhuru huo unadhibitiwa na dola kupitia Jeshi la Polisi na vyombo vingine. Chaguzi zilizopita hazikuwa huru na za haki. TEMCO ilionesha kwamba uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 ulikuwa huru lakini si wa haki, na chaguzi zilizofuata zilikuwa huru na za haki kiasi tu. Tanzania imefaulu jaribio la pili la Venezuela la mwaka 1992 ambalo linaonesha kwamba nchi inaimarika kidemokrasia kama inafanya chaguzi baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vyingi. Tanzania imeendesha chaguzi nne kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2020. Kwa maneno mengine, demokrasia ya mfumo wa vyama vingi imekuwapo kwa miaka 25. Kwa hiyo, Tanzania imefaulu jaribio la muda mrefu la Rustow (1970). Hakika, siasa za upinzani zimedumu muda mrefu. Hata hivyo, Tanzania haijawahi kushuhudia vyama vya siasa vikibadilishana madaraka.

Wanachama wamebadilishana uongozi ndani ya chama tawala. Hali ya kwamba chama tawala kinaweza kukubali kushindwa na kukabidhi madaraka kwa chama cha upinzani, kitu ambacho ni muhimu sana katika kuimarisha demokrasia, haijawahi kutokea (Huntington, 1991; Przeworski, 1991). Ni wazi kwamba jitihada za kuimarisha demokrasia nchini Tanzania bado zinaendelea, hivyo ni muhimu kuendelea kutazama mwenendo wa uchaguzi. Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulipaswa kuwa mwepesi kwa sababu Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa anatetea kiti chake. Chama tawala kilihakikisha kwamba mgombea wake anapita bila kupingwa ndani ya chama, na hivyo kutekeleza kanuni ambayo haijaandikwa kwamba Rais aruhusiwe kugombea muhula wa pili bila kupingwa. Ukizingatia ugumu wa kawaida wa kumwondoa Rais aliyoko madarakani, watu walidhani kwamba ushindani na mwamko wa kisiasa ungekuwa mdogo. Hata hivyo, REDET iliona ni muhimu na lazima kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwani matumizi ya faida ya kuwa madarakani dhidi ya vyama vya upinzani

yalikuwa makubwa.

Vitu viwili vilijitokeza kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kwanza ni mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19) ambao umeikumba dunia nzima, ikiwamo Tanzania. Lakini wasiwasi wa kwamba uchaguzi ungeweza kufanyika uliondolewa na Rais Magufuli mwanzoni mwa kipindi cha uchaguzi. Rais Magufuli alikataa kuweka zuio la watu kutoka nje kama jitihada za kupambana na janga hilo. Matokeo yake shughuli zote za kisiasa, kijamii na kiuchumi ziliendelea kama kawaida.

Pili, kutungwa kwa sheria mpya inayosimamia asasi zisizo za kiserikali, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2019), kuliathiri zoezi la utazamaji uchaguzi. Mwaka 1995 TEMCO ilikuwa na wanachama 22. Idadi iliongezeka hadi 183 wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015 unafanyika. TEMCO ilijumuisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS). Kifungu cha 2(b) cha sheria hiyo mpya, Sura 337, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 (2019), inakataza asasi za kidini kujishughulisha na shughuli za kisiasa. Hali hii iliinyima REDET/TEMCO michango ya watazamaji hawa wazoefu kutoka asasi za kidini. Hata hivyo, REDET ilitengeneza timu ya watu mahiri na waliojotoa kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Tunaomba kuwasilisha matokeo yao.

**Profesa Rwekaza S. Mukandala**

**REDET/TEMCO**
**Mwenyekiti na Mkuu wa Timu ya Kutazama Uchaguzi**

# SURA YA KWANZA

# USULI NA METHODOLOJIA

## 1.1 UTANGULIZI

Utazamaji uchaguzi una nafasi kubwa ya kuchochea uwazi na uwajibikaji, pamoja na kuongeza imani ya wananchi kuhusu michakato na matokeo ya uchaguzi. Pia, unaweza kusaidia kuona kama haki za kiraia na kisiasa zinalindwa. Utazamaji ukifanyika kwa weledi na uhalisia unasaidia kusahihisha makosa hata wakati uchaguzi unaendelea. Vivyo hivyo, utazamaji uchaguzi unaweza kuzuia uchakachuaji na wizi wa uchaguzi na kuweka wazi matatizo kama yatatokea. Taarifa nzuri kuhusu utazamaji uchaguzi zinaongeza uhalali wa serikali inayoundwa kutokana na uchaguzi, lakini taarifa mbaya zinaondoa uhalali huo.

## 1.2 USULI

Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania (REDET) ina historia ndefu nzuri ya kutazama uchaguzi tangu kuanzishwa kwa Idara ya Sayansi ya Siasa mwaka 1964 (baadaye Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wakati wa mfumo wa chama kimoja, kuanzia mwaka 1965 hadi mwaka 1990, Idara ilikuwa na majukumu ya kutazama na kufanya tafiti juu ya uchaguzi nchini Tanzania. Kufuatia kuanzishwa tena kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, Idara ilianzisha REDET kama kitengo cha kufanya tafiti juu ya demokrasia na kutoa elimu ya uraia kwa Watanzania. Lengo lake kuu ni kuchangia kwenye mchakato wa kujenga demokrasia nchini Tanzania kupitia tafiti, machapisho na kutoa elimu. Hususan, inakusudia kuimarisha demokrasia na utawala wa kidemokrasia. Muda mfupi baadaye, ikiongozwa na REDET, Idara iliamua kukusanya rasilimali zake na kuzishirikisha asasi zingine kutazama uchaguzi wa kwanza uliofanyika chini ya mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1995. Mnamo mwaka 1994, ushirika uliojulikana kama Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) ulianzishwa na asasi za kiraia 24 zikiongozwa na REDET. Tangu hapo TEMCO imetazama uchaguzi wa mwaka 1995, 2000, 2003 (chaguzi ndogo), 2005, 2010 na 2015. REDET iliipatia TEMCO msaada wa kiufundi na kitaalamu wakati huo.

Waanzilishi wakuu wa TEMCO walikuwa asasi za kidini kama Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza la Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na vyama vya wafanyakazi kama Chama cha

Walimu Tanzania (CWT). Kwa sababu ya mabadiliko, pamoja na sheria mpya chini ya kifungu cha 2 (b) Sura 337 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 3 ya Asasi Zisizo za Kiserikali (2019), asasi za kidini zilipoteza sifa ya kushiriki katika masuala ya kisiasa. Vivyo hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilizikataza asasi zilizosajiliwa kushirikiana na asasi zisizosajiliwa kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kwa sababu hiyo, Tume iliiruhusu REDET, kama asasi kiongozi ya TEMCO, kutazama uchaguzi kwa sababu msingi wa TEMCO ulikuwa umetikiswa kutokana na mabadiliko ya kisheria kama tulivyokwishaeleza. Katika kutazama uchaguzi, REDET inaongozwa na kanuni za uwajibikaji, usawa, uaminifu, uhalisia, kuaminika, uwazi na weledi.

## 1.3 SABABU NA MADHUMUNI YA REDET KUTAZAMA UCHAGUZI

Ili kuchochea uwazi na uwajibikaji, kujenga kuaminika na kuongeza imani ya wananchi kuhusu uhalali wa michakato na matokeo yote ya uchaguzi, REDET ilitazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Ilitaka kufanya tathmini ya kina na kamili ya mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2020-2021 ili:

i. kuwezesha usimamizi na ushiriki wa wananchi katika chaguzi, na hatimaye kujenga imani;

i. kubaini ni kwa kiasi gani chaguzi ni za kuaminika, huru, haki na amani;

ii. kuonesha dosari na matatizo ya kiuchaguzi yanayojitokeza kipindi cha uchaguzi;

iii. kutathmini vitu vinavyolinda ili kuwa na upigaji kura wa watu wote na wenye usawa kama ulinzi na uboreshaji wa haki za binadamu, zikiwamo haki za kiraia na kisiasa;

iv. kutoa mapendekezo kwa wadau wa uchaguzi, hususan serikali ya Tanzania na vyombo vinavyosimamia uchaguzi, juu ya hatua za kuchukua ili kuboresha usimamizi na ubora wa uchaguzi kwa lengo la kufikia viwango vya kimataifa vinavyokubalika katika chaguzi za kidemokrasia; na

v. kuonesha maeneo yanayoweza kusababisha migogoro, wakiwamo watekelezaji wa sheria ili watengeneze mikakati ya kutatua migogoro.

Lengo kuu la TEMCO lilikuwa kuangalia, kwa niaba ya wananchi, michakato ya uchaguzi wa mwaka 2020-2021 ili kubaini ni kwa kiasi gani ilikuwa ya kuaminika, huru, haki, amani na inayofuata sheria za nchi na viwango vya kimataifa vya chaguzi za kidemokrasia. Malengo ya Programu ni:

i. kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 uliofanyika nchini Tanzania (wa Muungano) na wa Zanzibar ili kubaini ni kwa kiasi gani ulifuata sheria za nchi na kanuni na vigezo vya kimataifa vya chaguzi za kidemokrasia

zinazoaminika;


ii. kutazama na kutathmini usawa katika kusimamia uchaguzi kwa ujumla, hususan ukamilifu wa miundombinu ya kisheria (sheria, kanuni na maelekezo ya uchaguzi) na vyombo vya dola vinavyosimamia sheria na amani;

iii. kutathmini usawa katika ugawaji na matumizi ya rasilimali za serikali kwa vyama vya siasa mbalimbali vinavyoshindana; na

iv. kutathmini ni kwa kiasi gani uchaguzi unaweza kuonekana kwamba ulikuwa wa kuaminika, huru na haki.

## 1.4 MAWANDA YA UTAZAMAJI

Utazamaji wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 uliofanywa na REDET ulikuwa wa kina na ulihusisha nchi nzima na mchakato wote wa uchaguzi (tazama Kiambatisho I). Utazamaji ulihusisha michakato yote ya uchaguzi kuanzia shughuli zilizofanywa kabla ya uchaguzi (uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Taifa la Wapiga Kura (PNVR), utoaji wa elimu ya mpiga kura, ugawaji wa majimbo, uteuzi wa wagombea na kampeni za uchaguzi), shughuli zilizofanywa siku ya uchaguzi (ufunguzi wa vituo vya kupigia kura, upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo) na matukio yaliyotokea baada ya uchaguzi. Utazamaji wa REDET ulitoa kipaumbele katika maeneo yafuatayo: (i) mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa ajili ya uchaguzi mkuu; (ii) ugawaji wa majimbo ya uchaguzi; (iii) uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa; (iv) uteuzi wa wagombea; (v) kampeni; (vi) upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo; (vii) matukio yaliyojitokeza baada ya uchaguzi; (viii) nafasi ya vyombo vya habari; (ix) elimu ya mpiga kura; na (x) ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. REDET iliandaa taarifa nyingine juu ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Taifa la Wapiga Kura, kwani Tume ilikamilisha zoezi hilo miezi mingi kabla ya uteuzi wa wagombea na kampeni za uchaguzi kuanza.




*Umbo Na. 1.1: Muundo wa Programu ya REDET*

## 1.5 UTEUZI NA UTOAJI MAFUNZO KWA WATAZAMAJI

### 1.5.1 Uteuzi wa Watazamaji

REDET ilitumia njia ya wazi na kuzingatia vigezo katika kuteua watazamaji wake wa muda mrefu (LTOs) na wa muda mfupi (STOs) ambapo waliopenda walituma maombi. Waombaji wote walisailiwa na jopo la wataalamu na baadaye baadhi yao walichaguliwa. Ili kuzingatia hatua za kupambana na UVIKO-19, usaili wa ana kwa ana haukufanyika. Katika kuchagua watazamaji wa muda mrefu, jopo lilizingatia sifa zifuatazo: (i) kuwa na shahada ya kwanza kutoka chuo kikuu kinachotambulika, hususan katika masomo ya sayansi ya jamii, (ii) utendaji mzuri wa siku za nyuma kama mtazamaji uchaguzi nchini, (iii) uwezo wa kuandika taarifa, (iv) uaminifu, ukamilifu na kutopendelea, (v) upatikanaji, na (vi) kuzingatia jinsia. Hivyo, kati ya watazamaji 200 wa muda mrefu walioteuliwa, 110 (asilimia 55) walikuwa wanaume na 90 (asilimia 45) walikuwa wanawake.

Watazamaji wa muda mfupi walitoka katika vyanzo vitatu vya msingi, yaani wanafunzi wa vyuo vikuu (kama vile wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Zanzibar); walimu ambao ni wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na mtu mmojammoja ambaye amewahi kushiriki katika michako ya uchaguzi ya siku za nyuma. Mtu aliruhusiwa kufanya kazi kama mtazamaji wa

muda mfupi endapo alikuwa mkazi wa jimbo husika. Kwa ujumla, watazamaji wa muda mfupi 3,100 waliteuliwa, kati yao 1,787 (asilimia 58) walikuwa wanaume na 1,313 (asilimia 42) wanawake. Kati ya watazamaji wa muda mfupi walioteuliwa, REDET iliwapangia vituo watazamaji 2,353. Waliobaki hawakuweza kutumika kutokana na changamoto za dakika za mwisho zilizojitokeza na kushindikana kupatikana kwa watu wa kuziba pengo lao.

### 1.5.2 Utoaji Mafunzo kwa Watazamaji

Watazamaji wote wa muda mrefu walipata mafunzo kwa siku mbili, tarehe 25 na 26 Septemba 2020, kabla hawajaenda kufanya kazi majimboni. Mafunzo yalitolewa juu ya mada zifuatazo: (i) utumiaji wa vifaa vya kukusanyia data; (ii) sheria na kanuni za uchaguzi; (iii) maadili ya watazamaji wa uchaguzi wa REDET; (iv) kanuni za maadili kwa ajili ya watazamaji wa ndani zinazotolewa na vyombo vya kusimamia uchaguzi; (v) kutunza kumbukumbu kuhusu wanawake, vijana na watu wenye ulemavu walioshiriki katika uchaguzi mkuu; na (vi) TEHAMA.

Timu ya watoa mafunzo ilijumuisha Mwenyekiti na Mkuu wa Usimamizi wa Uchaguzi, Profesa Rwekaza Mukandala; kamishna mstaafu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Profesa Amon Chaligha; Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Emmauel Kawishe; Mtaalamu wa Masuala ya Kijinsia wa REDET, Profesa Bernadeta Killian; Msajili wa Vyama vya Siasa Msaidizi, Ndugu Sisty Nyahoza; Mtaalamu wa TEHAMA wa REDET, Ndugu Captain Patrick; Mwanahabari, Ndugu Egbert Mkoko; na Mkurugenzi wa REDET, Dkt. Rasul Minja. Mafunzo yalikuwa shirikishi, ya kimazungumzo na yalimlenga mwanafunzi. Lugha za Kiingereza na Kiswahili zilitumika. Hali kadhalika, mafunzo hayo yalikuwa ni uwanja wa kujifunza kwa watoa mafunzo, hususan watazamaji wa muda mrefu ambao walipaswa kutoa mafunzo kwa watazamaji wa muda mfupi kwenye majimbo husika. Watazamaji wa muda mfupi walifunzwa kwa siku moja, kati ya tarehe 16 hadi tarehe 20 Oktoba 2020. Mada zilikuwa sawa na zile zilizotolewa kwa watazamaji wa muda mrefu.

## 1.6 MBINU NA METHODOLOJIA

Ili kufanya uchambuzi wa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2020 bila upendeleo wowote REDET ilitumia mbinu ya kisayansi. Mbinu hiyo ilijumuisha matumizi ya mikakati na njia za wazi za kutazama uchaguzi na matumizi ya watazamaji uchaguzi mahiri, wa kuaminika na wafanisi ambao walifanya kazi kwa

bidii. Walitumia madodoso na vifaa kukusanya taarifa.

### 1.6.1 Madodoso ya Kukusanyia Data

Aina tano ya madodoso ya kutazamia uchaguzi yaliandaliwa: (a) Dodoso la Kabla ya Siku ya Uchaguzi (ambalo lilijikita kwenye kampeni); (b) Dodoso la Siku ya Uchaguzi; (c) Dodoso la Matukio Baada ya Uchaguzi; (d)Dodoso la Matukio Hatarishi; na (e) Dodoso la Watazamaji wa Uchaguzi wa Mikoa (REOCs). Madodoso haya yaliunganishwa na Programu ya Data ya Kompyuta ya Wazi (Open Data Kit-ODK). ODK iliwezesha kukusanya data haraka na hivyo kuwafanya watazamaji watume taarifa mara moja. Iliweka vifaa vya kutazamia uchaguzi mtandaoni ambavyo vilipelekwa kwenye kituo cha kukusanyia data kwa kutumia simu za mkononi. Pia, ODK ilichambua data na kutoa majedwali mtambuka kwa ajili ya kufanya mahitimisho. Kwa sababu ya umuhimu na nafasi ya vyombo vya habari katika chaguzi za Tanzania, REDET ilitengeneza chombo maalumu cha kukusanyia data kutoka vyombo vya habari ambavyo vilitoa taarifa juu ya uchaguzi. Kazi hiyo ambayo ilijumuisha uchambuzi wa maudhui ilihusisha vyombo vya habari vya siku nyingi (magazeti, redio na televisheni) na vyombo vya habari vya mtandaoni (kama vile WhatsApp, televisheni za mtandaoni, blogi, Twitter na Facebook).

### 1.6.2 Usambazaji wa Watazamaji wa Muda Mrefu na wa Muda Mfupi

REDET ilipeleka watazamaji wa muda mrefu kwenye majimbo 200 (kati ya majimbo 264, sawa na asilimia 76). Kati ya watazamaji hao, 150 walisambazwa kwenye majimbo ya Tanzania Bara na 50 kwenye majimbo ya Zanzibar (asilimia 100). Watazamaji wa muda mrefu walifanya kazi kwenye majimbo yao siku ya tarehe 28 Septemba 2020 na kubaki huko mpaka tarehe 5 Novemba 2020. Majimbo hayo 200 yalichaguliwa baada ya kufanya tafakari ya mahitaji ya data, hali ya kisiasa katika baadhi ya wilaya na maeneo na sababu zingine muhimu (tazama Kiambatisho I). Siku ya uchaguzi REDET ilisambaza watazamaji wa muda mfupi 2,353 kwenye vituo. Vigezo vilivyotumika kufanya usambazaji huo ni (a) kufikika na mgawanyiko wa kijiografia wa kata kwenye majimbo; (b) kuwa karibu na makazi ya watazamaji wa muda mfupi; na (c) tathmini ya awali ya hali ya kisiasa kwenye kata iliyofanywa na watazamaji wa muda mrefu.

### 1.6.3 Ziara za Usimamizi na Ufuatiliaji

Ili kuhakikisha kazi ya kutazama uchaguzi inakwenda vizuri, REDET iliandaa ziara za usimimamizi na ufuatiliaji majimboni. Ziara hizo zililenga:

i. Kubaini ni kwa kiasi gani watazamaji wa muda mrefu walikuwa wanatekeleza majukumu yao;
ii. Kujadidili na kutatua masuala na changamoto kubwa zilizokuwa zinazowakabili katika kufanya kazi yao;
iii. Kufuatilia shughuli ya kutazama uchaguzi inavyokwenda ili kuhakikisha kwamba inafanyika kulingana na masharti ya mkataba wao wa kazi; na
iv. Kupata taarifa halisi kuhusu mchakato wa uchaguzi, kwa kuzingatia matokeo ya awali ya waratibu wa utazamaji uchaguzi wa mikoa na watazamaji wa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Mradi aliwatembelea watazamaji wa muda mrefu wa Kagera, Manyara, Simiyu na Arusha (kwa upande wa Tanzania Bara) na Unguja kwa upande wa Zanzibar. Pia, aliwatembelea waliokuwa wanafanya kazi mikoa ya Kigoma, Singida na Dodoma, wakati Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini aliwatembelea watazamaji wa Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa na Morogoro. Msimamizi huru wa nje alitembelea mikoa miwili ya Pemba Kaskazini (Wilaya ya Micheweni na Wete) na Pemba Kusini (Wilaya ya Mkoani na Chakechake). Ufuatiliaji na usimamizi huo ulisaidia kutoa msaada wa papo kwa papo kwa watazamaji wa muda mrefu na waratibu wa utazamaji uchaguzi wa mikoa ambao waliangalia mwenendo wa uchaguzi kwenye mikoa mbalimbali.

Njia tatu zilitumika kukusanya taarifa katika ufuatiliaji huo. Mosi, usaili uliotumia maswali yaliyokwishaandaliwa ulifanyika na waratibu wa utazamaji uchaguzi wa mikoa na watazamaji wa muda mrefu. Pili, waliangalia utendaji kazi wa watazamaji wa muda mrefu, vifaa vyao, mavazi yao, orodha zilizopo katika simu zao na uchangamani wao na wananchi. Mwisho, wasimamizi walifanya mahojiano kikundi na watazamaji wa muda mrefu ili kufahamu changamoto zilizokuwa zinawakabili wakati wa kutazama uchaguzi.

### 1.6.4 Hatua za Kukabiliana na UVIKO-19

Kwa kutambua changamoto zinazosababishwa na UVIKO-19, REDET ilichukua hatua kadhaa kuwalinda watazamaji wa muda mrefu na watazamaji wa muda mfupi na wadau wengine dhidi ya ugonjwa huo. Mosi, kama ilivyokwishaelezwa REDET ilitumia njia mbadala kupata watazamaji ili kuzuia mikusanyiko ya watu wengi kadiri iwezekanavyo. Moja ya njia hizo ni kutowasaili watazamaji uchaguzi wa muda mrefu, zoezi ambalo hukusanya watu wengi mno katika ofisi za REDET. Pale ilipokuwa ni lazima kukusanyika pamoja, kama ilivyokuwa kipindi cha mafunzo,

REDET ilichukua hatua za kukaa mbali pamoja na hatua zingine za tahadhari kama vile matumizi ya vitakasa mikono. Watazamaji uchaguzi wa muda mrefu walipatiwa mafunzo na walisisitizwa kuchukua tahadhari watakapokuwa katika maeneo yao ya kazi na kujilinda dhidi ya hali yeyote hatarishi. Mawasiliano yalikuwa wazi na watazamaji wa muda mrefu walihimizwa kutoa taarifa juu ya dalili zozote za homa na kuchukua hatua za haraka, ikiwamo kwenda vituo vya afya vya karibu. Hususan, REDET iliangalia namna ambayo wadau wengine walichukua hatua dhidi ya UVIKO-19. Moja ya madodoso lilikuwa na maswali yaliyohusu suala hilo. REDET ilifurahishwa kwamba hakuna mtazamaji uchaguzi hata mmoja aliyeugua katika kipindi chote cha kutazama uchaguzi.

## 1.7 VIGEZO VYA KUTATHMINI UCHAGUZI

Kwa kufahamu desturi za kimataifa na kwa kuelewa pia kwamba Tanzania imesaini mikataba mingi ya kikanda na ya kimataifa kuhusu haki za binadamu, demokrasia na uchaguzi, REDET ilitumia vigezo vya kutathmini uchaguzi vilivyoandaliwa na TEMCO. Tathmini hii inajumuisha matumizi ya njia za kitamuli na kitakwimu ili kufanya hitimisho mahususi kuhusu uhalali wa uchaguzi. Vigezo hivyo vinamruhusu mtu kufanya tathmini ya mchakato wa uchaguzi katika mzunguko wa uchaguzi ili kutoa hitimisho juu ya ubora wa mchakato mzima wa uchaguzi. Utaratibu wa kufanya tathmini unajumuisha makadirio yanayofanywa kwenye kigezo kinachoanzia “A” hadi “F”. Kila herufi moja inapewa thamani ya asilimia 0 hadi 100. Utaratibu huu uliwawezesha watazamaji wa REDET kufanya tathmini huru juu ya ubora wa uchaguzi katika majimbo waliyopelekwa kufanya kazi. Kwa hiyo, tathmini ya jumla ni wastani wa pointi zilizotolewa na mtu mmoja mmoja katika majimbo yaliyotazamwa.

Ili kuandaa taarifa hii, watazamaji wa muda mrefu na wa muda mfupi walipeleka taarifa kuhusu uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi na shughuli zilizofanywa siku ya uchaguzi (hadi kutangaza matokeo) kwenye makao makuu ya REDET jijini Dar es Salaam. Tathmini hizi zilisaidia kubaini hali ya mchakato wa uchaguzi na kwa kiasi gani uchaguzi ulikuwa “huru” na wa “haki”. Kwa kila mchakato wa uchaguzi pointi zilikuwa kama ifuatavyo:

i. Asilimai 80-100 au herufi A inamaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ulikuwa na changamoto chache ambazo haziathiri matokeo ya jumla ya uchaguzi. Ni uchaguzi safi, wa kuaminika, huru na wa haki.
ii. Asilimia 60-79 au hefuri B inamaanisha uchaguzi (au hatua ya uchaguzi)

ambao kwa ujumla ni huru na wa haki, lakini una dosari ambazo zinawaathiri baadhi ya wadau (wapiga kura, wagombea na vyama vya siasa). Ni uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao unaonekana kuwa huru na wa usawa.

iii. Asilimia 50-59 au herufi C inamaanisha kwamba ni uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) unaoruhusu ushiriki huru wa wadau (wapiga kura, wagombea, vyama vya siasa na wengine), lakini kuna matukio mengi ya vyama vya siasa kunyimwa fursa. Hali hii ina maana kwamba uchaguzi ni "huru lakini si wa haki".

iv. Asilimia 40-49 au herufi D inamaanisha kwamba mchakato wa uchaguzi una vurugu, vitisho, upendeleo na rushwa. Uchaguzi huu unastahili kupewa cheti "kinachoonesha kwamba si huru na si wa haki".

v. Asilimia 1-39 au herufi E maana yake ni kwamba ni uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) wenye changamoto nyingi kuhusu usimamizi na dosari ambazo wadau walio wengi (wapiga kura, wagombea na vyama vya siasa ) na ambao matokeo yake yanakataliwa au yanaweza kukataliwa. Unapewa cheti kinachoonesha kwamba "haukuendeshwa vizuri hata kidogo".

vi. Asilimia 0 au herufi F inamaanisha kwamba uchaguzi (au hatua ya uchaguzi) ambao umeshindwa kabisa katika nyanja ya usimamizi, uzingatiaji wa kanuni za uchaguzi na maadili ya uchaguzi na usawa, na kwa hiyo haukumalizika kama ambavyo chaguzi zinavyomalizika. Uchaguzi kama huo ni "uchaguzi ulioharibika".

## 1.8 MUUNDO WA TAARIFA HII

Taarifa hii ina sura tisa, ikiwamo sehemu hii ya usuli na methodolojia. Sura ya Pili inajikita katika muktadha wa uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2020. Inaangalia masuala ya kiuchumi, kijamii na kisisasa ambayo yalikuwa na athari fulani katika uchaguzi huo. Sura ya Tatu inaangalia mfumo wa kisheria na kitaasisi uliotumika kuendesha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sura ya Nne inahusu uteuzi wa wagombea na Sura ya Tano inajikita kwenye kampeni za uchaguzi. Sura ya Sita inajadili namna vyombo vya habari vilivyofanya kazi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na Sura ya Saba inatazama ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uchaguzi huo. Sura ya Nane inatazama uendeshaji wa uchaguzi wa Zanzibar wa mwaka 2020 na Sura ya Tisa inatoa tathmini ya jumla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

## 1.9 SHUKRANI

Taarifa hii ni matokeo ya jitihada za asasi na watu mbalimbali. Kama si ushiriki na

msaada wao, utazamaji wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 usingefanyika. Kwa hiyo, REDET inatoa shukrani kwa watu wa Marekani kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID) kwa kufadhili mradi wa kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Hali kadhalika, tunatoa shukrani kwa Shirika la Kimataifa la Misaada la Denmark (DANIDA) na Ubalozi wa Denmark kwa msaada wa kifedha waliotoa.

REDET inavishukuru vyombo vya kusimamia uchaguzi nchini Tanzania (Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar) kwa kuiruhusu kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, kwa wakati wote kutoa msaada ili kufanikisha zoezi hilo na kwa kuisajili REDET na kutoa msaada kwa watazamaji wetu 2,353 wa muda mrefu na wa muda mfupi waliosambaza kwenye majimbo mbalimbali. Tunawashukuru wadau wa REDET kutoka nchi nzima waliokuwa tayari kushiriki katika zoezi hili na kututumia maelezo yao binafsi ili tuchague watazamaji. Watazamaji waliochaguliwa walikuja kupata mafunzo na walikubali kusambazwa na kufanya kazi kwa ufanisi. Tunakishukuru sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuendelea kuisadia REDET. Makamu Mkuu wa Chuo Profesa William A. L. Anangisye na uongozi wote wa chuo wanastahili shukrani za dhati kwa kutupatia nyenzo kama vile ofisi na sehemu za kufanyia mikutano na warsha. Tunatoa shukrani zetu kwa wanaidara wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kwa kufanya kazi kwa kujitolea katika hatua za awali za kuandika pendekezo wakati ambapo upatikanaji wa fedha haukuwa wa uhakika. Shukrani ziwafikie Profesa Rwekaza Mukandala, Dkt. Rasul Minja, Dkt. Lupa Ramadhani, Dkt. Kelvin Munisi, Profesa Bernadeta Killian, Dkt. Richard Mbunda, Dkt. Consolata Sulley, na Dkt. Dotto Kuhenga kwa kufanya kazi ya uadaaji wa muswada wa taarifa hii. Mwisho, tunatoa shukrani kwa kazi kubwa, kujitoa na msaada tuliopata kutoka kwenye sekretarieti yetu ikiongozwa na Profesa Rwekaza Mukandala. Alisaidiwa na Dkt. Rasul Minja, Mkurugenzi wa Mradi; Dkt. Lupa Ramadhani; Dkt. Deogratius Rugaimukamu; Ndugu Dunia Nassoro; Ndugu Captain Patrick; Bi. Hellen Nyukuri; Bi Matilda Mrosso; Bi. Mwati Kisesa; Bi. Anney Yamungu; na Ndugu Dismas Daniel.

Mara baada ya kusherehekea mwaka mpya, tulistushwa na kuhuzunishwa na taarifa ya kifo cha Dkt. Deogratias Rugaimukamu kilichotokea tarehe 23 Januari 2021 nyumbani kwake Kunduchi Mtongani, Dar es Salaam. REDET inamtabaruku ‘Dkt. Rugai’ kama alivyofahamika kwenye mazingira ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na zaidi katika ofisi za REDET. Dkt. Rugai alikitumikia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mkufunzi Msaidizi kuanzia mwaka 1973 na kupanda hadi ngazi ya

Mhadhiri Mwandamizi, nafasi ambayo alikuwa nayo hadi anastaafu mwaka 2009.

Dkt. Rugai alikuwa na uwezo wa kuwafikia watu kwa ukaribu. Hakuna mtu hata mmoja aliyewahi kukutana naye akalisahau tabasamu lake la kuambukiza na heshima aliyompa kila mtu aliyekuwa karibu naye. Tulivutiwa na uanataaluma wake na kujitoa kwake katika kuutumikia umma. Nguvu na kujitoa kwa Dkt. Rugai katika kufanya kazi kulikuwa kwa kiwango kikubwa sana. Kupatikana kwake katika Idara ya Sayansi ya Siasa ambapo REDET ipo hakukuwa na mfano. Tunatoa shukrani kwake kwa ushiriki wake katika kuandaa mradi wa TEPO mwaka 2019 hadi kipindi cha kukusanya data mwezi Oktoba 2020. Inahuzunisha kuona kwamba Dkt. Rugai alituacha kabla hajaisoma taarifa ya mwisho kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ambayo inajumuisha michango yake muhimu kadhaa, zikiwamo taarifa nzuri kutoka katika taarifa yake ya mkoa. Mwezi Oktoba 2020 Dkt. Rugai alifanya kazi kama Mratibu wa Uchaguzi wa REDET wa Mkoa kwenye mkoa wa Kagera wakati wa kukusanya data. Alikuwa mwanachama mwanzilishi wa REDET toka kuanzishwa kwake mwaka 1992, akiitumikia programu katika nyadhifa mbalimbali kama vile mchambuzi wa takwimu, mchambuzi wa methodolojia, mwandishi wa taarifa, mratibu wa programu na mratibu wa mkoa. Roho Yake Ipumzike kwa Amani.

Taarifa hii imedhaminiwa na watu wa Marekani kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Marekani. Hata hivyo, maudhui yaliyomo kwenye taarifa hii, yakiwamo maoni, dosari na kasoro, ni jukumu la REDET na hayaashirii maoni au msimamo rasmi wa USAID au Serikali ya Marekani.

# SURA YA PILI

# MUKTADHA WA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA WA MWAKA 2020

## 2.1 UTANGULIZI

Uchaguzi ni mchakato nyeti katika mfumo wowote wa siasa za upinzani. Unawapa fursa na mbinu watu na vikundi mbalimbali kushindana kwa amani ili kupata madaraka ya kisiasa. Uchaguzi unaathiriwa na mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ya wakati husika. Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 haukuwa tofauti, yaani miaka 25 baada ya kuanzishwa tena siasa za mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania. Sura hii inaangalia muktadha wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yaliathiriwa na masuala kadhaa kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara. Kufuatia kuchaguliwa kwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kama Rais mwaka 2015, uchaguzi huu ulitoa fursa kwa mpiga kura wa Tanzania kupima utendaji wake. Alipata asilimia 58 ya kura zote za urais mwaka 2015—kiwango cha chini zaidi alichowahi kupata mgombea urais wa Chama cha Mapinduzi tangu uchaguzi wa kwanza uliofanyika chini ya mfumo wa vyama vingi wa mwaka 1995. Kwa hiyo, swali lilikuwa: Je, Rais Magufuli angeweza kufanya vizuri kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020? Kama inavyofafanuliwa kwenye aya zifuatazo, alitoa ahadi nyingi sana na alijaribu kufanya kama alivyoahidi katika kipindi cha miaka mitano. Hivyo basi, swali lingine lililosumbua vichwa vya watu ni: Je, wapiga kura wangepimaje utendaji wake?

Upinzani ulifanya vizuri sana katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ukijipatia viti vingi zaidi ya viti ilivyowahi kuvipata. Walifanya vizuri pia katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014. Je, wangeweza kufanya hivyo tena au zaidi mwaka 2020? Je, vyama vya upinzani vingeweza kuishinda faida aliyokuwa nayo Rais Magufuli ya kuwa madarakani na utawala wa CCM?

Hakika, kuna watu walisema kwamba mazingira ya kisiasa hayakuwa mazuri kwa vyama vya upinzani kuendelea kuungwa mkono kutokana na nafasi finyu ya kidemokrasia ambayo ni matokeo ya vitendo vya Rais na sheria zilizotungwa na Bunge. Wasorajua hao walisema kwamba kuhama kwa wabunge, madiwani na wenyeviti wa mitaa ambako hakujawahi kutokea na kujiunga na chama tawala, kitu ambacho kilijitokeza zaidi kadiri uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulivyokaribia, kungeathiri ushindani.

Kwa upande wa Zanzibar kipindi cha mwaka 2015-2020 kilitawaliwa na kukosekana kwa serikali ya umoja wa kitaifa ambayo inajumuisha chama cha upinzani kama vifungu vya katiba juu ya serikali ya umoja wa kitaifa vinavyotaka. Chama cha Wananchi (CUF) kilisusia uchaguzi wa marudio wa Zanzibar wa mwaka 2015, wakipinga kufutwa kwa uchaguzi wa Oktoba 2015 na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambao waliamini kwamba walishinda. Kwa hiyo, wapiga kura, hususan wafuasi wa upinzani, wangepigaje kura?

Sehemu iliyobaki ya sura hii inaangalia masuala haya na mengine yaliyojitokeza kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Mambo hayo ni: (i) utendaji wa serikali ya awamu ya tano (2015-2020), (ii) masuala ya kisiasa, (iii) mkwamo wa kisiasa wa Zanzibar na (iv) muktadha wa kikanda na kimataifa. Mjumuisho wa masuala haya ni muhimu katika kuelewa mwenendo na matokeo ya uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2020.

## 2.2 UTENDAJI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO (2015-2020)

Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipoingia madarakani mwishoni mwa mwaka 2015 kaulimbiu yake ilikuwa *Hapa Kazi Tu*. Aliahidi kupambana na rushwa nchini na kupunguza matumizi ya serikali. Akiwa anazindua Bunge tarehe 11 Novemba 2015, Dkt. Magufuli aliorodhesha rushwa kubwa, ufujaji wa fedha za umma kwenye serikali za mitaa na kuacha kufanya uwekezaji wa kimkakati kwenye miundombinu na uvivu kama vikwazo vikuu kwenye maendeleo ya kiuchumi.

Aliahidi pia kuchukua hatua madhubuti kuchochea maendeleo ya kiuchumi na utoaji huduma za jamii. Hali kadhalika, aliahidi kupambana na umasikini na kuboresha hali za maisha ya watu hadi kufikia uchumi wa kati. Aliahidi kupanua fursa za kiuchumi kupitia ujenzi wa viwanda, hususan viwanda vya kutengeneza nguo, viwanda vya kusindika vyakula na viwanda vingine vinavyotumia malighafi ya kilimo. Kazi hii ilipaswa kwenda sambamba na maendeleo ya miundombinu, ikiwamo upanuzi na uboreshaji wa njia za usafiri, hususan reli, bandari na usafiri wa anga. Aliahidi kutoa huduma bora za afya, hususan kwa wanyonge, kutoa elimu bure, maji safi na huduma zingine za jamii.

Alitekeleza ahadi zake kwa vitendo. Mara tu baada ya kuingia madarakani Rais Magufuli alikataza safari za nje na ndani ya nchi za viongozi wa umma zisizo za lazima. Binafsi alijizuia kusafiri nje ya nchi. Alikataza kusafiri katika daraja la kwanza kwenye ndege miongoni mwa mawaziri na maofisa wa serikali, isipokuwa

Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Alikataza tabia ya kufanya mikutano na warsha kwenye hoteli na alitumia fedha zilizopangwa kutumika katika sherehe za Uhuru na Siku ya UKIMWI Duniani kutatua matatizo yanayoikabili jamii kama vile kununua vitanda vya hospitali na kupanua barabara ili kupunguza msongamano jijini Dar es Salaam. Alianzisha mchakato wa kuondolewa kwenye orodha ya malipo wafanyakazi hewa. Baraza lake la mawaziri la kwanza lilikuwa na mawaziri 34 (mawaziri kamili 19 na naibu mawaziri 15) ukilinganisha na mawaziri 55 wa serikali iliyotangulia. Hatua hizi zote zilikusudiwa kuokoa fedha za umma ili zitumike kutoa huduma za lazima za jamii, hususan huduma za watu masikini.

Kwa upande wa huduma za jamii, Rais aliongeza uandikishaji wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupitia sera yake ya elimu bure. Waraka wa Serikali Namba 15 wa mwaka 2015 uliwataka wazazi wasilipe ada au michango mingine katika shule za msingi na sekondari za umma. Kabla ya hapo shule za sekondari zilikuwa zinatoza ada ya shilingi 20,000 kwa shule za kutwa na shilingi 40,000 kwa shule za bweni. Hatua hizi ziliongeza uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi hizi na kuwapunguzia wazazi mzigo wa kulipa ada. Serikali ya awamu ya tano pia ilifanya uwekezaji mkubwa kwenye utoaji huduma za afya. Idadi ya vituo vya afya na hospitali iliongezeka kutoka 7,014 mwaka 2015 hadi 8,783 mwaka 2020 (*Daily News*, 2020). Hospitali za mikoa zilipandishwa hadhi na kuwa hospitali za rufaa. Dawa ziliongezeka na vivyo hivyo, maelfu ya madaktari na watoa huduma za afya wengine waliajiriwa. Matokeo yake ni kwamba ilikuwa rahisi kwa watu wa vijijini kupata huduma za afya. Kupitia mradi wa kusambaza umeme vijijini, asilimia 68.8 ya watu wa vijijini waliunganishwa na huduma ya umeme.

Katika awamu yake ya kwanza wananchi waliona kuwa Rais anapita kwenye nyayo za Mwalimu Nyerere. Yeye mwenyewe alisema mara nyingi kwamba alikuwa anajenga Tanzania ambayo Mwalimu Nyerere aliitaka. Alianzisha hatua za kutekeleza miradi kadhaa iliyoanzishwa na Rais Nyerere wakati wa utawala wake. Miradi hiyo inajumuisha mradi wa muda mrefu wa kuhamisha makao makuu ya serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma; ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Stigler's Gorge; kufufua msisitizo wa kujenga viwanda na kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL). Ilitarajiwa kwamba uanzishaji wa miradi hiyo yote ungewafanya wananchi wampende Rais Magufuli, ukizingatia heshima kubwa ambayo Mwalimu Nyerere bado anayo miongoni mwa Watanzania.

Kwa upande wa uongozi, Rais, mawaziri na viongozi wengine waandamizi

wa serikali walisimamia shughuli za umma moja kwa moja. Hii ni pamoja na kutembelea maeneo ya kazi mara nyingi, na kuchukua hatua za haraka na hatua za kinidhamu, pamoja na kuwafukuza au kuwasimamisha kazi maofisa au makandarasi ambao walibainika kuwa na kasoro. Serikali ilifanya jitihada kadhaa kuboresha utendaji na uwajibikaji wa watendaji wa serikali. Moja ya matokeo chanya ya hatua za Rais ni kuboreshwa kwa utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mathalani, katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 TRA ilikusanya asilimia 90 ya mapato (trilioni 17.2 kati ya trilioni 19.1) iliyokusudiwa. Hali kadhalika, kiwango cha rushwa kilishuka na utendaji wa TRA uliongezeka kwa sababu ya dhamira ya viongozi na utashi wa kisiasa. Viongozi waliondolewa mara kwa mara; mfumo wa kidijitali wa kukusanyia mapato ulianzishwa; maadili, sheria na kanuni za kupambana na rushwa zilisisitizwa; uchunguzi na ukaguzi wa haraka ulifanyika; na hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi walarushwa na kubadilishwa kwa viongozi wakuu wa TRA kulifanyika mara kwa mara (Makubi na Issa, 2019).

Rais alianzisha mabadiliko makubwa kwenye sekta ya madini mwaka 2017. Nchi ilibadilisha sheria zinazohusu utoaji mikataba ya madini, ikijipa yenyewe haki ya kupitia au kufuta mikataba kama kuna hujuma zozote zinazobainika. Sheria mpya zimeondoa haki ya kampuni za madini kufungua kesi kwenye mahakama za kimataifa. Malumbano yaliyohusu kodi dhidi ya kampuni ya Acacia ambayo ilionesha thamani ndogo ya dhahabu kwa miaka mingi na kutatuliwa kwa mgogoro huo yalitatuliwa. Tanzania ilipata asilimia 16 ya hisa zilizopo kwenye madini ya kampuni za kimataifa na mwezi Mei 2020 Acacia iliilipa serikali dola milioni 100 ili kumaliza mgogoro huo kama sehemu ya kwanza ya dola milioni 300 zilizoahidiwa.



***Waziri wa Katiba na Sheria wa Tanzania, Palamagamba Kabudi, akiwa na wajumbe wa Kampuni ya Dhahabu ya Barrick Ikulu Dar es Salaam waliokuja kutatua mgogoro wa Acacia tarehe 31 Julai 2017.***

Bunge lilifanya kazi kubwa katika sekta ya madini. Sekta hii ilikuwa ni eneo muhimu kwa sababu madini yalikuwa hayainufaishi nchi kwani sheria zilizokuwapo hazikuweka mbele masilahi ya nchi. Hivyo basi, mwaka 2017 Bunge lilitunga sheria tatu zilizoleta mapinduzi ya namna sekta ya madini inavyoendeshwa. Sheria hizo ni Sheria ya Mamlaka ya Mapitio (Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi) ya mwaka 2017, Sheria ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017 na the Written Laws Act. Pamoja na mambo mengine, sheria hizo zilirudisha uhuru wa serikali katika sekta ya madini (tofauti na kutekwa kwa serikali), zililipa nguvu Bunge kupitia mikataba au makubaliano yeyote kuhusu uchimbaji na utafutaji madini iliyoingiwa na serikali na watu binafsi, zilizitaka kampuni za madini kuipatia serikali hisa sawa katika biashara zao na ziliweka vikwazo juu ya usafirishaji madini  nje ya nchi na uchukuaji fedha kutoka kwenye shughuli za madini. Kitu kingine kilichojitokeza ni uanzishwaji wa Tume ya Madini, badala ya Bodi ya Ushauri ya Madini. Tume hiyo ina mamlaka ya kutoa leseni, kusimamia na kufuatilia sekta ya madini na shughuli zake, na kuhakikisha utafutaji na uchimbaji madini unafanyika vizuri. Sheria hizo zinakusudiwa kubadilisha namna sekta ya madini inavyoendeshwa na kuongeza faida kwa serikali na jamii za Watanzania zinazoishi katika maeneo husika.

Lakini, taarifa ya tathmini ya umasikini wa Tanzania Bara ya mwaka 2019 imeonesha kwamba pamoja na ukuaji uchumi endelevu na kupungua kwa umasikini endelevu, idadi ya watu masikini imeongezeka kutoka watu milioni 13 mwaka 2007 hadi watu milioni 14 mwaka 2019. Taarifa hiyo imeonesha kwamba idadi ya watu walioko hatarini ni kubwa kwa kuwa kati ya kila Watanzania wanne waliojinasua kutoka kwenye umasikini Watanzania watatu waliingia kwenye umasikini. Imeonesha pia idadi kubwa ya watu ambao si masikini lakini ambao wako juu kidogo tu ya mstari wa umasikini ambao wangeweza kuwa maskini tena. Hali kadhalika, imeonesha tofauti kubwa ya kusambaa kwa umasikini katika mikoa. Kwa hiyo, kadiri uchaguzi ulivyokaribia mjadala ulikuwa: Je, kipi muhimu zaidi kati ya "maendeleo ya vitu" na "maendeleo ya watu"? Watu hawakuwa na uhakika kama miradi iliyotekelezwa na serikali ilisaidia kuboresha maisha ya mtu mmoja mmoja. Lakini tarehe 1 Julai 2020 Benki ya Dunia ilitangaza kwamba Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati.

Bunge liliendelea kutunga sheria awamu ya kwanza ya Rais Magufuli. Kama moja ya vyombo vikuu vya serikali, Bunge lilitarajiwa kufanya kazi bila kuingiliwa ili kutetea masilahi ya wananchi. Awamu ya kwanza ya Rais Magufuli ilishuhudia

utungwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2017, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015.[1] Kutungwa kwa sheria hizi kumeleta hisia tofauti miongoni mwa wananchi kuhusiana na masuala kadhaa ya utawala kama nafasi ya vyombo vya habari, udhibiti wa sauti za wananchi, shughuli za kisiasa na utawala wa sheria. Sheria ya Vyama vya Siasa inampa Msajili wa Vyama vya Siasa mamlaka makubwa ya kudhibiti shughuli za vyama. Kuvunja sheria hiyo kunakaribisha adhabu za jinai. Baadhi ya wadau wa uchaguzi hawakuridhishwa na sheria hizo, wakidai kwamba zinaminya haki za binadamu, zikiwamo haki za kiraia na kisiasa za kupata taarifa na kujieleza.

Sheria zingine ambazo Bunge ilitunga au kuzibadilisha ni Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016. Sheria hii inasimamia shughuli nyingi za habari, inataka usajili wa wanahabari, inaweka masharti mengi kuhusu upatikanji wa leseni za kuendesha vyombo vya habari na inaipa dola nguvu nyingi za kuingilia kazi za vyombo vya habari. Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kieleketroniki na Posta ya mwaka 2019 na kanuni zake za mwaka 2020 zinaipa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nguvu ya kudhibiti maudhui na mawasiliano ya kimtandao (CRS, 2020).

Mazingira ya kisheria yaliyofuata yalileta shaka kuhusu haki ya waandishi wa habari kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo. Kupitia mitandao ya kijamii watu walieleza wasiwasi wao kuhusu unyanyasaji, vitisho, kukamatwa na hata kupotea kwa baadhi ya wanahabari kama vile wanahabari wa habari za uchunguzi Azory Gwanda na Joseph Gandye; kukamatwa na kushtakiwa kwa Erick Kabendera na kufungiwa kwa magazeti yanayokosoa na mabloga binafsi. Magazeti kadhaa, televisheni za mitandaoni na blogi zilisimamishwa, kutozwa faini na baadhi yao kufungiwa kabisa. Vyombo vya habari hivyo ni pamoja na gazeti la *The Citizen* na tovuti yake ambayo ilifungiwa kwa siku saba, *Televisheni ya Kwanza*, *Televisheni ya Millard Ayo* na *Televisheni ya Watetezi* (Human Rights Report, 2019). Vituo vingine vya televisheni na redio vilivyofungiwa kwa muda na TCRA ni *Clouds Fm*, *Wasafi Fm* na *Televisheni*, na gazeti la mtandaoni la *Mwananchi*.

Utendaji wa mahakama katika awamu ya kwanza ya Rais Magufuli pia uliangaziwa. Wakati anaahirisha Bunge Rais alisema kwamba mafanikio ya mahakama ni pamoja na kupunguza rushwa, kitu ambacho kilijumuisha pia kuwafikisha mahakamani watu wasiokuwa na hatia ya kufanya kosa lolote (*Daily News*, 2020). Aliteua majaji

1 Sheria ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019 ili kuondoa adhabu za jinai lakini kanuni ambazo ni mzigo zinazohusu ukusanyaji na uchapishaji data na ukosoaji takwimu rasmi hazikufutwa (CRS, 2020).

17 wa mahakama ya rufaa, 52 wa mahakama kuu na maofisa wa mahakama 859, pamoja na mahakimu 396 katika kipindi chake cha kwanza. Mahakama ilianzisha mahakama inayotembea Mwanza na Dar es Salaam; hadi kufikia mwaka 2020 kesi 337 zilikuwa zimeshasajiliwa, kati ya hizo kesi 274 zilikuwa zimeshasikilizwa (*Daily News*, 2020). Katika awamu yake ya kwanza wafungwa 42,774 waliachiwa huru na kwa hiyo kupunguza msongamano magerezani. Rais alianzisha mahakama ya mafisadi na wahujumu uchumi. Mahakama zilipokea kesi 407, kati ya hizo kesi 385 zimeshasikilizwa. TAKUKURU ilifungua kesi 2,252 na kushinda kesi 1,013.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisheria na kisiasa walikosoa hali hiyo. Rais alionekana kudhoofisha uhuru wa mahakama kupitia teuzi. Mahakama za Tanzania zilionekana kushirikiana na dola kwenye kesi kubwa kadhaa. Baadhi ya kesi ambazo vyombo vya habari mbalimbali zilizitangaza ni kama vile kesi iliyofunguliwa na asasi za haki za binadamu dhidi ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ambayo Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara iliitupilia mbali. Nyingine ni pamoja na uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wa Januari 2019 wa kutupilia mbali ombi la watunga sheria kuzuia sheria inayopanua mazingira ambayo wanachama wa vyama vya upinzani wanaweza kusimamishwa au kufungwa, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya mpiga kura bila ruhusa ya serikali. Mwezi Septemba 2019 Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilitupilia mbali pingamizi la kiongozi wa upinzani Tundu Lissu dhidi ya kufukuzwa kwake ubunge wakati akiwa nje ya nchi anapatiwa matibabu kufuatia jaribio la kutaka kumuua. Tukio lingine lililotajwa katika mitandao ya kijamii ni lile ambalo mahakama ilionekana kumpendelea Rais kwa kumsimamisha bila ukomo Fatma Karume, Rais wa zamani wa Chama cha Wanasheria Tanganyika, kufanya shughuli za kisheria mwezi Septemba 2019. Alituhumiwa kuanzisha pingamizi kali na lisilo sahihi dhidi ya uteuzi wa Adelardus Lubango Kilangi kama Mwanasheria Mkuu akidai kwamba hana sifa na kwamba ni mwanachama kindakindaki wa CCM.



*Fatma Karume, Rais wa zamani wa TLS, ambaye alisimamishwa bila ukomo wa muda kufanya shughuli za kisheria Septemba 2019*

## 2.3 MIENENDO YA VYAMA VYA SIASA

Nchi ilipokuwa inaelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, mambo mengi yalitokea kwenye vyama vya siasa – CCM, chama tawala;  na vyama vya CUF na ACT-Wazalendo kwa upande wa upinzani. Mambo hayo yalionesha kuendelea kutawala na kuimarika kwa CCM na kujipanga, kuvunjika na kushuka kwa vyama vya upinzani. Katika harakati za kuibadilisha CCM, Rais aliunda kikosi kazi cha kuhakiki mali na madeni ya CCM. Baadhi ya watu hawakufurahi kwani taarifa ilionesha uozo mkubwa. Taarifa ilimfanya Rais Magufuli kuagiza kurudishwa kwenye chama mali zilizokuwa mikononi mwa watu binafsi. Katika harakati za kukibadilisha chama Dkt. Bashiru Ally, aliyekuwa mwenyekiti wa kikosi kazi hicho, aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama.

Dkt. Bashiru Ally hakuwahi kushika wadhifa wowote katika chama mbali ya kuwa mwanachama tu. Mazungumzo ya simu yalisikika mitandaoni yakisema kwamba Rais alikuwa amemleta mgeni kwenye chama. Sauti hizo zilikuwa za Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani, Bernard Membe, Makatibu Wakuu wa zamani wa Chama cha Mapinduzi Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba na mawaziri wa zamani January Makamba, William Ngeleja na Nape Nnauye. Wote walituhumiwa na Kamati Kuu kwa utovu wa nidhamu na kwa kukiuka maadili na katiba ya chama kwa kufanya kampeni za njama dhidi ya Rais. Kwa nyakati tofauti kila mmoja

aliomba msamaha kwa Rais, isipokuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani, Bernard Membe ambaye alikataa kuomba radhi. Chama kikamfukuza.

CCM ilinufaika na wahamiaji kutoka vyama vya upinzani. Mikakati mingi ilitumika kuwafanya wahame. Moja ya mikakati hiyo ilikuwa ni kuwateuwa watu wa upinzani kwenye nafasi za serikali. Profesa Kitila Mkumbo, mwanachama mwandamizi wa ACT-Wazelendo, aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Bi. Anna Mghwira ambaye aligombea urais mwaka 2015 kupitia ACT-Wazalendo aliteuliwa kuwa mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Ingawa awali Profesa Mkumbo na Bi. Mghwira waliendelea kuwa wanachama wa ACT-Wazalendo, hatimaye waliondoka ACT-Wazalendo na kujiunga na CCM. Ndugu Julius Mtatiro ambaye alikuwa mwenyekiti wa muda wa CUF alijikuta kwenye migogoro ya ndani ya chama na kuamua kuhamia CCM na baadaye kuteuliwa kuwa mkuu wa Wilaya ya Tunduru. Mwita Waitara ambaye alikuwa mbunge wa jimbo la Ukonga kupitia CHADEMA aliteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa baada ya kuhamia CCM. Dkt. Wilbroad Slaa ambaye ni Katibu Mkuu wa CHADEMA wa zamani aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Sweden. Njia nyingine ni wahamiaji kuhakikishiwa kwamba wakihamia CCM watagombea ubunge kwa tiketi ya CCM bila kupingwa na kuhakikishiwa ushindi. Kanuni na utaratibu mpya kama kuminya shughuli za vyama vya siasa kwa kuruhusu shughuli hizo kwenye majimbo husika ya wabunge pia ilifanya iwe vigumu sana kwa vyama vya upinzani kuungwa mkono na watu wa chini. Baadhi ya wanachama wa vyama vya upinzani (wakiwamo Ndugu Peter Lijualikali na Ndugu Joseph Mbilinyi) walishitakiwa na kupewa adhabu ya kifungo cha miezi mitano. Wengine wengi walitumia muda mwingi mahakamani kujibu tuhuma kadhaa dhidi yao. Ni wazi kwamba shughuli za kisiasa zingeweza kufanyika kwa usalama ndani ya CCM lakini si ndani ya upinzani. Ghafla kuhama kulikiimarisha chama tawala huku kukividhoofisha vyama vya upinzani.

Mchakato wa kutengeneza Muungano wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) uliviacha baadhi ya vyama hususan CUF na CHADEMA vikiwa na migogoro. Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt. Wilbrod Slaa, alijiuzulu wadhifa wake kwa sababu hakukubaliana na kupokelewa kwa Edward Lowassa kama mgombea urais wa UKAWA. Profesa Ibrahimu Lipumba pia alijiuzulu uenyekiti wa CUF kwa sababu hiyohiyo. Miezi kadhaa baada ya uchaguzi kumalizika, Profesa Lipumba aliiondoa barua yake ya kujiuzulu na kuanza kuchukua mamlaka ya juu ya vyombo vikuu vya chama na mali, zikiwamo fedha za chama. Maalim Seif Sharif Hamad,

Katibu Mkuu wa CUF, alipinga hatua hiyo. Hata hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa na Mahakama Kuu walisema Profesa Lipumba alikuwa na haki ya kuendelea. Maalimu Seif Sharif Hamad aliamua kuondoka CUF mara moja na kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo akiambatana na maelfu ya wafuasi wake. Kuhama kwa Maalim Seif kuliidhoofisha sana CUF huko Zanzibar ambayo ilikuwa ngome yake na hata uimara wake Tanzania Bara.

Matukio hayo yalipelekea vyama kujipanga upya, ambapo ACT-Wazalendo ilikuwa na wagombea wapya wa urais wa Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao walikuwa wanachama wa zamani wa CCM na CUF. CHADEMA ilimsimamisha Tundu Lissu kama mgombea wake wa urais wa Jamhuri ya Muungano. Tundu Lissu alirejea kutoka Ubelgiji ambako alikuwa anapatiwa matibabu baada ya kupata majeraha ya risasi wakati anahudhuria vikao vya Bunge mjini Dodoma. Hadi leo hii waliompiga risasi hawafahamiki. Ingawa ACT-Wazalendo ilimpendekeza Ndugu Bernard Membe kama mgombea siku zilivyozidi kusonga na kwa sababu mgombea alifanya mikutano ya kampeni michache mno waliamua kumuunga mkono Ndugu Tundu Lissu. Cha kushangaza dakika za mwisho Ndugu Membe alijitokeza mbele ya waandishi wa habari akidai kwamba alikuwa na majukumu ya kimataifa na alikumbwa ukata wa fedha na hivyo kushindwa kufanya kampeni za uchaguzi kama ilivyotarajiwa. Pamoja na changamoto hiyo aliwaambia Watanzania watarajie ushindi wake wa dakika ya tisini.



*Maalim Seif Sharif Hamad na Freeman Mbowe wakimsikiliza Tundu Lissu kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye jimbo la Moshi Mjini.*

CCM iliendelea na faida yake ya kihistoria ya kuwa na rasilimali na uungwaji mkono. Kilitumia faida ya watangulizi wake, yaani TANU na ASP ambavyo vilipambana na ukoloni, na kujipambanua kama chama cha ukombozi na mapinduzi. Uhusiano wake na waasisi wa taifa, Mwalimu J. K. Nyerere na Sheikh Abeid A. Karume, unaipa CCM hadhi ya kipekee. CCM ina mtandao wa matawi na ofisi hadi ngazi ya nyumba kumi, mtandao ambao hakuna chama kingine chochote ulionacho. Idadi kubwa ya wanachama wake na mali nyingi ilikihakikishia kuendelea kupata rasimali muhimu, hususan watu na fedha. Watu wengi wanavutiwa kuwa wanachama wa CCM kwa sababu uanachama huo unatoa fursa za ajira na nafasi za kisiasa. Na kitendo cha Rais kuwa mwenyekiti wa chama kinawahakikishia siyo tu fahari na mbwembwe katika shughuli za CCM bali pia ustahimilivu wa kitaasisi. Hali kadhalika, kinatoa fursa za kutumia vyombo vya dola kwenye mkakati wa kuendelea kisiasa na kuendelea kutawala.

Kwa upande mwingine, vyama vya upinzani viliendelea kuchechemea na kupata mafanikio kidogo, pamoja na kukabiliwa na changamoto nyingi. CHADEMA kiliongeza nguvu yake kwa kushinda mabaraza ya madiwani ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kwa ujumla, ilishinda viti 72 vya ubunge kati ya viti 378, na takribani moja ya tano ya viti vyote vya udiwani, kama Jedwali Namba 2.1 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 2.1: Mgawanyo wa Viti vya Ubunge na Udiwani kwa Mwaka 2015**

| Na. | Chama cha Siasa | Wabunge Wakuchaguliwa | Wabunge Wakuteuliwa | Jumla | Madiwani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CCM | 195 | 66 | 261 | 2,875 |
| 2 | CHADEMA | 34 | 37 | 72 | 801 |
| 3 | CUF | 32 | 10 | 42 | 212 |
| 4 | ACT-Wazalendo | 1 | 0 | 1 | 32 |
| 5 | NCCR-Mageuzi | 1 | 0 | 1 | 23 |
| 6 | NLD | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 7 | TLP | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **TOTAL** | **265** | **113** | **378** | **3,946** |

*Chanzo: Ripoti ya TEMCO, 2016 & NEC, 2016.*



*Dkt. Vicent Mashinji*



*Dkt. Wilbroad Slaa*



*Julius Mtatiro*



*Prof. Kitila Mkumbo*



*Edward Lowasa*



*Fredrick Sumaye*

*Baadhi ya watu maarufu waliohamia CCM kati ya mwaka 2015 na 2019*

Hata hivyo, kama vyama vya upinzani vilidhani kwamba vilikuwa vinaelekea kuongeza umaarufu, matukio ya mwaka 2015 hadi mwaka 2020 yaliifanya hali hiyo kuwa ni matamanio tu.

Tanzania ilifanya uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ulisimamiwa na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wagombea wengi wa vyama vya upinzani walishindwa kupata fomu za uteuzi. Waliopata fomu walishindwa kukusanya fomu zilizojazwa vizuri kwa wakati na waliojaza waliondolewa, wakiwamo asilimia 94 ya wagombea wa CHADEMA (Ripoti ya CRC, 2020). Matokeo yake ni kwamba vyama vya upinzani vilisusia uchaguzi na CCM kushinda viti vyote vya mijini na asilimia 99 ya viti vya vijijini.

## 2.4 MKWAMO WA KISIASA ZANZIBAR

Mara nyingi mijadala yote ya uchaguzi juu ya Zanzibar inahusu uhuru na usawa. Matokeo ya chaguzi zote zilizofanyika Zanzibar chini ya mfumo wa vyama vingi yamehojiwa na kukataliwa na chama cha CUF kuwa ni ya uongo. Tukio kubwa zaidi lilitokea wakati wa uchaguzi wa mwaka 2000 ambao TEMCO ilisema uliharibika. Katika harakati za kupinga matokeo hayo watu 22 waliuawa Pemba mwezi Januari

2001. Watu wengine wengi walikimbilia Kenya kama wakimbizi. Rais wa zamani anakiri kwamba "tukio hili litakuwa doa wakati wote kwa urais wangu" (Mkapa, 2020: 170). Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilisaidia kupoza joto la kisiasa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Kwa bahati mbaya mgogoro na kususiwa kwa uchaguzi wa mwaka 2015 kuliharibu taswira za chaguzi za Zanzibar. Kwa hiyo, maswali ni: Je, uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ungekuwa tofauti? Je, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ingeandaa uchaguzi ambao matokeo yake yangekubaliwa na wote? Maswali haya yalihitaji majibu.

Mwisho wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, CUF ilikataa kushiriki katika uchaguzi wa marudio na kuwa sehemu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hivyo, uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulitoa fursa kwa vyama vya upinzani kujipatia kile walichodai kwamba waliibiwa mwaka 2015. Lakini mazingira yalikuwa yamebadilika. CUF ilikuwa na mgogoro. Viongozi wake wa juu na wanachama wake wengi walikuwa wamehamia ACT-Wazalendo. Je, hali hii ingekuwa na athari gani kwa upinzani Zanzibar?

## 2.5 MUKTADHA WA KIKANDA NA KIMATAIFA

Kwa desturi, chaguzi za Tanzania zinavutia jumuiya ya kimataifa. Mwishoni mwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 mataifa makubwa yalitishia kuiwekea Tanzania vikwazo, wakidai kwamba hawakuridhishwa na namna uchaguzi ulivyofanyika. Kwa nyakati tofauti tarehe 15 Oktoba 2020 wawakilishi wa kimataifa, Balozi wa Marekani, Dkt. Donald Wright; Balozi wa Kenya, Dan Kazungu; Balozi wa Msumbiji, Monica Mussa; Balozi wa Umoja wa Ulaya, Manfredo Fenti; na mabalozi wengine nane kutoka nchi za Umoja wa Ulaya (Anders Sjoberg wa Sweden, Adrian Fitzgerald wa Ireland, Regme Hess wa Ujerumani, Jorean Verheul wa Uholanzi, Peter Van wa Ubelgiji, Krytt Buzalde wa Poland, Roberto Nengoni wa Italia na Mette Dissing wa Denmark) walimtembelea Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Bashiru Ally, kwenye ofisi ndogo za Chama cha Mapinduzi zilizopo Lumumba jijini Dar es Salaam. Balozi wa Marekani alifanya mazungumzo pia na mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Ndugu James Mbatia. Siku ya tarehe 1 Oktoba 2020 serikali ya Marekani ilitoa wito kwa serikali ya Tanzania kuunga mkono mchakato wa kidemokrasia, huku ikitahadharisha kwamba isingesita kuchukua hatua dhidi ya watu watakaochezea uchaguzi. Lakini msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China alisema kuwa ana imani kuwa serikali ya Tanzania inaweza kuendesha uchaguzi kwa amani. China iliziomba nchi zingine kutoingilia masuala ya ndani

ya nchi zingine.

Tarehe 2 Septemba 2020 ofisi 10 za ubalozi zilitoa tamko zikisisitiza uwazi na usawa kwa wanawake, vijana na wazee katika mchakato wa uchaguzi. Sehemu ya tamko hilo ilisomeka hivi: "Kama wawakilishi wa nchi zetu tunatambua masilahi yetu ya muda mrefu katika kusaidia maendeleo na demokrasia nchini Tanzania yaliyojengwa kwa uhusiano wetu wa kihistoria na wa karibu" (*The Guardian*, Alhamisi, 3 Septemba 2020).

Hisia zingine kuhusu mwenendo wa uchaguzi zilitolewa na Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa. Katika tamko lake la tarehe 16 Septemba 2020 serikali ya Tanzania, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilipinga taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna wa Haki za Binadamu kwamba inadhoofisha demokrasia na uhuru wa kujieleza nchini. Serikali ilisisitiza kwamba taarifa hiyo haikuakisi ukweli uliopo, ikidai kwamba wagombea urais wote 17 walikuwa wanafanya kampeni bila vikwazo.

Tarehe 16 Oktoba 2020 mwakilishi mkazi wa UNDP alivisihi vyama vyote vya siasa kuwa na staha, uvumilivu na ukomavu wa kisiasa kabla ya siku ya uchaguzi. Alizungumzia nafasi ya Umoja wa Mataifa huku akisisitiza kwamba walikuwa hawaungi mkono chama chochote au mgombea yeyote kwenye mchakato wa uchaguzi nchini Tanzania na kwenye nchi zingine. Alisema kwamba tamko lililokuwa linasambaa kwenye mitandao ya kijamii kwamba UNDP ilikuwa inaunga mkono wagombea fulani halikuwa la kweli. Vivyo hivyo, tarehe 26 Oktoba 2020 msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliwataka wadau wate wa taifa kuhakikisha kwamba uchaguzi unaendeshwa kwa kushirikisha watu wote na amani, pamoja na kuhakikisha kwamba vyama vya siasa na wagombea wao, hususan wanawake, wanashiriki katika uchaguzi kwa kiasi kikubwa. Aliwasihi viongozi wote wa vyama vya siasa na wafuasi wao kushiriki katika zoezi la uchaguzi kwa amani.

Kwenye tamko la mwezi Machi 2020 kipindi ambapo UVIKO-19 ulipoingia Tanzania serikali ilikosoa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani kuhusu ugonjwa huo, pamoja na kuacha kutoa takwimu kuhusu maambukizi ya ugonjwa na tarehe 5 Juni 2020 kutangaza kwamba Tanzania haikuwa na UVIKO-19. Ilipinga tamko la tarehe 14 Septemba 2020 lililotolewa na Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa kwamba mazingira ya haki za binadamu yaliendelea kuwa mabaya kadiri uchaguzi mkuu ulivyokaribia na kusema kwamba ni ajenda ya

kibaguzi ya nchi za magharibi (Amnesty International, 2020). Sambamba na hilo ili kupunguza athari za nje kwenye masuala ya ndani ya nchi, hususan uchaguzi, serikali iligharimia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Hali hiyo iliutofautisha uchaguzi huo na chaguzi zilizopita ambazo kwa asilimia kubwa zilitegemea fedha au rasilimali kutoka mashirika ya kimataifa na nchi za magharibi.

Itakumbukwa kwamba mwaka 2018 Tanzania ilimwamrisha Balozi wa Umoja wa Ulaya, Roeland De Geer, kuondoka nchini mara moja kwa sababu ambazo hazikuwekwa wazi. Mwaka 2017 Tanzania ilimfukuza Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Awa Dabo, ambaye ni Mgambia, kwa "kutokuwa na mahusiano mazuri na wafanyakazi". Katika tamko lake Wizara ya Mambo ya Nje ya Tanzania iliitaka UNDP kuwakumbusha wafanyakazi wake kwamba kipaumbele chao ni kufanya kazi kwa ukaribu na serikali ya Tanzania ili kuisaidia kufikia vipaumbele vyake vya maendeleo. Kutumia fedha zake zenyewe na kukataa jitihada zozote za mataifa ya kigeni kuingilia masuala yake ya ndani kuliiwezesha Tanzania kujiamini zaidi katika misimamo yake.

## 2.6 HITIMISHO

Sura hii imejadili muktadha wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Imeangalia matukio kadhaa ambayo yangeweza kuathiri uchaguzi huo. REDET inahitimisha kwamba wananchi walifikiri kwamba CCM ingepata ushindi wa kishindo kwa sababu muktadha ulikuwa unakipendelea chama hicho. Kuna watu waliodhani kwamba utendaji wa serikali ya awamu ya tano na kuminywa kwa nafasi ya vyama vya upinzani kufanya siasa kuliipa CCM faida ya kushinda uchaguzi. Hali kadhalika, migogoro ndani ya vyama vikuu vya upinzani kama CUF na CHADEMA iliyochangiwa na kuhama kwa wanasiasa wengi maarufu na kwenda CCM kulivimaliza vyama hivyo na kufifisha uwezekano wa wao kushinda uchaguzi.

# SURA YA TATU

# MFUMO WA KISHERIA NA KITAASISI KWA AJILI YA KUENDESHA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

## 3.1 UTANGULIZI

Muktadha wa kisheria na kitaasisi wa uchaguzi ni muhimu katika kuamua matokeo, hali na mtazamo kuhusu uchaguzi. Sura hii inatathmini mfumo wa kisheria na kitaasisi uliotumiwa kuendesha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili kubaini athari zake katika kuendesha uchaguzi huo. Imegawanyika katika sehemu kuu nne, pamoja na utangulizi huu. Sehemu ya Pili inatazama mifumo ya kisheria na kitaasisi ya uchaguzi. Sehemu ya Tatu inajikita katika masuala ya kusimamia uchaguzi. Sehemu ya Nne inatoa hitimisho.

## 3.2 MFUMO YA KISHERIA KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Mfumo wa kisheria kwa ajili ya uchaguzi mkuu kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatoka katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (Sura ya 343 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2015) inaweka sheria inayosimamia uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano. Uchaguzi wa Madiwani unaendeshwa kwa kutumia Sheria ya Serikali za Mitaa (Sura ya 292 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2015). Sheria zingine zinazosimamia uchaguzi ni pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na Sheria Namba 6 ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 ambayo inahusu gharama za michakato ya uchaguzi ili kudhibiti matumizi ya fedha na vitendo vinavyokatazwa. Hali kadhalika, sheria inaeleza namna ya kutoa, kusimamia na uwajibikaji kuhusu matumizi ya fedha za uchaguzi. Uchaguzi wa Zanzibar unaendeshwa kwa kutumia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya mwaka 1984 na marekebisho yake ya mwaka 2018.

Sheria, taratibu na kanuni kadhaa mpya zilitungwa. Baadhi ya watu walisema kwamba matukio haya yanaathiri shughuli za kisiasa na kuminya uwanja wa demokrasia. Matukio hayo ni utungwaji wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 (ambapo Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki iliviona vipengele vyake vya uchochezi, udhalilishaji na habari za kutunga vinaminya uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza); Sheria ya Takwimu ya

mwaka 2018 (ambayo marekebisho yake yanaondoa kosa la kukusanya na kutoa takwimu zinazokinzana na zile za Ofisi ya Takwimu ya Taifa); Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 (ambayo utekelezaji wake umeibua hisia kuhusu uvunjaji wa haki ya kujieleza); Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali ya mwaka 2019 ambayo inapiga marufuku asasi za kidini kushiriki katika shughuli za kisiasa kama vile kutazama uchaguzi); Sheria ya Vyama vya Siasa (kama ilivyofanyiwa marekebisho) ya mwaka 2019 (inayompa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama vya Siasa na kuanzisha hatua ya kuimarisha demokrasia ya ndani ya vyama, ikiwamo kuwapa nguvu wanawake.

Katika kipindi cha wiki mbili za mwisho za kampeni za uchaguzi Wizara ya Mambo ya Ndani ilitoa tamko kuwaonya viongozi wa dini kutokumpendelea mgombea au chama chochote katika uchaguzi wa tarehe 28 Oktoba 2020. Sehemu ya tamko lililotolewa na wizara inasomeka hivi: "Baadhi ya viongozi wa dini wanaenda mbali na kusema kwamba wafuasi wao watampigia kura mgombea fulani. Kitendo hicho kinapingana na kifungu cha 17 cha Sheria ya Asasi, Sura ya 337, Namba 3 ya mwaka 2019 (*The Citizen*, Alhamisi, 22 Oktoba 2020). Viongozi wa dini walionekana kwenye kampeni za uchaguzi za Rais aliyekuwa anatetea kiti chake, John Magufuli, na mgombea wa upinzani, Tundu Lissu, kipindi cha kampeni za uchaguzi wa mwaka 2020 kama inavyooneshwa kwa kina kwenye sura inayohusiana na kampani za uchaguzi.

### 3.2.1 Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari

Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 Sura ya 229 ni moja ya sheria muhimu zinazohusu namna ya kuendesha uchaguzi kwenye siasa za ushindani kiasi kwamba sheria hiyo ilitajwa kwenye maadili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kifungu cha 2.1 (f) cha maadili hayo kinaelezea wajibu wa vyama vya siasa na wagombea kutumia vyombo vya habari kunadi sera zao kwa kuzingatia Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, Sura ya 229. Kutungwa kwa sheria hiyo kulipingwa vikali, hususan na asasi za kiraia, kwa sababu sheria hiyo inaminya utendaji wa vyombo vya habari. Mwaka 2017 Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) zilishinda kesi iliyofunguliwa katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki kwa sababu serikali ilikuwa imevunja kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuminya uhuru wa kujieleza, utawala bora, demokrasia na

utawala wa sheria, pamoja na kuvunja haki za binadamu.[2] Tarehe 18 Machi 2019 Divisheni ya Kwanza ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki iliwapa ushindi. Tarehe 28 Machi 2020 Kitengo cha Rufaa cha mahakama hiyo kilitoa hukumu dhidi ya rufaa ya serikali ya Tanzania na kuitaka serikali hiyo ifanye marekebisho yaliyotolewa kwa kurekebisha vifungu vilivyopigiwa kelele.[3] Divisheni ya Kwanza ya mahakama hiyo ilisema kuwa amri iliyotolewa tarehe 10 Agosti 2016 na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya kulifungia gazeti la *Mseto* kwamba lilikuwa limevunja vifungu vya 6 na 7 vya Mkataba ulionzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sababu vifungu hivyo havijafutwa toka uamuzi wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki itolewe, sheria bado inampa Waziri mamlaka makubwa ya kufuatilia vyombo vya habari. Sheria hiyo haisemi chochote kuhusu nini maana ya kauli ya kichochezi au kutishia usalama wa taifa na inajumuisha baadhi vya vifungu hatari vya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 (MSA, 2016:7).

### 3.2.2 Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni)

Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni zilizopitishwa na Bunge mwaka 2018 zinaipa mamlaka makubwa sana Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutoa leseni na kufuatilia maudhui ya mtandaoni kama blogi na tovuti. Mwaka 2018 LHRC, MCT na THRDC zilifungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara kupinga Kanuni Zinazohusiana na Maudhui ya Mtandaoni. Mwezi Januari 2019 Mahakama Kuu ilitupilia mbali shauri hilo na kuhitimisha kwamba waleta shauri walishindwa kuthibitisha pasi na shaka yeyote kwamba kanuni hizo zitaathiri haki zao na mwasiliano ya kimtandao (*Daily News*, 10 Januari 2019).

### 3.2.3 Sheria ya Takwimu

Kutungwa kwa Sheria ya Takwimu mwaka 2015 kulivuta hisia za watu wengi kwani ilikuwa ni kosa kwa wamiliki wa vyombo vya habari kutoa takwimu ambazo hazikupitishwa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS). Kifungu cha 37(5) cha sheria hiyo kimefanya kuwa kosa kutoa takwimu ambazo zinaweza kupelekea kuharibu ukweli bila kufafanua ni kitu gani kinaweza kuharibu ukweli. Kukamatwa kwa kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, kwa madai ya kuvunja Sheria ya

2 Mahakama ilinukuu vifungu vingi vya MSA na kusema kwamba inavunja vifungu vya 6(d), 7(2) na 8(1) vya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzanai.

3 Mahakama ya Haki ya Afrika Msharikí, Baraza la Habari Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Umoja wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania v Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Divisheni ya Kwanza ya 28 Machi 2019.

Takwimu kufuatia matamko yake juu ya kukua kwa uchumi wa nchi kuliuvutia umma. Kuondolewa kwa kosa la jinai kwa kuchapisha takwimu binafsi na kifungu kuhusu ufafanuzi juu ya tofauti kati ya takwimu rasmi na zisizo rasmi ni baadhi ya maboresho yaliyofanywa mwezi Juni 2019 kwenye mabadiliko ya Sheria ya Takwimu.

### 3.2.4 Kanuni za Maadili ya Uchaguzi

Kabla marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ya mwaka 2010 kufanyika, maadili ya uchaguzi hayakuwabana walioyasaini. Maadili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yalipewa nguvu za kisheria chini ya kifungu cha 124 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Vyama vya siasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi walisaini maadili hayo, lakini ilifafanuliwa kwamba chama chochote ambacho hakikusaini maadili hayo kisingeshiriki kampeni za uchaguzi. Kwa kusaini maadili hayo, vyama vya siasa vilijipa jukumu la kuhakikisha kwamba maadili ya uchaguzi yanasambazwa na kuzingatiwa na wagombea na wanachama wao. Maadili ya uchaguzi yalianza kufanya kazi kuanzia siku ambayo wagombea walipoteuliwa hadi siku ambayo matokeo ya uchaguzi yalipotangazwa.

Ili kutekeleza maadili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020, Tume iliunda kamati za maadili ya uchaguzi zifuatazo zilizojumuisha watu kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi, vyama vya siasa na serikali:

Tume ya Rufaa,

- Tume ya Kitaifa,
- Tume za Ngazi ya Majimbo, na
- Tume za Ngazi ya Kata.

Mchakato wa utiaji saini wa maadili tarehe 27 Mei 2020 na wahusika (yaani vyama vya siasa, wagombea, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi) ulitanguliwa na kipindi cha siku 14 ambapo vyama vya siasa vilivyosajiliwa vilipewa fursa ya kusoma rasimu ya maadili ya uchaguzi. Tume ilitoa rasimu hiyo kwa vyama vya siasa tarehe 24 Aprili 2020. Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, vyama tisa kati ya vyama 26 vilitoa maoni yao ndani ya siku kumi lakini vyama vitatu (NCCR-Mageuzi, CHADEMA na ACT-Wazalendo) vilishindwa kufanya hivyo.4 Kifungu cha 2.2 (h) cha maadili hayo

4 Vyama tisa vilivyotajwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi ni: Democratic Party (DP), ADA-TADEA, Civic United Front (CUF), Chama cha Jamii (CCK), Alliance for Tanzania Farmers Party (AAFP), United People's Democratic Party (UPDP), Union for

kilisababisha malumbano makali wakati wa kupitia rasimu. Kifungu hiki kiliminya ukusoaji miongoni mwa vyama na wagombea kuhusu sera, programu na shughuli zilizofanywa. Kilikataza ukosoaji wa vyama vingine au wagombea bila kuwa na ushahidi. Ujumbe wa CHADEMA ukiongozwa na Katibu Mkuu wake Ndugu John Mnyika ulikipinga kifungu hicho, wakisema kwamba kingevinyima vyama vya upinzani fursa ya kuzungumzia utendaji wa serikali ya CCM. Baada ya majadiliano ya muda mrefu malumbano hayo yalitatuliwa kwa kupiga kura. Wajumbe 16 walikiunga mkono kifungu hicho, lakini wajumbe wawili walikipinga (*Habari Leo*, 25 Mei 2020). Maelezo ya kina juu ya athari na utekelezaji wa maadili ya uchaguzi yanatolewa kwenye sura inayohusu kampeni za uchaguzi.

Moja ya matukio kuhusu utekelezaji wa maadili ya uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kinahusu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Tume kumfungia kufanya kampeni kwa siku saba (tarehe 3 hadi 9 Oktoba 2020) mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu. Kamati ya Maadili ilitoa adhabu hiyo kufuatia Tundu Lissu kuvunja kifungu cha 2.1 (a), (b), (d) na (n) cha maadili hayo kwa kutumia lugha ya kichochezi na kutoa madai yasiyokuwa na ushahidi (*Daily News*, 3 Oktoba 2020). Uamuzi huo ulichukuliwa kufuatia Ndugu Lissu kushindwa kujibu madai yaliyotolewa na CCM na NRA ambao walidai kwamba mgombea urais huyo alidai kwamba Rais Magufuli, mgombea urais wa CCM, alifanya kikao na watendaji wa uchaguzi kutoka nchi nzima ili kuhujumu uchaguzi wakati wa mikutano yake ya kampeni mkoani Mara (*The EastAfrican*, 3–9 Oktoba 2020). CHADEMA nayo ilipeleka malalamiko kwenye Kamati ya Maadili ya Tume dhidi ya mgombea urais wa CCM, John Magufuli, kwa kufanya kampeni wakati wa kuweka jiwe la msingi la kituo cha mabasi cha Mbezi Louis, Dar es Salaam, tarehe 10 Oktoba 2020. Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CHADEMA, Ndugu John Mnyika, lile halikuwa tukio la CCM, badala yake lilikuwa tukio la kiserikali ambalo lilitumia fedha za walipa kodi. "Lakini Dkt. Magufuli alijipigia kampeni mwenyewe na wagombea wengine wa chama chake na hivyo kuvunja kanuni za maadili ya uchaguzi, pamoja na kufanya kampeni kinyume na ratiba iliyotolewa alitumia rasilimali za serikali. Kwa hiyo, tulipeleka malalamiko kwenye Kamati ya Maadili ya Tume siku ya Ijumaa na kuipa Tume jaribio lingine" (*The Citizen on Sunday*, 11 Oktoba 2020).

### 3.2.5 Sheria ya Vyama vya Siasa

Utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa unasimamiwa na Ofisi ya Msajili wa

Multiparty Democracy (UMD), Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Umma (CHAUMMA).

Vyama vya Siasa ambayo ni taasisi huru ya serikali ambayo lengo lake kuu ni kutaasisisha, kukuza na kuimarisha siasa za kidemokrasia. Ofisi hiyo pia inatekeleza na kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010. Ofisi inaendeshwa na Msajili wa Vyama vya Siasa akisaidiwa na Naibu Msajili ambaye kituo chake cha kazi ni Zanzibar, pamoja na wasajili wasaidizi.

Ni muhimu kueleza kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 1 ya mwaka 2019 (marekebisho) iliyoleta mabadiliko na masharti mengi kuhusu utoaji wa elimu ya uraia, kutengeneza ushirikiano, demokrasia ndani ya vyama, uwajibikaji wa kifedha, pamoja na mambo mengine, haikuungwa mkono na vyama vyote vya siasa. Vyama vitatu vya siasa vya upinzani (CHADEMA, ACT-Wazalendo na CHAUMMA), vikiwakilishwa na watu watano, vilifungua kesi Namba 2 ya mwaka 2019 katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki tarehe 27 Mei 2019 bila mafanikio. Katika kesi hiyo (*Freeman A. Mbowe & others vs The Attorney General of the United Republic of Tanzania*) waliofungua kesi walitaka Divisheni ya Kwanza ya mahakama hiyo kumzuia mshitakiwa hasitumie vifungu vya Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 1 ya mwaka 2019.

Walalamikaji walidai kwamba matumizi ya sheria hiyo yangepunguza haki ya Watanzania kupata habari kupitia elimu ya uraia na kukandamiza haki yao ya kutoa elimu ya uraia bila kupata kibali cha Msajili wa Vyama vya Siasa. Walieleza kwamba utoaji wa elimu ya uraia bila kutoa taarifa ungewafanya kukamatwa, kuwekwa kizuizini, kushitakiwa, kutozwa faini, kufungwa au kufukuzwa uanachama. Vitu vyote hivi vingesababisha hasara kubwa. Walalamikaji hao walipinga nguvu aliyopewa Msajili kuamua nani atoe elimu ya uraia na maudhui ya elimu hiyo. Walidhani kwamba kama wangenyimwa haki ya kutoa elimu ya uraia wananchi wasingejua umuhimu wa kushiriki katika zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na hatimaye kunyimwa haki yao ya kupiga kura, kitu ambacho ni hasara kubwa.

Katika majibu yake mshitakiwa (Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) alisema: "Sharti la kumfahamisha Msajili kuhusu nia ya kutoa elimu ya uraia linazihusu asasi zisizo za kiserikali na taasisi zinazokusudia kutoa elimu ya uraia kwa vyama vya siasa na si wananchi kama inavyodaiwa. Sharti hilo linakusudia kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, ulinzi, usalama na utulivu wa nchi unakuwapo ... sheria iliyopitishwa, pamoja na mambo mengine, inadhibiti vitendo vya vyama vya siasa kwa lengo la kuimarisha utaasisi, demokrasia ya ndani ya

vyama na uwajibikaji wa kisiasa na kifedha, ambavyo ni vitu muhimu kwenye nchi yeyote ya kidemokrasia."[5] Mahakama ilitupilia mbali ombi hilo katika hukumu yake ya tarehe 17 Juni 2020 iliyotolewa kwa njia ya video kipindi cha UVIKO-19.

Pamoja na kuleta vifungu kuhusu udhibiti wa utoaji elimu ya uraia na mafunzo ya kujenga uwezo na kuipa mamlaka Ofisi ya Msajili kuomba taarifa yeyote kutoka katika chama cha siasa, kiongozi au mwanachama, Sheria ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa marekebisho inatambua kuundwa kwa ushirika wa vyama vya siasa. Utaratibu wa kuunda ushirika huo ndiyo uliosababisha mgogoro kati ya Ofisi ya Msajili na vyama vya siasa vya upinzani. Utaratibu huo unawataka wanachama wa vyama husika kuunga mkono makubaliano ya kuunda ushirika katika mkutano mkuu wa chama wa kitaifa na kupeleka nakala ya makubaliano yaliyosainiwa kwa Msajili miezi mitatu kabla ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume.[6] Kipindi cha kampeni za uchaguzi Ofisi ya Msajili ilivipatia CHADEMA na ACT-Wazalendo barua za tarehe 18 Septemba 2020 ikivitaka vieleze nia yao ya kuingia makubaliano ya kufanya ushirikiano usiowabana (*The Citizen*, Alhamisi, 24 Septemba 2020). Naibu Msajili pia alieleza kwamba Ofisi ya Msajili iliiomba TLP kutoa maelezo kutokana na maelezo yake kwamba ingemuunga mkono mgombea urais wa CCM, John Magufuli, katika uchaguzi wa Oktoba 2020. Katibu Mkuu wa TLP Richard Lymo alikiri kupokea na kujibu barua hiyo ya Msajili akisema kwamba uamuzi wa kumuunga mkono mngombea urais wa CCM ulifikiwa tarehe 9 Mei 2020 bila ridhaa ya CCM wakisema kuwa hawakuwa wanaunga mkono CCM, bali utendaji mzuri wa Dkt. Magufuli (*The Citizen*, Alhamisi, 24 Septemba 2020).

### 3.2.6 Sheria ya Gharama za Uchaguzi

Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 ambayo inafanya kazi kwenye uchaguzi wa Muungano ni sheria ambayo inatekelezwa na Ofisi ya Msajili na Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji kati ya taasisi hizo mbili zinairuhusu Ofisi ya Msajili kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo na kufanya uchunguzi kuhusu uvunjaji wa sheria husika. Ofisi ya Msajili ina mamlaka ya kuomba taarifa kutoka chama cha siasa au mgombea kuhusu utekelezaji wake wakati TAKUKURU inajikita kwenye kuzuia vitendo hivyo. Kuhusu kudhibiti matumizi ya fedha nyingi kwenye uchaguzi kwa kuweka ukomo wa fedha inayoweza kutumika na kulazimisha kutolewa, Sheria ya

5 Kesi Namba 2 ya mwaka 2019 (iliyotokana na Kumbukumbu Namba 3 ya mwaka 2019) Freeman A. Mbowe & Wenzake v Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

6 Ibara ya 11A ya Sheria ya Vyama vya Siasa (Marekebisho) Namba 1 ya mwaka 2019.

Gharama za Uchaguzi inazuia watu wa nje ya nchi kugharamia uchaguzi, inaonesha mambo yanayokatazwa wakati wa uchaguzi, inakitakaza chama cha siasa kutunza kumbukumbu za matumizi na inamlinda mtoa taarifa. Kuelekea uchaguzi mkuu wa tarehe 28 Oktoba, Ofisi ya Msajili haikutoa adhabu yeyote kati ya adhabu zifuatazo ambazo zipo katika Sheria ya Gharama za Uchaguzi:

- Kuweka pingamizi kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi linalomuomba akiondoe katika uchaguzi chama cha siasa na/au mgombea aliyeshindwa kuweka wazi gharama zake za uchaguzi; na
- Kutoza faini au kutoa kifungo kwa kuvunja katiba, mathalani kushindwa kupeleka taarifa ya gharama za uchaguzi zilizotumika, kufanya kitu kilichokatazwa, kutumia zaidi ya kiwango cha juu cha fedha kinachoruhusiwa na kutoheshimu masharti ya kutotumia fedha za kutoka nje ya nchi.

Aina mbili za changamoto zinaikabili Ofisi ya Msajili katika kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Changamoto hizo zinahusu uwezo wa Ofisi ya Msajili na zingine zinahusu kundi lengwa, yaani vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura. Katika moja ya mawasilisho yake, Ofisi ya Msajili ilitaja changamoto zifuatazo inayokumbana nazo katika kutekeleza sheria hiyo[7]:

1. Ni vigumu kutekeleza vifungu kuhusu matumizi ya juu ya fedha;
2. Ufahamu wa sheria bado ni mdogo, hususan miongoni mwa wanachama wa vyama vya siasa na wapiga kura;
3. Mambo mengi yanayokatazwa yamejificha na yanafanywa kwa siri;
4. Mafunzo hafifu ya kujenga uwezo yanayotolewa na vyama vya siasa kwa sababu vyama vya siasa vinatumia rasilimali nyingi zaidi kwenye masuala ya ushindani;
5. Hatua zisizojitosheleza za kinidhamu ndani ya vyama, yaani vyama vichache vina kanuni za maadili; na
6. Kushuka kwa maadili katika jamii na kukosekana kwa uaminifu binafsi.

Maelezo ya kina kuhusu matukio na vitu ambavyo havikufanyika vinavyohusiana na utekelezaji wa sheria hiyo wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2020 yanatolewa kwenye Sura ya Tano (mwenendo wa kampeni za uchaguzi).

7 Sisty L. Nyahoza, Msajili wa Vyama vya Siasa Msaidizi, Kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa 2020 Unakuwa Huru na wa Haki: Wajibu wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, katika mafunzo ya watazamaji wa muda mrefu wa REDET, 26 Septemba 2020.

## 3.3 USIMAMIAJI WA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

### 3.3.1 Uteuzi na Utoaji Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi

Wakati REDET inapeleka watazamaji wake, Tume ilikuwa tayari imeshateua baadhi ya watendaji wake. Waliokuwa tayari wamekwishapatikana walikuwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa Manispaa (ROs) na Wasimamizi Wasaidizi (AROs). Kuna aina mbili ya wasimamizi wasaidizi: waliowasaidia wasimamizi wa uchaguzi wa manispaa katika ngazi ya jimbo na wale waliofanya kazi kama wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi ya kata. Watendaji wa uchaguzi walipatikana kutoka katika jamii. Hatimaye, Tume iliteua waratibu wa uchaguzi 28, wasimamzi wa uchaguzi 194, wasimamizi wasaidizi 742 katika ngazi ya jimbo na wasimamizi wasaidizi 7,912 katika ngazi ya kata.[8]

Picha ya jumla kutoka kwa watazamaji wa muda mrefu wa REDET ni kwamba mchakato wa uteuzi ulikuwa wa wazi. Kwa mfano, Songea Mjini, tangazo la kutafuta watendaji (Kumb.Na.SO/MC/E.20/1/111/42) la tarehe 21 Septemba 2020 liliwekwa katika ofisi zote za Watendaji wa Kata na katika ofisi ya Halmashauri ya Wilaya kuanzia tarehe 21 hadi tarehe 27 Septemba 2020, likiwataka watu wenye sifa kutoka jimboni humo kupeleka maombi (Ripoti ya LTO, Ruvuma, 2020). Watu walioomba walipaswa kuwa na sifa zifuatazo: (i) raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18, (ii) asifungamane na upande wowote, (iii) ikiwezekana awe mkazi wa kata husika, (iv) awe walau na elimu ya kidato cha nne na (v) awe mwaminifu. Watu waliopenda walipaswa kupeleka taarifa zao kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa. Waliofanikiwa walipaswa kufanya kazi kama Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi wa Vituo Wasaidizi na Makarani Waongozaji.

Uombaji ulikuwa wa wazi na hakuna malalamiko yaliyotolewa kuhusiana hatua hii ya mchakato wa uteuzi. Hata hivyo, huko Kigoma Mjini baadhi ya waombaji hawakuridhishwa na namna usaili ulivyoondeshwa. Majina ya waombaji waliofanikiwa yaliwekwa kwenye mbao za matangazo za ofisi ya manispaa tu na jitihada hazikufanyika kutumia njia mbadala za kuwapa taarifa waliochaguliwa kwamba walipaswa kuhudhuria usaili tarehe fulani (Ripoti ya LTO, Kigoma, 2020). Waombaji wote walifanya usaili wa ana kwa ana kwa sababu wasaili walitaka kujua uelewa wao wa mfumo wa uchaguzi wa nchi. Kama ilivyoelezwa awali, majina ya watu waliochaguliwa yaliwekwa katika mbao za matangazo mbalimbali katika ofisi za kata husika. Baadhi ya watazamaji wa REDET wa muda mrefu walihudhuria

8 Hotuba ta Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kufungua kikao kazi cha wasimamizi wa uchaguzi tarehe 24 Julai 2020 katika ukumbi wa Morena Hotel, Jijini Dodoma.

mafunzo ya watendaji wa uchaguzi.

Watendaji wa uchaguzi walipatiwa mafunzo muda tofauti. Watendaji wa uchaguzi wote waandamizi walipatiwa mafunzo na Tume kwa kutumia ratiba iliyoandaliwa na Tume. Katika ngazi za chini mafunzo yalitolewa katika ngazi ya jimbo wiki ya tatu ya mwezi Oktoba. Mafunzo yalitolewa kwa siku moja hadi tatu. Makarani Waongozaji walipatiwa mafunzo kwa siku moja na Wasimamizi wa Vituo vya uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya uchaguzi walipatiwa mafunzo kwa siku mbili. Watoaji mafunzo walikuwa Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi kutoka ofisi ya manisapaa na baadhi yao kutoka Sekretarieti ya Tume.

Mafunzo hayo yalitolewa ili kujenga uwezo wa watendaji watakaosimamia mchakato wa uchaguzi kwenye vituo vyao. Vijitabu viliwi vilitumika kutoa mafunzo hayo. Mada ambazo zilitolewa nchi nzima zilikuwa: Maelekezo kwa Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura  na Maelekezo kwa Makarani Waongozaji. Vitabu hivyo vilikuwa na maudhui yafuatayo:

a) Mada ya 1: Majukumu ya watendaji wa uchaguzi siku ya uchaguzi.

b) Mada ya 2: Utaratibu wa kupiga kura na vitu muhimu vya kuzingatia kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

c) Mada ya 3: Utaratibu wa kuhesabu kura na namna ya kutunza vifaa.

d) Mada ya 4: Tahadhari kwa watendaji wa uchaguzi.

Mafunzo yalitolewa kwa njia shirikishi. Yalihusisha mihadhara na matumizi ya video ambazo zilionesha shughuli za uchaguzi zikifanyika kwenye vituo vya kupigia kura. Iliwapa fursa washiriki kufanya baadhi ya shughuli zinazohusiana na mchakato wa uchaguzi. Mafunzo yalikuwa mazuri na taarifa za kina zilitolewa ili waelewe namna na vitu gani vilihusu mchakato wa uchaguzi, pamoja na taratibu na kanuni za kuzingatia.



*Watazamaji wa REDET wakifuatilia mafunzo ya Wasimamizi wa Vituo na Wasimamizi wa Vituo Wasaidizi tarehe 26 Oktoba 2020 kwenye ukumbi wa Mkapa jijini Mbeya.*



*Washiriki wa moja ya vipindi vya mafunzo ya Wasimamizi wa Vituo na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo katika jimbo la Mbeya Mjini wakipatiwa mafunzo ya namna ya kuandaa vituturi kwenye mafunzo yaliyotolewa tarehe 26 Oktoba 2020 kwenye ukumbi wa Mkapa.*

### 3.3.2 Usajili wa Watazamaji Uchaguzi na Watoaji Elimu ya Mpiga Kura

REDET ilikuwa miongoni mwa asasi 97 zilizoruhusiwa kutazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kama tulivyoeleza awali, kutokana na mabadiliko ya sheria ambayo yaliweka vigezo mbalimbali kwa asasi za kiraia, REDET ilitazama uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 bila washirika wake muhimu wa siku zote, yaani asasi za kidini. Kwenye orodha ya Tume ya asasi 97 zilizoruhusiwa kutazama uchaguzi na asasi 245 za kijamii zilizoruhusiwa kutoa elimu ya mpiga kura mwezi Julai 2020 hazikuwapo asasi muhimu za ndani ambazo wakati wote zilishiriki katika kutazama uchaguzi na kutoa elimu ya mpiga kura. LHRC ambayo ilishirikiana na REDET katika chaguzi zilizopita kupitia TEMCO na asasi zingine za kiraia kama THRDC na Jukwaa la Katiba Tanzania (TCF) hazikuruhusiwa.

Pamoja na nia njema ya kuanzisha mfumo wa menejimenti ya watazamaji, lilikuwa ni kosa kubwa kwa Tume kuanzisha mfumo mwingine wa kusajili watazamaji bila kwanza kuwafahamisha wadau, wakiwamo REDET na asasi zingine ambazo zilifanya kazi kipindi cha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mfumo wa kidijitali wa kuweka na kuchakata taarifa za watazamaji kupitia, kwa kiasi fulani, ulipunguza kasi badala ya kuongeza kasi ya zoezi kutokana na (i) seva kufanya kazi polepole na kuchukua muda mrefu kuweka taarifa; (ii) mtandao hafifu; (iii) kushindikana kurekebisha taarifa kuhusu majimbo waliyopangiwa watazamaji (changamoto hii ilijitokeza kabla maboresho kufanyika kwenye OMS na wataalamu wa TEHAMA wa Tume); na (iv) programu ya kimtandao muda mwingine ilikuwa haipatikani kipindi ambacho tarehe ya mwisho ya kuchakata vitambulisho vya watazamaji ikikaribia.

Kwa ujumla, watazamaji wa muda mrefu wa REDET walipokelewa vizuri na Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi kwenye majimbo yao. Maafisa na wagombea wa vyama mbalimbali nao walitoa ushirikiano. Kwenye majimbo yaliyo mengi watendaji wa uchaguzi waliwapatia watazamaji orodha za wagombea ubunge na udiwani, ratiba ya kampeni za uchaguzi, barua za utambulisho kwenye taasisi mbalimbali zilizohusika na usimamizi wa mchakato wa uchaguzi na orodha ya asasi zilizotoa elimu ya uraia.

Kwenye maeneo machache kama vile jimbo la Temeke, uongozi wa CHADEMA ulikuwa na wasiwasi na REDET. Walisita kushirikiana nayo mpaka walipojiridhisha juu ya jukumu la REDET kwenye uchaguzi. Walitaka kujua kama watazamaji wangeingilia masuala ya uchaguzi kwa niaba yao kama haki zao zingevunjwa.

Kwenye jimbo la Kawe, baadhi ya vyama vya siasa vilidhani kwamba REDET ilikuwa inawachunguza. Vivyo hivyo, kwenye jimbo la Mbagala baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa walidhani kwamba REDET ilikuwa inaunga mkono serikali na kwa mantiki hiyo chama tawala. Hisia hizi ziliongezeka kufuatia uvumi kwenye mitandao ya kijamii kwamba REDET iliendesha kura za maoni kwa nia ya kupandisha kiwango cha kukubalika kwa serikali kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika (REOC Dar es Salaam, 2020a). Lakini kadiri ilivyofahamika kwamba zilikuwa habari za uongo, ushirikiano na wadau uliongezeka.

### 3.3.3 Kuapishwa kwa Mawakala wa Uchaguzi

Moja ya shughuli za uchaguzi zilizotawala vyombo vya habari vya ndani wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ni namna zoezi la kuapisha mawakala wa uchaguzi lilivyoendeshwa. Kwa mujimu wa Ibara za 57 na 58 za Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, zikisomwa pamoja na Ibara ya 50 (4) na (5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 (zilizoandaliwa chini ya kifungu cha 124) na Ibara ya 43 (4) na (5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2020 (zilizoandaliwa chini ya kifungu cha 125), mawakala wa uchaguzi wanapaswa kula kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi na hakuna wakala angeruhusiwa kuingia kituo cha kupigia kura bila kula kiapo hicho.

Zoezi la kuwaaapisha mawakala wa vyama vya siasa lilikwenda vizuri katika baadhi ya maeneo lakini kulikuwa na malalamiko katika maeneo mengine mengi. Mathalani, kwenye jimbo la Arusha zaidi ya mawakala wa uchaguzi 1,000 wa CHADEMA walikuwa wa kwanza kuapishwa na zoezi lilienda vizuri kama alivyoeleza mgombea ubunge wa jimbo hilo, “Hadi sasa sijapokea malalamiko yeyote kwa upande wa Arusha. Zoezi linakwenda vizuri” (*The Citizen*, Alhamisi, 22 Oktoba 2020). Katika maeneo mengine vyama vya siasa na wagombea, hasusan wa upande wa upinzani, waliulalamikia utaratibu wa kufanya zoezi hilo sehemu moja, kinyume na maelekezo ya nani asimamie kiapo hicho na wapi kitolewe (kata, mamlaka ya serikali za mtaa, tarafa), sharti la kupeleka picha mbili za rangi zilizopigwa siku za hivi karibuni na taarifa binafsi za mtu (nakala ya kitambulisho cha taifa, kitambulisho cha mpiga kura au pasi ya kusafiria).

Kwenye mkoa wa Shinyanga, kama ilivyokuwa kwenye majimbo mengine nchini, zoezi la kula kiapo halikukamilika tarehe 21 Oktoba 2020 kama ilivyopangwa kwa sababu kuu nne. Mosi, kulikuwa na idadi kubwa ya mawakala waliopaswa kula

kiapo, waliohitaji muda wa kuhakiki taarifa zao na kula kiapo. Pili, mazingira ya kijiografia ya majimbo yalifanya iwe vigumu kwa Wasimamizi wa Uchaguzi au watendaji wa uchaguzi walioteuliwa kuwa kwenye maeneo mengi na kula viapo kwa muda. Tatu, vyama vya siasa vilichelewa kupeleka majina ya mawakala kwenye ofisi za uchaguzi katika ngazi ya jimbo. Nne, baadhi ya mawasilisho kutoka baadhi ya vyama yalikosa viambatisho muhimu kama vile barua za utambulisho, kitu ambacho kilipelekea iwe vigumu kwa wao kula kiapo kama ilivyopangwa, na badala yake walitumia muda mwingi kutafuta nyaraka. Kwa mfano, katika eneo la Msalala mchakato ulienda vizuri, isipokuwa kwa mawakala 10, saba kutoka CUF na watatu kutoka CHADEMA, ambao hawakuwa na barua za utambulisho kutoka kwenye vyama vyao. Kwa upande wa Kishapu na Kahama mchakato haukukamilika siku ya tarehe 21 Oktoba kutokana na idadi kubwa ya mawakala wa uchaguzi waliohitaji kula kiapo. Huko Kishapu, mchakato wa kula kiapo ulikuwa mgumu kwa sababu za kijiografia ambazo zilimtaka Msimamzi wa Uchaguzi kwenda kwenye kata mbalimbali kutoa kiapo kwani ilikuwa vigumu kuwakusanya mawakala kwenye vituo vichache. Mkoani Shinyanga kulikuwa na ucheleweshaji wa kupeleka majina na kwa hiyo kusababisha kusimama kwa mchakato na tofauti kwenye takwimu.

Idadi kamili ya mawakala wa vyama vya siasa waliokula kiapo mkoani Shinyanga (7,382) inaonekena kwenye Jedwali Namba 3.1. CCM na CHADEMA waliweka mawakala wengi zaidi kuliko nyama vingine vyote. Vyama vya UDP, TLP na Demokrasia Makini walimweleza Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa wa REDET kwamba hawakuwa na mawakala wa kutosha wa uchaguzi kwa sababu ya ukosefu wa fedha na idadi ndogo ya wanachama.

**Jedwali Na. 3.1 Idadi ya Mawakala wa Vyama Mkoani Shinyanga**

| Jimbo | Idadi ya Mawakala wa Vyama vya Siasa | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ACT-W | ADA-TADEA | CCM | CHADE-MA | CUF | DM | DP | NC-CR-M | TLP | UDP | Total |
| Kahama | 304 | 2 | 567 | 560 | 268 | 0 | 40 | 282 | 0 | 0 | **2023** |
| Kishapu | 21 | 0 | 467 | 483 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 0 | **982** |
| Msalala | 11 | 0 | 423 | 262 | 29 | 0 | 0 | 32 | 0 | 0 | **757** |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shinyanga Mjini | 274 | 0 | 326 | 326 | 0 | 213 | 0 | 256 | 149 | 126 | **1670** |
| Solwa | 17 | 0 | 572 | 304 | 55 | 0 | 0 | 28 | 0 | 0 | **976** |
| Ushetu | 11 | 0 | 491 | 366 | 54 | 0 | 0 | 52 | 0 | 0 | **974** |
| **Jumla** | **638** | **2** | **2,846** | **2301** | **406** | **213** | **40** | **661** | **149** | **126** | **7382** |

***Chanzo: Ripoti ya LTO ya Shinyanga, 2020.***

Kwa kuwa CCM ilikuwa imeshawasilisha orodha ya mwakala wake na vyama vingine vya siasa vilikuwa katika hatua tofauti za kuandaa orodha hizo, watendaji wa uchaguzi waliamua kubadilisha mpango wa awali wa kutoa viapo kwa kigezo cha kata na kwenda kwenye vyama ambavyo mtu alitokea. Kwa mfano, kundi la kwanza kula kiapo katika kituo cha Buhangija lilikuwa la CCM, likufuatiwa na CHADEMA, ACT-Wazelendo na vyama vingine vya siasa. Viapo walivyokula mawakala wa CCM vilikwenda vizuri kwa sababu walitosha kwenye ukumbi. Lakini kulikuwa na ucheleweshaji kwa upande wa vyama vingine kutokana na mawasiliano mabaya kati ya wasimamizi wa uchaguzi wasaidizi na mawakala wa vyama. Baadaye, wasimamizi wa uchaguzi wasaidizi waliomba mawakala wa vyama wale kiapo. Hata hivyo, chumba kilikuwa kidogo kwa mawakala wote kutosheleza, kitu ambacho kiliwafanya Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi kuwaomba mawakala ambao walikuwa hawajaketi kutoka nje ya ukumbi. Baada ya muda mfupi Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi waligundua kwamba mawakala wa kila chama walipaswa kuapishwa peke yao. Mawakala walichoka kusubiri. Kadiri Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi walivyoendelea kujadili namna ya kuendesha zoezi hilo, mawakala waliokuwamo ukumbini walianza kuimba "Tunataka kuapishwa; tunataka kuapishwa." Polisi wakaletwa.

Wakati huohuo nje ya ukumbi ugomvi ulitokea kati ya mawakala wa ACT-Wazalendo na Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi pindi mawakala walipomwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi awaeleze majukumu na wajibu wa mawakala wa vyama vya siasa katika uchaguzi. Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi aliwajibu kwamba wajibu wa kutoa taarifa hiyo ulikuwa wa vyama vya siasa na si watendaji wa uchaguzi. Mawakala waliliona jibu hilo ni la kijeuri na lisilotoa taarifa kwa hiyo wakaanza kumzomea, "Tunakuuliza kwa sababu hatujui." Wengine walihoji kama kweli wajibu ulikuwa wa vyama vya siasa na vyama havikutekeleza wajibu wake. Je, mawakala walipaswa kwenda wapi kupata ushauri? Afisa wa uchaguzi

alisisitiza kuwa utoaji wa elimu ya mpiga kura lilikuwa jukumu la vyama vya siasa husika. Suala hilo lilisababisha vurugu mpaka pale ambapo kiongozi mmoja wa ACT-Wazalendo alipowaomba watulie kwa kuwahakikishia kwamba taarifa hiyo itatolewa baada ya wao kula kiapo. Taarifa hii iliwatuliza na waliendelea na mchakato wa kujiandikisha.

Baada ya zoezi la kula kiapo kumalizika, changamoto ya nne ilijitokeza. Walipoomba uthibitisho wa kiapo, mawakala walidai kwamba kwa kuwa walikuwa wamekula kiapo kama kikundi, ingeweza kuthibitishwa vipi kwamba wote walikuwa wamekula kiapo? Watendaji wa uchaguzi walivieleza vyama vya siasa na mawakala kwamba orodha ya mahudhurio ingetumika kuonesha nani alikula kiapo. Uthibitisho wa nani alistahili kuwa wakala ungewekwa kwenye barua ya utambulisho itakayoambatishwa na orodha ya mawakala. Barua zingepelekwa kwenye vyama husika kabla ya siku ya uchaguzi. Ingawa vyama vya upinzani vilikubali maelezo hayo, walisema kwamba ilikuwa ni muhimu kuweka stika kwa kila mtu aliyekula kiapo kama ushahidi wa ushiriki wake. Mmoja wa viongozi wa NCCR-Mageuzi alisema alipoulizwa ni kwa nini uthibitisho ulikuwa muhimu. “Unaweza kuwa na mawakala 11 waliokula kiapo lakini barua ya utambulisho inapokuja inataja mawakala saba tu. Utawezaje kuthibitisha kwamba ulikula kiapo wakati wamekataa kutupatia fomu za mahudhurio?”

Suala la mwisho lilikuwa tofauti kati ya idadi ya mawakala iliyotajwa na vyama vya siasa na idadi iliyotolewa na watendaji wa uchaguzi kama Jedwali Namba 3.2 linavyoonesha Ifahamike kwamba taarifa rasmi hazikutolewa kwa vyama vya siasa; alipewa mtazamaji kwa lengo la kuweka kumbukumbu. Hata hivyo, Mtazamaji wa Muda Mrefu wa jimbo la Shinyanga Mjini alipenda kulinganisha takwimu kwa sababu kuu tatu. CCM ilikuwa imeapisha mawakala 326 na mawakala wa ziada 85. Hivyo, mtazamaji alipenda kuona kama vyama vingine vingekuwa na mawakala wa ziada. Pili, viongozi wa ACT-Wazalendo wa Shinyanga Mjini waligombana wakisema kwamba orodha mbili zilikuwa zimepelekwa kwenye ofisi za uchaguzi. Tatu, mtazamaji aliambiwa na viongozi wa ACT-Wazalendo, CHADEMA na NCCR-Mageuzi kuwa mawakala feki walikuwa wameongezwa kwenye orodha ya CCM.

**Jedwali Na. 3.2: Tofauti ya Idadi ya Mawakala wa Vyama katika Jimbo la Shinyanga Mjini**

| Shinyanga Mjini | Idadi ya Mawakala wa Vyama vya Siasa | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ACT-W | ADA-TADEA | CCM | CHADEMA | CUF | DM | DP | NCCR-M | TLP | UDP | **Jumla** |
| Takwimu rasmi | 274 | 0 | 326 | 326 | 0 | 213 | 0 | 256 | 149 | 126 | **1670** |
| Takwimu zisizo rasmi | 243 | 0 | 411 | 246 | 0 | 326 | 50 | 77 | 21 | 50 | **1424** |

*Chanzo: Ripoti ya LTO ya Shinyanga, 2020.*

CCM ilimpa mtazamaji orodha iliyoonesha kwamba mawakala wake 411 walikuwa wamekula kiapo. Kulingana na takwimu rasmi, ni mawakala 326 tu wa CCM waliokula kiapo. ACT-Wazalendo walikuwa na mawakala 243 kinyume na takwimu rasmi ya mawakala 274. Tofauti pia zilijitokeza kwa upande wa vyama vya TLP na NCCR-Mageuzi. TLP ilikuwa inagombea nafasi ya udiwani kwenye kata moja kwa sababu za ukosefu wa fedha na kwa hiyo ilikuwa na mawakala 21. Cha kushangaza ni kwamba orodha rasmi ilionesha kwamba TLP ilikuwa na mawakala 149 wa uchaguzi. Tofauti hiyo ilionekana pia katika orodha ya chama cha NCCR-Mageuzi ambayo ilionesha mawakala 77, ingawa orodha rasmi ilikuwa na mawakala 256.

Kwa sababu ya malalamiko na changamoto zilizojitokeza katika zoezi hilo, Tume iliongeza siku tatu (tarehe 21 hadi 23 Oktoba 2020) kwa ajili ya zoezi ambalo lilipangwa kufanyika kwa siku moja. Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Dkt. Wilson Mahera, "Kwa sababu baadhi ya maeneo ni vigumu kuyafikia kwa sababu za kijiografia, ilikuwa vigumu kwa watendaji wa uchaguzi kukamilisha zoezi kwa wakati" *(Daily News*, Alhamisi, 22 Oktoba 2020).

### 3.3.4 Ugawaji wa Maeneo ya Uchaguzi

Tume ilitangaza marekebisho madogo kwenye majimbo ya uchaguzi tarehe 23 Julai 2020. Mabadiliko hayo hayakuhusisha kuongeza idadi ya majimbo, badala yake yalihusu mabadiliko ya majina ya majimbo matatu: Jimbo la Chilonwa, Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma lilibadilishwa na kuwa Chamwino; Jimbo la Mtera kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Dodoma lilibadilika na kuwa

Mvumi na Jimbo la Kijitoupele la Magharibi B Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar lilibadilika na kuwa Pangawe. Idadi ya majimbo na kata zilibaki 264 na 3,956 kama zilivyokuwa mwaka 2015. Tarehe 2 Julai 2020 Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilitangaza kufutwa kwa majimbo manne, yaani Mahonda, Mtopepo, Kijitoupele na Chukwani. Matokeo yake Zanzibar ilikuwa na majimbo 50: 32 Unguja na 18 Pemba, badala ya majimbo 54 ya awali. Tume ya Uchaguzi Zanzibar pia ilibadilisha jina la jimbo la Mgogoni la Wete na kuwa Pandani.

### 3.3.5 Gharama za Uchaguzi

"Uchaguzi unaweza kusimamiwa kwa ufanisi na kwa weledi kama fedha za kutosha zitapatikana mapema" (Chaligha, 2010, 403). Sheria ya Taifa ya Uchaguzi inataka fedha za kugharimia uchaguzi zitoke kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini Tume ilipendekeza kuanzishwa kwa mfuko wa fedha za uchaguzi kwenye taarifa yake juu ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Hata hivyo, Tume iliendelea kupokea fedha za uchaguzi kutoka serikalini. Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Uchaguzi, serikali ilitoa fedha zote za uchaguzi kutoka kwenye fedha za walipa kodi na ilipeleka shilingi bilioni 120 kwenye wilaya (*The Guardian*, 22 Ockoba 2020). Serikali ilipitisha shilingi 331,728,258,035 kwa ajili ya uchaguzi.[9]

### 3.3.6 Uandikishaji Wapiga Kura

Kama tulivyoeleza awali, REDET ilitazama uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kuandaa taarifa ya kina juu ya zoezi hilo. Kuanzia tarehe 1 Desemba 2019, REDET ilipeleka watazamaji wake wa muda mrefu kwenye mamlaka 89 za serikali za mitaa kwenye mikoa 16 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Tume ilizindua zoezi hilo rasmi Mkoani Kilimanjaro tarehe 18 Julai 2019. Hili lilifanyika kulingana na masharti ya kifungu cha 40 (1) cha Kanuni za Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 792 na Namba 793 tarehe 28 Desemba 2018) na kifungu cha 42 (1) cha Kanuni za Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Serikali za Mtaa za mwaka 2018.

Kuelekea siku ya uchaguzi, Tume ilitangaza kwamba wapiga kura wangeruhusiwa kutumia vitambulisho vingine kama vile leseni ya udereva, kitambulisho cha taifa na pasi ya kusafiria kama kadi ya mpiga kura imepotea au mtu hakumbuki ameiweka wapi. Uamuzi huu haukuwa na athari kubwa kwenye idadi ya watu

9 Tazama Jarida la Tume (halina tarehe) "Maandalizi Kuelekea Uchaguzi Mkuu, 2020", uk. 50.

waliojitokeza kupiga kura mwaka 2020.

Kwa kiasi kikubwa uandikishaji wapiga kura ulifanyika kwa mafanikio kwenye mamlaka 89 zilizotazamwa. Tume ilifanya mipango yote muhimu, pamoja na kuandaa ratiba ya kuandikisha wapiga kura kwa awamu. Kwa sehemu kubwa, vifaa vya kuandikishia wapiga kura vilitosha na kusambazwa kwa wakati. Uteuzi, utoaji mafunzo na usambazaji wa waandikishaji wapiga kura uliwaridhisha wadau walio wengi, ikiwamo REDET.

### 3.3.7 Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura

Kifungu cha 4c cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343, kinaipa Tume jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, na kuratibu na kuwasimamia watu wanaotoa elimu hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo, mwezi Novemba 2019 Tume ilizialika asasi zilizopenda kutoa elimu hiyo kupeleka maombi kwa ajili ya kusajiliwa. Mwezi Julai 2020 Tume ilitoa vibali kwa asasi za kiraia 245 nchi nzima ili zitoe elimu ya mpiga kura (*The Citizen*, Julai 2020).

Kama Jedwali Namba 3.3 linavyoonesha, elimu ya mpiga kura ilitolewa zaidi na asasi za kiraia na siyo Tume. REDET ilipenda kufahamu kama kuna elimu yeyote ya mpiga kura iliyotolewa kuhusu UVIKO-19 kutokana na madhara yake makubwa kwenye jamii. Kwa ujumla, si Tume na wala si asasi za kiraia zilitoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo. Jedwali Namba 3.3 linaonesha kwamba ni watazamaji wa muda mrefu na wa muda mfupi 461 kati ya 5,131 (asilimia tisa) walioshuhudia elimu juu ya namna ya kujikinga na UVIKO-19 ikitolewa.

**Jedwali Na. 3.3: Utolewaji wa Elimu ya Mpiga Kura na Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi na Asasi za Kiraia**

| Swali | Jibu | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (asilimia) |
| Je, ulishuhudia elimu yeyote ya mpiga kura ikitolewa na asasi za kiraia kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020? | 2763 (53.9) | 2368 (46.2) | 5131 (100) |
| Je, ulishuhudia elimu yeyote ya mpiga kura ikitolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020? | 7,101 (13.8) | 4421 (86.2) | 5131 (100) |
| Je, ulishuhudia elimu yeyote kuhusu namna ya kujikinga na UVIKO-19 ikitolewa? | 461 (9.0) | 4670 (91) | 5131 (100) |

Tume na wadau wengine walitumia njia mbalimbali kuwafanya watu wajiandikishe:

i. Mikusanyiko rasmi na isiyo rasmi: Tume ilitoa elimu ya mpiga kura wakati wa shughuli za kitaifa ambazo ziliwavutia watu wengi kama vile wakati wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Simiyu (31 Julai hadi 8 Agosti 2019), Wiki ya Sheria iliyoadhimishwa Dodoma (31 Januari hadi 6 Februari 2020), tamasha la funga mtaa lililoandaliwa na kituo cha redio cha *efm* na kufanyika Mabibo Dar es Salaam, tamasha la muziki la daftari lililofanyika viwanja vya Mwembe Yanga, Temeke, Dar es Salaam, na tamasha la waendesha bodaboda lililofanyika Kondoa;[10]

ii. Kuwalenga wanafunzi wa shule za sekondari: kwa mfano shule nyingi za sekondari za jimbo la Kinondoni zilifikiwa na timu ya Tume ya watoa elimu ya mpiga kura; Wilayani Korogwe wanafunzi walisaidia kupeleka taarifa kwa wazazi wao;

iii. Programu za redio na televisheni: maigizo ya kwenye redio na televisheni, matangazo na vipindi maalumu vya televisheni kama *Malumbano ya Hoja, Kumekucha* and *Kipima Joto*;

iv. Mitandao ya kijamii: Tume ilitengeneza jumbe fupifupi zilizowekwa katika mitandao yake ya kijamii kama Instagram, Twitter, Facebook na televisheni ya Tume ye mtandaoni; na

v. Njia zingine: Matumizi ya magari ya matangazo, vipeperushi na mabango yaliyowekwa katika barabara kuu.

Kama Jedwali Namba 3.4 linavyoonesha, Tume ilitumia njia mbalimbali kutoa elimu ya mpiga kura, lakini njia zilizotumika zaidi zilikuwa matangazo ya redio na televisheni.

**Jedwali Na. 3.4: Njia Zilizotumika kutoa Elimu ya Mpiga Kura**

| Njia | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Hakuna elimu ya mpiga kura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 2141 | 41.7 |
| Vipeperushi | 1221 | 23.8 |
| Matangazo katika magazeti | 553 | 10.8 |
| Matangazo ya redio | 1993 | 38.8 |
| Matangazo ya televisheni | 2011 | 39.2 |
| Mitandao ya kijamii | 1114 | 21.7 |
| Magari ya matangazo | 604 | 11.8 |
| Mafunzo katika maeneo ya wazi kama masoko, vituo vya mabasi, n.k. | 251 | 4.9 |

10 Tazama Jarida la Tume (halina tarehe) "Maandalizi Kuelekea Uchaguzi Mkuu, 2020", kur. 20-30.

| | | |
|---|---|---|
| Zingine | 205 | 4.0 |

***Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2019.***

*Zingatia: Majibu yote = 5131; Matokeo haya yametokana na majibu mengi.

Takribani watazamaji wa majimbo yote ya Dar es Salaam waliona elimu ya mpiga kura ikitolewa na Tume, asasi za kiraia na vyama vya siasa. Kwanza haikutolewa kwa wakati. Kama ilivyokwishaelezwa, elimu ya mpiga kura ilianza kutolewa wiki ya pili ya mwezi Oktoba, wiki mbili kabla ya siku ya uchaguzi. Pili, ilitolewa katika baadhi ya maeneo tu. Mathalani, vipeperushi vya Tume vilivyoonesha namna ya kupiga kura na nini kifanyike baada ya kupiga kura viliwekwa kwenye maeneo ambayo yangekuwa vituo vya kupigia kura. Maeneo kama shule za msingi na sekondari siyo maeneo ambayo watu wengi hutembelea. Ni watu wachache waliokwenda kwenye maeneo hayo kama majina yao yalikuwapo kwenye daftari la wapiga kura. Tatu, asasi nyingi zilifanya kazi katika maeneo machache na kwa hiyo wasingeweza kufanya kazi katika maeneo mengi kwenye jimbo au mkoa wenye majimbo 10 na kata 102. Vyama vya siasa vilianza kutoa elimu ya mpiga kura wiki mbili kabla ya siku ya uchaguzi. Walijikita katika kutoa elimu kuhusu karatasi za kura za mfano ambazo walizionesha katika kila mkutano wa kampeni na kuwaonesha wananchi wapi katika karatasi la kura waweke alama ya vema. Kwenye majimbo kama majimbo ya Serengeti, Bunda, Tarime Mjini na Musoma Mjini, vyama vya siasa na wagombea wao waliamua kutoa elimu ya mpiga kura katika mikutano ya kampeni. Lakini elimu iliyotolewa katika mikutano hiyo ilihusu kuvipigia kura vyama husika. Kipindi cha wiki mbili za mwisho za kampeni za uchaguzi, CCM na CHADEMA zilitumia hadi dakika tano katika kila mkutano wa kampeni kuwaonesha wananchi namna ya kuwapigia kura bila kuharibu kura (Mara Ripoti ya LTO, 2020).

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania wananchi walipiga kura siku ya juma, badala ya mwishoni mwa juma (Jumapili). Siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba 2020 ilitangazwa kuwa siku maalumu ya uchaguzi. Mwanzoni wananchi hawakulewa nini maana ya siku maalumu ya kupiga kura. Wengine hawakujua kama wafanyakazi wa sekta za umma na binafsi wangeenda kazini siku hiyo. Ufafanuzi kuhusu suala hili ulitolewa pale Rais aliposema wiki mbili za mwisho za kampeni yake kuwa siku hiyo itakuwa siku ya mapumziko na wafanyakazi wa sekta za umma na binafsi hawatakwenda kazini ili kazi isiwazuie kupiga kura.

Suala la pili ni kwamba Tume, asasi za kiraia na vyama vya siasa hawakusema katika

elimu ya mpiga kura waliyotoa kwamba ilikuwa ni lazima na muhimu kwa wapiga kura kwenda kwenye vituo vya kupigia kura kuvitambua vituo watakavyopigia kura. Matokeo yake watu kadhaa walihangaika kutafuta vituo vya kupigia kura na baadhi yao walidhani ni pale walipoandikishwa kwa mara ya kwanza. Wengi kati ya wapiga kura hao hawakujua kuwa kulikuwaa na njia ya jumbe fupi ulioanzishwa na Tume kwa ajili ya mtu kutambua kituo chake cha kupigia kura. REDET ilikutana na watu wachache waliokata tamaa na kurudi nyumbani bila kupiga kura.

Kwa ujumla, njia zilizotumiwa kutoa elimu ya mpiga kura zilikuwa na mapungufu katika baadhi ya maeneo, kama pale ambapo REDET ilibaini kwamba ingawa asasi za kiraia zilidai kuyalenga makundi maalumu ya watu waliojiandikisha kama vijana na watu wenye ulemavu, kazi yao haikuwa maalumu kiasi hicho. Njia waliyoitumia ni kutoa elimu katika maeneo ya wazi kama masokoni na vituo vya mabasi ambapo vijana na watu wenye ulemavu wangeweza kupatikana. Lakini hii haikumaanisha kwamba elimu ya mpiga kura ingeyafikia makundi maalumu.

## 3.4 HITIMISHO

Uchambuzi wa mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 umeonesha ubora na mapungufu. Kuhusiana na ubora, uchaguzi uligharamiwa na fedha za walipa kodi ambazo zilitolewa kwa wakati kwa Tume na mamlaka za serikali za mitaa. Pili, uteuzi wa watendaji wa uchaguzi kiushindani ilikuwa njia nzuri. Watendaji wa uchaguzi waliteuliwa kwa sifa zao baada ya watu wenye sifa stahiki kutuma maombi. Mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi yalikuwa mazuri, ya kueleweka na ya kina. Tatu, uamuzi wa kuwaruhusu wapiga kura ambao walikuwa wamepoteza vitambulisho vyao kutumia vitambulisho vya taifa, pasi ya kusafiria au leseni za udereva ulikuwa uamuzi mzuri uliowapa wapiga kura wengi fursa ya kutekeleza haki yao ya kikatiba ya kupiga kura.

Kwa upande wa mapungufu, baadhi ya sheria (kama vile Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari) zilisababisha migogoro kwani vyama vya siasa, vyombo vya habari na wananchi waliziona sheria hizo kama ni kizuizi badala ya kuwa wezeshi. Baadhi ya wagombea na vyama vya siasa viliitaka Kamati ya Maadili ya Tume na Ofisi ya Msajili kutekeleza vifungu vya maadili ya uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa kwa haki kwa washiriki wote wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Uapishaji wa mawakala wa vyama haukwenda vizuri labda ni kwa sababu ya kuyumbayumba na upendeleo. Mwisho, baadhi ya viongozi wa dini waliwaunga mkono au kuwapinga baadhi ya wagombea na kwa hiyo kutishia umoja na mshikamano wa

Watanzania. Hivyo basi, vyombo vinavyosimamia uchaguzi ilipaswa viingilie kati ili kuliongezea nguvu tamko lililotolewa na Waziri kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Asasi za Kiraia, Sura ya 337.

# SURA YA NNE

# UTEUZI WA WAGOMBEA

## 4.1 UTANGULIZI

Uteuzi wa wagombea ni sehemu ya demokrasia ya ndani ya vyama na inaamua ugombea wa mtu kwenye jamii ambazo wagombea binafsi wanaruhusiwa. Ina athari katika mchanganyiko wa watu waliomo kwenye vyombo vya kutunga sheria za nchi na sera zinazotungwa.[11] Sura hii inaangalia uteuzi wa wagombea uliofanywa na vyama vya siasa na vyombo vya kusimamia uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Sura hii ina sehemu nane, pamoja na utangulizi huu. Sehemu ya Pili inaelezea mifumo ya kisheria na kitaasisi, pamoja na taratibu na kanuni za uteuzi za vyama vya siasa. Uteuzi wa wagombea urais unatazamwa katika Sehemu ya Tatu. Sehemu ya Nne inaangalia uteuzi wa wagombea uliofanywa na Tume na Sehemu ya Tano inatazama namna rufaa zilivyoshughulikiwa. Sehemu ya Sita inajadili kupita bila kupingwa kwa wagombea na Sehemu ya Saba inafanya tathmini ya jumla ya mchakato wa uteuzi. Sehemu ya Nane inatoa hitimisho.

## 4.2 MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI

Sheria kuu zinazosimamia uteuzi wa wagombea nchini Tanzania ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343, ya mwaka 1985, Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 na Sheria ya Vyama vya Siasa kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Suala mtambuka katika sheria hizi zote linahusu vifungu kuhusu sifa za mgombea. Kimsingi ni vyama vya siasa ambavyo vinateua wagombea, wakisubiri kupitishwa na vyombo vinavyosimamia uchaguzi. Uteuzi wa wagombea unaofanywa na vyombo vya kusimamia uchaguzi unafuata sifa za kugombea zilizoanishwa kwenye Katiba na sheria za uchaguzi. Ibara za 39(1) na 67(1) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinaainisha sifa za wagombea urais na ubunge na kifungu cha 39(1) sha Sheria za Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 kinaonesha sifa za kugombea udiwani. Sifa hizo ni (i) kuwa mwanachama na kudhaminiwa na chama cha siasa, (ii) umri (miaka 40 kwa urais na miaka 21 kwa ubunge na udiwani, (iii) elimu (shahada ya chuo kikuu kwa urais na kujua

11 Gallagher M. and Marsh M. (1988). *Candidate Selection in Comparative Perspective: The Secret garden of Politics*, London: Sage..

kusoma na kuandika kwa ubunge na udiwani, na (iv) kutokufanya kosa la kukwepa kodi kwa kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi. Sharti la kwamba mtu ni lazima awe mwanachama wa chama cha siasa haliruhusu wagombea binafsi. Haya ni mapungufu katika demokrasia kwani wanaotaka kugombea kama wagombea binafsi hawawezi kutekeleza haki yao ya kidemokrasia.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zinasimamia uchaguzi Tanzania Bara na Zanzibar. Ndiyo wanaohusika na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea baada ya kujiridhisha kwamba wote walioteuliwa wana sifa stahiki. Vyombo hivyo vya kusimamia uchaguzi pia vina jukumu la kupanga siku ya kuteua wagombea kwa kutoa matangazo katika Gazeti la Serikali. Sheria inasema kwamba siku ya kufanya uteuzi kwa ajili ya majimbo isiwe chini au zaidi ya siku 25 kwa uchaguzi wa Muungano na si zaidi ya siku 21 kwa uchaguzi wa Zanzibar baada ya kuvunjwa kwa Bunge na Baraza la Wawakilishi kwa Tanzania Bara na Zanzibar.[12]

### 4.2.1 Taratibu na Kanuni za Vyama

Vyama vya siasa vinafuata taratibu na kanuni zao katika kuteua wagombea wa nafasi mbalimbali. Msharti hayo yamo katika katiba za vyama husika na kanuni zingine za vyama. Lakini vyama vyote vya siasa vinafuata vifungu vya kitaifa kuhusu sifa za mgombea. Vivyo hivyo, kila chama cha siasa kina taratibu na kanuni za kufuata wakati wa uteuzi. Hakuna tofauti kubwa kati ya chama na chama kwa upande wa taratibu za kufanya uteuzi.

Kitu kingine kinachovifanya vyama vya siasa vifanane ni kutokufuata kwao vifungu kuhusu kanuni za kidemokrasia zinazohusiana na masuala ya jinsia. Ingawa katiba za vyama za siasa zina vifungu kuhusu kanuni za kushiriki na kutobagua watu, kwa uhalisia hawazifuati na, kwa ujumla, kuna wagombea wa kiume wengi zaidi ya wagombea wa kike. Moja ya sababu ya hali hii ni kukosekana kwa njia ndani ya vyama na katika taratibu za kitaifa zinazotaka uwepo wa usawa wa kijinsia katika uteuzi wa wagombea.[13]

## 4.3 UTEUZI WA WAGOMBEA URAIS

Mwamko na mshawasha kuhusu uteuzi wa wagombea wa uchaguzi wa kiti cha Rais katika vyama katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulikuwa tofauti na kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Uchaguzi wa

12 Ibara ya 37 (1) (a) ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura, 343, Toleo la 2015, na Ibara ya 42 (1) (a) ya Sheria ya Uchaguzi Zanzibar Namba 4 ya mwaka 2018.

13 Sulley, C. 2020. Intraparty candidate nomination in Tanzania.

mwaka 2015 uliwafanya wengi waelekeze masikio yao katika uteuzi wa mgombea urais atakayemrithi Rais aliyekuwa anamaliza muda wake. Kitu hiki hakikujitokeza mwaka 2020. Rais na kiongozi wa CCM aliyekuwa anatetea kiti chake, John Pombe Magufuli, alipita bila kupingwa. Uteuzi wa mgombea urais wa CHADEMA Ndugu Tundu Lissu ulipokelewa na Watanzania wengi waliomwona kama ni mtu ambaye anaweza kuyasema yale ambayo wengi wasingeyasema. Kuteuliwa kwa Ndugu Bernard Membe kama mgombea urais wa ACT-Wazalendo kulifufua kumbukumbu za mwaka 2015 ambapo Waziri Mkuu wa zamani Ndugu Edward Lowassa aligombea urais kupitia CHADEMA baada ya kuhama kutoka CCM. Kwa kiasi fulani, hii iliathiri ushawishi wa Ndugu Membe kwani alionekana kwamba asingetofautiana na Ndugu Lowassa aliyegombea urais kupitia CHADEMA na baadaye kurudi nyumbani, yaani CCM. Kuteuliwa kwa Ndugu Seif Sharif Hamad kama mgombea urais wa Zanzibar kulionekana kama ni mwendelezo wa harakati zake za muda mrefu za kutaka kuwa Rais wa Zanzibar. Kupokelewa na kuteuliwa kwake kama mgombea urais kulionekana kama ni mbinu za viongozi wa ACT-Wazalendo kutaka kutumia ushawishi wake kupata kuungwa mkono huko Zanzibar.


### 4.3.1 Uteuzi wa Mgombea Urais katika Chama cha Mapinduzi

Ingawa katiba ya Chama cha Mapinduzi inaeleza kwamba mwanachama yeyote mwenye sifa anaweza kugombea nafasi yeyote ya siasa, hakuna mwanachama yeyote wa chama tawala, mbali ya Rais John Magufuli, aliyeomba kuteuliwa na chama hicho kama mgombea urais wa mwaka 2020. Mtetezi huyo wa kiti cha urais ambaye pia ni mwenyekiti wa CCM alipita bila kupingwa. Wapiga kura wote 1,822 wa Halmashauri Kuu ya Taifa iliyokutana Dodoma tarehe 11 Julai 2020 kwa kauli moja walimpitisha Rais Magufuli kama mgombea urais wa CCM.[14]

14 *The Voice of Africa*, 11 Julai 2020.



*Rais Magufuli baada ya kuchukua fomu za uteuzi Dodoma*




*Bango likionesha uteuzi wa Rais Magufuli.*

Baadhi ya viongozi wa upinzani waliunga mkono uteuzi wa mgombea urais wa CCM. Kiongozi wa UDP, Ndugu John Cheyo, alimuunga mkono Magufuli baada ya kupewa fursa ya kuzungumza katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa. Mwingine aliyemuunga mkono alikuwa Ndugu Augustino Mrema, Mwenyekiti wa TLP.

### 4.3.2 Uteuzi wa Mgombea Urais wa CHADEMA

Watu 12 walitaka kugombea urais kupitia CHADEMA. Kwa mujibu wa taratibu za chama, wanachama walipewa siku 12 kuonesha nia ya kugombea urais kupitia chama hicho kwa kuandika barua kwa Katibu Mkuu wa chama kwa kuzingatia kanuni za chama kuhusu wanachama wanaotaka kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika vyombo vya uwakilishi kama Bunge. Chama kiliwapitisha watu 11, isipokuwa mwendesha bodaboda mmoja ambaye alisema kwamba alishindwa kufuata kanuni za chama zinazowahusu watu wanaotaka kugombea. Ni wanachama saba pekee waliochukua fomu na kurudisha kuanzia siku ya tarehe 4 hadi tarehe 19 Julai 2020: Ndugu Isaya Mwita, Ndugu Leonard Manyama, Dkt. Maryrose Majinge, Wakili Gasper Mwanalyela, Ndugu Lazaro Nyalandu, Wakili Samba Neo na Ndugu Tundu Lissu.

Siku ya tarehe 22 Julai 2020 Kamati Kuu ya CHADEMA ilipitisha majina matatu kugombea nafasi ya urais: Ndugu Tundu Lissu, Ndugu Lazaro Nyalandu na Dkt. Maryrose Majinge. Ndugu Lissu alipata kura 405 kati ya kura 442, Ndugu Lazaro Nyalandu alipata kura 36 na mwanamke pekee Dkt. Maryrose Majinge alipata kura moja. Kwa hiyo, jina la Ndugu Lissu lilipelekwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ili lilipitishwe na tarehe 29 Julai 2020 Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama ilimteua Ndugu Tundu Lissu kama mgombea urais wa chama hicho. Halmashauri Kuu pia ilimteua Ndugu Salim Mwalimu kuwa mgombea mwenza wake.




*Tundu Lissu na Salim Mwalimu baada ya kuteuliwa*

### 4.3.3 Uteuzi wa Mgombea Urais wa ACT-Wazalendo

Uamuzi wa mwanachama maarufu wa CCM na Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani Bernard Membe kuchukua fomu ili kugombea urais kupitia ACT-Wazalendo tarehe 17 Julai 2020 ulipokelewa kwa hisia tofauti na wananchi. ACT-Wazalendo ilimteua mgombea urais wake kupitia Halmashauri Kuu ya chama iliyoketi tarehe 5 Agosti 2020. Wajumbe 420 wa Kamati Kuu ya Taifa ya chama hicho ilimpitisha Ndugu Bernard Membe kama mgombea urais wa Muungano wa chama hicho. Ndugu Membe alikuwa mtu pekee aliyechukua fomu kugombea urais wa Muungano kupitia ACT-Wazalendo na Ndugu Seif Sharif Hamad alikuwa mgombea pekee wa urais Zanzibar.



*Ndugu Bernard Membe na Maalim Seif Sharif Hamad*

### 4.3.4 Uteuzi katika Vyama Vingine

Vyama vingine 12 viliteua wagombea urais: ADA-TADEA, NRA, SAU, MAKINI, NCCR-Mageuzi, CUF, ADC, UPDP, DP, CHAUMMA, AAFP na UMD. Wanachama wachache wa vyama hivyo walijitokeza kuomba kuteuliwa kugombea urais kupitia vyama hivyo. Mathalani, ni wanachama watatu tu, Ndugu Samuel Ruhuza, Ndugu Peterson Mushenyera na Ndugu Yeremia Maganja, walioomba kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia NCCR-Mageuzi na mwanachama mmoja tu alijitokeza kufanya hivyo kwa upande wa Zanzibar. Katibu Mkuu wa ADA-Tadea, Ndugu John Shibuda, aliteuliwa na Halmashauri Kuu ya chama hicho tarehe 28 Julai 2020 kugombea urais. Ni watu wawili tu waliofanya hivyo ili kugombea urais

wa Muungano. Shibuda alipata kura 120 kati ya kura 130 zilizopigwa. Mpinzani wake pekee, Ndugu Mustadia Hilali, alipata kura 10.

Katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa iliyoketi tarehe 18 Julai 2020, Ndugu Leopold Mahona wa NRA alipata kura 61 na kumshinda Ndugu Mwanaenzi Kibwana aliyepata kura 8 na Janken Kasambala aliyepata kura 38. Kikao hicho pia kilimteua Ndugu Khamis F. Magau kugombea urais Zanzibar kwa kumpa kura 75 na kumshinda Ndugu Marshed Humud aliyepata kura 23 na Bi. Amina Rashid aliyepata kura 4. Wanachama sita walitaka kugombea urais wa Muungano na wanne urais wa Zanzibar.

### 4.4.6 Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Utazamaji wa REDET unaonesha kwamba ni vyama vichache sana vina utaratibu wa wazi, wa kueleweka, wa kiushindani na wa kidemokrasia katika kuteua wagombea ubunge, yaani CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo na CUF. Utaratibu katika vyama vingi ni kuwa uteuzi wa wagombea unafanywa na vyombo vya juu vya chama wakati vyombo vya ngazi ya mkoa vinateua wagombea udiwani.


#### 4.3.6.1 Uteuzi wa Wagombea Ubunge Ndani ya CCM

Idadi ya wanachama 10,367 walichukua fomu ili kugombea ubunge kupitia CCM. Baadhi ya wachambuzi walisema nia yao haikuwa kuwatumikia wananchi, bali ni kutafuta malipo mazuri yanayoambatana na kazi hiyo (*The EastAfrican*, 27 Julai 2020). Kura za maoni zilizofanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 20 Julai 2020 zilikuwa ni mwanzo wa mchakato wa kuwapata watu watakaogombea ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba. Ingawa baadhi ya watu walioshiriki katika kura za maoni hawakuteuliwa walikuwa na nafasi nzuri ya kuteuliwa kwenye vyombo vingine vya maamuzi vya chama. Wakati wa kura za maoni za wagombea ubunge wa mwaka 2020 baadhi ya wanachama maarufu na wabunge wa zamani waliondolewa na vyombo vya juu vya chama.

Katika CCM kuongoza katika kura za maoni kulimpa mtu uwezekano wa kuteuliwa na vyombo vya juu. Lakini katika baadhi ya maeneo vyombo hivyo vilimteua mshindi wa pili au hata wa tatu, kwa mfano David Silinde wa Momba, Patrobas Katambi wa Shinyanga Mjini, Samweli Xaday wa Hanang na Josephat Gwajima wa Kawe. Ingawa baadhi ya wagombea hawakupendezwa na uamuzi huo hakuna aliyehamia vyama vya upinzani.

Kitu kingine kilichojitokeza katika kura hizo za maoni ni tuhuma za rushwa.

Tuhuma nyingi zilihusu kura za maoni za CCM. Baadhi ya makada wa CCM walikamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU kuhusu tuhuma za rushwa. Tuhuma za rushwa wakati wa kura za maoni za CCM zilikuwa nyingi sana kiasi kwamba TAKUKURU iliiruhusu CCM kushughulikia tuhuma hizo yenyewe.[15] Uamuzi wa TAKUKURU unaleta hisia kuhusu nguvu yake dhidi ya nguvu ya chama tawala. Matukio kama hayo yanaonesha udhaifu wa kitaasisi kwenye kughughulikia rushwa kama sheria iliyoanzisha mamlaka hiyo inavyosema.




*Kibonzo cha matokeo ya uteuzi wa wagombea ubunge ndani ya CCM (The Citizen, 2 Agosti 2020).*

### 4.3.6.2 Uteuzi wa Wagombea Ubunge Ndani ya CHADEMA

Watu wengi walitangaza nia ya kutaka kugombea ubunge kupitia CHADEMA, ingawa idadi ya watu waliochukua fomu ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya watu waliofanya hivyo kupitia CCM. Ingawa CHADEMA na, kwa kiasi fulani, ACT-Wazalendo pia, ilikuwa na watia nia wengi idadi kamili ya watu hao haikufahamika.

## 4.4 UTEUZI WA TUME

Tume ilitangaza kwamba mwisho wa kuchukua fomu ungekuwa tarehe 29 Julai 2020. Fomu za uteuzi kwa ajili ya wagombea urais na umakamu wa rais zilianza kutolewa tarehe 5 Agosti 2020 katika ofisi za Tume mjini Dodoma. Fomu za wagombea ubunge zilitolewa kuanzia tarehe 12 hadi 25 Agosti 2020 katika ofisi

15 Tazama TAKUKURU kuiruhusu CCM kushughulikia tuhuma za rushwa yenyewe, *The Citizen* 13 Agosti 2020

za Tume za mamlaka za serikali za mitaa husika. Fomu za wagombea udiwani zilitolewa kuanzia tarehe 12 hadi 25 Agosti 2020 katika ofisi za kata husika. Fomu zote zilipaswa kurudishwa si zaidi ya saa kumi jioni tarehe 25 Agosti 2020.

### 4.4.1 Uteuzi wa Wagombea Urais

Kama Jedwali Namba 4.1 linavyoonesha, Tume ilipitisha wagombea 15 kugombea urais wa Muungano.

**Jedwali Na. 4.1: Wagombea Urais na Wagombea Mwenza**

| Na. | Chama cha Siasa | Mgombea Urais | Jinsia | Mgombea Mwenza | Jinsia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CCM | Dkt. John Pombe Magufuli | Kiume | Bi. Samia Suluhu Hassan | Kike |
| 2 | ADA-TADEA | Ndugu John Paul Shibuda | Kiume | Ndugu Hassan Kornely Kijogoo | Kiume |
| 3 | NRA | Ndugu Leopord Lucas Mahona | Kiume | Ndugu Khamis Ali Hassan | Kiume |
| 4 | SAU | Ndugu Muttamwega Bhatt Mgaywa | Kiume | Ndugu Satia Mussa Bebwa | Kiume |
| 5 | Demokrasia Makini | Bi. Cecilia Augustino Mwanga | Kike | Bi. Tabu Mussa Juma | Kike |
| 6. | NCCR-Mageuzi | Ndugu Yeremia Kulwa Maganja | Kiume | Ndugu Khamis Haji Ambar | Kiume |
| 7. | CUF | Profesa Ibrahim Haruna Lipumba | Kiume | Bi. Hamida Huweishil Abdalla | Kike |
| 8. | ACT-Wazalendo | Ndugu Bernard Kamillius Membe | Kiume | Profesa Omar Fakih Hamad | Kiume |
| 9. | ADC | Bi. Queen Cuthbert Sendiga | Kike | Ndugu Khamis Juma Shoka | Kiume |
| 10. | UPDP | Ndugu Twalib Ibrahim Kadege | Kiume | Ndugu Ramadhan Ali Abdallah | Kiume |
| 11. | DP | Ndugu Phillipo John Fumbo | Kiume | Bi. Zaina Juma Khamis | Kike |
| 12. | CHAUMMA | Ndugu Hashim Spunda Rungwe | Kiume | Ndugu Mohammed Massoud Rashid | Kiume |
| 13. | AAFP | Ndugu Seif Maalim Seif | Kiume | Ndugu Rashid Ligania Rai | Kiume |
| 14. | UMD | Ndugu Khalfan Mohammed Mazrui | Kiume | Ndugu Mashavu Alawi Haji | Kiume |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15. | CHADEMA | Ndugu Tundu Antipas Lissu | Kiume | Ndugu Salum Mwalimu Juma | Kiume |

***Chanzo: Tume, 2020***

Awali watiania 17 walichukua fomu za uteuzi kutoka Tume ya Taifa ya Uchguzi. Lakini wagombea wawili, Ndugu David Mwaijolele wa CCK na mgombea mwenza wake Ndugu Said Juma, waliondolewa kwa kukosa sifa kwa sababu picha na sahihi ya Ndugu Juma ilikosekana katika Fomu Namba 10 na Ndugu Maisha Mapya Muchunguzi wa NLD alichelewa kurudisha fomu za uteuzi kwenye makao kuu ya Tume.




***Wagombea urais (NEC, 2020)***

### 4.4.2 Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Kama Jedwali Namba 4.2 linavyoonesha, Tume iliteua wagombea ubunge wa CCM kwenye majimbo yote 264, 209 wa CHADEMA, 156 wa ACT-Wazalendo na 153 wa CUF. Kama tulivyoeleza awali, uwezo wa kuweka wagombea unaonesha uwezo wa chama ki rasilimali na wanachama. Baadhi ya wagombea wa CHADEMA waliondolewa baada ya kuwekewa pingamizi na vyama vingine vya siasa, hususan CCM.

**Jedwali Na. 4.2: Watu Walioteuliwa Kugombea Ubunge**

| Na. | Chama | Kiume | Kike | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | 239 | 25 | **264** |
| 2. | CHADEMA | 150 | 59 | **209** |
| 3. | ACT-Wazalendo | 135 | 21 | **156** |
| 4. | NCCR-Mageuzi | 63 | 20 | **83** |
| 5. | CUF | 113 | 40 | **153** |
| 6. | TLP | 17 | 8 | **25** |
| 7. | CHAUMMA | 22 | 6 | **28** |
| 8. | ADC | 33 | 15 | **48** |
| 9. | AAFP | 15 | 10 | **25** |
| 10. | NRA | 21 | 8 | **29** |
| 11. | UDP | 24 | 9 | **33** |
| 12. | UPDP | 8 | 13 | **21** |
| 13. | SAU | 12 | 7 | **19** |
| 14. | DP | 17 | 7 | **24** |
| 15. | UMD | 3 | 13 | **16** |
| 16. | ADA-TADEA | 22 | 11 | **33** |
| 17. | MAKINI | 32 | 11 | **43** |
| 18. | NLD | 7 | 2 | **9** |
| 19. | CCK | 11 | 6 | **17** |

*Chanzo: NEC, 2020*

## 4.5 KUSHUGHULIKIA RUFAA

Sheria na kanuni za uchaguzi zinaruhusu kukata rufaa endapo mgombea hakubaliani na uamuzi wa Tume. Rufaa hizi huwa zinashughulikiwa na vyombo vya juu vya Tume. Tume illipokea rufaa 616. Kati ya rufaa hizo 160 zilihusu uchaguzi wa ubunge na rufaa 456 zilihusu uchaguzi wa udiwani. Kati ya rufaa 160 za ubunge zilizoamuliwa na Tume, wagombea 66 walirudishwa, 32 waliondolewa na rufaa za wagombea 57 zilikataliwa. Rufaa tano zilikuwa zimejirudia. Baadhi ya sababu za kukata rufaa na kuweka pingamizi zilikuwa kukwepa kodi, ujazaji mmbovu wa fomu za uteuzi na idadi pungufu ya wadhamini kinyume na matakwa ya sheria. Rufaa na pingamizi dhidi ya wagombea wa vyama vya upinzani vilipelekea kuwepo kwa idadi kubwa ya wagombea ubunge na udiwani wa CCM kupita bila kupingwa kuwahi kutokea katika historia ya mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania. Kwenye sehemu inayofuata tunaangalia suala la wagombea waliopita bila kupingwa.

## 4.6 WAGOMBEA WALIOPITA BILA KUPINGWA

Baada ya tarehe ya kuweka pingamizi na kukata rufaa kupita, wagombea ubunge 28 walipita bila kupingwa kulingana na kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Kulikuwa na malalamiko kutoka vyama vya upinzani kwamba CCM ilitumia Tume kupata viti kabla ya uchaguzi kufanyika. Wagombea wote waliopita bila kupingwa walikuwa wa Chama cha Mapinduzi (tazama Jedwali Namba 4.3). Wagombea udiwani waliopita bila kupingwa walikuwa 870 na wote walikuwa wa CCM.[16]

**Jedwali Na. 4.3: Wagombea Ubunge Waliopita bila Kupingwa**

| Na. | Jimbo | Jina | Chama cha Siasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Kongwa | Job Yustino Ndugai | CCM |
| 2. | Mafinga Mjini | Cosato David Chumi | CCM |
| 3. | Katavi | Isack Aloyce Kamwelwe | CCM |
| 4. | Mtama | Nape Moses Nnauye | CCM |
| 5. | Ruangwa | Majaliwa Kassim Majaliwa | CCM |
| 6. | Babati Mjini | Pauline Philipo Gekul | CCM |
| 7. | Babati Vijijini | Daniel Baran Sillo | CCM |
| 8. | Butiama | Jumanne Abdallah Sagini | CCM |
| 9. | Gairo | Ahmed Mabkhut Shabiby | CCM |
| 10. | Kilosa | Palamagamba John Kabudi | CCM |
| 11. | Mlimba | Godwin Emmanuel Kunambi | CCM |
| 12. | Morogoro Kusini | Innocent Edward Kalogeris | CCM |
| 13. | Morogoro Kusini-Mashariki | Hamisi Shabani Taletale | CCM |
| 14. | Mvomero | Jonas Van Zeeland | CCM |
| 15. | Misungwi | Alexander Pastory Mnyeti | CCM |
| 16. | Ludewa | Joseph Zacharius Kamonga | CCM |
| 17. | Lupembe | Edwin Enosy Swalle | CCM |
| 18. | Chalinze | Ridhiwani Jakaya Kikwete | CCM |
| 19. | Kalambo | Josephat Sinkamba Kandege | CCM |
| 20. | Madaba | Joseph Kizito Mhagama | CCM |
| 21. | Msalala | Iddi Kassim Iddi | CCM |
| 22. | Ushetu | Elias John Kwandikwa | CCM |

16 NEC 2020.

| Na. | Jimbo | Jina | Chama cha Siasa |
|---|---|---|---|
| 23. | Ileje | Eng. Godfrey Msongwe Kasekenya | CCM |
| 24. | Songwe | Philipo Augustino Mulugo | CCM |
| 25. | Ulyankulu | Rehema Juma Migilla | CCM |
| 26. | Nzega Vijijini | Dr. Hamisi Andrea Kigwangalla | CCM |
| 27. | Bumbuli | January Yusuf Makamba | CCM |
| 28. | Pangani | Jumaa Hamidu Aweso | CCM |

***Chanzo: NEC, 2020***

## 4:7 TATHMINI YA JUMLA YA MCHAKATO WA UTEUZI

Jedwali Namba 4.4. linaonesha kwamba kati ya watazamaji wa muda mrefu 200, watazamaji 88 (asilimia 44) walisema kwamba kwa ujumla teuzi zilikuwa huru na za haki. Kati yao, 85 (asilimia 42.5) walisema kwamba kwa ujumla teuzi zilikuwa huru na za haki lakini walibaini dosari chache ambazo zingeweza kuwaathiri baadhi ya wagombea. Ni watazamaji 22 wa muda mrefu (asilimia 10) ambao walisema kwamba teuzi ziligubikwa na uvunjifu wa taratibu na kanuni za uteuzi bila hatua kuchukuliwa na kwamba kulikuwa na upendeleo ambao ungeweza kuwaathiri baadhi ya wagombea.

**Jedwali Na. 4.4: Tathmini ya Mchakato wa Uteuzi**

| Asili na Mwenendo wa Teuzi | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Teuzi zilikuwa na mapungufu machache sana ambayo hayakuathiri matokeo ya jumla ya mchakato wa uteuzi. Mchakato ulikuwa safi, huru na wa haki. | 80-100 | A | 88 | 44.0 |
| Kwa ujumla, mchakato ulikuwa huru na wa haki lakini kulikuwa na mapungufu machache ambayo yangeweza kuwaathiri baadhi ya wagombea. | 60-79 | B | 85 | 42.5 |
| Mchakato uliruhusu ushiriki wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) lakini kulikuwa na uvunjifu mkubwa wa taratibu na kanuni za uteuzi bila hatua kuchukuliwa na kulikuwa na upendeleo ambao uliwaathiri baadhi ya wagombea. | 50-59 | C | 22 | 10.0 |

| Asili na Mwenendo wa Teuzi | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Teuzi ziligubikwa na dosari nyingi zilizohusu kutokunzingatiwa kwa baadhi ya taratibu na kanuni  Kulikuwa na matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 5 | 2.5 |
| Teuzi ziliingiliwa au kuendeshwa vibaya kiasi kwamba wadau hawakuwakubali watu walioteuliwa. Ilikuwa ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 1 | 0.5 |
| Uteuzi ulifanyika vibaya. Kulikuwa na upendeleo mwingi, dosari na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujiondoa kwenye mchakato huo wa upendeleo au kutoa malalamiko rasmi. Teuzi ziliharibika. | 0 | F | 1 | 0.5 |
| **Jumla** | | | **200** | **100.0** |

## 4.8 HITIMISHO

Sura hii imetazama uteuzi wa wagombea uliofanywa na vyama vya siasa na Tume. Kwa ujumla, REDET iliona kwamba uteuzi ulikuwa huru na wa haki. Pamoja na hilo, kulikuwa na malalamiko kadhaa na mapungufu kuhusu uteuzi wa wagombea nchi nzima. Malalamiko makubwa yalihusu kuondolewa kwa idadi kubwa ya wagombea wa upinzani, kitu ambacho hakijawahi kutokea, na kupelekea idadi kubwa ya wagombea wa CCM kupita bila kupingwa. Kuondolewa kwa wagombea wa upinzani kulileta wasiwasi na shaka kuhusu Tume kutokupendelea na kufanya kazi kama taasisi huru. Malalamiko mengine yalihusu namna baadhi ya vyama, hususan CCM na CHADEMA, vilivyowaacha wagombea walioshinda kura za maoni na kuwachukua waliopata kura chache. Mapungufu mengine yalihusu kukosekana taratibu na kanuni za uteuzi zinazozingatia jinsia. Ukiachilia mbali vifungu vinavyohusu viti maalumu, sheria za nchi na kanuni za vyama hazina vifungu maalumu kwa ajili ya kuhakikisha usawa wa kijinsia wakati wa kuteua wagombea. Kwa kiasi fulani, mapungufu haya ya kisheria yanaonesha kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika matokeo ya teuzi ambapo wagombea wa kiume walikuwa wengi zaidi ya wagombea wa kike. Nne, kitendo cha sheria kuwapa ushindi wa moja kwa moja wagombea waliopita bila kupingwa kinaibua maswali mengi. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wagombea ubunge 28 na wagombea udiwani 780 wa CMM walipita bila kupingwa na kuibua maswali na malalamiko kuhusu sheria.

# SURA YA TANO
# MWENENDO WA KAMPENI ZA UCHAGUZI

## 5.1 UTANGULIZI

Kampeni za uchaguzi ni sehemu ya mchakato wa uchaguzi kwani zinaruhusu wagombea na vyama vya siasa kuandaa na kunadi mawazo, ilani na misimamo yao kuhusu masuala mbalimbali kwa wapiga kura kipindi cha kuelekea siku ya uchaguzi. Tarehe za kufanya kampeni za uchaguzi rasmi zinapangwa na chombo cha kusimamia uchaguzi. Kwa kiasi kikubwa, kuaminika kwa uchaguzi kunategemea ni fursa gani sawa zinatolewa kwa wagombea na vyama vya siasa ili wafikishe ujumbe wao kwa wananchi ili wapiga kura wafanye uamuzi sahihi. Kampeni pia zinasaidia kushawishi wapiga kura na kuwafanya washiriki katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi, kama vile kujiandikisha na kupiga kura. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 uliofanyika nchini Tanzania kampeni za uchaguzi zilianza tarehe 26 Agosti 2020. Kwa maneno mengine, kampeni za uchaguzi ziliendeshwa kwa takribani miezi miwili hadi tarehe 27 Oktoba 2020.

Sura hii inachambua namna kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 zilivyofanyika. Imegawanyika katika sehemu kumi, pamoja na hii ya utangulizi. Sehemu ya Pili inahusu mfumo wa kisheria na kitaasisi unaosimamia kampeni za uchaguzi. Sehemu ya Tatu inaangalia gharama za kamapeni na Sehemu ya Nne inahusu kanuni za kampeni za nyumba kwa nyumba au mtaa kwa mtaa na maadili ya uchaguzi. Mtiririko wa kampeni, taratibu na mikakati inatazamwa katika Sehemu ya Tano. Sehemu ya Sita inahusu matukio hasi ya kampeni za uchaguzi na Sehemu ya Saba inaangalia ilani za uchaguzi. Sehemu ya Nane inahusu mipango ya kiusalama na utendaji wa polisi na Sehemu ya Tisa inafanya tathmini ya jumla ya kampeni za uchaguzi. Sehemu ya Kumi inatoa hitimisho.

## 5.2 MIFUMO YA KISHERIA NA KITAASISI INAYOSIMAMIA KAMPENI

Nchini Tanzania kampeni za uchaguzi zinasimamiwa na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 (sehemu ya VI); Kanuni za Taifa za Uchaguzi za mwaka 2020 [Uchaguzi wa Rais na Wabunge]; Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020 [Uchaguzi wa Madiwani]; Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010; na Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 (yaliyoandaliwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343). Kabla ya marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, maadili ya uchaguzi

hayakuwa na meno. Baada ya marekebisho ya mwaka 2010 imekua ni lazima kwa vyama vyote vya siasa, wagombea, Tume na serikali kuzingatia maadili hayo. Ili kutekeleza Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020, Tume iliunda kamati za maadili ya uchaguzi ili kuyatekeleza, yaani Kamati ya Rufaa, Kamati ya Kitaifa, Kamati za Ngazi ya Jimbo na Kamati za Ngazi ya Kata. Kamati hizi zilijumuisha wawakilishi kutoka Tume, vyama vya siasa na serikalini.

Pamoja na mambo mengine, lengo la sheria hizi ni kusimamia mwenendo wa kampeni za uchaguzi ili kuhakikisha kuna usawa na uchaguzi unakuwa huru, wa haki na wa kuaminika. Kifungu cha 51 (vifungu vidogo vya 1 hadi 6) na kifungu cha 53 (vifungu vidogo vya 1 hadi 4) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 (sehemu ya VI) vinatoa mwongozo kwa ajili ya kufanya mikutano ya kampeni ya amani na isiyo na vurugu. Pia, vinatoa haki ya kutumia vyombo vya habari vya umma kwa wagombea na vyama vya siasa kipindi cha kampeni rasmi za uchaguzi. Kanuni za Kitaifa za Uchaguzi za mwaka 2020 (Uchaguzi wa Rais na Wabunge) za mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2020 [Uchaguzi wa Madiwani] za mwaka 2020 zimerahisisha sheria za uchaguzi. Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 inaelezea namna ya kugharamia kampeni za uchaguzi ili kudhibiti matumizi ya fedha na vitendo vilivyokatazwa katika kampeni za uchaguzi na uchaguzi.

Kifungu cha 15 (vifungu vidogo vya 1 hadi 2) kinavitaka vyama vya siasa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu fedha zote (misaada, mikopo, amana au michango) zilizotolewa na chama, kikundi cha watu au mtu. Kifungu cha 17(3) kinasema kwamba "bodi ya wadhamini ya chama cha siasa itapeleka kwa Msajili matumizi ya kila mgombea aliyedhaminiwa na chama hicho ndani ya siku 90 baada ya uchaguzi kumalizika ili kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1) na kuonesha kiasi alichopatiwa kila mgombea." Kifungu cha 21(1) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kinakataza vitendo visivyo vya haki kama matumizi ya fedha ambayo hayaeleweki (rushwa, kutoa zawadi na ahadi). Hata hivyo, sheria ina dosari kwani inaacha mwanya kwa wagombea waovu. Kifungu cha 21(2) kinasema kwamba "pale ambapo kitendo kilichokatazwa kinafanywa na wakala au mtu mwingine yeyote yule kwa niaba ya mgombea, mgombea hatakuwa na hatia endapo atasema kwamba kitendo hicho kilifanyika bila yeye kuwa na taarifa au kuridhia au bila wakala wake kuwa na taarifa au kuridhia." Watu wa aina hiyo wanaweza kutumia mwanya huu kujitetea. Utekelezaji wa sheria za uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania ulihusisha taasisi kadhaa.

Taasisi hizo ni Tume, Msajili, Jeshi la Polisi na Kamati za Maadili ya Uchaguzi.

## 5.3 KUGHARAMIA KAMPENI ZA UCHAGUZI – UTEKELEZAJI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Gharama za uchaguzi zinasimamiwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010. Kifungu cha 7(1) kinasema kwamba gharama za uchaguzi ni fedha zote zilizotumika au gharama zote zilizoingiwa na chama cha siasa, mgombea au serikali katika kuendesha na kusimamia mchakato wa kuteua wagombea, kampeni za uchaguzi na uchaguzi. Kwa hiyo, gharama za uchaguzi zinazotajwa kwenye sheria zinajumuisha gharama zote zinazohusiana na mchakato wa kuteua wagombea, uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi na gharama zingine zinazojitokeza wakati wa uchaguzi, pamoja na kulipa vikundi vya sanaa, kununua chakula, vinywaji, malazi na usafiri (kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010).

Kwa upande wa Tanzania Bara, Sheria ya Gharama za Uchaguzi inadhibiti matumizi ya fedha yanayofanywa na vyama vya siasa na wagombea urais wa Jamhuri wa Muungano, ubunge na udiwani. Kwa upande wa Zanzibar, sheria hiyo inadhibiti matumizi ya fedha yanayofanywa na vyama vya siasa na wagombea urais na ubunge wa Jamhuri ya Muungano. Usimamizi na utekelezaji wa sheria hiyo upo mikononi mwa Msajili wa Vyama vya Siasa (kifungu cha 4 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010). Kifungu cha 10(a) cha sheria hiyo kinampa Waziri anayehusika na masuala ya vyama vya siasa mamlaka ya kuweka ukomo wa fedha inayoweza kutumika katika uchaguzi kwa kuchapisha amri kwenye Gazeti la Serikali. Kiwango cha juu kinategemea tofauti ya ukubwa wa jimbo, aina ya wagombea, idadi ya watu na miundombinu ya mawasialiano. Chama cha siasa kinachotumia zaidi ya fedha inayoruhusiwa kinafanya kosa na kinaweza kutozwa faini ya hadi shilingi milioni tatu; kama ni mgombea faini yake haizidi shilingi milioni moja na kama ni asasi, shirika au taasisi ni faini isiyozidi shilingi milioni tano (kifungu cha 26).

Kuhusu utekelezaji wa sheria katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, REDET iliona masuala kadhaa. Moja ni kwamba kulikuwa na makadirio ya gharama za uchaguzi kwa kila jimbo. Maofisa kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa waliwasiliana na Wasimamizi wa Uchaguzi na Maafisa Uchaguzi kwenye majimbo yao kabla ya kwenda kwa vyama vya siasa na kuwapa fomu za gharama za uchaguzi ili zijazwe na vyama vya siasa na wagombea husika. Hata hivyo, ilidhihirika kwamba Ofisi ya Msajili haikuwa na uwezo wa kufuatilia vizuri utekelezaji wa

sheria hiyo kwa sababu ina wafanyakazi wachache. Mathalani, Ofisi ya Msajili ilipeleka ofisa mmoja kwenye Mkoa wa Mara kufuatilia utekelezwaji wa sheria hiyo na vyama vya siasa na wagombea. Mkoa wa Mara una majimbo 10 na vyama vya siasa kadhaa vinavyoshindana kwenye kila jimbo. Matokeo yake ni kwamba ofisa kutoka Ofisi ya Msajili muda wote alikuwa anasafiri kutoka jimbo moja hadi lingine kiasi kwamba watazamaji wote nane wa muda mrefu waliokuwa mkoani humo hawakuonana naye ingawa jitihada zilifanyika (Ripoti ya Mtazamaji wa Mkoa wa Mara, 2020).

Mbili na suala linalohusiana na hilo, mbinu za kukusanya taarifa zilikuwa dhaifu. Kama sheria inavyosema Msajili wa Vyama vya Siasa anategemea taarifa inayotolewa na vyama vya sisasa, wagombea na bodi ya wadhamini. Wakati mwingine taarifa hii haipelekwi kwa Msajili kama sheria inavyotaka. Kwa mfano, makatibu wa wilaya wa ACT-Wazalendo wa majimbo ya Musoma Mjini na Tarime Mjini walisema kwamba Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haikuchukua hatua zinazohitajika ili kukusanya fomu za gharama za uchaguzi kutoka kwao kama sheria inavyotaka. Hii inaonesha utayari wa chama cha siasa kufanya taarifa zao kuhusu fedha zihakikiwe na inaonesha pia ukosefu wa uwezo kwa upande wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Tatu, makadirio ya gharama za uchaguzi yaliyowekwa na Waziri kwenye majimbo husika yalikuwa chini mno. Kwenye majimbo mengi kiwango cha juu ambacho wagombea ubunge waliruhusiwa kutumia ni shilingi milioni 30. Vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine waliona kwamba kiwango hicho hakikuendana na uhalisia na kisingeweza kutosha kugharamia matumizi ya lazima kama magari ya matangazo, usafiri, chakula na gharama zingine kwa miezi miwili ya kampeni za uchaguzi. Tutaona kama vyama vyote vya siasa na bodi zao za wadhamini vilizingatia sheria kwa kupeleka taarifa za matumizi ndani ya siku 180 baada ya uchaguzi kumalizika.

## 5.4 KANUNI NA MAADILI YA UCHAGUZI

Tarehe 5 Juni 2020, Tume ilichapisha Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa [Uchaguzi wa Madiwani] za mwaka 2020 kwenye Gazeti la Serikali Namba 401 na Kanuni za Uchaguzi [Uchaguzi wa Rais na Wabunge] za mwaka 2020 kwenye Gazeti la Serikali Namba 402. Siku hiyohiyo Tume ilichapisha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 kwenye Toleo la Sheria za Ziada Namba 23 la Gazeti la Serikali. Sheria zote zinavitaka vyama vya siasa, wagombea

na timu zao za kampeni kufanya kampeni za amani na kistaarabu.

Kwa ujumla maadili ya uchaguzi yalivunjwa kwa kiasi fulani na vyama vya siasa, wagombea na timu zao za kampeni. Utazamaji wa REDET unaonesha kwamba watazamaji 132 wa muda mrefu kati ya watazamaji 200 (asilimia 66) walitoa taarifa juu ya kutokea kwa matukio yanayokatazwa na sheria (kanuni na maadili ya uchaguzi). Kwenye majimbo kadhaa ratiba ya kampeni haikufuatwa na wagombea ubunge na udiwani. Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 zinaeleza kwamba vyama vya siasa vinavyotaka kubadilisha maeneo ya kampeni au ratiba ni lazima vitoe taarifa mara moja kwa Mkurugezi wa Uchaguzi [kwa upande wa wagombea urais] na Msimamizi wa Uchaguzi [kwa upande wa wagombea ubunge] wakitoa sababu za kutaka kufanya mabadiliko hayo. Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi wanapaswa, kabla ya kufanya uamuzi, kuitisha mkutano wa vyama vya siasa au wagombea wanaohusika ili kukubaliana juu ya suala hilo. Watazamaji wa uchaguzi wa muda mrefu walishuhudia mabadiliko ya maeneo na ratiba ya kampeni yaliyofanywa na vyama vya siasa na wagombea bila Wasimaizi wa Uchaguzi kupewa taarifa.

Kitu kingine ambacho watazamaji wa muda mrefu walikishuhudia ambacho kinaonesha uvunjifu wa Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 kinahusu kifungu cha 2.1(k) kinachovitaka vyama vya siasa na wagombea kuhakikisha kwamba mikutano ya kampeni inafanyika kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, wagombea urais, ubunge na udiwani, timu zao za kampeni na viongozi wa vyama walitumia lugha za asili. Kiwango cha kutumia lugha za asili kilikuwa kikubwa kwenye mikoa ya kanda ya ziwa (watazamaji wa muda mrefu wa Mikoa ya Simiyu, Kagera, Geita, Oktoba 2020), hususan kwenye mikutano ya kampeni ya wagombea urais. Kifungu cha 2.1(1) kinakataza vyama vya siasa na wagombea kufanya kampeni za uchaguzi kwenye nyumba za ibada na kutumia viongozi wa dini kuwafanyia kampeni. Hata hivyo, watazamaji wa muda mrefu wa REDETwalibaini uvunjaji wa mara kwa mara wa kifungu hiki kwenye majimbo mengi.



***Mgombea urais wa CHADEMA Ndugu Tundu Lissu na Askofu Emaus Mwamakula wa Kanisa la Ufufuo la Moravian nchini Tanzania walifanya mikutano mingi ya kampeni za uchaguzi pamoja.***



***Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Alhad Mussa Salum akimpigia kampeni mgombea urais wa CCM Dkt. John Magufuli katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, tarehe 9 Oktoba 2020.***

Uvunjifu mwingine wa kanuni na maadili ya uchaguzi ulihusisha matumizi ya wanamgambo/walinzi wa vyama unaokatazwa na sheria. Hii ilishuhudiwa kwa kiasi

kikubwa na watazamaji wa muda mrefu wa mikoa ya Manyara, Arusha na Ruvuma (CCM ilitumia walinzi wao wajulikanao kama "green guards" na CHADEMA ilitumia "red brigade"). Watazamaji wa muda mrefu wa mikoa ya Ruvuma na Katavi walishuhudia vurugu na vitisho mara nyingi. Kitu kingine kilichojitokeza ni kutozingatiwa kwa muda wa kufanya kampeni za uchaguzi. Sheria inasema kwamba mikutano ya kampeni ianze saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni. Watazamaji wa muda mrefu walishuhudia mikutano mingi ya kampeni ikifanyika baada ya saa kumi na mbili jioni.

## 5.5 MATUMIZI YA FAIDA YA KUWA MADARAKANI

Matumizi ya faida ya kuwa madarakani yalipingana na kanuni inayotaka uwanja sawa kwani chama tawala kilitumia rasilimali za nchi wakati wa kampeni, hususan mgombea wake wa urais. Mathalani, mgombea huyo alitoa ahadi na kufanya maamuzi kama Rais wakati wa kampeni zake za uchaguzi na kufanya iwe vigumu kuweka mpaka kati ya ugombea wake na urais wake. Baadhi ya matukio makubwa yaliyotokea kipindi cha kampeni za uchaguzi ni kumwalika Rais wa Uganda Museveni siku ya terehe 13 Septemba 2020. Wakati wa ugeni huo, Museveni na Magufuli walisaini taarifa ya pamoja kuhusu upatanishaji wa masuala mengi mtambuka yanayohusu ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 3.5 katika uwanja wa ndege wa Chato. Rais Museveni alimpigia kampeni mgombea urais wa CCM, John Magufuli. Alisema hivi: "Nafahamu kwamba sasa hivi Rais anatafuta kura. Nitamwombea na nitawaombea wagombea wote wa CCM. Nawatakia ushindi usio na shaka" (*Daily News*, Jumatatu, 14 Septemba 2020).

Wakati anafanya kampeni kwenye jimbo la Ubungo, mgombea urais wa CCM alitoa amri ya soko la Mabibo lijulikanalo kwa jina la Mahakama ya Ndizi kuwekwa chini ya himaya ya watu na siyo Kiwanda cha Nguo cha Urafiki. Alisema kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo sasa wanapaswa kuwa na vitambulisho vya machinga vinavyogharimu shilingi 20,000 kwa mwaka (*The Citizen*, Jumatano, 14 Oktoba 2020). Vivyo hivyo, tarehe 13 Oktoba 2020 Rais Magufuli alipokea gawio la shilingi bilioni 100 kutoka Kampuni ya Madini ya Serikali (STAMICO) katika tukio lililotangazwa (*The Citizen*, Jumatano, 14 Oktoba 2020). Mgombea huyo alizindua miradi kadhaa kama Rais wa nchi.

Baadhi ya Mawaziri walitekeleza majukumu yao kwenye majimbo yao na kwa hiyo kuongeza uwezekano wa wao kuchaguliwa tena kwa kutumia faida ya kuwa

madarakani. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na mgombea ambaye alikuwa anatetea kiti chake kupitia CCM kwenye jimbo la Kisarawe alipokea vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi milioni 17 kwa ajili ya ujenzi wa shule Wilayani Kisarawe kutoka NMB tarehe 22 Septemba 2020.



Minister Jafo says delivery by NMB of 17m/- building materials to Kisarawe schools timely

Maelezo ya picha yanasema: Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Jokate Mwegelo (kushoto) akitoa shukran kwa Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB Benedict Baragomwa (wapili kulia) baada ya kupokea mabati yenye thamani ya shilingi milioni 17 kwa ajili ya shule za umma wilayani kwake huku Waziri Selemani Jafo (wa pili kushoto) na Meneja wa Kanda ya Mashariki wa NMB Dismas Prosper wakishuhudia. Picha kwa hisani ya NMB.

## 5.6 MBINU NA MIKAKATI YA KAMPENI

Nchini Tanzania kampeni za uchaguzi zinaratibiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa Kanuni za Serikali za Mitaa [Uchaguzi wa Madiwani] za mwaka 2020, vifungu vya 36 na 37 na vifungu vya 41, 42, 43 na 44 vya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 Tume inapaswa kuhakikisha kwamba kampeni za uchaguzi zinakwenda vizuri. Ili kufikia lengo hilo, kwa kushirikiana na vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi Tume iliandaa ratiba ya kampeni kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Mbinu na mikakati mingi ilitumika. Ilijumuisha mikutano ya kampeni, kampeni za nyumba kwa nyumba, mitandao ya kijamii, jumbe fupi za simu, vyombo vya

habari, matumizi ya watu maarufu – hususan kutoka katika tasnia ya muziki na burudani, mabango, vipeperushi, wanamuziki wa muziki wa asili na magari ya matangazo. Mikutano ya kampeni za uchaguzi ilitumika zaidi katika kampeni za urais zikifuatiwa na kampeni za ubunge. Waandaji wa kampeni na watengenezaji mikakati waliandaa kampeni ambazo zingeweza kuwavutia watu wengi. Maandalizi hayo yalihusisha gharama, kwa mfano gharama ya magari ya matangazo yenye vipaza sauti ili kuwafanya watu wahudhurie mikutano ya kampeni za uchaguzi. CCM na CHADEMA, vyama ambavyo vilikuwa vinashindana, vilifanya mikutano ya kampeni za uchaguzi yenye manufaa sana.

Moja ya mbinu zilizozaa matunda kwa kiasi kikubwa ambazo timu ya kampeni ya CCM ilizitumia ili mgombea urais wao na mgombea mwenza wake wapate watu wengi katika mikutano yao ni kutumia watu maarufu, hususan wanamuziki wanaopendwa ambao walitumbuiza katika kampeni zao. Mkakati huu uliwapa watu fursa ya kuwaona wasanii wa *Bongo Fleva* wakitumbuiza katika majukwaa huku wakisikiliza jumbe za kisiasa. Watu wengine maarufu waliotumbuiza katika mikutano ya kampeni ya CCM walikuwa wachekeshaji na waigizaji kutoka *Bongo Movie*. CCM iliweza kuingia gharama hizo kwa sababu ndiyo chama kikongwe na chenye rasilimali za kutosha ukilinganisha na vyama vingine.



***Mgombea urais wa CCM Dkt. John Magufuli akimvalisha msanii wa Bongo Fleva Diamond Platnumz kofia yake baada ya Diamond kutumbuiza katika mkutano wake wa kampeni uliofanyika Mwanza tarehe 7 Septemba 2020.***

Kampeni za nyumba kwa nyumba zilifanywa zaidi na baadhi ya vyama vya siasa na wagombea wake. Katika kufanya aina hiyo ya kampeni CCM na CHADEMA zilivishinda vyama vingine vya siasa kwani vilionesha umakini, uwezo na uharaka wa kuwafikia kuwashawishi watu wawapigie kura. Kwa mfano, CHADEMA ilikuwa na mpango mkakati wa kupeleka watu waliojitolea – hususan vijana – kufanya kampeni kwenye mitaa na kata maalumu kila siku Mkoani Mara (Ripoti ya Mtazamaji wa Mkoa wa Mara, 2020). Kampeni za nyumba kwa nyumba zilisaidia kuimarisha mikutano ya kampeni za uchaguzi. Timu za kampeni za CHADEMA, ACT-Wazalendo Zanzibar na CCM zilikuwa na wazungumzaji wazuri sana. Kwa asilimia kubwa vyama vingine vya siasa havikuwa na vifaa na rasilimaliwatu na kwa hiyo hawakufanya kampeni za nyumba kwa nyumba kwa kiasi kikubwa.

Mitandao ya kijamii kama Facebook, Twitter na Instagram ilitumiwa kwa kiasi kikubwa na ilipendwa na vijana. Chaneli za Youtube zilitangaza mikutano ya kampeni mubashara. WhatsApp ambayo inatumika sana kutuma jumbe fupi za maneno na jumbe za kawaida ilitumika kwa kiwango kikubwa na vyama viwili vilivyoongoza ili kuwashawishi watu wawapigie kura.

Suala moja lililojitokeza zaidi kuhusiana na mabango yaliyowekwa katika barabara kuu nchi nzima. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 mabango yote yalibeba picha ya mgombea urais wa CCM, Dkt. John Magufuli. Hali hii ilikuwa tofauti na hali iliyokuwapo mwaka 2015 na kampeni za chaguzi zilizotangulia tangu 1995 ambapo wagombea wa upinzani pia waliweka mabango ya kutosha katika barabara kuu. Kwa kiasi kikubwa mabango kitita yalitumika katika mikutano ya kampeni za uchaguzi na yalionesha mafanikio ya wagombea (kwa wale waliokuwa wanatetea viti vyao) na masuala ya msingi ambayo yalikuwa ni vipaumbele vya wagombea ambao hawakuwa madarakani. Mabango yalitumika kwa kiasi kikubwa na yaliwekwa katika kuta, madaraja na miti. Vipeperushi vilisambazwa katika mikutano ya kampeni na kaya. Magari ya matangazo ya wazi ambayo yalitumika kutangaza na kuwafanya watu wahudhurie mikutano ya kampeni ya CCM yalibeba wasanii ambao waliburudisha watu. Kabla na wakati wa mikutano ya kampeni wacheza muziki waliombwa kuburudisha umma.



*Mwenyekiti wa TLP, Ndugu Augustine Mrema, akizungumza wakati wa kampeni ya mgombea urais wa CCM aliposimama katika kampeni zake huko Himo.*

## 5.7 KAMPENI HASI

Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 yanakataza kampeni hasi. Hata hivyo, kampeni hasi zilifanyika katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kampeni hasi zilifanywa zaidi katika mikutano ya kampeni ya CCM na CHADEMA na zilihusisha kumshambulia mtu, kujenga hofu, kusambaza uongo, kuharibu vifaa vya kampeni, vurugu na ukabila. Kumshambulia mtu ni moja ya aina kuu ya kampeni hasi iliyotumika katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Wagombea, timu za kampeni na vyama vya siasa zilitumia lugha hasi dhidi ya wapinzani wao ili kuwachafua. Mathalani, kwenye majimbo ya Geita Mjini, Bunda na Tarime Mjini wagombea ubunge na udiwani wa kike walitukanwa na wagombea wa kiume. Matusi hayo yalihusu hali zao za ndoa ambazo walidai zingewafanya wawe viongozi wazuri. Watazamaji wa muda mrefu wa majimbo ya Geita Mjini, Bunda na Tarime Mjini walisema kwamba Upendo Peneza, Ester Bulaya na Esther Matiko (wagombea ubunge wa kike) waliitwa 'malaya' na wagombea wa kiume (Ripoti za Watazamaji wa REDET za Geita, Bunda na Tarime, 2020).

## 5.8 MATUKIO HATARISHI WAKATI WA KAMPENI ZA UCHAGUZI

Watazamaji wa muda mrefu walifundishwa namna ya kufuatilia kwa karibu na kutoa taarifa kuhusu matukio hatarishi yaliyojitokeza wakati wa kampeni. Matukio ambayo yalikuwa hatarishi ni yale ambayo yalikuwa na athari hasi katika mwenendo wa kampeni za uchaguzi kama vile vitendo vya rushwa, uharibifu wa vifaa vya

kampeni, kuwanyima wengine sehemu za kufanyia kampeni, kuingilia mikutano ya kampeni ya watu wengine, vitisho, kusambaza uongo na vurugu. Kama Jedwali Namba 5.1 linavyoonesha, tukio hatarishi lililoripotiwa sana lilihusu matumizi ya lugha ya kibaguzi dhidi ya wagombea, vyama vya siasa au wafuasi.

**Jedwali Na. 5.1: Matukio Hatarishi**

| Maswali | Majibu | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (asilimia) |
| Je, ulishuhudia matukio yeyote yanayoonesha au kuashiria vitendo vya rushwa wakati wa kampeni za uchaguzi? | 107 (2.1) | 5024 (97.9) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia matukio yeyote yanayoonesha au kuashiria kwamba wagombea walihonga watu? | 171 (3.3) | 4960 (96.7) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia watu wakisafirishwa na vyama vya siasa kwenda kwenye mikutano ya kampeni? | 511 (10.0) | 4620 (90.0) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia matukio ambayo wapiga kampeni au wazungumzaji walizomewa, kutukanwa au kushambuliwa? | 41 (0.8) | 5090 (99.2) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia matumizi ya lugha ya unyanyasaji dhidi ya wagombea (kwa sababu ya kabila, rangi au dini ya mtu)? | 10 (13.3) | 65 (86.7) | **75 (100)** |
| Je, ulishuhudia usambazaji wa habari za uongo kuhusu mchakato wa kampeni za uchaguzi? | 6 (8) | 69 (92) | **75 (100)** |
| Je, ulishuhudia wafuasi wa vyama wakishambuliana/kupigana wakiwa njiani kuelekea kwenye sehemu za kufanyia kampeni za uchaguzi? | 4 (5.3) | 71 (84.7) | **75 (100)** |
| Je, ulishuhudia wafuasi wa vyama wakishambuliana/kupigana baada ya kuondoka kwenye maeneo ya kampeni za uchaguzi? | 7 (9.3) | 68 (90.7) | **75 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET , 2020*

## 5.9 ILANI ZA UCHAGUZI: AJENDA NA MASUALA

Ilani za uchaguzi ni muhimu kwani zinaonesha ahadi ambazo wanasiasa wanazitoa kwa wapiga kura. REDET ilishuhudia vyama vichache vya siasa vikizindua ilani za uchaguzi. Sehemu hii inalinganisha vyama vinne vya siasa (CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, na CUF) kuhusu masuala manne: kilimo, rushwa, elimu na madini.

### 5.9.1 Kilimo

Moja ya masuala manne ambayo vyama vya siasa vilielezea kwa msisitizo tofauti ni kilimo. Masuala yalitofautiana kati ya CCM ambayo ilisisitiza kilimo cha umwagiliaji na biashara, ACT-Wazalendo ambayo ilisisitiza utafiti na CHADEMA ambayo iliahidi kuwapa wakulima bima, kama Jedwali Namba 5.2 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 5.2: Ilani za Uchaguzi na Kilimo**

| Chama cha Siasa | Maeneo ya Kipaumbele na Masuala ya Msingi ya Kuyafanyia Kazi |
|---|---|
| CCM | • Ilitaka kupanua miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekari 561,383 hadi hekari milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025;<br>• Kuanzisha mfuko wa umwagiliaji wa taifa;<br>• Kuihimiza sekta binafsi iwekeze kwenye kilimo cha kisasa cha kibiashara;<br>• Kuanzisha vitalu vya mashamba kwa ajili ya kulima mazao ya kimkakati yanayohitajika sana; na<br>• Kuwahakikishia wakulima kwamba watapatiwa huduma za kilimo za kisasa, uhakika wa masoko na bei nzuri za mazao yao. |
| ACT-Wazalendo | • Ingetenga asilimia 20 ya bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kilimo, ufugaji na uvuvi;<br>• Kuwekeza shilingi bilioni 100 kwenye utafiti na mbegu;<br>• Kuanzisha mamlaka ya kilimo kwa ajili ya kusimamia sekta hiyo;<br>• Kubaini aina ya mazao ya kimkakati kwa kila mkoa au kanda;<br>• kuanzaisha mfuko maalumu wa kilimo ili kutoa ruzuku kwa ajili ya miradi ya kilimo ya kimkakati; na<br>• kuimarisha huduma za benki ya kilimo. |
| CHADEMA | • Kuhakikisha kuna soko la uhakika la mazao;<br>• Kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kusindika mazao;<br>• Kuanzisha bima ya wakulima;<br>• Kundoa vikwazo vya kuuza mazao; |
| CUF | • Kutenga asilimia 10-15 ya bajeti yote ya serikali kwa ajili ya sekta ya kilimo;<br>• Kuimarisha utafiti na huduma za mabwana na mabibi shamba;<br>• Kuwawezesha wakulima kwa kuwatafutia masoko mazuri ya kimataifa; na<br>• Kutengeneza mazingira mazuri ili wakulima wafanye kilimo mseto. |

*Chanzo: Ilani za Uchaguzi, 2020*

### 5.9.2 Rushwa

Ingawa CCM ilifanya kampeni kwa kutumia jukwaa imara la vita dhidi ya rushwa na jitihada ya kuimaliza, vyama vyote vikuu vya siasa vilitoa ahadi kuhusu mapambano dhidi ya rushwa. Kama Jedwali Namba 5.3 linavyoonesha, hatua zilizofikiriwa na vyama ni kuongeza uwazi, kuhusisha jamii, mfumo rafiki wa ulipaji kodi na kuongeza mishahara ya watumishi wa umma.

**Jedwali Na. 5.3: Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Rushwa**

| | |
|---|---|
| CCM | • Kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa;<br>• Kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU);<br>• Kuhamasisha na kushirikisha jamii kwenye vita dhidi ya rushwa; na<br>• Kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali ya kazi. |
| ACT-Wazalendo | • Kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kuhakikisha kwamba mkurugenzi wake anapitishwa na Bunge;<br>• Kuongeza uwazi katika shughuli za serikali; na<br>• Kujenga uelewa miongoni mwa wananchi kuhusu rushwa na namna wanavyoweza kushirki katika kuzuia. |
| CHADEMA | • Kuzuia mikataba inayohusisha rushwa kwa kukumbatia uwazi kwenye mchakato wa kuingia mikataba;<br>• Kuhakikisha kwamba mikataba yote inapitishwa na Bunge; na<br>• Kutengeneza mfumo rafiki wa ulipaji kodi ambao hauwafanyi walipakodi wajihusishe na vitendo vya rushwa. |
| CUF | • Kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kuiruhusu ifungue kesi bila kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka wa Umma;<br>• Kuwatangaza hadharani watu wenye makosa ya rushwa; na<br>• Kuongeza mishahara ya watumishi wa umma ili wasishawishike kufanya vitendo vya rushwa. |

*Chanzo: Ilani za Uchaguzi*

### 5.9.3 Elimu

Elimu ni suala lingine lililotawala ilani za uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na lililosababisha mjadala mkali. Ulinganishaji wa ilani za vyama vinne vya siasa kuhusu elimu unaoneshwa katika Jedwali Namba 5.4. CCM ilijivunia mafanikio iliyoyapata kuanzia mwaka 2015, CHADEMA ilizungumzia masilahi ya walimu na ACT-Wazalendo ilisema ingetoa elimu bure kwa wanafunzi

wa kada ya afya.

**Jedwali Na. 5.4: Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Elimu**

| | |
|---|---|
| CCM | • Kuendelea na jitihada za kuimarisha utoaji elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita;<br>• Kuboresha programu za elimu ya ufundi;<br>• Kuongeza rasilimali watu kwenye taasisi za elimu ya juu; na<br>• Kuboresha viwango vya elimu katika ngazi zote kwa kusisitiza kujitegemea. |
| ACT-Wazalendo | • Kutoa elimu bora shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya afya;<br>• Kujenga madarasa 24,000 kila mwaka ili kuendana na idadi ya wanafunzi inayoongezeka; na<br>• Kuzalisha walimu takribani 20,000 kila mwaka kwa kuongeza udahili katika vyuo vya ualimu. |
| CHADEMA | • Kushughulikia masilahi ya walimu;<br>• Kuhakikisha kwamba watu wote wanaostahili kuingia vyuo vikuu wanapata mikopo bila ubaguzi; na<br>• Kupunguza kiwango cha kurejesha mikopo na kuongeza muda wa kulipa hadi miaka 25 tangu mkopaji apate ajira. |
| CUF | • Kushughulikia hali za walimu;<br>• Kuongeza mishahara ya walimu; na<br>• Kutenga asilimia 25 ya bajeti ya taifa kila mwaka kwa ajili ya sekta ya elimu. |

*Chanzo: Ilani za Uchaguzi*

### 5.9.4 Madini

Kwa muda mrefu sekta ya madini iliachwa bila udhibiti au ufuatiliaji. Serikali ya awamu ya tano ilionesha kwamba sekta hiyo inaweza kuwa chanzo cha mapato. Ingawa ilani ya CCM ilionesha kuna maboresho yaliyofanyika kwenye mazingira ya uwekezaji, CUF ilisisitiza uwekezaji kwenye kuchenjua madini, suala ambalo hata CCM ililisisitiza.

**Jedwali Na. 5.5: Ulinganishaji wa Ilani za Vyama Kuhusiana na Sekta ya Madini**

| | |
|---|---|
| CCM | • Kuendelea kuboresha mazingira ili kuvutia uwekezaji zaidi;<br>• Kuimarisha kanuni na usimamizi wa uchimbaji madini wa kati na wa juu;<br>• Kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo; na<br>• Kuimarisha Kampuni ya Madini ya Serikali. |
| ACT-Wazalendo | • Kubadilisha mfumo wa umiliki;<br>• Kujenga mahusiano kati ya jamii na mwekezaji kwenye madini; na<br>• Kubadilisha miradi ya Mchuchuma na Liganga na machimbo ya nikeli ya Kabanga. |
| CHADEMA | • Kutumia madini kama dhamana ili kupata fedha za kugharamia miradi ya miundombinu na maji;<br>• Ushirikiano kati ya wazawa na wageni;<br>• Kuondoa kodi ili kupunguza gharama; na<br>• Kupitia sheria za madini ili ziendane na viwango vya kimataifa. |
| CUF | • Kubaini changamoto zinazoikabili sekta ya madini;<br>• Kuanzisha mazungumzo na wawekezaji wa ndani na wa nje ili kuweka mazingira yanayonufaisha pande zote mbili;<br>• Kuimarisha sheria za madini ili kuzuia udanganyifu;<br>• Kutoa ushuru kwa asilimia 100 katika kusafirisha madini; na<br>• Kuanzisha viwanda vya kuchakata madini. |

***Chanzo: Ilani za Uchaguzi***

Suala lingine lililojitokeza kwenye ilani za uchaguzi ni utengenezaji wa ajira. CCM iliahidi kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi na CHADEMA iliahidi kutengeneza ajira milioni 10 ndani ya miaka mitano. CHADEMA na ACT-Wazalendo waliahidi kupunguza kodi ya wafanyakazi ili kuongeza kipato cha wafanyakazi. REDET ilibaini kwamba ilani hizo za uchaguzi hazikuwa na tofauti kubwa za kiitikadi na masuala makubwa yalihusu maendeleo ya kiuchumi na utoaji huduma za jamii. Jedwali Namba 5.6 linaonesha kauli mbiu za vyama vya siasa.

**Jedwali Na. 5.6: Kauli mbiu Zilizotumiwa na Vyama vya Siasa Kuhamasisha Wapiga Kura**

| Na. | Chama cha Siasa | Kauli mbiu |
|---|---|---|
| | ACT-Wazalendo | • 2020! Kazi na Bata!<br>• ACT-Wazalendo! Taifa kwanza, leo na kesho! |
| | CCM | • Mshikamano Wetu! Ushindi Wetu!<br>• Hapa Kazi Tu!<br>• CCM Mbele kwa Mbele<br>• Tumetekeleza kwa Kishindo, Tunasonga Mbele Pamoja |
| | CHADEMA | • Hakuna Chuki Hakuna Hofu<br>• CHADEMA Vema!<br>• Uhuru, Haki na Maendeleo ya Watu |
| | CUF | • Haki na Usawa kwa Wote<br>• Asiyeijua haki??? Aelimishwee<br>• Haki sawa na Furaha kwa Wote |
| | NCCR-Mageuzi | • Kuwajibika ni Utu<br>• Pamoja Tutashinda |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Mwanzoni mwa mwezi Septemba 2020, Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, alimuonya mgombea urais wa CHAUMMA, Ndugu Hashim Rungwe, dhidi ya kuwashawishi watu wahudhurie mikutano yake ya kampeni kwa kuahidi kuwapatia ubwabwa. Afisa huyo wa TAKUKURU alisema kwamba kutoa chakula wakati wa kampeni za uchaguzi ni kuvunja Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010. Kwa upande wake, Rungwe alisema kwamba angetumia ubwabwa kuwashawishi watu wahudhurie mikutano yake ya kampeni kama ambavyo CCM ilivyokuwa inatumia wasanii (Millard Ayo, 5 Septemba 2020).

## 5:10 MIPANGO YA KIUSALAMA NA UTENDAJI WA POLISI

Ibara ya 3.1 (c) ya Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 inaeleza kwamba vyombo vya usalama vinapaswa kutoa ulinzi katika mikutano ya kampeni na mikusanyiko mingine ya kisiasa ili kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo. Kwa kiasi kikubwa, kampeni za uchaguzi za mwaka 2020 zilikuwa za amani, kama Jedwali Namba 5.7 linavyoonesha. Yalitokea matukio machache ya vurugu lakini Jeshi

la Polisi lilikuwa imara katika kuhakikisha usalama unakuwapo. Watazamaji wa REDET walisema kwamba kiwango cha usalama kilikuwa cha juu katika mikutano ya uchaguzi ya wagombea urais zaidi ya mikutano ya uchaguzi ya wabunge na madiwani. Mikutano ya kampeni ya CCM na CHADEMA ilikuwa na kiwango kikubwa cha usalama kwani ilivutia watu wengi zaidi ya mikutano ya vyama vya siasa vingine.

**Jedwali Na. 5.7: Utendaji wa Polisi katika Kampeni za Uchaguzi**

| Maswali | Majibu | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (asilimia) |
| Je, ulishuhudia polisi wakizuia mkutano wowote wa kampeni za uchaguzi? | 6 (8) | 69 (92) | **75 (100)** |
| Je, walikuwapo askari polisi waliovaa sare katika mikutano ya kampeni za uchaguzi? | 1385 (27.0) | 3749 (73.0) | **5131 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Kwenye mkutano na waandishi wa habari wa tarehe 26 Septemba 2020, mgombea urais wa CHADEMA aliwapongeza polisi kwa kufanya kazi ya ulinzi kwa weledi. Aliwapa sifa polisi kwa kuhakikisha usalama unakuwapo wakati wa mikutano yake ya kampeni kwenye mikoa ya Geita na Songwe. Wakati mwingine msafara wa CHADEMA ulirushiwa mawe na vikundi vya watu wasiojulikana kwenye Manispaa ya Bukoba, Katoro na Geita. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro alisema kwamba baadhi ya vijana waliurushia mawe msafara wa mgombea urais wa CHADEMA. Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya alichukulia tukio hilo kama kitendo cha vijana kumtaka mgombea urais wa CHADEMA aliyekuwa anakusanya sahihi za wadhamini aeleze sera zake. Msaidizi wa mgombea urais huyo Queen Sendiga alidai kwamba akiwa anaelekea kwenye eneo la mkutano wa kampeni katika kituo cha mabasi cha Iringa alipigwa kofi na dirisha la gari lake kuvunjwa na wafuasi wa chama pinzani ambacho hakukitaja (*Mtanzania*, Jumamosi, 17 Oktoba 2020). Siku ya Jumatano tarehe 19 Septemba 2020, polisi walivamia makazi ya mgombea ubunge wa CHADEMA wa jimbo la Singida Mjini na kumkamata mgombea huyo na watu wengine 10 wakidai kwamba alikuwa anamiliki silaha kinyume cha sheria (*The Guardian*, Ijumaa, 11 Septemba 2020).

REDET ilibaini kwamba pamoja na Jeshi la Polisi kupiga marufuku matumizi ya vikosi vya ulinzi binafsi, hususan “green guards” wa CCM na “red brigade” wa

CHADEMA, matukio machache ya ugomvi kati ya wagombea na wafuasi wao na polisi yalilipotiwa, lakini hayakuwa ya vurugu. Kwenye jimbo la Hai, malumbano kati ya mwenyekiti na mgombea ubunge wa CHADEMA Ndugu Freeman Mbowe na Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya terehe 7 Oktoba 2020 yalirekodiwa kwenye video. Tukio hilo halikusababisha vurugu zozote.




*Mlinzi binafsi wa mgombea ubunge wa CCM jimbo la Hai akiwa amevaa fulana yenye jina la Mkuu wa Wilaya ya Hai (Lengai ole Sabaya) wakati wa kuzindua kampeni za mgombea udiwani wa kata ya Boma Ng'ombe (Evod Njau) kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye viwanja vya Snow View tarehe 7 Oktoba 2020*

Kama tulivyokwishaeleza, kuna baadhi ya mikutano ya kampeni ilipitisha muda wa saa kumi na mbili kamili jioni. REDET ilishuhudia mikutano 466 ya kampeni kati ya mikutano 5,131 (asilimia 9) iliyopitisha muda. Pamoja na uvunjaji huo wa ratiba ya kampeni, kwa ujumla polisi walivumilia na kwa hiyo kuzuia kutokea kwa mapambano ambayo yangeweza kutokea iwapo wangeingilia kati. Kati ya matukio hatarishi 75 yaliyojitokeza, sita (sawa na asilimia saba) yalihusisha polisi kuzuia mikutano ya kampeni.

## 5.11 TATHMINI YA JUMLA YA KAMPENI ZA UCHAGUZI

Tathmini ya jumla ya kampeni za uchaguzi iliyofanywa na REDET inaonekana katika Jedwali Namba 5.8.

**Jedwali Na. 5.8: Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi**

| Asili na Mwenendo wa Kampeni | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Kampeni zenye dosari chache ambazo haziathiri matokeo ya uchaguzi. Zilikuwa safi, huru na za haki. | 80-100 | A | 52 | 35.9 |
| Kampeni ambazo kwa ujumla zilikuwa huru na za haki lakini pia zilikuwa na baadhi ya changamoto ambazo zingeweza kuwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) | 60-79 | B | 74 | 51.0 |
| Kampeni ambazo ziliruhusu ushiriki huru wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). Lakini kulikuwa na matukio mengi ambapo vyama vingi vikubwa au chama tawala kilivunja kanuni bila kuchukuliwa hatua na kulikuwa na upendeleo ambao uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | 50-59 | C | 15 | 10.3 |
| Kampeni ziligubikwa na mapungufu mengi kuhusiana na kutokuzingatiwa kwa sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi, matatizo ya kiusimamizi, vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 4 | 2.8 |
| Kampeni zilivurugwa au kuendeshwa vibaya. Ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 0 | 0.0 |
| Mwenendo wa kampeni ulikuwa mbovu. Kulikuwa na upendeleo mwingi, makosa na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijitoa kwenye mchakato wa uchaguzi wa upendeleo au walitoa malalamiko rasmi. Teuzi ziliharibika. | 0 | F | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | | | **145** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 5.12 HITIMISHO

Kwa kiasi kikubwa, kampeni za uchaguzi zilizofanywa na vyama vya siasa na wagombea wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilifanyika kwa mujibu wa sheria na maadili husika. Ratiba ya kampeni iliandaliwa kwa kuishirikisha Tume, vyama vya siasa na wagombea. Kwa kiasi kikubwa polisi walikuwapo katika kampeni za uchaguzi, hususan katika kampeni za vyama viwili vilivyokuwa vinaongoza (CCM na CHADEMA). Mwenendo wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2020 ulikuwa wa amani na wenye manufaa ingawa ulihusisha vyama vya siasa 19. Kampeni zilizoandaliwa vizuri na kuvutia watu wengi zilikuwa za CCM na CHADEMA kwa upande wa Tanzania Bara, hususan kampeni za wagombea urais. Kwa upande wa Zanzibar, CCM na ACT-Wazalendo walifanya kampeni zenye manufaa, hususan wagombea urais wao.

Sheria zinazosimamia kampeni za uchaguzi zilionekana kujitosheleza. Changamoto ilikuwa ni utekelezaji wake. Kama sura hii ilivyoonesha, uvunjifu wa sheria ungeleta madhara fulani. Ushirikishaji wa viongozi wa dini katika kampeni na matumizi ya lugha za asili siyo viashiria vizuri na kungemong'onyoa mshikamo wa kitaifa ambao watu wanaweza kufikiri kwamba utakuwapo siku zote kwa sababu ya amani iliyopo. Kwa hiyo, kuna haja ya kuboresha utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Kama tulivyoeleza awali, viwango vilivyowekwa haviendani na hali halisi, hususan kwa kampeni za ubunge. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ina watendaji wachache wa kufuatilia utekelezaji wake. Kwa upande mwingine, vyama vya siasa vilibadilisha maeneo ya kampeni bila kufuata sheria. CCM, CHADEMA na ACT-Wazalendo walifanya kampeni kila siku lakini vyama vingine vilifanya kampeni mara mojamoja au walisitisha kwa muda. Kampeni hasi zilivihusisha vyama vya CCM na CHADEMA. Kwa ujumla, askari polisi walionesha kiwango kikubwa cha weledi, umahiri na bidii katika kutekeleza majukumu yao. Hali hii ilichagiza amani na usalama katika kipindi chote cha kampeni za uchaguzi.

# SURA YA SITA

# VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI

## 6.1 UTANGULIZI

Sura hii inaangalia nafasi ya vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Imegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya Kwanza ni ya utangulizi. Sehemu ya Pili inaangalia Maadili ya Vyombo vya Habari katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sehemu ya Tatu inajikita kwenye athari za Sheria ya Makosa ya Mtandao katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kuhusu kutoa taarifa. Sehemu ya Nne inatazama nafasi ya mamlaka zinazodhibiti vyombo vya habari, kama Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) wakati wa mchakato wa uchaguzi. Sehemu ya Tano inachambua utoaji taarifa wa vyombo vya habari na Sehemu ya Sita inahitimisha sura hii.

## 6.2 KANUNI ZA MAADILI KWA WANAHABARI KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Katika kutathmini ni kwa namna gani vyombo vya habari na waandishi wa habari walifanya kazi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, REDET iliangalia ni kwa namna gani vyombo vya habari na waandishi wa habari walizingatia Kanuni za Maadili kwa Wanahabari wakati wa uchaguzi wa mwaka 2020 zilizotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na wadau wengine. MCT ilisema kwamba kanuni hizo zilikusudiwa kuwezesha ufanyikaji wa uchaguzi huru, wa haki na wa kidemokrasia, na kuwasaidia wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Kanuni hizo zinazotumika sambamba na kanuni za maadili zilizotolewa na Baraza la Habari Tanzania kwa ajili ya kufanya shughuli za habari za kiweledi ziliwataka waandishi wa habari kuutafuta ukweli na kuuripoti kwa usahihi. Vilevile walitakiwa kuhakikisha usahihi, usawa, ukamilifu, utoaji taarifa za uchaguzi usiokuwa wa upendeleo na kufuata maadili kwa kulinda utambulisho wa vyombo vyao vya habari.

Miongozo mingine katika kanuni hizo za maadili haikutofautisha baina ya ukweli na maoni, vyombo vya habari vya umma kutokupendelea chama cha siasa au mgombea yeyote; waandishi wa habari kutokuwezesha aina yeyote ya uchakachuaji; na wamiliki na wasimamizi wa vyombo vya habari kupigania utangazaji wa shughuli za uchaguzi wa huru na wa haki. Kanuni hizo pia zilivitaka vyombo vya habari

kutangaza shughuli za uchaguzi kwa usawa na haki na kutokuruhusu matumizi ya lugha au matamko ya chuki na kutokuyatenga makundi ya watu walio pembezoni. Hali kadhalika, vyombo vya habari na waandishi wa habari walipaswa kushirikiana na TCRA, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na mamlaka zingine katika masuala kama kubaini nia (kama ni ya makusudi au ya bila kukusudia) kwa kuingiliwa kwa mawimbi ya redio au televisheni wakati wa uchaguzi mkuu na upotevu wa magazeti mengi au kutokufika yalikokusudiwa. Vyombo vya habari vilipaswa kupanga na kutoa viwango sawa vya gharama ya matangazo kutoka vyama vyote vya siasa na kushirikiana na asasi za kiraia katika kutoa elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura, na kufuatilia na kutathmini mchakato wa uchaguzi. Kanuni hizo za maadili zilisisitiza kwamba waandishi wa habari lazima wawe na vitambulisho vyao vya kazi; watoe taarifa kuhusu mashambulizi ya aina yeyote au vitisho dhidi yao kwa waajiri wao na polisi; wajue mchakato wa uchaguzi, vyombo, kanuni na sheria ili kutoa taarifa na elimu kwa wapiga kura kwa manufaa; wachunguze na kufichua vitendo vya ovyo katika uchaguzi; na wasifungamane na chama au mgombea yeyote.

Wakati huohuo kanuni hizo ziliandaliwa kwa sababu ya nafasi na umuhimu wa vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi huku zikitambua athari zake pia. REDET iliuona mtanziko huo na ukweli kwamba matumizi ya kanuni hizo yalikuwa ya hiari. Kanuni za maadili hazikuweka adhabu yeyote kama zisingefuatwa. Hata hivyo, kuwa na kanuni za maadili ilikuwa ni ishara ya utayari wa taaluma ya habari ya kufanya kazi ya kufuatilia ya vyombo vya habari ambayo inaingiliana na kazi inayofahamika ya vyombo vya habari ya kuwa mlinzi wa masilahi ya umma ambayo kwa kupitia kazi hiyo vyombo vya habari havina uhusiano na serikali.

Kuhusiana na kanuni za maadili, vifungu mahususi vya sheria na sera vilitumika kudhibiti vyombo vya habari (vya kuchapisha na vyombo vya habari vya mtandaoni na mitandao ya kijamii) wakati wa mchakato wa uchaguzi. Sera ambazo zinahusika na masuala ya vyombo vya habari ingawa siyo moja kwa moja ni Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, Sera ya Habari ya Taifa ya mwaka 1997, Sera ya Taifa ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano ya mwaka 2016 na Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003.

Sheria ambazo zinaathiri shughuli za vyombo vya habari na waandishi wa habari moja kwa moja ni Sheria ya Kupata Habari ya mwaka 2015 ambayo inadhibiti matumizi na upatikanaji wa habari na Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 ambayo

inadhibiti matumizi na uchapishaji wa taarifa za kitakwimu. Sheria zingine ni Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 ambayo inadhibiti matumizi ya taarifa kwenye mitandao ya kijamii inatoa adhabu kama matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yatatokea na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 inayohusika na weledi wa waandishi wa habari na kufuatilia uchapishaji na maudhui ya vyombo vya habari vya kuchapisha (hususan magazeti). Sheria zingine ni Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2010 inayotoa leseni na kudhibiti utendaji na upatikanaji habari, na inayodhibiti maudhi na usambazaji wa habari kwa upande wa vyombo vya habari vinavyotangaza, Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996 na Sheria ya Taifa ya Usalama ya mwaka 1970. Kuna Sheria ya Magereza Tanzania ya mwaka 1967 na Kanuni za Kudumu za Serikali ambazo zinakataza kumiliki na kuchapisha vitu ambavyo havijathibitishwa ambavyo vinaweza kuharibu siri rasmi za serikali na usalama wa nchi au vyombo vya dola. Kanuni hizo zinadhibiti mienendo ya waandishi wa habari na ukusanyaji habari. Sheria ya Jeshi la Polisi la Tanzania na Majeshi Mengine ya mwaka 2002 na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 ambayo ina vifungu vinavyohusiana na vyombo vya habari zinavitaka vyombo vya habari vya serikali kutoa taarifa kwa usawa kuhusu vyama vyote vya siasa.

## 6.3 MFUMO WA KISHERIA WA VYOMBO VYA HABARI KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Mfumo wa sheria wa Tanzania umeendelea kuwa mkali kwa vyombo vya habari na mara nyingi umekuwa kikwazo badala ya kuvilinda vyombo vya habari na kazi zake. Moja kati ya sheria ambazo ni kikwazo ni Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016. Vifungu vyake vya uhaini, kuvunjia hadhi na uchapishaji wa habari za uongo vilionwa na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki kuwa vinaminya uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza. Sheria ya Takwimu ya mwaka 2018 imeendelea kuminya uhuru wa vyombo vya habari ingawa marekebisho yake yameondoa makosa ya jinai yaliyowekwa kwa kukusanya na kuchapisha takwimu zinazokinzana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Kabla ya mabadiliko hayo uandishi wa habari wa data na utafiti binafsi yalikuwa makosa ya jinai. Hata hivyo, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, hususan utekelezaji wake, imeibua hisia za watu wengi, hasa kuhusu uvunjaji wa uhuru wa kujieleza na uminyaji wa shughuli nyingi wakati wa uchaguzi kama watu kutoa maoni yao kuhusu wagombea katika mitandao ya kijamii.

Sheria ya Makosa ya Mtandao ilitungwa kimsingi kwa lengo la kuzuia uwekaji wa video za ngono kwa ajili ya watoto wadogo katika mifumo ya kompyuta, mashumbulizi ya mtandaoni, utungaji wa mambo mitandaoni, makosa yanayohusu utambulisho, uchapishaji wa habari za uongo, ubaguzi wa rangi, chuki, matusi, jumbe ambazo mtu hakuziomba, utoaji taarifa za uchunguzi, kuzuia uchunguzi, uvunjaji wa hati miliki na nyingine nyingi. Kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha sheria hiyo, kuchapisha maana yake ni kusambaza, kutuma, kupeleka, kuonesha, kubadilishana, kunakili, kuuza au kutoa kwa lengo la kuuza, kupanga au kutoa kwa lengo la kupanga,  na kutoa kwa njia nyingine yeyote. Hizi ndizo shughuli ambazo waandishi wa habari wanazifanya kila siku na kwa hiyo Sheria ya Makosa ya Mtandao inaionea tasnia ya habari.

## 6.4 MAJUKUMU YA WADHIBITI WA VYOMBO VYA HABARI

Wadhibiti wa mawasialiano na vyombo vya habari ni TCRA, MCT na TEF. Wadhibiti hawa walikuwa na nafasi muhimu katika kuweka mwelekeo wa namna vyombo vya habari vilivyofanya shughuli zake wakati wa uchaguzi. Kupitia kamati yake ya maudhui, TCRA ilizifanyia marekebisho kanuni zake za mawasiliano ya kieleketroniki na posta (Maudhui ya Redio na Televisheni) za mwaka 2020 kwa kuweka vifungu vidogo katika kifungu cha 37 ambavyo, pamoja na mambo mengine, vinavitaka vyombo vya habari vya utangazaji vya ndani kupata kibali cha mdhibiti kabla ya kutangaza maudhi ya kitaifa au kimataifa ambayo imeyapata kutoka kwa watoa maudhui wengine. Tarehe 10 Agosti 2020, TCRA iliita R*adio Free Africa* kwa mahojiano, ikiituhumu redio hiyo kuwa ilikuwa imevunja vifungu vya 15(2) (b), (c) na 16 vya Kanuni za Mawasiliano ya Kieleketroni na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) za mwaka 2018. Hii ilitokana na kitendo cha kipindi cha amka na *BBC* kufanya mahojiano na Tundu Lissu tarehe 29 Julai 2020. Hatua hiyo iliashiria muktadha ambao vyombo vya habari ungejikuta katika malumbano na TCRA kama mdhibiti.

TCRA ilivisimamisha baadhi ya vituo vya redio na gazeti la *Mwananchi* la mtandaoni kwa madai kwamba lilivunja Kanuni za Maadili za Mawasiliano ya Kieleketroniki na Posta za mwaka 2018. Mwezi Agosti 2020 TCRA ilizifungia *Clouds TV* na *Clouds FM Radio* kwa madai kwamba zilivunja maadili kwa kutangaza takwimu ambazo hazikutolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *Wasafi FM*, *Wasafi TV* na *Ihasaan FM* pia vilisimamishwa lakini kwa sababu tofauti. TCRA ilisimamisha leseni ya gazeti la *Mwananchi* la mtandaoni tarehe 16 Aprili 2020 na kutoza faini

ya shilingi milioni tano kwa madai kwamba walichapisha habari ya upotoshaji ambayo iliichanganya jamii.

MCT ni chombo huru kinachodhibiti habari nchini Tanzania kinachohamasisha uzingatiaji wa kanuni za uandishi wa habari kwa kutoa habari ambazo ni sahihi, huru, kamilifu, za utu na uwajibikaji. Ilifanya kazi ya udhibiti wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Mwezi Julai 2020, baraza hilo liliwaonya waandishi wa habari katika kada zote kutochukua rushwa kutoka kwa vyama vya siasa au chombo kingine chochote ili kuchapisha habari za uchaguzi. Hali hii ilitokana na mhariri ambaye jina lake halikutajwa kutoka gazeti la serikali ambaye alikuwa chini ya uchuguzi wa TAKUKURU akidaiwa kwamba alikuwa amepokea rushwa. Kwa ujumla, MCT imeweka mwongozo wa maadili ya waandishi wa habari na wadau wa tasnia ya habari ambao unadhibiti utafutaji ukweli, usawa na haki, ulinzi wa watu walioko hatarini, haki ya kujibu, kuonekana kutokuwa na hatia na kujua kitu gani ni kuzuri. Kanuni hizi zimezaa Kanuni za Madili ya Wanahabari katika kutangaza habari za uchaguzi nchini Tanzania.

TEF ilifanya kazi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Iliingilia kati ili kuweka sawa uhusiano kati ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) na CHADEMA. TEF imekuwa chachu katika kutoa ushauri na kuvisuluhisha vyombo vya habari na wadau katika mchakato wa uchaguzi. Hali hii ilijitokeza pindi Peter Msigwa, Mbunge wa zamani wa Iringa Mjini kupitia CHADEMA, alipowatuhumu waandishi wa habari kuwa walikataa kuripoti mikutano ya kampeni ya Tundu Lissu mkoani Iringa. TEF iliingilia kati kwa kuelezea kusikitishwa kwake na kutoa onyo kuhusu utoaji wa tuhuma zisizokuwa na msingi ambazo zinaweza kuhatarisha maisha ya waandishi wa habari.





*Wawakilishi wa TEF, CHADEMA, Tume na TBC wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mazungumzo ya upatanisho*


## 6.5 UCHAMBUZI WA UTOAJI TAARIFA JUU YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

REDET iliangalia aina tano ya vyombo vya habari, yaani magazeti, televisheni, redio (vinavyopatikana nchi nzima), redio za kijamii na vyombo vya habari vya mtandaoni ili kuona namna walivyotoa taarifa juu ya uchaguzi. Kwa upande wa magazeti, ilichambua makala za habari kutoka gazeti la *Habari Leo* na *Daily News*, *Mwananchi* na *The Citizen*, *Nipashe* na The *Guardian*, *The EastAfrican*, *Uhuru* na *Mtanzania*. Kwa upande wa redio, watazamaji waliangalia *TBC Taifa*, *Radio One* na *Clouds* FM. Kwa upande wa televisheni, waliangalia *Uhai TV* (UTV au maarufu kama Azam), *TBC*, *ITV* na *Clouds TV*. Na kwa upande wa vyombo vya habari vya mtandaoni, watazamaji waliangalia michango kutoka *East Africa* (ukurasa wa Facebook, *Dar 24* na *Millard Ayo Blogi*. Kwa upande wa redio za kijamii, watazamaji walitazama *Boma Hai FM* (Kilimanjaro), *Kahama FM* (Shinyanga), *Chai FM* (Mbeya), *Dodoma FM* (Dodoma), *Ruangwa FM* (Lindi) na *Tumbatu FM* (Zanzibar).

Pamoja na mifumo iliyotajwa hapo juu, kanuni na mambo mengine, sehemu zifuatavyo zinaonesha kwamba vyombo vya habari vilitoa taarifa kwa kiasi kikubwa juu ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

### 6.5.1 Wigo wa Magazeti


REDET ilichambua makala za magazetini 629 zilizochapishwa kuanzia tarehe 26 Agosti hadi tarehe 27 Oktoba 2020, kama inavyooneshwa katika Umbo Namba 6.2. Kati ya makala hizo, 110 (asilimia 17.5) zilihusu Zanzibar,105 (asilimia 16.7) zilihusu majiji makubwa. Dar es Salaam ilikuwa na makala 58 (asilimia 9.2) na miji mingine na maeneo ya vijijini yalikuwa na makala 356 (asilimia 56.6). Kulikuwa na masuala nyeti machache sana (34, asilimia 5.4) ukilinganisha na masuala mepesi (592, asilimia 94.1) na makala kuhusu taarifa za watu. Vyanzo vikuu vya makala hizo vilikuwa wanasiasa (565, asilimia 89.8) ukilinganisha na watu wa kawaida (5, asilimia 0.8). CCM ilitangazwa zaidi (makala 351, asilimia 55.8) na vyama vya upinzani vilitangazwa kiasi kidogo (makala 198, asilimia 31.5).




*Umbo Na. 6.1: Uchambuzi wa Kitakwimu wa Matangazo ya Magazetini*

### 6.5.2 Vyombo vya Habari vya Mtandaoni

REDET ilichambua habari 989 za kielektroniki au za mtandaoni zilizohusiana na uchaguzi kuanzia tarehe 27 Agosti hadi tarehe 27 Oktoba 2020. Kwa upande wa vyombo vya habari vya kieleketroniki na vyombo vya habari vinavyotangaza, habari 737 (asilimia 74.5) zilitangazwa na redio, yaani *Radio One* (50), *TBC FM Radio* (68) na *Clouds FM Radio* (101), na televisheni, yaani *ITV* (141), *UTV* (228) na *TBC1* (149). Kwa upande wa vyombo vya habari vya mtandaoni, habari 252 (asilimia 25.5) zilihusu Dar es Salaam (habari 54), ukurasa wa Facebook wa EATV (habari 133) na ukurasa wa Facebook wa Millard Ayo (habari 65). Kati ya habari 989 za mtandaoni zilizotazamwa, habari 855 zilitoka Tanzania Bara na habari 134 zilitoka Zanzibar. Habari 830 zilitumia wanasiasa kama chanzo cha habari. Wakati huohuo, habari 296 (pamoja na zile ambazo zilitumia wanasiasa kama chanzo cha habari) zilihusu watu wa kawaida kama chanzo cha habari au sehemu ya maudhui ilihusu masuala yao.




*Umbo 6.2: Uchambuzi wa Kitakwimu wa Habari za Mtandaoni*

### 6.5.3 Maudhui na Mwelekeo katika Matangazo ya Vyombo vya Habari

Utazamaji wa REDET ulibaini maudhui makuu/mwelekeo katika matangazo ya vyombo vya habari kuanzia siku ya kuzindua kampeni tarehe 26 Agosti hadi siku ya kufunga kampeni tarehe 27 Oktoba 2020. Kwanza, Tume ilijibu na kakanusha taarifa za uongo ambazo wakati mwingine ziliilazimisha itumie majukwaa ya kijamii kuondoa hofu na uongo kuhusu namna inavyosimamia mchakato wa uchaguzi. Mifano ni kama kauli ya Mwenyekiti wa Tume aliyoitoa katika mkutano na wadau uliofanyika Tanga tarehe 2 Oktoba 2020 kukanusha taarifa kwamba Tume ilikuwa imekataza watazamaji wa kimataifa kutazama uchaguzi mkuu (*The Guardian*, Jumamosi, 3 Oktoba 2020). Mkuu huyo wa chombo cha kusimamia uchaguzi alitoa data juu ya vibali vilivyotolewa kwa vikundi vya watazamaji wa kimataifa ambavyo vilikuwa bado havijawekwa hadharani. Mkurugenzi wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura wa Tume Giveness Aswile alisema kwamba "kukosekana kwa elimu ya uraia kumesababisha watu kutokupiga kura" na "Watanzania wengi hawana elimu ya uraia" (*The Guardian*, Jumamosi, 3 Oktoba 2020). Habari zingine kutoka Tume zilihusu majibizano kati ya Tume na wagombea, hususan mgombea urais wa upinzani Tundu Lissu (mifano michache ni pamoja na Tume kusisitiza kwamba Lissu lazima azingatie hukumu; Lissu ameambiwa: "Zingatia au subiri matokeo"; "Asiyekuwa na hofu Lissu kupuuza amri za Tume, polisi wamwita mtoa habari"; "CHADEMA inataka majibu kutoka Tume, polisi."

REDET ilibaini kwamba hisia za watu wa kawaida na maoni yao hayakutangazwa kiasi kikubwa na vyombo vya habari. Watu wa kawaida ni raia, kwa kawaida wapiga kura walio wengi, ambao wanataka kuchagua serikali mpya. Masuala yao yanahusu matatizo ya kila siku ambayo hupungua au hutatuliwa kupitia serikali kutunga na kutekeleza sera zake. Maoni ya watu wa kawaida yanatoa mitazamo au lenzi tofauti ambazo watu hao huzitumia kutazama hali zao. Masuala haya hayakuangaziwa na vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Hata hivyo, yalijumuishwa kama hisia na kwa kiasi kikubwa kuthibitisha misimamo ya wagombea waliowapenda au wasiowapenda, kuzungumzia wanasiasa badala ya wao wenyewe au masuala yao, matatizo ya watu wa kawaida. Hata pale walipojaribu kuanzisha mjadala kuhusu masuala yao, muda na nafasi iliyotolewa ilikuwa finyu sana kuwezesha kutazama masuala kwa mitazamo ya watu wa kawaida.

Vyanzo vingi vya habari vilikuwa wagombea, vyama vya siasa, maafisa kutoka mamlaka, hususan Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar na Jeshi la Polisi. Kuna njia nne ambazo vyombo vya kusimamia uchaguzi, hususan Tume ya Taifa ya Uchaguzi, vilikuwa vyanzo muhimu vya habari wakati wa kuelekea uchaguzi wa Oktoba 2020. Ingawa inawezekana waandishi wa habari na watazamaji waliona ni vigumu kupata taarifa ya kina kuhusu pingamizi na rufaa za wagombea, muhtasari wa maamuzi ya Tume juu ya rufaa ulichapishwa kwenye magazeti mengi *"Taarifa kwa Umma: Muhtasari wa Maamuzi ya Rufaa za Udiwani Zilizopokelewa na Kuamuliwa na Tume ya Uchaguzi*. Inaonekana kwamba Tume ililipia kurasa nyingi kwenye magazeti yote yanayosambazwa sana (tazama kwa mfano *Daily News*, Alhamisi, 1 Oktoba 2020; *Nipashe Jumamosi*, 3 Oktoba 2020). Kulikuwa na habari juu ya vyombo vya kusimamia uchaguzi: 'habari za tume za uchaguzi' (Habari za Uchaguzi) na Elimu ya Mpiga Kura, kwa mfano "Tume yatoa mfano wa karatasi za Rais, Makamu wa Rais." Zilikuwapo habari za kawaida za kila siku kuhusu shughuli zilizofanywa na Tume. Mathalani, Tume iliandaa mikutano mingi na wadau na warsha za mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi wake nchi nzima. Matamko ya maafisa waandamizi kama vile Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Uchaguzi na makamishna yalitangazwa kwa kiasi kikubwa kwenye magazeti na vyombo vya habari vya mtandaoni. Mifano ya habari za tume: "Tume yaahidi kutoa kipaumbele kwa wenye mahitaji maalumu" (*Mtanzania,* Jumamosi, 3 Oktoba 2020), "Tume yaahidi uchaguzi wa haki na wazi" (*Daily News*, Alhamisi, 1 Oktoba 2020) na "Tume ya Uchaguzi Zanzibar yawataka wasimamizi wa uchaguzi kukariri vipengele vya sheria ya uchaguzi".

Vyanzo vya habari vya kimataifa pia vilitumika. Vyombo vya habari vya ndani vilitangaza habari za wawakilishi wa kimataifa waliotoa matamko kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kwa mfano, Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Bashiru Ally, afanya mazungumzo na Mabalozi wa Umoja wa Ulaya, Marekani, Kenya na Msumbiji kwa wakati tofauti lakini siku moja katika ofisi za chama Lumumba tarehe 15 Oktoba 2020 (Tazama "Marekani, EU zavutiwa na kampeni za kistaarabu," *Uhuru*, 16 Oktoba 2020). Balozi wa China Wang Ke alitembelea Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere cha mjini Kibaha tarehe 10 Oktoba 2020. Alikutana na Dkt. Bashiru Ally, Katibu Mkuu. Habari hii ilikuwa na kichwa kisemacho "China yafurahishwa na uchaguzi wa amani" lakini ukurasa wa mbele ulikuwa na kichwa cha habari kisemacho "Balozi wa China afurahishwa na mwenendo wa kampeni za uchaguzi Tanzania" (*The Citizen*, Jumapili, 11 Oktoba 2020).

Baadhi ya wagombea waliomba kuungwa mkuno na jumuiya ya kimataifa badala ya kuomba kuungwa mkono na wananchi. Kampeni na matangazo zilijikita zaidi katika vyama vya siasa, hususan vyama vikuu viwili, CCM na CHADEMA, na wakati mwingine ACT-Wazalendo (kwa upande wa Zanzibar) au wagombea wao wakuu. Kama si vyama vya siasa vilivyotoa habari, basi lilikuwa ni Jeshi la Polisi, maafisa wa serikali kama wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, viongozi wa dini maarufu (wanaoshikilia nafasi ambazo ni tata zaidi) na asasi za kiraia.

Ingawa vyombo vya habari vya umma vilivitenga vyama vikubwa vya upinzani, hususan CHADEMA na ACT-Wazalendo, vyombo vingine vya habari havikutaka kukosana na mteja yeyote. Vyombo vya habari vya umma kwa upande mwingine vilitangaza kwa asilimia kubwa habari za CCM na wagombea wake. Vilipotangaza habari juu ya vyama vya upinzani havikutangaza habari za CHADEMA na ACT-Wazalendo, badala yake vilitangaza habari za vyama kama CHAUMMA, ADC na UDP na habari juu ya masuala ambayo zilivifanya vyama hivyo vionekane kichekesho. Pale ambapo walitangaza masuala ya CHADEMA na ACT-Wazalendo walitangaza habari hasi kuhusu vyama hivyo. Mathalani, gazeti la serikali la *Sunday News* lilitoa habari kama "Nafurahishwa na hotuba za kampeni za CCM-Bwege (24 Oktoba 2020) na nyingine dhidi ya ACT-Wazalendo "Wanachama 200 kutoka ngome ya Zitto wahamia CCM."

Tarehe 25 Septemba gazeti la *Nipashe* lilikuwa na kichwa cha habari kisemacho "Msajili, Upinzani wazidi kuvutana". Habari ilihusu uwezekano wa vyama vya CHADEMA na ACT-Wazalendo kuungana. Msajili wa Vyama vya Siasa alisema

kwamba ilikuwa ni kinyume cha sheria lakini upinzani ulisema unaweza kuamua nani ushirikiane nae muda wowote. Makala yanaunukuu upinzani na Msajili wa Vyama vya Siasa. Kutokupendelea kunaweza kuwa ni udhibiti binafsi unaofanywa na vyombo vya habari ambao umekuwa wazi miaka ya hivi karibuni. Lakini, iliwanyima wasomaji uchambuzi wa kina kuhusu nani alikuwa sahihi na nani hakuwa sahihi, kwa mujibu wa katiba na sheria husika.

Matangazo ya vyombo vya habari yanaonesha kwamba, ukiachilia mbali baadhi ya vyombo vya habari, hasa vile vya mtandaoni, vyombo vya habari havikuchochea mashambulizi ya watu au kudhalilisha watu, propaganda na habari za kishabiki. Hata hivyo, matangazo hasi yalihusu masuala ambayo hayakuhusiana na mada kuu ya habari, kama kitu cha kuwaondoa watu katika masuala makuu kama vile waandishi wa habari kutaka kubadilisha mada ya uchaguzi. Mfano mmoja wa habari hizo ulichapishwa kwenye gazeti la *Daily News* (26 Septemba 2020) ukiwa na kichwa cha habari kisemacho "Urais siyo kitu cha kujaribu – Waziri Mkuu". Habari hii inauwasilisha upinzani kwa namna hasi na CCM kwa namna chanya. Habari ya ndani inaonesha kwamba upinzani ni kipingamizi cha maendeleo kwa kupinga kila wazo linalotolewa na serikali. Ukisoma kwa makini, habari inahusu zaidi maneno ya Waziri Mkuu kuliko uchambuzi wa waandishi wa habari.

Pale ambapo hoja hasi zilionekana ni zenye manufaa kwa kiasi fulani zilihusu zaidi mashumbulizi ya watu kuliko masuala ya msingi. Kulikuwa na matukio machache Zanzibar ambapo vyombo vya habari bila umuhimu wowote vilichochea vitu hasi kama taharuki, lugha ya chuki na hofu juu ya vitu vitakavyotokea baada ya uchaguzi kwa kuangazia zaidi vitendo vya wanasiasa au vitendo vya wafuasi wa vyama vya siasa kuhusu malumbano na maneno ya uchonganishi, na mashambulizi ya watu yaliyopita mpaka. Kwa ujumla, vyombo vya habari vilichukua mrengo chanya zaidi ya hasi kuhusiana na vyanzo vya habari.

CCM, CHADEMA na ACT-Wazalendo vilitangazwa zaidi ya vyama vingine vya siasa. Kwa kiasi fulani, CCM ilipendelewa kwa kutangazwa moja kwa moja, ingawa, kama kichekesho, CHAUMMA na SAU au vyama vingine isipokuwa CHADEMA na ACT-Wazalendo navyo vilitangazwa katika vipindi maalumu vya habari. Baadhi ya maoni yaliyotolewa kwenye mitandao ya kijamii yaliashiria kwamba baadhi ya waandishi wa habari/watumiaji wa mitandao ya kijamii (kwenye ukurasa wa Facebook wa *East Africa* wa maoni ya wasomaji) walilalamika kwamba vyombo vya habari viliipendelea CCM. Ilishangaza kuona ni kwa namna gani kila

siku vyombo vya habari vilitoa taarifa ileile kwa kuangalia mtizamo badala ya kupata habari kutoka vyanzo vingi iwezekanavyo. Habari hizo ziliangaliwa nje ya muktadha kama tuilivyokwishaeleza. Kwa hiyo, vyombo vya habari vya umma vilivikuza baadhi ya vyama vya siasa vidogo na kupuuza misimamo ya vyama vikubwa, hususan CHADEMA na ACT-Wazalendo. Hata hivyo, kitu kimoja kiko wazi: CCM haikukosa nafasi/kuangaziwa katika chombo chochote cha habari.

Vyombo vya habari vilitangaza kwa kiwango kikubwa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Habari nyingi zilihusu kampeni za vyama vikubwa, hususan CCM na CHADEMA, na mikutano ya waandishi wa habari na Tume na polisi kuhusu uchaguzi. Lakini matangazo hayo yalijikita zaidi katika serikali, vyombo vingi vya habari vikishindwa kutenganisha kati ya shughuli za kichama na shughuli za kiutawala za wanasiasa. Vyombo vya habari viliongeza kiwango cha kutangaza habari kutoka siku ya kuanza kampeni mpaka tarehe ya mwisho bila kwenda mbali zaidi ya vitu vilivyosemwa na wagombea. Habari nyingi zilikuwa na uchambuzi mwepesi. Uchambuzi wa kidadisi unaofanywa na vyombo vya habari ulikuwa bidhaa adimu.

Badala ya kuwa na uchambuzi mzuri vyombo vya habari vilibeba matangazo zaidi (matangazo ambayo yaliyoonekana kama maudhui ya mhariri), hususan kwenye magazeti. Matangazo ya kisiasa ya mawakala wa serikali yalijaa kwenye vyombo vya habari. Hali hii haikuwa ya kawaida na ilianza katikati ya mwezi Oktoba 2020 ambapo mawakala na mashirika ya serikali yaliweka matangazo kwenye kurasa nzima za magazeti kuhusiana na utendaji wao katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (si zaidi, si pungufu). Baadhi ya mifano ni: Tangazo la TANESCO la ukurasa nzima katika gazeti la *The Guardian*, Jumatano, 14 Oktoba 2020 “TANESCO: Mafanikio Makubwa katika Uzalishaji Umeme Ndani ya Miaka 5”, na mkutano na waandishi wa habari uliofanyika ili kufikisha jumbe za kisiasa: “NEMC imefanya kazi kubwa miaka 5 iliyopita”; NEMC Yajivunia Miaka 5 ya JPM”; “TPSF yamsifia JPM”. Kulikuwa na matangazo mengine mengi ya aina hiyo.

### 6.5.4 Matangazo ya Redio za Kijamii

REDET ilibaini kwamba habari nyingi zilitoka kwenye majiji, yaani Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma na Tanga, kuliko kwenye miji mingine. Habari zilitoka kwenye miji ambayo wagombea wakubwa walitembelea, yaani miji ya ukanda wa kusini kama vile Lindi, Mtwara na Songea, miji ya ukanda wa magharibi

kama vile Kigoma, Chato na Bukoba na baadhi ya maeneo ya kati ya Tanzania kama vile Singida na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Mara. Maeneo haya ni yale ambayo wagombea urais wa CCM na CHADEMA walifanya kampeni zaidi. Zanzibar haikutengwa kwani ilitangazwa kiasi cha kutosha magazetini, redioni, kwenye televisheni na kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni yawezekana kwa sababu ya mnyukano mkali kati ya wagombea urais wa CCM na ACT-Wazalendo. Kwa ujumla, maeneo ya vijijini yalitangazwa zaidi ya maeneo ya mijini, hasa mwanzoni mwa kampeni na matangazo yalijikita mijini kipindi ambapo wagombea walifanya kampeni za mwisho mijini. Kati ya habari 252 zilizochambuliwa, 142 (asilimia 57) zilihusu habari za maeneo husika na masuala ya wagombea ubunge. Vyombo vya habari vilijikita walikopita wagombea na wagombea walitumia muda mwingi vijijini. Redio za kijamii pia ziliangazia zaidi wagombea na vyama vilivyoko kwenye maeneo yao kuliko wagombea wa kitaifa (kama wagombea urais) kama Jedwali Namba 6.1 linavyoonesha:

**Jedwali Na. 6.1: Matangazo katika Redio za Kijamii**

| Na. | Redio | Mkoa/Kanda | Habari kuhusu masuala ya maeneo/ majimbo ya wagombea (asilimia) | | Habari kuhusu masuala ya wagombea wa kitaifa/ urais (asilimia) | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dodoma FM | Dodoma/Kati | 24 | 50 | 24 | 50 | 48 |
| 2. | Triple A | Arusha/ Kaskazini | 33 | 75 | 12 | 25 | 45 |
| 3. | Kahama FM | Shinyanga/ Kanda ya Ziwa | 29 | 55 | 23 | 45 | 52 |
| 4. | Nuru FM | Iringa/Nyanda za Juu Kusini | 23 | 70 | 10 | 30 | 33 |
| 5. | Jamii FM | Mtwara/Kanda ya Kusini | 16 | 50 | 16 | 50 | 32 |
| 6 | Tumbatu FM | Visiwa vya Zanzibar / Zanzibar | 17 | 40 | 25 | 60 | 42 |
| | **Jumla** | | **142** | **57** | **110** | **43** | **252** |

*Chanzo: REDET Uchambuzi wa Redio za Jamii, 2020*

### 6.5.5 Makala za Magazetini na Vijarida

Ingawa majina ya wanasiasa yaliongoza na baadhi ya habari za matukio zilikuwapo au udhalilishaji wa majina ya watu, habari nyingi zilionesha kwamba vyombo vya habari vilijihusisha na masuala, na hivyo kuufanya uchaguzi wa mwaka 2020 kujikita kwenye masuala ya maendeleo badala ya mashambulio ya watu. Nafasi na muda ulitolewa kwa masuala yanayoikabili jamii ya Kitanzania. Kulikuwa na matukio ambapo ilani za uchaguzi ziliangaziwa na magazeti mengi ya kila siku na kila wiki ambayo yalikuwa na vipengele vilivyochapisha habari za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 tu, yaani gazeti la *Mwananchi*, *The Citizen*, *Nipashe* na *Sunday News*. Zilikuwapo makala kuhusu habari za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 tu. Mathalani, kwa muda mrefu gazeti la *The Citizen* liliangazia ilani za vyama kwenye meza yake ya masuala ya uchaguzi kukusu maudhui mengi muhimu na ilikuwa na kipengele kilichojulikana kwa jina la "Ubaoni: Walipo wagombea wako leo" kilichotoa taarifa muhimu kuhusu ratiba za kampeni za wagombea urais wengi. Baadhi ya makala za habari zilionesha masuala halisi, hususan makala zilizochapishwa kwenye gazeti la *Mwananchi*.

### 6.5.6 Mchango wa Mitandao ya Kijamii

REDET iliangalia matumizi ya mitandao ya kijamii kama jukwaa la kubadilishana habari. Lakini, labda ni kwa sababu ya Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015 na kanuni zingine, mitandao ya kijamii haikutumika kwa kiasi kikubwa kwenye uchaguzi mkuu. Mchango wa bingwa wa masuala ya teknolojia, Facebook, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kupitia kuangalia ukurasa wa Facebook wa EATV ulionesha kwamba mtandao huo ulitumiwa zaidi na watu wa kawaida ambao hawakufahamika wako wapi badala ya kutumiwa zaidi na waandishi wa habari. Maoni mengi yenye mrengo wa malalamiko hayakupatiwa majibu. Mchango wa Facebook kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulionekana kwa njia tatu kupitia programu na bidhaa zake. Walikuwa na programu kwa ajili ya kupunguza usambazaji wa habari za uongo huku wakiunga mkono ushirikishwaji wa umma. Facebook ilianzisha ushirikiano na *Pesa Check*, asasi uhuru inayoangalia ukweli wa mambo nchini Tanzania na kuhakiki na kuangalia usahihi wa maudhui yanayowekwa Facebook na Instagram. Facebook ilizindua mfumo uliowakumbusha watu tarehe ya uchaguzi kwenye uzi wao wa habari kuelekea siku ya uchaguzi kama sehemu ya

kampeni yao ya kuishirikisha jamii. Walikuwa na kampeni ya kuwawezesha watu kufanya maamuzi ya nini wasome, waamini na wawaambie watu wengine. Uwazi wa matangazo ya kisiasa ulikuwa kifaa muhimu kwa mtu yeyote aliyetaka kutoa matangazo ya aina hiyo. Waliotaka kufanya hivyo walipaswa kuhakikiwa ili kupata utambulisho na ukazi wao nchini Tanzania. Facebook ilionekana kama haifanyi kazi na watumiaji wake walikuwa hivyo hivyo kwenye suala la kufanya kampeni za kimkakati. Watu walipiga kelele kwa kutumia Facebook lakini hawakupatiwa majibu.

## 6.6 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchaguzi mkuu wa Tanzania wa mwaka 2020 ulitangazwa kwa kina na vyombo vya habari kama vyombo vya habari vilivyotazamwa vilivyoonesha (magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii) (kwa mfano, zaidi ya makala za habari 1,500, mbali ya programu na makala maalumu). Vyombo vya habari vilijikita zaidi kwenye habari za ndani kuliko za nje ya nchi. Habari nyingi zilikuja mijini kuliko habari zilizotoka mijini, kitu ambacho ndiyo desturi, hususan kwa kipindi ambacho siyo cha uchaguzi. Kama ilivyotarajiwa, watu wa kawaida, masuala ya watu wa kawaida na mitizamo ya watu wa kawaida haikutangazwa sana. Hakukuwa na uchambuzi na mijadala ya masuala, ukizingatia kwamba ni jukumu la vyombo vya habari kusaidia watazamaji au wasomaji ili wafanye maamuzi sahihi siku ya uchaguzi.

# SURA YA SABA

# USHIRIKI WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 NCHINI TANZANIA

## 7.1 UTANGULIZI

Wakati ambapo Watanzania walikuwa wanakwenda kupiga kura tarehe 28 Oktoba 2020 moja ya masuala ya msingi yaliyohitaji kushughulikiwa ni ushiriki wa makundi maalum katika mchakato wa uchaguzi. Taarifa hii inafanya tathmini ya kiwango ambacho wanawake, vijana na watu wenye ulemavu walishiriki katika usimamizi, zoezi la kuandikisha wapiga kura, elimu ya mpiga kura, mchakato wa uteuzi, kampeni na siku ya uchaguzi. Matokeo yanatoka kwenye taarifa za vyombo vya kusimamia uchaguzi, vyombo vya habari na sheria husika.

## 7.2 MFUMO WA KISHERIA KWA AJILI YA MAKUNDI MAALUM

Ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mchakato wa uchaguzi unatambuliwa kwenye mifumo ya kisheria, ikiwamo katiba ya nchi, sheria, taratibu, kanuni na sera mbalimbali. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inaeleza kwamba kila mtu ana haki ya kutambuliwa na kupewa hadhi (Ibara ya 12[2]) na inakataza unyanyasaji dhidi ya mtu yeyote na mtu yeyote au mamlaka (Ibara ya 13[4]). Ibara ya 21(1) inatambua haki ya wananchi kushiriki katika kutawala nchi moja kwa moja au kupitia wawakilishi. Ili kukabiliana na kukosekana usawa wa kijinsia wa kihistoria, kijamii na kitamaduni, kuna hatua za kisheria za kuwawezesha wanawake kushiriki katika uwakilishi wa udiwani na ubunge. Hivyo, wanawake wanapaswa kuwa walau asilimia 30 ya wabunge wote. Idadi ya wanawake iliongezwa hadi kufikia asilimia 40 kupitia waraka wa serikali wa mwaka 2015 kama sehemu ya upendeleo maalumu. Wabunge wanawake wa vitu maalum wanagawanywa kwa wastani kwenye vyama vya siasa vinavyofanikiwa kupata walau asilimia tano ya kura zote halali zilizopigwa katika uchaguzi wa wabunge. Kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ni vyama viwili tu vilivyofanikiwa kufikia kigezo hicho cha asilimia tano – CCM na CHADEMA – kwenye uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Haki za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zinatambuliwa kwenye sera mbalimbali kama vile Sera ya Wanawake na Maendeleo ya Kijinsia (2000), Sera

ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) na Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2010). Ingawa vifungu hivi vyote vipo, ushirikishwaji wa makundi haya maalumu kwenye mchakato wa uchaguzi umekuwa mdogo kama ilivyojitokeza katika chaguzi zilizotangulia tangu mwaka 1995. Wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, wanawake walikuwa asilimia 19 tu ya watu wote waliogombea ubunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kati ya viti vya ubunge 264, ni viti 25 tu vilivyochukuliwa na wanawake (asilimia 9.5) (Ripoti ya NEC, 2016). Katika muktadha huu timu ya watazamaji wa REDET iliamua kutathmini kiwango cha ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Sura hii imepangwa kama ifuatavyo. Sehemu ya Kwanza inatoa utangulizi na Sehemu ya Pili inawasilisha matokeo ya ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kusimamia uchaguzi. Sehemu ya Tatu inajishughulisha na hali ya ushiriki wa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kama wapiga kura. Sehemu ya Nne inaangalia utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa makundi maalumu. Sehemu ya Tano inashughulikia uteuzi wa wagombea kuhusiana na makundi haya maalumu. Ushiriki wao katika kampeni za uchaguzi na kupiga kura siku ya uchaguzi unatazamwa kwenye Sehemu ya Sita na ya Saba. Matokeo ya siku ya uchaguzi yanayowahusu wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yanatazamwa kwenye Sehemu ya Nane. Sehemu ya mwisho inahitimisha sura hii.

## 7.3 WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWENYE USIMAMIZI WA UCHAGUZI

Ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kusimamia uchaguzi unatathminiwa kwa kuangalia watu waliomo kwenye vyombo vya kusimamia uchaguzi na watendaji wa uchaguzi wa ngazi mbalimbali walioteuliwa. Kwa kuanzia, kukosekana kwa uwiano wa kijinsia kunatazamwa kwa kuangalia watu waliomo kwenye vyombo vya kusimamia uchaguzi. Matokeo yanaonesha kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 hakukuwa na usawa wa kijinsia katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambako ni makamishna wawili tu walikuwa wanawake kati ya makamishna sita na katika Tume ya Uchaguzi Zanzibar mwanamke alikuwa mmoja tu kati ya makimishna saba.

Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, inaipa Tume mamlaka ya kuteua Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi (vifungu vya 10-13). Kila Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kuteuwa Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji

(kifungu cha 14 [1]). Kwa kuanzia, zoezi la kuandikisha wapiga kura na uteuzi wa waandikishaji wapiga kura haukutengenezwa kwa makusudi ili kuyavutia makundi maalumu. Matangazo ya maombi yalizingatia uwezo wa mtu kwa mtindo wa ushindani wa wazi. Waombaji walipaswa kuwa Watanzania wenye umri wa maika 18 au zaidi, wenye walau elimu ya kidato cha nne au zaidi na walipaswa kuwa wakazi wa kata husika. Walipaswa kuwa na uwezo wa kutumia kompyuta, wasipendelee na wawe waaminifu.

Pamoja na kutoyajali makundi maalumu, ilibainika kwamba kiwango cha ushiriki wa wanawake na vijana kiliongezeka. Kwa kutumia data kutoka kata 13, ingawa wanaume walikuwa asilimia 55 ya waandikishaji wapiga kura, asilimia 45 ya waandikishaji wapiga kura walikuwa wanawake. Kama Jedwali Namba 7.1 linavyoonesha, wanawake walikuwa wengi zaidi miongoni mwa waandikishaji wapiga kura kwenye Manispaa ya Songea, Handeni, Ubungo, Chakechake na Jiji la Tanga:

**Jedwali Na. 7.1: Mgawanyo wa Waandikishaji Wapiga Kura kwa Jinsia**

| Na. | Wilaya | Jumla | Wanaume | Wanawake | Asilimia ya Wanawake |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | 344 | 147 | 197 | **57.3** |
| 2 | Njombe | 200 | 124 | 76 | **38.0** |
| 3 | Namtumbo | 290 | 168 | 122 | **42.1** |
| 4 | Handeni | 532 | 390 | 312 | **58.6** |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara | 558 | 367 | 191 | **34.2** |
| 6 | Halmashauri ya Wilaya ya Newala | 206 | 128 | 78 | **37.8** |
| 7 | Ruangwa | 260 | 186 | 74 | **28.5** |
| 8 | Mkinga | 384 | 234 | 150 | **39.1** |
| 9 | Bumbuli | 362 | 248 | 114 | **31.5** |
| 10 | Ubungo | 624 | 212 | 412 | **66.0** |
| 11 | Chakechake | 14 | 5 | 9 | **64.3** |
| 12 | Korogwe | 580 | 402 | 178 | **30.7** |
| 13 | Halmashauri ya Manispaa ya Tanga | 484 | 198 | 286 | **59.1** |

| Wastasni (asilimia) | 45.2 |
|---|---|

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliteua wasimamizi wa uchaguzi 100, wengi wao wakiwa ni wanaume kama Jedwali Namba 7.2 linavyoonesha. Wasimamizi wa Uchaguzi wengi walioteuliwa walikuwa vijana ambao walikuwa asilimia 83 ya wasimamizi wote. Picha ni nzuri zaidi kwa upande wa Wasimamizi Uchaguzi Wasaidizi walioteuliwa. Kati ya Wasimamizi Uchaguzi Wasaidizi 5,528, wanawake walikuwa 2,838 (asilimia 54) na vijana walikuwa 4,783 (asilimia 86.5).

**Jedwali Na. 7.2: Mgawanyo wa Watendaji Walioteuliwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa Umri na Jinsia**

| | Kiume | Asilimia | Kike | Asilimia | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasimamizi wa Uchaguzi | 85 | 85 | 15 | 15 | **100** |
| Vijana (18-35) | 69 | 83 | 14 | 17 | **83** |
| Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi | 2690 | 49 | 2838 | 51 | **5528** |
| Vijana (18-35) | 2195 | 46 | 2588 | 54 | **4783** |

*Chanzo: Usaili wa Watendaji wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, 2020*

Kuhusu uteuzi siku ya uchaguzi, matokeo kutoka kwenye wilaya nyingi nchini yanaonesha kwamba wanawake na vijana wengi walikuwa watendaji wa uchaguzi katika ngazi ya jimbo. Hata hivyo, ushiriki wa makundi maalumu ulitofautiana kati ya mkoa na mkoa.



*Idadi kubwa ya vijana na wanawake wakishiriki katika mfunzo ya watendaji wa uchaguzi CDTI Monduli, jimbo la Monduli, tarehe 25 Oktoba 2020.*

Kinyume chake ni kwamba watu wenye ulemavu walikuwa wachache sana katika kusimamia uchaguzi. Kama tulivyokwishaeleza, uteuzi wa waandikishaji wapiga kura ulitegemea uwezo wa mtu kwa mwombaji yeyote aliyependa kuomba. Kwenye wilaya nyingi watazamaji wa REDET hawakuona watu wenye ulemavu wakiandikisha wapiga kura. Kwenye Wilaya ya Njombe kati ya waandikishaji wapiga kura 200 ni wawili tu walikuwa walemavu. Kwenye Wilaya ya Namtumbo kati ya waandikishaji wapiga kura 290 ni mmoja tu alikuwa mlemavu. Kwenye Wilaya ya Newala kati ya waandikishaji wapiga kura 206 ni watano tu walikuwa walemavu. Kwenye Wilaya wa Mkinga kati ya waandikishaji wapiga kura 384 ni wawili tu walikuwa walemavu na wawili wengine walikuwa ni watu wanoishi na virusi vya UKIMWI waliojitangaza wenyewe. Kwa upande wa Mkoa wa Kagera, ni waandikishaji wapiga kura saba tu walikuwa walemavu kwenye majimbo yote saba ya mkoani humo.

Kuhusu watendaji wa uchaguzi waliopatiwa mafunzo ili wafanye kazi siku ya uchaguzi, usawa wa kijinsia ulikosekana kwa kiwango kikubwa kwani wengi wao walikuwa wanaume. Kwa mfano, kwenye jimbo la Mchinga kati ya watendaji wa uchaguzi 588, wanawake walikuwa 232 (asilimia 39.5). Kwenye baadhi ya wilaya wanawake walikuwa wa kutosha. Mathalani, kwenye jimbo la Biharamulo Magharibi iliripotiwa kwamba asilimia 60 ya watendaji wa uchaguzi (pamoja na Wazimamizi wa Vituo, Wasimamizi wa Vituo Wasaidizi na Makarani Waongozaji) walikuwa wanawake na kati ya hao wengi walikuwa vijana. Hali hii inaashiria kwamba ushiriki wa wanawake na vijana kama watendaji wa uchaguzi katika ngazi ya wilaya ulikuwa nzuri kiasi. Ni muhimu kueleza kwamba kwenye majimbo yaliyo mengi Tume haikutoa, pale ilipoombwa na watazamaji wa muda mrefu wa REDET, data za watendaji wa uchaguzi walioteuliwa kwa kigezo cha umri, jinsia au ulemavu.

## 7.4 UANDIKISHAJI WAPIGA KURA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

Mchakato wa kuandikisha wapiga kura unafanyika mara kwa mara ili kuandikisha wapiga kura wapya na kuboresha daftari. Kifungu cha 17(1) cha Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Taifa la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2018 kinasema: “Mtu yeyote anayestahili kuandikishwa kama mpiga kura anaweza kumwomba mwandikishaji amwandikishe ndani ya kipindi ambacho uandikishaji wapiga kura unafanyika kwenye eneo husika ili kuboresha Daftari.” Kwa ajili ya

uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 mchakato wa kuboresha Daftari ulifanyika kati ya Julai 2019 na Mei 2020 nchi nzima. Kufuatia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, wapiga kura 29,188,347 waliandikishwa. Kwa mujibu wa Tume (2021), miongoni mwa watu walioandikishwa, wanawake walikuwa 14,691,743 (asilimia 50.3) na wanaume 14,496,604 (asilimia 49.67). Kwa upande wa Zanzibar, kati ya watu 566,352 walioandikishwa, wanawake walikuwa wengi (asilimia 51.9) na wanaume walikuwa wachache kidogo (asilimia 48.1). Hii inaonesha kwamba wanawake wengi zaidi waliandikishwa kuliko wanume kwa upande wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 uliwavutia vijana wengi kujiandikisha kama wapiga kura. Kwa mujibu wa Tume, zaidi ya nusu ya watu walioandikishwa walikuwa vijana wa umri wa kati ya miaka 18 hadi 35. Kama Jedwali Namba 7.3 linavyoonesha, asilimia 54 ya watu walioandikishwa walikuwa vijana.

**Jedwali Na. 7.3: Mgawanyo wa Watu Walioandikishwa kwa Umri**

| Umri | Kiume | Kike | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 18-35 | 7,849,598 | 7,895,901 | 15,745,499 | 54 |
| 36-60 | 4,583,718 | 4,558,514 | 9,142,232 | 31 |
| 61 na zaidi | 2,063,288 | 2,237,328 | 4,300,616 | 15 |
| **Jumla** | **14,496,604** | **14,691,743** | **29,188,347** | **100** |

*Chanzo: NEC, 2020*


Watu wengi wenye ulemavu walijiandikisha. Kwa mara ya kwanza Tume ilitunza kumbukumbu na kutoa data za watu wenye ulemavu waliojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la mwaka 2019 na 2020. Jedwali namba 7.4 linaonesha kwamba watu wenye ulemavu 13,211 waliandikishwa kama wapiga kura.

**Jedwali Na. 7.4: Watu wenye Ulemavu Walioandikishwa Kupiga Kura**

| Aina ya Ulemavu | Jumla |
|---|---|
| Upofu | 2,223 |
| Ulemavu wa viungo vya mwili (mikono) | 4,911 |
| Aina zingine za ulemavu | 6,077 |
| **Jumla** | **13,211** |

*Chanzo: NEC, 2020*

Vituo vingi vya kuandikisha wapiga kura vilivyotazamwa vilionekana kuwa vinafikika na vilizingatia mahitaji ya walemavu. Kama Chati Namba 7.1 unavyoonesha, kati ya vituo 614, asilimia 51 vilikuwa vinafikika na watu wenye ulemavu, asilimia 37 vilikuwa vinafikika kiasi na asilimia 12 vilikuwa havifikiki.




**Chati Na. 7.1: Ufikikaji wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga kura na Watu wenye Ulemavu**

Kulikuwa na vituo vingine vya kuandikisha wapiga kura ambavyo vilikuwa havifikiki na watu wenye ulemavu.




*Mtu mwenye ulemavu akisaidiwa kuingia kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura kwenye Manispaa ya Mtwara-Mikindani (Kagera-A)*

Kwa ujumla, uandikishaji wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulionesha ushiriki mkubwa wa wanawake na vijana kama wapiga kura. Idadi kubwa ya vituo vya kuandikisha wapiga kura havikuwa na mzingira rafiki kwa ajili ya ushiriki kamilifu wa watu wenye ulemavu.

## 7.5 UTOAJI WA ELIMU YA MPIGA KURA KWA WATU WA MAKUNDI MAALUMU

Watazamaji wa REDET waliangalia ni kwa kiasi gani utoaji wa elimu ya mpiga kura uliwalenga wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi, hususan kipindi cha kuandikisha wapiga kura na kampeni. Tume ina jukumu kisheria la kutoa elimu ya mpiga kura nchini na kuratibu na kusimamia asasi zingine ambazo zinapenda kutoa elimu hiyo. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 (sehemu ya 4C).

REDET ilibaini kwamba kampeni chache zinazohusu elimu ya mpiga kura zilifanyika kwenye wilaya nyingi nchini wakati wa mchakato wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Idadi kubwa ya watazamaji wa muda mrefu (asilimia 79) walisema kwamba hawakuona asasi yeyote ikitoa elimu ya mpiga kura kwenye maeneo yao ya kazi. Ni asilimia 36 tu ya watazamaji wa muda mrefu ambao walishuhudia baadhi ya shughuli za utoaji elimu ya mpiga kura zikifanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi/Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwenye maeneo fulani ya nchi kwa kutumia televisheni, redio na vipeperushi. Elimu hiyo finyu ya mpiga kura ilitolewa kwa njia ya redio (asilimia 53), televisheni (asilimia 27) na vipeperushi (asilimia 21). Kwa asilimia kubwa, hakukuwa na elimu yeyote ya mpiga kura iliyolenga makundi maalumu. Badala yake elimu ya mpiga kura juu ya uandikishaji ililenga wapiga kura wote waliopenda kujiandikisha bila kujali tofauti zao. Ilikuwa ni elimu ya mpiga kura iliyowalenga watu wote.

Kwenye maeneo machache elimu iliyolenga makundi maalumu ilitolewa. Kwa upande wa Kwimba, SHIVYAWATA (asasi ya kiraia ya watu wenye ulemavu) ilitoa elimu ya mpiga kura na kufanya kampeni ya kuvifanya vituo vya kupigia kura vifikike na watu hao. Kwenye jimbo la Arusha Mjini vipeperushi vichache vilivyowalenga watu wenye ulemavu viliandikwa hivi *Kijana na Kura yako: Utaratibu wa Kupiga Kura*. Vipeperushi hivyo viliwekwa katika masoko na vituo vya basi na *Tanzania Youth Vision Association*. Mkoani Kigoma, asasi ya kiraia ijulikanayo kwa jina la *Upendo Women Disabled* ilikutwa ikitoa elimu ya mpiga kura iliyowalenga zaidi watu wenye ulemavu.




*Kipeperushi cha kutolea elimu ya mpiga kura chenye jina "Kijana na Kura yako: Utaratibu wa Kupiga Kura" katika kituo cha mabasi cha Kilombero kata ya Levolosi, jimbo la Arusha Mjini*.

Wakati wa kampeni za uchaguzi watazamaji wa muda mrefu wa REDET walishuhudia shughuli chache za elimu ya mpiga kura zilizolenga makundi maalumu zikifanyika. Kama Jedwali Namba 7.5 linavyoonesha, watazamaji 1,830 kati ya watazamaji 5,131 (asilimia 36) waliona elimu ya mpiga kura ikitolewa ili kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uchaguzi. Ni watazamaji 1,221 (asilimia 24) tu walioshuhudia elimu ya mpiga kura ikitolewa ili kuongeza ushiriki wa watu wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 7.5: Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

| Swali | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (asilimia) |
|---|---|---|---|
| Je, ulishuhudia elimu yeyote ya mpiga kura iliyokusudiwa kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ikitolewa? | 1830 (35.7) | 3301 (64.3) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia elimu yeyote ya mpiga kura iliyokusudiwa kuongeza ushiriki wa vijana katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ikitolewa? | 1779 (34.7) | 3352 (65.3) | **5131 (100)** |
| Je, ulishuhudia elimu yeyote ya mpiga kura iliyokusudiwa kuongeza ushiriki wa watu wenye ulemavu katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ikitolewa? | 1221 (23.8) | 3910 (76.2) | **5131 (100)** |

## 7.6 UZINGATIAJI WA JINSIA WAKATI WA KUTEUA WAGOMBEA

Je, vyama vya siasa vilizingatia jinsia kwenye mchakato wa kuteua wagombea wa nafasi mbalimbali? Kwa kuzingatia mambo yaliyoonekana jibu ni kwamba vyama havikuzingatia hilo. Wanaume walikuwa wengi zaidi ya wanawake kama watia nia na wagombea wa karibu nafasi zote. Kwa upande wa Zanzibar, kati ya watia nia 32 wa CCM, wanawake walikuwa watano tu (asilimia 15).[17] Kwa upande wa Lindi Mjini, kati ya watia nia 19 wa kiti cha ubunge wanawake walikuwa watatu tu (asilimia 15.8). Kwenye jimbo la Mchinga kati ya watia nia 21 wanawake walikuwa wanne tu (asilimia 19). Kwa upande wa uchaguzi wa madiwani kati ya watia nia 93 wa Lindi Mjini wanawake walikuwa 13 (asilimia 14). Nachingwea ilikuwa na watia nia waliotaka kugombea udiwani 164 kwenye kata 36. Kati ya hao, wanawake walikuwa 28 (asilimia 17). Kwenye jimbo la Bukoba Mjini, CHADEMA ilikuwa na wastani wa asilimia 14 na CCM asilimia 12 ya wanawake waliotia nia kama wagombea udiwani.

Ni wanawake wachache sana walifanikiwa kwenye ushindani ndani ya vyama na ni wanawake wachache zaidi waliteuliwa na Tume kugombea nafasi mbalimbali. Mathalani, kwenye jimbo la Lindi kati ya wagombea 75 wa udiwani wanawake walikuwa tisa (asilimia 12). Kwa upande wa Kilwa Kusini, kati ya wagombea 36 walioteuliwa wanawake walikuwa wawili tu. Nachingwea ilikuwa na wagombea 84 walioteuliwa na wanawake walikuwa watano tu (asilimia 6). Jimbo la Arusha Mjini lilikuwa na wanawake watatu (asilimia 4) kati ya wagombea 74 wa viti vya udiwani kwenye jimbo lote. Kwenye jimbo la Nyamagana, kati ya wagombea udiwani 18 wa CCM mwanamke alikuwa mmoja tu. Kwenye jimbo la Mbeya Mjini, kati ya wagombea udiwani 64 wanawake walikuwa sita (asilimia 5.5.). Mkoa wa Ruvuma ulikuwa na wagombea udiwani 186, lakini wanawake walikuwa 13 tu. Hali hii inaashiria kwamba ni wanawake wachache sana wanajitokeza kugombea nafasi za uongozi. Idadi ya watu wenye ulemavu ilikuwa ndogo sana kwenye vyama vya siasa vyote. Kigoma Mjini wanawake wawili wenye ulemavu waliogombea ubunge wa viti maalumu kupitia CCM hawakufanikiwa kwani hawakufikisha idadi ya kura iliyohitajika.[18]

17 https://www.malunde.com/2020/07/tamwa-siasa-wanawake.html

18 Usaili na Ndugu Mohammad Nshekanabo, Mratibu wa Mradi, uliofanyika katika ofisi za UDW, kata ya Katubuka, tarehe 26 Oktoba 2020

### 7.6.1 Wagombea Urais Wanawake Walioteuliwa

Kama Jedwali Namba 7.6 linavyoonesha, wagombea wa kiume walitawala mbio za urais. Wanawake walikuwa wawili (asilimia 13) kati ya wagombea urais 15. Kwa upande wa wagombea wenza, idadi ya wanaume ilikuwa mara mbili zaidi ya ile ya wanawake. Kwa mara ya kwanza chama cha siasa, Demokrasia Makini, kiliteua mwanamke mgombea urais na mwanamke mgombea mwenza.

**Jedwali Na. 7.6: Mgawanyo wa Wagombea wa Kiti cha Urais cha Muungano kwa Jinsia**

| Na. | Chama cha Siasa | Mgombea Urais | | Mgombea Mwenza | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiume | Kike | Kiume | Kike |
| 1 | CCM | 1 | 0 | 0 | 1 |
| 2 | ADA-TADEA | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 3 | NRA | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 4 | SAU | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 5 | Demokrasia Makini | 0 | 1 | 0 | 1 |
| 6 | NCCR-Mageuzi | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 7 | CUF | 1 | 0 | 0 | 1 |
| 8 | ACT-Wazalendo | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 9 | ADC | 0 | 1 | 1 | 0 |
| 10 | UPDP | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 11 | DP | 1 | 0 | 0 | 1 |
| 12 | CHAUMMA | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 13 | AAFP | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 14 | UMD | 1 | 0 | 1 | 0 |
| 15 | CHADEMA | 1 | 0 | 1 | 0 |
| | **Jumla** | **13** | **2** | **11** | **4** |

*Chanzo: NEC, 2020*

Wagombea wawili wanawake waliteuliwa na vyama viwili vidogo vyenye rasilimali chache na kwa hiyo kuwa vigumu kwa wao kufanya kampeni zenye manufaa nchi nzima.




*Mgombea urais wa Demokrasia Makini, Bi. Cecilia Augustino Mmanga, akifanya kampeni katika kituo cha mabasi cha Mbinga tarehe 13 Oktoba 2020*.

### 7.6.2 Wagombea Ubunge Wanawake Walioteuliwa

Kwa upande wa uchaguzi wa ubunge, mchakato wa uteuzi kwenye majimbo mengi uliwapendelea wanaume zaidi ya wanawake. Kama Jedwali Namba 7.7 linavyoonesha, kati ya wagombea ubunge 1,235 kutoka vyama vyote vilivyogombea wanawake walikuwa 291 (asilimia 23.6). Hili ni ongezeko dogo ukilinganisha na mwaka 2015 ambapo wanawake walikuwa asilimia 19 ya wagombea ubunge wote. Kwenye Mkoa wa Dar es Salaam kati ya wagombea 144, wagombea 65 (asilimia 45) walikuwa wanawake. Kwenye Mkoa wa Mjini Magharibi wa Zanzibar wanawake walikuwa asilimia 37.5 kati ya wagombea ubunge 120. Pamoja na ongezeko hilo la idadi ya wagombea ubunge wanawake kutoka asilimia 13 katika uchaguzi wa mwaka 2005 hadi asilimia 23.7 katika uchaguzi wa mwaka 2020, bado wanawake ni wachache ukilinganisha na wanaume. Ingawa idadi kubwa ya wanawake waligombea nafasi za uongozi Mkoani Dar es Salaam, wengi waligombea nafasi ambazo hazikuwa za ubunge. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, CCM, CHADEMA, CUF na ACT-Wazalendo vilikuwa vyama vikuu lakini vilikuwa na idadi ndogo sana ya wagombea wanawake. CCM ilikuwa na wagombea wa kike wawili, mmoja kwenye jimbo la Temeke na mwingine kwenye jimbo la Segerea, na ACT-Wazalendo ilikuwa na mgombea mmoja wa kike kwenye jimbo la Kigamboni. Kukosekana kwa wagombea wa kike kulijitokeza sana kwenye majimbo kama vile Njombe Mjini ambako hakuna mwanamke aliyegombea ubunge au udiwani.

**Jedwali Na. 7.7: Mgawanyo wa Wabunge wa Kuteuliwa kwa Jinsia**

| Na. | Chama cha Siasa | Kiume | Kike | Jumla | Asilimia ya Wabunge Wanawake |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CCM | 239 | 25 | **264** | 9.5 |
| 2 | CHADEMA | 150 | 59 | **209** | 28.2 |
| 3 | ACT-Wazalendo | 135 | 21 | **156** | 13.5 |
| 4 | NCCR-Mageuzi | 63 | 20 | **83** | 24.1 |
| 5 | CUF | 113 | 40 | **153** | 26.1 |
| 6 | TLP | 17 | 8 | **25** | 32.0 |
| 7 | CHAUMMA | 22 | 6 | **28** | 21.4 |
| 8 | ADC | 33 | 15 | **48** | 31.3 |
| 9 | AAFP | 15 | 10 | **25** | 40.0 |
| 10 | NRA | 21 | 8 | **29** | 27.6 |
| 11 | UDP | 24 | 9 | **33** | 27.3 |
| 12 | UPDP | 8 | 13 | **21** | 61.9 |
| 13 | SAU | 12 | 7 | **19** | 36.8 |
| 14 | DP | 17 | 7 | **24** | 29.2 |
| 15 | UMD | 3 | 13 | **16** | 81.3 |
| 16 | ADA-TADEA | 22 | 11 | **33** | 33.3 |
| 17 | MAKINI | 32 | 11 | **43** | 25.6 |
| 18 | NLD | 7 | 2 | **9** | 22.2 |
| 19 | CCK | 11 | 6 | **17** | 35.3 |
| | | **944** | **291** | **1,235** | **23.6** |

*Chanzo: NEC, 2020*

### 7.6.3 Uteuzi wa Wanawake wa Viti Maalumu

Kuhusu viti maalumu vya wanawake, hakukuwa na njia moja ya uteuzi kwa vyama vyote katika ngazi zote. Kila chama cha siasa kilikuwa na namna yake ya kuteua wanawake wa viti maalumu. Kwa upande wa CCM, mchakato wa kuteua wanawake wa viti maalumu vya ubunge ulifanyika katika ngazi ya wilaya ambapo wawakilishi wa wanawake kutoka matawi yote ya CCM kwenye wilaya walipata fursa ya kumpigia kura mgombea waliompenda kupitia kura za upendeleo maalumu. Mchakato ulikuwa hivyohivyo katika ngazi ya kata. Kwa upande wa CHADEMA, mchakato wa kuteua wabunge wa viti maalumu wanawake ulifanyika kupitia Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA) au Baraza la Vijana la CHADEMA (CHAVITA) kwa kupiga kura. Baadaye majina yao yalipelekwa kutoka ngazi ya wilaya ili yaende kwenye Kamati Kuu kwa ajili ya uteuzi wa

mwisho. Kwenye baadhi ya maeneo CHADEMA ilitumia njia ya kupendekeza nani awe mgombea. Vyama vingine vilitumia upigaji kura wa upendeleo maalumu. Hata hivyo, baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa uteuzi wa wabunge wa viti maalumu wa CHADEMA ulichukua mwelekeo tofauti kama inavyoelezwa kwenye Sehemu ya Nane.

## 7.7 USHIRIKI KATIKA KAMPENI ZA UCHAGUZI

Vyama vya siasa vilitofautiana ki uwezo wa kufanya kampeni za uchaguzi kwenye majimbo mbalimbali. Kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 zilivutia makundi yote ya kijamii, hususan vijana na wanawake. Ushiriki wa wanawake na vijana katika kampeni za uchaguzi ulikuwa mkubwa zaidi ya ule wa wanaume. Pamoja na kuhudhuria mikutano ya kampeni ya vyama vya siasa mbalimbali, wanawake walikuwa watoa burudani pia.




*Kikundi cha kwaya kikiburudisha watu waliohudhuria mkutano wa kampeni wa CUF uliofanyika Mchinga.*



*Wanawake wakicheza kwenye mkutano wa kampeni wa CCM kwenye jimbo la Kigoma Mjini.*

REDET ilibaini kwamba mazingira ya kampeni yalikuwa salama kwa wanawake na makundi mengine yaliyo hatarini. Kama Jedwali Namba 7.8 linavyoonesha, kulikuwa na matukio machache (134 kati ya 2,892, au asilimia 7) ambapo wagombea wa kike walishambuliwa au kuzomewa.

**Jedwali Na. 7.8: Usalama na Vitendo dhidi ya Wagombea Wanawake na Wafuasi wa Vyama wa Kike**

| Swali | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| Je, mazingira ya kampeni ni salama kwa wanawake? | 2129 (73.5) | 768 (26.5) | 2897 (100) |
| Je, ulishuhudia wagombea wa kike wakitishwa/ kuzomewa? | 134 (6.7) | 2758 (93.3) | 2892 (100) |
| Je, ulishuhudia kuonyeshwa kwa jumbe za uchochezi na matusi zilizokusudiwa kumnyanyasa/kumdhalilisha mgombea au chama? | 429 (2.7) | 4702 (97.3) | 5131 (100) |

*Chanzo: REDET, 2020*

Yalikuwapo matukio machache ya vurugu dhidi ya wagombea wa kike yaliyojitokeza kwenye wilaya chache. Kwa mfano, kwenye Wilaya ya Kigoma Mjini REDET ilishuhudia tukio kwenye mkutano wa kampeni ambapo mgombea wa kiume alimwambia mpinzani wake ambaye alikuwa mgombea wa kike kwamba alipendekezwa na chama chake baada ya kudaiwa kufanya mapenzi.[19] Kwenye Manispaa ya Tabora, kauli za matusi kuhusu jinsia ya mtu zilitolewa na mgombea wa kiume wa CCM dhidi ya mgombea wa kike wa CHADEMA, Hawa Mwaifunga, ambaye mume wake anatokea Arusha. Mgombea huyo wa kiume alidai kwamba kwa kuwa Hawa alikuwa ameolewa na mume anayetokea Arusha basi Hawa hakutokea jimboni hapo. Alisema pia kwamba mwanamke akiolewa anakuwa mtu wa sehemu anayotokea mume wake. Kwa hivyo, Hawa hakuwa na haki ya kugombea kwenye jimbo hilo. Kwa hiyo, watu wa Manispaa ya Tabora walihimizwa "kutoruhusu jimbo liongozwe na mtu ambaye siyo mtu wa eneo hilo tena."

Katika mkutano wa kampeni wa Sokoni Dampo wa tarehe 18 Oktoba, mpinzani wa Bi. Mwaifunga alidai kwamba alikutwa amelala na mume wa mtu usiku uliopita: "Bado hajachaguliwa lakini ameshaanza kuchukua waume zenu; hali itakuwaje

19 Kampeni za Clayton Chipando ambaye alikuwa mgombea udiwani wa ACT-Wazalendo zilizofanyika Mwanga Kaskazini tarehe 4 Oktoba 2020

akichaguliwa!" Hizi zilikuwa kauli zilizohusu jinsia ya mtu zinazotokana na mila na desturi za mfumo dume. Tarehe 22 Oktoba wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika Zahanati ya Ng'ambo, mgombea wa ACT-Wazalendo, Nassoro Kirumbi Ruti, alimtukana mgombea wa kike wa CCM wa kata ya Kidongo Chekundu akisema kwamba alikuwa *msimbe* (hajaolewa) na kwa hiyo hastahili kuwa kiongozi.

## 7.7 KUHUDUMIA MAKUNDI MAALUMU SIKU YA UCHAGUZI

Kutokana na kukosekana kwa data juu ya wapiga kura waliojitokeza siku ya uchaguzi ilibainika kwamba wanawake na vijana walio wengi walijitokeza katika vituo vingi vya kupigia kura. Kwa mujibu wa taarifa za watazamaji wa muda mrefu na wa muda mfupi, mazingira ya kupigia kura kwa ujumla yalikuwa salama. Walipoulizwa kama kulikuwa na vurugu zozote au vitisho dhidi ya wapiga kura vituoni, asilimia 97 ya watazamaji wa muda mrefu na wa muda mfupi walisema hakukuwa na matukio ya aina hiyo na asilimia 2.2 walisema yaikuwapo. Jedwali Namba 7.9 linaonesha kuwa makundi maalumu yalipewa upendeleo wakati wa kupiga kura, yaani wanawake wajawazito, akina mama wenye watoto na watu wenye ulemavu.

**Jedwali Namba 7.9: Kuhudumia Makundi Maalumu Siku ya Uchaguzi**

| Swali | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| Je, watu wenye ulemavu waliweza kukifikia kituo cha kupigia kura? | 2380 (93.2) | 173 (6.8) | **2553 (100)** |
| Je, wanawake wajawazito na akina mama wenye watoto walipewa kipaumbele? | 2515 (98.5) | 38 (1.5) | **2553 (100)** |
| Je, watu wenye ulemavu walipewa kipaumbele wakati wa kupiga kura? | 2506 (98.2) | 47 (1.8) | **2553 (100)** |
| Je, watu wenye ulemavu wa macho walipewa karatasi za kupigia kura za nukta nundu? | 1697 (66.5) | 856 (33.5) | **2553 (100)** |

*Chanzo: REDET, 2020*

Kwa ujumla kati ya wapiga kura walioandikishwa 29,754,696, watu 15,091,950 (asilimia 50.7) walipiga kura. Takribani nusu ya wapiga kura walioandikishwa (asilimia 49.3) walikwenda kupiga kura. Wakati wa uchaguzi mkuu wa 2015, asilimia 67 ya watu waliojiandikisha walipiga kura (Ripoti ya NEC, 2016, 2020).

## 7.8 MATOKEO YA UCHAGUZI YA WAGOMBEA WA KIKE

REDET ilishuhudia kwamba wagombea wa kiume walipata matokeo mazuri zaidi ya wagombea wa kike katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa upande wa uchaguzi wa wabunge, idadi ya wanawake waliochaguliwa kama wabunge iliongezeka kidogo sana kutoka 25 mwaka 2015 hadi 26 mwaka 2020. Jedwali Namba 7.10 linaonesha idadi ya wanawake waliochaguliwa kama wabunge wa Bunge la Muungano.

**Jedwali Na. 7.10: Wabunge Wanawake wa Kuchaguliwa katika Uchaguzi wa Mwaka 2020**

| Na. | Jina | Chama cha Siasa | Jimbo |
|---|---|---|---|
| 1 | Dkt. Tulia Ackson | CCM | Mbeya Mjini |
| 2 | Bi. Jesca Msambatavangu | CCM | Iringa Mjini |
| 3 | Bi. Shamsia Mtamba | CUF | Mtwara Vijijini |
| 4 | Profesa Joyce Ndalichako | CCM | Kasulu Mjini |
| 5 | Bi. Stella Manyanya | CCM | Nyasa |
| 6 | Bi. Margareth Sitta | CCM | Urambo |
| 7 | Bi. Anna Lupembe | CCM | Nsimbo |
| 8 | Bi. Dorothy George | CCM | Temeke |
| 9 | Bi. Hamida Abdallah | CCM | Lindi Mjini |
| 10 | Bi. Maimuna Mtanda | CCM | Newala Vijijini |
| 11 | Dkt. Angelina Mabula | CCM | Ilemela |
| 12 | Bi. Paulina Gekul | CCM | Babati Mjini |
| 13 | Bi. Bonnah Kamoli | CCM | Segerea |
| 14 | Bi. Mwanahamis Kasimu Said | CCM | Magomeni |
| 15 | Bi. Jenista Mhagama | CCM | Peramiho |
| 16 | Bi. Condester Sichalwe | CCM | Momba |
| 17 | Bi. Zubeda Hamisi Shaibu | CCM | Mfenesini |
| 18 | Bi. Aida Khehani | CHADEMA | Nkasi Kaskazini |
| 19 | Bi. Salma Kikwete | CCM | Mchinga |
| 20 | Bi. Leah Jeremiah | CCM | Meatu |
| 21 | Bi. Anne Kilango Malecela | CCM | Same Magahribi |
| 22 | Bi. Ummy Mwalimu | CCM | Tanga Mjini |
| 23 | Dkt. Ashatu Kijaji | CCM | Kondoa |
| 24 | Bi. Maryam Omar Said | CUF | Pandani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25 | Bi. Mwantakaje H. Juma | CCM | Bububu |
| 26 | Bi. Rehema Migilla | CCM | Ulyankulu |

*Chanzo: NEC, 2020*

Idadi kubwa ya wabunge wanawake kutoka upinzani walipoteza viti vyao katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kati ya wabunge 26 walioshinda, 23 walitoka CCM na watatu walitoka vyama vya upinzani. Hali kadhalika, kupitia viti maalumu, wanawake 113 wamejiunga na Bunge. Ni vyama viwili tu vina wabunge wanawake wa viti maalumu. CCM ilipata viti 94 na CHADEMA viti 19. Wakati huohuo Bi. Samia Suluhu Hassan alitetea kiti chake cha Umakamu wa Rais katika Serikali ya Muungano. Manaibu Spika wa kike wa zamani pia walitetea viti vyao kwenye Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi.

### 7.8.1 Ukinzani wa Suala la Wabunge wa Viti Maalumu wa CHADEMA

Kwa mujibu wa sheria, CHADEMA kilistahili kuwa na wabunge 19 wa viti maalumu. Mchakato wa kuchagua wabunge wa viti maalumu wa CHADEMA ulikumbwa na matatizo mengi kwa sababu CHADEMA ilisema kwamba matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yalikuwa ya uongo. Katikati ya mkwamo huo, Katibu Mkuu wa CHADEMA, Ndugu John Mnyika, alitangaza kwamba CHADEMA isingepeleka orodha rasmi ya wabunge wanawake wa viti maalumu kwa Tume kwa ajili ya uteuzi. Hata hivyo, uongozi wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA uliamua kuendelea na mchakato wa uteuzi na kuchagua wanawake 19 kwa ajili ya viti maalumu. Wanawake hao walifukuzwa uanachama baada ya kuapishwa na Spika wa Bunge, Ndugu Job Ndugai. Wanawake hao ni mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CHADEMA, Bi. Halima Mdee na wengine 18, yaani Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Pareso, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Salome Makamba, Conchesta Rwamlaza, Agnesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau na Stela Fiyao. Wabunge hao wote walikata rufaa kupinga uamuzi huo. Cha kufurahisha ni kwamba Spika wa Bunge alisema anawatambua kama wabunge ingawa walikuwa wamefukuzwa uanachama.



***Picha Na. 7: Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CHADEMA, Bi. Halima Mdee, akiapishwa na Spika wa Bunge tarehe 24 Novemba 2020.***

## 7.9 HITIMISHO

Ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mzunguko wa uchaguzi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 nchini Tanzania ulikuwa mkubwa kiasi. Ingawa inawezekana kupata data zinazohusu jinsia kwenye mchakato wa uchaguzi bado ni vigumu kubaini hali halisi ya ushiriki wa vijana na watu wenye ulemavu, hususan watia nia, wagombea na wawakilishi waliochaguliwa. Lakini ni muhimu kukubali kwamba kwa mara ya kwanza toka chaguzi za vyama vingi zianze mwaka 1995, Tume imetoa data ambazo hazikunyambuliwa ili kuonesha jinsia ya wapiga kura walioandikishwa kwa kuonesha idadi ya watu wenye ulemavu. Haya ni mafanikio makubwa ambayo ni lazima yatambuliwe na kuongezwa ili kuingiza vipengele vingine vya mzunguko wa uchaguzi. Hali kadhalika, mazingira ya uchaguzi wakati wa kampeni na siku ya uchaguzi yalikuwa salama kiasi kwa makundi maalumu na makundi yaliyopo hatarini kuweza kushiriki. Ingawa matukio ya kutukana wagombea wa kike na wafuasi wa vyama wa kike yalikuwa machache, matokeo yanaonesha kwamba kulikuwa na matukio ya vurugu za kijinsia kwenye baadhi ya maeneo. Pia, ni muhimu kukubali kwamba wanawake na vijana walikuwa kundi kubwa la wapiga kura waliojiandikisha katika uchaguzi wa mwaka 2020. Mapungufu makubwa yaliyojitokeza ni utoaji finyu wa elimu ya mpiga kura kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Inawezekana hali hii ilichangia kupunguza idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ukilinganisha na uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

# SURA YA NANE

# UCHAGUZI WA ZANZIBAR

## 8.1 UTANGULIZI

Uchaguzi wa mwaka 2020 wa Zanzibar ulitarajiwa kuwa wa upinzani kwa sababu ya mabadiliko makubwa na kujipanga upya kwa wahusika wa uchaguzi, vikiwamo vyama vya siasa na wagombea. Tangu kuanzishwa tena kwa siasa za ushindani, Zanzibar imeshuhudia mapambano ya kisiasa kati ya CCM na CUF. Ushindani kati ya vyama hivyo ulikuwa mkubwa sana mwaka 1995 na 2010 kiasi kwamba mshindi wa uchaguzi wa rais Zanzibar ilibidi aamuliwe kwa pungufu ya kura asilimia moja kati ya kura zote zilizohesabiwa. Muundo wa kisiasa ulikuwa tofauti mwaka 2020. Ingawa umaarufu wa CUF ulikuwa unapungua, ACT-Wazalendo kimekuwa chama kikuu cha upinzani Zanzibar. Kwa upande wa wagombea, Seif Sharif Hamad aligombea mara ya sita mfululizo kama mgombea wa upinzani, lakini CCM ilikuwa na mgombea urais mpya, yaani Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Sababu kubwa ya pili na tukio tata kuhusu uchaguzi mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2020 lilikuwa ni upigaji kura wa mapema kama kifungu cha 82(1) cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018 kinavyotaka.

Sura hii inaangalia utazamaji wa uchaguzi uliofanywa na REDET, ikiangalia hatua zote za mchakato wa uchaguzi. Sehemu ya Kwanza inaangalia kwa ufupi matukio yaliyotengeneza mazingira ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa upande wa Zanzibar na Sehemu ya Pili inatazama uteuzi wa wagombea ambao ulikuwa na utata. Sehemu ya Tatu inaangalia masuala ya kampeni na matukio na athari zake katika uchaguzi na Sehemu ya Nne inajikita kwenye matukio yanayohusiana na upigaji kura wa mapema. Sehemu ya Tano inatazama siku ya kupiga kura, uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo. Sehemu ya Mwisho inatazama hali ilivyokuwa baada ya matokeo kutangazwa, na inatoa hitimisho na mapendekezo.

## 8.2 MUKTADHA WA KISIASA KUELEKEA UCHAGUZI WA ZANZIBAR WA MWAKA 2020

Kama chaguzi zilizopita, Wazanzibari waliwapigia kura wagombea watano siku ya tarehe 27 na 28 Oktoba 2020. Walimchagua Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani. Walimpigia kura rais wa Jamhuri wa Muungano na wabunge wa Bunge la Jamhuri wa Muungano. Ili kuelewa muktadha wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa upande wa Zanzibar ni muhimu kuangalia

matukio makubwa yaliyotokea kipindi cha maandalizi ya uchaguzi. Moja ya matukio makubwa ni kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Zanzibar na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Ndugu Jecha Salim Jecha, akidai kuwa mchakato wa uchaguzi ulikuwa na dosari nyingi (TEMCO, 2016). Kitendo hicho kilifanyika tarehe 28 Oktoba 2015, siku tatu tu baada ya mchakato wa kupiga kura kumalizika. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar aliamrisha uchaguzi mpya ufanyike mapema mwaka 2016. Haikushangaza kwamba Chama cha CUF ambacho kilidai kuwa kilishinda uchaguzi wa Rais wa mwaka 2015 kilisusia uchaguzi wa marudio. Matokeo yake CCM ilichukua viti vyote Zanzibar. Hii pia ilimaanisha kwamba CUF isingeweza kuwa sehemu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU) kama ilivyokuwa tangu mwaka 2010.

Kwa kuwa nje ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, CUF ilikosa fursa ya kuwakilisha kambi ya upizani kwenye vyombo vingi muhimu vya kufanya maamuzi na ilishindwa kuzuia mabadiliko ya kisheria ambayo yangeweza kuiathiri kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Mathalani, Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2017 na Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2018 zilipitishwa kipindi hicho. Hakukuwa na malalamiko yeyote kuhusu Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2017 lakini Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2018 iliyofuta Sheria ya Uchaguzi Zanzibar Namba 11 ya mwaka 1984 ilikosolewa sana na kambi ya upinzani huko visiwani Zanzibar. Kifungu cha 82(1)-(2) cha sheria hiyo kinaitaka Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuandaa mazingira kwa ajili ya upigaji kura wa mapema kwa watu ambao watashiriki katika kusimamia uchaguzi, pamoja ya watendaji wa Tume na maafisa usalama, nafasi ambayo ilithibitishwa na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Ndugu Thabit Faina, wakati anafanya mazungumzo na kituo cha televisheni cha Azam tarehe 19 Septemba 2019. Watu waliopiga kura mapema walimpigia kura Rais wa Zanzibar tu.

Tukio lingine muhimu lililoathiri uchaguzi wa Zanzibar wa mwaka 2020 ni kuibuka kwa ACT-Wazalendo na kuanguka kwa CUF. Jambo tunaloliangalia hapa ni uamuzi wa Profesa Lipumba aliouchukua tarehe 13 Juni 2020 wa kujirudisha kama mwenyekiti wa CUF, baada ya kujiuzulu kwake miezi 10 iliyopita kupinga kupokelewa kwa Ndugu Lowassa kama mgombea urais. Uamuzi huo tata wa Profesa Lipumba ulipata baraka za Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye alimtambua kama mwenyekiti halali wa chama hicho kupitia barua yake ya tarehe 23 Septemba 2016. Uamuzi huo ulipingwa na Seif Sharif Hamad ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa CUF na wafuasi wake. Mwaka 2016 kesi ilifunguliwa na bodi ya wadhamini wa

CUF wakiitaka Mahakama Kuu ibatilishe uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa wa kumtambua Profesa Ibrahim Lipumba. Mahakama Kuu ilitupilia mbali ombi hilo tarehe 18 Machi 2019 ikisema kwamba barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliyomtambua Profesa Lipumba kama mwenyekiti halali wa CUF ilikuwa sahihi kisheria.

Mara bada ya uamuzi huo wa Mahakama Kuu Seif Sharif Hamad na wafuasi wake waaminifu, wakiwemo baadhi ya viongozi wa CUF, walihamia ACT-Wazalendo. Ni dhahiri kwamba Ndugu Hamad na wafuasi wake walikuwa wamezungumza na ACT-Wazalendo na Kiongozi wake Mkuu, Zitto Zuberi Kabwe. Katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya uamuzi huo wa Mahakama Kuu, Ndugu Hamad alithibitisha kwamba alikuwa amezungumza na viongozi wengine wa CUF na kwa pamoja walikubaliana kutafuta jukwaa lingine kuendelea na mapambano yao ya kisiasa (Said 2019). Kuhamia kwake ACT-Wazalendo kulikuwa ni mwanzo wa wanachama wengi wa CUF huko Zanzibar, hususan Pemba, kuhamia ACT-Wazalendo na kukiacha chama cha CUF kikiwa kimedhoofika mno. Mara moja Ndugu Hamad aliteuliwa kuwa Mshauri Mkuu wa chama na mwezi Januari 2020 aligombea na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho. Kwa hiyo, ACT-Wazalendo kikawa chama kikuu cha upinzani Zanzibar na kukiondoa chama cha CUF. Wachambuzi wa masuala ya kisiasa walitabiri kwamba ACT-Wazalendo ingefanya vizuri kwenye uchaguzi wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wa Zanzibar, hususan Pemba ambako kaulimbiu ilikuwa *Alipo Tupo*, ikimaanisha kwamba wangejiunga na chama chochote cha siasa ambacho Maalim Seif Sharif Hamad angeamua kuhamia.

## 8.3 UTEUZI WA WAGOMBEA ZANZIBAR

Uteuzi wa wagombea Zanzibar ulifanywa na vyama na vyombo vya kusimamia uchaguzi. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 vyama vitatu vya siasa, yaani CCM, ACT-Wazalendo na CHADEMA vilifanya uteuzi kupitia michakato ya wazi na ya kishindani au ya nusu ushindani. CCM na ACT-Wazalendo walifanya teuzi za ndani ya vyama za wazi kuanzia ngazi ya jimbo hadi ngazi ya taifa.

### 8.3.1 Uteuzi wa Wagombea Urais Zanzibar Ndani ya CCM

Uteuzi wa mgombea urais Zanzibar kupitia CCM ungewavutia watia nia wengi kwani mihula miwili ya Dkt. Ali Mohamed Shein ilikuwa inamalizika. Ilikuwa hivyo kwani watia nia 33 walichukua fomu ili wagombee urais. Mgombea mmoja

ajulikanae kwa jina la Hussein Ibrahim Makungu alijitoa katika kinyang'anyiro hicho. Chini ya Mwenyekiti Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar mkutano wa Kamati Maalumu ya CCM Zanzibar ulipendekeza majina matano kwa kamati ya CCM Dodoma ili yachujwe zaidi na kufanya uteuzi: Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Dkt. Khalid Salum Mohammed, Ndugu Shamsi Vuai Nahodha, Profesa Makame Mbarawa na Ndugu Khamis Mussa Omar. Kamati Kuu ya CCM ilipitisha majina matatu na kuyapendekeza kwa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa: Dkt. Hussein Mwinyi, Dkt. Khalid Salum Mohammed na Ndugu Shamsi Vuai Nahodha. Dkt. Hussein Mwinyi aliibuka mshindi kwa kupata kura 129 (asilimai 78.6) na kuteuliwa tarehe 10 Julai 2020. Dkt. Khalid Salum Mohamed alipata kura 19 (asilimia 11.6) na Shamsi Vuai Nahodha alipata kura 16 (asilimia 9.8).

### 8.3.2 Uteuzi wa Wagombea Ubunge Ndani ya CCM

CCM ilitangaza nafasi za kuchaguliwa za kisiasa na wanachama waliombwa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi zilizojazwa vizuri kulingana na ratiba ambayo ilikuwa imekubaliwa. Fomu hizo zilipitiwa na kamati ya siasa ya wilaya kabla mapendekezo hayajapelekwa kwenye kamati ya siasa ya mkoa. Matokea yaliyopitiwa yalipelekwa kwenye Kamati Kuu ambayo maamuzi yake ya mwisho yalipitishwa na Halmashari Kuu. Tofauti na chaguzi zilizotangulia, CCM ilishuhudia wanachama wake wengi wakitafuta kuteuliwa. Karibu majimbo yote yalikuwa na watia nia zaidi ya kumi wa kiti cha ubunge au Baraza la Wawakilishi. Dimani ilivunja rekodi kwa kuwa na wagombea ubunge 178 na wagombea viti vya uwakilishi 90. Viti vya udiwani viligombaniwa na watia nia 125.

### 8.3.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ACT-Wazalendo

ACT-Wazalando na CHADEMA walifuata mchakato sawa na ule wa CCM. Tofauti ilikuwa katika idadi ya watia nia kwani baadhi ya majimbo yalikuwa na watia nia wachache waliochukua fomu za kugombea ubunge na hivyo kupunguza kiwango cha ushindani.

### 8.3.4 Uteuzi wa Vyombo vya Kusimamia Uchaguzi na Pingamizi

#### 8.3.4.1 Uteuzi wa Wagombea Urais

Baada ya kupata uteuzi kwenye vyama vya siasa husika wagombea walihitaji kuteuliwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar au Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa

upande wa Zanzibar na Muungano. Uteuzi wa vyombo vya kusimamia uchaguzi ulikuwa wa mwisho na ni wagombea ambao walipitishwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo waliotokea katika karatasi za kura. Vifungu vya 43-45 vya Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2018 vinaonesha sifa za kuteuliwa kugombea urais Zanzibar ambazo zinaendana na zile zilizopo kwenye Ibara ya 68 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

#### 8.3.4.2 Pingamizi Dhidi ya Teuzi za Wagombea Urais

Kifungu cha 51(1) cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar ya mwaka 2018 kinaruhusu pingamizi kuwekwa dhidi ya wagombea wanaotafuta uteuzi kwa vigezo vitatu: kwanza kama taarifa zilizopo katika fomu hazimtambulishi mgombea kiasi cha kutosha, mgombea ametoa taarifa za uongo katika fomu ya uteuzi na tatu kama fomu ya uteuzi haikujazwa au haikuwasililishwa kwa mujibu wa miongozo ya kisheria. Kifungu cha 50 cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar kinaitaka Tume ya Uchaguzi Zanzibar au Wasimamizi wa Uchaguzi kuweka fomu zote sehemu ya wazi kwa saa 24 ili zihakikiwe na pingamizi ziwekwe. Sheria pia inaruhusu wagombea kuweka pingamizi dhidi ya wagombea wengine kwa vigezo hivyo.

Tarehe 10 Septemba 2020 Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliteua wagombea urais 16, isipokuwa mwanasiasa mkongwe, Ndugu Hamad. Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar aliuambia umma kwamba Tume haikumteua Ndugu Hamad kwa sababu aliwekewa pingamizi. Siku mbili kabla ya tarehe 8 Septemba 2020 akiwa anazungumza katika mkutano wa vijana wa ACT-Wazalendo, Ndugu Hamad alisema kwamba vyama viwili vidogo vilipanga kumwekea pingamizi ili asiteuliwe kugombea urais mwaka 2020. Hata hivyo, tarehe 11 Septemba 2020 Tume hiyo ilimpatia Ndugu Hamad cheti cha kumteua na kumruhusu kuanza kampeni.

#### 8.3.4.3 Uteuzi wa Wagombea wa Baraza la Wawakilishi na Wagombea Udiwani

Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliteua wagombea 251 wa viti vya Baraza la Wawakilishi. Kati ya wagombea hao, 61 (asilimia 24) walikuwa wanawake. Wanawake wachache zaidi (asilimia 21) waliteuliwa kugombea kiti cha udiwani kama Jedwali Namba 8.1 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 8.1: Wagombea wa Baraza la Wawakilishi na wa Udiwani Walioteuliwa**

| Nafasi | Kiume (asilimia) | Kike (asilimia) | Jumla (asilimia) |
|---|---|---|---|
| Baraza la Wawakilishi | 190 (76) | 61 (24) | 251 (100) |
| Madiwani | 276 (79) | 74 (21) | 350 (100) |

*Chanzo: Mahojiano na Maofisa wa ZEC yaliyofanyika mwezi Februari 2021*

#### 8.3.4.4 Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge, Baraza la Wawakilishi na Udiwani

Katika tukio ambalo halikuwahi kutokea siku za nyuma, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wagombea ubunge, wagombea wa Baraza la Wawakilishi na wagombea udiwani kadhaa wa ACT-Wazalendo waliondolewa kufuatia pingamizi zilizowekwa na wagombea wa vyama vingine vya siasa dhidi yao. Kama Jedwali Namba 8.2 linavyoonesha, sababu kubwa ya kuwaondoa ni kwamba watumishi wa umma hawakuambatisha barua za ruhusa kutoka kwa waajiri wao. REDET ilibaini kwamba Bi. Hasne Abdallah Abeid ambaye alikuwa mgombea wa kiti cha Baraza la Wawakilishi kwenye jimbo la Bububu kupitia ACT-Wazalendo alisema kwamba likizo yake bila malipo ya miezi miwili ilipitishwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Uvuvi. ACT-Wazalendo ilipata pigo kubwa sana kutokana na kuondolewa kwa wagombea wake. Kati ya wagombea 28 walioondolewa ambao wanaonekana katika Jedwali Namba 8.1, wagombea 24 walikuwa wa ACT-Wazalendo. Simulizi za watazamaji wa muda mrefu kutoka majimbo tofautitofauti ya Zanzibar zinaonesha kwamba ACT-Wazalendo ililalamika ikidai kwamba chama tawala na vyombo vya kusimamia uchaguzi vilikuwa vimeshirikiana kuwaondoa wagombea wenye ushawishi mkubwa, hususan Pemba ambako ACT-Wazalendo – na CUF kwa siku za nyuma – ilikuwa inaungwa mkono na watu wengi.

**Jedwali Na. 8.2: Baadhi ya Wagombea Waliooondolewa**

| Na. | Sababu za Kuwaondoa | Chama cha Siasa Kilichoathirika (Idadi ya Wagombea) | Jimbo | Nafasi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtumishi hakupata ruhusa ya mwajiri. | ACT-Wazalendo (9) | Nungwi; Bububu; Paje; Wawi; Chonga; Kiwani; Konde | Wabunge (3); Wawakilishi (6) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | Fomu hazikujazwa vizuri. | ACT-Wazalendo (4) | Kijini (3); Mtoni (1) | Mbunge (1); Wawakilishi (2); Diwani (1) |
| 3. | Kutofautiana kwa umri. | ACT-Wazalendo (3) | Mahonda (1); Tumbatu (1); Magomeni (1) | Wawakilishi (2); Diwani (1) |
| 4. | Hakuwa na idadi ya wadhamini inayohitajika. | CHADEMA (1); NRA (1); ACT-Wazalendo (1); NCCR-Mageuzi (1) | Mkwajuni (1); Kwahani (1); Shaurimoyo (2) | Madiwani (4) |
| 5. | Hajui kusoma na kuandika. | ACT-Wazalendo (2); CCM (1) | Chumbuni (1); Tumbatu (1); Tumbe (1) | Mwakilishi (1) Madiwani (2); |
| 6. | Jina lilikosewa; picha ilikuwa kubwa sana. | ACT-Wazalendo (2); CHADEMA (1) | Mkoani (1); Gando (1); Chambani (1) | Wabunge (2); diwani (1) |
| 7. | Katibu wa chama wa wilaya alisaini fomu zake mwenyewe. | NCCR-Mageuzi (1) | Mkoani (1) | mbunge (1) |
| 8. | Alidanganya kwamba alikuwa na shahada moja ya chuo kikuu ilhali Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilisema alikuwa na shahada mbili. | ACT-Wazalendo (1) | Wete (1) | Mwakilishi (1) |
| 9. | Hakuweka viambatisho kwenye fomu. | CCM (1) | Mtambwe (1) | Mwakilishi (1) |

*Chanzo: Ripoti za LTO wa REDET, Oktoba 2020*

Sababu nyingine ya kuwaondoa ilikuwa ni makosa katika ujazaji fomu. Kwenye nchi ambayo inatafuta kutatua migogoro ya muda mrefu kama Zanzibar, makosa madogo kama hayo yangeweza kurekebishwa ili kuwaruhusu wagombea kugombea badala ya kuwaondoa kwa sababu ya dosari za kiufundi.

Tathmini ya jumla ya mchakato wa uteuzi iliyofanywa na vyombo vya kusimamia uchaguzi, kama Jedwali Namba 8.3 linavyoonesha, inaonesha kwamba asilimia 62 ya watazamaji wa REDET walihitimisha kuwa mchakato wa uteuzi kwa ujumla ulikuwa huru na wa haki, lakini kulikuwa na dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wagombea. Wakati huohuo, kati ya watazamaji wa muda mrefu 50 ni mtazamaji mmoja tu (asilimia 2) ambaye alisema kwamba teuzi

ziligubikwa na dosari nyingi zilizohusu kutoheshimu taratibu, kanuni na maadili ya uteuzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo.

**Jedwali Na. 8.3: Tathmini ya Teuzi**

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Teuzi zilikuwa na dosari chache ambazo hazikuathiri matokeo ya jumla ya mchakato wa uteuzi. Uteuzi ulikuwa safi, huru na wa haki. | 80-100 | A | 13 | 26.0 |
| Kwa ujumla teuzi zilikuwa huru na za haki, lakini ulikuwa na dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wagombea. | 60-69 | B | 31 | 62.0 |
| Teuzi zilitoa fursa kwa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) kushiriki kwa uhuru lakini kulikuwa na matukio mengi ya uvunjifu wa taratibu na kanuni za uteuzi bila adhabu yeyote kutolewa na kulikuwa na upendeleo ambao inawezekana uliwaathiri baadhi ya wagombea. | 50-59 | C | 5 | 10.0 |
| Teuzi ziligubikwa na dosari nyingi sana zilizohusu kutokuzingatia taratibu, kanuni na maadili ya uteuzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 1 | 2.0 |
| Teuzi ziliharibiwa au kuendeshwa vibaya kiasi kwamba wadau waliwakataa wagombea walioteuliwa. Ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 0 | 0.0 |
| Mwenendo wa teuzi ulikuwa mbovu. Kulikuwa na upendeleo mwingi, dosari nyingi na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijiondoa au walitoa malalamiko rasmi. Teuzi zilikuwa ni mchakato ulioharibika. | 0 | F | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | | | **50** | 100.0 |

*Chanzo: Ripoti za LTO wa REDET, 2020*

### 8.3.5 Mabadiliko na Ushirikiano baada ya Uteuzi

Kama tulivyoeleza awali, ACT-Wazalendo iliathirika sana na kuondolewa kwa wagombea wake. REDET iligundua kwamba CCM ilitengeza uhusiano usio rasmi na CUF – iliyotetereka kutokana na Seif Sharif Hamad kuhamia ACT-Wazalendo – na muda mwingine UPDP kiasi kwamba CUF ikaonekana kama “CCM-B” kwa wafuasi wa ACT-Wazalendo.

Kwa mfano, wakati mjumbe wake wa Baraza la Wawakilishi wa Nungwi, Hassan Jani Masoud, alipoondolewa, ACT-Wazalendo ilimuunga mkono mgombea wa CHADEMA, Khamis Juma Shomari. Kwenye jimbo la Chumbuni, ACT-Wazalendo ilimkana mgombea wake wa Baraza la Wawakilishi ambaye walidai alikuwa amerubuniwa na kumuunga mkono mgombea wa CHADEMA. Kwenye jimbo la Kijini, ACT-Wazalendo ilipata pigo kubwa kwa upande wa nafasi tatu za wagombea ubunge, Baraza la Wawakilishi na udiwani. Iliamua kuiunga mkono CHADEMA dhidi ya CCM. Kwenye majimbo ya Ole na Wawi ambako wagombea wote wawili wa ubunge na uwakilishi waliondolewa, ACT-Wazalendo iliamua kuwaunga mkono wagombea wa CHAUMMA. Viongozi wa ACT-Wazalendo wa majimbo ya Ole na Wawi waliamini kwamba CUF na NRA walikuwa hawazungumzi lugha ya upinzani.




*Bango la mgombea wa CHADEMA Khamis Juma Shomari likionyeshwa kwenye mkutano wa kampeni wa ACT-Wazalendo eneo la Kendwa, jimbo la Nungwi.*

Kulikuwa na ushirikiano usio rasmi kati ya viongozi wa juu wa CHADEMA na ACT-Wazalendo. Mapemba mwezi Septemba akiwa anahutubia kwenye mkutano wa kampeni Mjini Unguja, mgombea urais wa Muungano wa CHADEMA, Tundu Lissu, alisema chama chake kilikuwa kinamuunga mkono Ndugu Hamad kwa sababu alikuwa mpinzani asiyeyumba kwa miaka 35 na alikuwa na uwezekano mkubwa wa kuishinda CCM katika uchaguzi wa Oktoba. Ndugu Lissu alimuunga mkono mgombea wa ACT-Wazalendo ingawa CHADEMA ilikuwa na mgombea urais wake Ndugu Said Issa Mohammed. Kutokana na ushirikiano huo watazamaji wa muda mrefu walishuhudia ushirikiano kati ya ACT-Wazalendo na CHADEMA kwenye majimbo kadhaa, kama vile Gando, Konde, Kiwani, Chonga na takribani kwenye majimbo yote mengine ambapo wagombea wa ACT-Wazalendo waliondolewa. Baada ya mgombea wa nafasi ya Baraza la Wawakilishi wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, mwanasiasa wa upinzani wa siku nyingi Zanzibar, kuondolewa kugombea nafasi hiyo kufuatia pingamizi alilowekewa na mgombea wa Democratic Party, wagombea wa CHADEMA, DP, UPDP na CUF walijiondoa kwenye kinayang'anyiro na kumwacha mgombea wa CCM akipita bila kupingwa. Ingawa CHADEMA haikujiondoa kwenye kinyang'anyiro kama hatua ya kupinga na kumuunga mkono Ndugu Juma Duni Haji, kujitoa kwa wagombea wa CUF, DP na UPDP kulithibitisha habari kwamba kulikuwa na ushirikiano usiokuwa rasmi. Tarehe 6 Oktoba 2020 takribani wanachama 600 wa CCM walijiunga na ACT-Wazalendo wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya Good Hope.



***Zaidi ya wanachama 500 wa CCM walihamia ACT-Wazalendo wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika Kivunge katika viwanja vya Good Hope huko Kijini.***

## 8.4 KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Zanzibar zilisimamiwa na mfumo wa kisheria, kwa kiasi kikubwa Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 na Maadili ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2020 kwa ajili ya uchaguzi wa Muungano na uchaguzi wa Zanzibar. Kwa kuzingatia miongozo hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar walitoa ratiba za kampeni kwa kila jimbo na kata na kwa ajili ya wagombea urais. Tathmini ya shughuli za kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 inaonesha kwamba shughuli hizo zilikuwa za kiwango cha chini. Vyama vya upinzani kama vile CHADEMA, NRA, ADC, AAFP, CUF, NCCR-Mageuzi, UPDP, UDP na Demokrasia Makini havikuzindua kampeni zao mapema kama ilivyotarajiwa. REDET ilibaini kwamba vyama hivi vya siasa havikuwa vinafanya kampeni kwenye majimbo. Vyama vingi vya siasa vilidai kwamba vilichelewa au havikuzindua kampeni zao za uchaguzi kwenye majimbo kutokana na ukosefu wa fedha.

Ni ACT-Wazalendo na CCM pekee ambavyo vilifanya uzinduzi rasmi wa kampeni. Hata hivyo, ilibainika kwamba hata vyama hivi vya siasa vilisitisha baadhi ya mikutano yao ya kampeni kutokana na ukosefu wa fedha. REDET ilibaini kwamba kiasi cha chini cha fedha kilichohitajika ili kufanya mikutano ya kampeni ya kiwango cha chini ni shilingi 500,000. Kwa mfano, gharama ya kukodi gari la matangazo ni kuanzia shilingi 200,000 hadi shilingi 250,000. Kwa vyama vya siasa ambavyo vilikuwa havipati ruzuku ilikuwa vigumu kwa wao kupata kiasi hicho cha fedha. Matokeo yake ni kwamba wagombea wengi walishindwa kufanya mikutano ya kampeni.

Vyama vya siasa vilitumia mikakati kadhaa kupunguza gharama za kampeni. Vyama vya siasa vilivyokuwa vinashindana viliandaa mikutano ya kampeni ya pamoja kwa ajili ya wagombea ubunge, wa Baraza la Wawakilishi na udiwani. Baadhi ya vyama hivyo vilisema kwamba wagombea wengi wa udiwani hawakufanya mikutano binafsi. Kwa kiasi kikubwa, wagombea wa nafasi za udiwani na hata wa nafasi za ubunge na uwakilishi walijaribu bahati yao kupitia mikutano ya wagombea urais iliyofanyika kwenye kata na majimbo yao. Hivyo basi, mikutano ya kampeni ya wagombea urais wa Muungano na ile ya wagombea urais wa Zanzibar ilivutia watu wengi. Wagombea wa majimbo na kata hizo pia walipata fursa ya kuomba kura kutoka kwa watu waliohudhuria.

Kampeni zenye mafanikio zinahusisha pia uwezo wa kuvutia watu wengi. Mikutano

mikubwa ya kampeni ni muhimu kwani inaongeza hali na kuonesha uimara wa mgombea na kukubalika kwake kwa wapiga kura. Ukiachilia mbali CCM na ACT-Wazalendo, ilikuwa vigumu kwa vyama vingine kuvutia watu wengi isipokuwa kwenye majimbo ya Mtambile na Pandani Pemba ambako CUF bado ilikuwa inaungwa mkono. Mbinu kadhaa zilitumika kuvutia watu kwenye mikutano ya kampeni. Mbinu mojawapo iliyotumika ni kuwakaribisha wasanii kama waimba taarabu na *qaswida*, washairi wa kiume na wa kike, na wacheza muziki waliocheza mitindo ya Kiswahili ijulikanayo kama kigodoro au singeli. Ilikuwa ni kawaida kuwaona vijana wakicheza sarakasi katika mikutano ya kampeni ili kuwaburudisha watu waliohudhuria au bendi ya wapiga ala ya vijana ambayo inafuatana na wahudhuriaji kutoka mitaani hadi kwenye mkutano wa kampeni. Mbinu hii ilitumiwa zaidi na CCM, ACT-Wazalendo, CUF na CHADEMA.




***Bendi ya wapiga ala ya vijana wa CCM ikielekea kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika viwanja vya Banda la Taka kwenye Kata ya Madungu jimboni Chakechake.***

### 8.4.1 Kampeni za Uchaguzi za Mgombea Urais wa CCM

Kampeni za uchaguzi za mgombea urais wa Zanzibar wa CCM zilizinduliwa kwenye Uwanja wa Demokrasia Kibandamaiti, Unguja, tarehe 12 Septemba 2020. Zilivutia kwa sababu ya upya wa mgombea. Pili, mgombea alileta mitindo mipya ya kampeni za uchaguzi kama vile kuyafuata makundi tofautitofauti ya watu sokoni au ufukweni kwa upande wa wavuvi na kuzungumza nao badala ya kuandaa mikutano ya kampeni. Mtindo huu ulikusudiwa kusikiliza changomoto zinazoyakabili makundi hayo badala ya kutoa hotuba na kumpa Mwinyi umaarufu kiasi. Mikutano

ya kampeni iliongezeka katika wiki za mwisho za kuelekea uchaguzi mkuu.

Kama angechaguliwa Dkt. Mwinyi aliahidi kuyaimarisha Mapinduzi, na kuulinda na kuuhifadhi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Maeneo yake ya kipaumbele yalikuwa ni pamoja na kuimarisha uchumi wa bluu, hususan uvuvi wa maji makubwa. Kuhusu suala hilo, aliahidi kujenga bandari ya uvuvi ya kisasa. Kuhusu uchumi alisisitiza sekta za uvuvi, utalii, viwanda na kilimo. Aliangazia pia huduma za jamii kama afya na elimu na alisisitiza kwamba angehakiki mtaala, alisisitiza elimu ya ufundi na kuahidi kuondoa ada kutoka shule za msingi hadi sekondari.

Kwenye mkakati wa kisiasa wa CCM ambao ulivutia makundi mbalimbali ya kijamii ni mgombea urais wake Dkt. Hussein Mwinyi ambaye aliandaa mikutano na makundi tofautitofauti ya kijamii, kidini na kiuchumi ili kusikiliza matakwa yao na hisia zao. Dkt. Mwinyi alikutana na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika Hoteli ya Park Hyatt iliyopo Mji Mkongwe ambapo alisisitiza uwezekano wa wao kuwa washirika. Alikutana na viongozi wa wavuvi wadogo wadogo wa Unguja, wakulima wa samaki na mwani, wakausha dagaa wa vijijini kwenye jimbo la Tumbatu na viongozi wa makanisa ya Zanzibar.



***Kampeni za kijiji hadi kijiji za Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwenye kijiji cha Kiwengwa Kumbaurembo***

Dkt. Mwinyi alitembelea makundi tofautitofauti ya watu wenye ulemavu tarehe 9 Oktoba 2020, viongozi wa dini na wakulima wa mwani wa Mjini Magharibi

na Kiembe Samaki akiwaahidi kuboresha upatikanaji wa mtaji na huduma za mabwana na mabibi shamba. Vivyo hivyo, alikutana na wavuvi na wauza samaki kwenye maeneo tofautitofauti ya uvuvi na masoko Mjini Magharibi na kuahidi kuboresha mazingira ya uvuvi. Hususan, aliahidi kuboresha masoko, shughuli za kugandisha na kuhifadhi na kuwawezesha kupanda kutoka wavuvi wadogo hadi wavuvi wakubwa wenye uwezo wa kuvua samaki katika bahari kuu.

Dkt. Mwinyi alifanya mkutano maalumu na Wamasai ambao wengi wao wameajiriwa kama walinzi kwenye makazi binafsi akiwaahidi kulinda haki zao kufuatia maelezo yao kwamba walikuwa wananyonywa na waajiri wao na walikuwa hawatambuliwi na mamlaka za serikali kama wana haki ya kuishi Zanzibar. Alifanya mkutano na jumuiya ya wafanyabiashara na kujadili masuala yanayohusiana na kodi, ushuru na utendaji wa bandari ya Zanzibar kwa lengo la kuipanua ili iweze kuhudumia makontena 105 badala ya makontena 80 ya sasa. Hali kadhalika, alizungumza na watumishi wa umma ambao suala lao kuu lilikuwa mishahara mizuri na uboreshaji wa mazingira ya kazi. Aliwaahidi kwamba angefanya maboresho kama angechaguliwa. Mikutano hii ilimruhusu kujikita katika masuala maalumu, hususan mahitaji ya makundi haya ya wapiga kura.

### 8.4.2. Mikakati ya Kampeni ya CCM

Sanaa zilikuwa kifaa muhimu cha kampeni kilichotumiwa kwa malengo tofautitofauti. Zilihusisha kumsifu mgombea kama vile wimbo wa *Tanzania ya Sasa* wa Zuhura Othman Soud ajulikanaye kama Zuchu ulioisifu CCM na mgombea urais wake wa Muungano kwamba wameibadilisha nchi. Alizungumzia miradi mikubwa iliyotekelezwa, yakiwamo madaraja ya juu, reli ya kisasa, huduma za bure za jamii kama vile elimu na afya. Wimbo huo ulikusudiwa kuwafanya watu wamchague Mwinyi, wamchague tena Rais Magufuli na CCM yake.

Wimbo mwingine uliosikika katika mikutano yote ya kampeni ya CCM ni wimbo wa 'Magufuli Baba Lao' wa Naseeb Abdul Juma maarufu kama Diamond Platinumz ambaye ni manamuziki wa Bongo Fleva anayependwa sana.

Hizi ni nyimbo chache tu, lakini nyimbo nyingi sana ziliimbwa na wasanii waliotumiwa na CCM wakati wa kampeni kuwaburudisha na kufikisha ujumbe kwa wapiga kura. Baadhi ya nyimbo hizo ni 'CCM Chama la Wana' wa Mzee wa Bwax na 'CCM Ileile' wa TOT Plus Band ambao ulimaanisha kwamba hadhi na utendaji wa CCM usingebadilika.

Dkt. Mwinyi alitumia mitindo mbalimbali ya kufanya kampeni, pamoja na kampeni za nyumba kwa nyumba na kuwatembelea watu kwenye makazi yao na kuzungumza nao. Alifanya mikutano ya ndani na sekta husika na watu kutoka makundi tofautitofauti.

Kama ilivyokuwa kwa kampeni za mgombea urais wa Muungano, matumizi ya wasanii na watu maarufu yalikuwa makubwa. Wasanii maarufu kama Harmonize, Diamond Platinumz na Zuchu walisaidia kuvutia watu wengi, wakiwamo wanawake, vijana na watoto.

### 8.4.3 Kampeni za Uchaguzi za Mgombea Urais wa ACT-Wazalendo

ACT-Wazalendo ilizindua kampeni za mgombea urais wake wa Zanzibar tarehe 13 Septemba 2020 katika Uwanja vya Demokrasia Kibandamaiti, Unguja, ambao ulitumiwa na CCM siku moja iliyopita. Kitu kilichovutia kwa upande wa ACT-Wazalendo ni kwamba walikuwa wameandaa ilani ya uchaguzi tofauti kwa ajili ya Zanzibar ambayo ilizunduliwa sambamba na kampeni. Kwenye jalada la ilani iliandikwa hivi: "Zanzibar Kwanza Leo na Kesho". Ilani hiyo ilibeba kauli mbiu ya: "Zanzibar yenye Mamlaka Kamili na Maisha ya Raha na Furaha". Siku ya uzinduzi na kwenye mikutano ya kampeni iliyofuata mgombea urais Ndugu Maalim Seif Sharif Hamad alisisitiza kuwa angehakikisha kwamba katiba mpya kingekuwa kipaumbele chake ili Wazanzibari wafaidi haki zao za msingi za binadamu bila ubaguzi wowote. Aliahidi kuifanya Zanzibar kuwa nchi tajiri kama ilivyo Singapore. Hali kadhalika, aliahidi kununua meli kubwa ili kusafirisha karafuu moja kwa moja kwenda masoko ya kimataifa.

Ingawa ACT-Wazalendo ilikuwa na mgombea mpya na Zanzibar ilikuwa na chama kipya cha siasa ambacho kilichukua nafasi ya CUF kama chama kikuu cha upinzani, mgombea wake wa urais hakuwa mpya. Maalim Seif Sharif Hamad alikuwa mgombea wa CUF tangu kuanzishwa kwa chaguzi za mfumo wa vyama vingi mwaka 1995. Ilivutia kuona ni kwa namna gani mikakati ya kampeni na ahadi zingebadilika.

### 8.4.4 Mikakati ya Kampeni ya Mgombea Urais wa ACT-Wazalendo

Kama CCM, ACT-Wazalendo iliwekeza kiasi kikubwa kwenye kampeni kwa kutumia wasanii, ikijumuisha uandaaji wa nyimbo za muziki ambazo hazikuwa za wanamuziki fulani. Nyimbo hizo zilivutia sana kwa sababu ya mtindo wa Zenji

Fleva. [20] Muziki huo unaazima na kuchanganya vizuri ladha za *hip-hop*, taarab na *qaswida*. Moja ya nyimbo maarufu zilizoimbwa wakati wa kampeni ni Ulipo Tupo. Wimbo huo ulimwonesha Maalim Seif kama ni mtu pekee anayeweza kuwafanya Wazanzibari wawe huru. Wimbo huo unapopigwa, makundi ya watu yanakwenda jukwaani na kuanza kucheza kwa mzunguko na kupepea mikono na kuwaburudisha baadhi ya wahudhuriaji.

Wimbo wa *Singeli*[21] wa Clayton Chipando, maarufu kama Baba Levo, 'Maalim Seif Tena' unamwonesha mgombea urais wa ACT-Wazalendo kama ni mtu maarufu na anayependwa kwa sababu ya msimamo wake usioyumba linapokuja suala la masilahi ya Wazanzibari. Uliwavutia wanawake na vijana na ulikuwa unaimbwa katikati ya hotuba ili kuwafanya watu waingie na kucheza huku wakimsifu Maalim Seif kama shujaa wao. Kama ni kujibu mapigo kwa wimbo wa 'Magufuli Baba Lao' wa Diamond wakati wa kampeni wimbo wa 'Shangilia Ushindi' unakuja wa B.O.O. Mnyama uliimbwa. Katika wimbo huo mwimbaji aliwataja waandamizi wa ACT-Wazalendo, wakiwamo Ismail Jusa, Nassor Mazrui na Yusuph Mansour na kuwaambia watu wawaambie CCM kwamba Maalim Seif ambaye ni mshindi asiyewezekana anakuja. Ni amari maarufu sana inayowataka watu wapige makofi, watikise bendera na washikane mikono kuashiria kwamba Maalim Seif tayari ameshashinda uchaguzi. Wimbo huo uliibua hisia kali miongoni mwa wafuasi wa ACT-Wazalendo na kuwafanya wacheze kwa ari huku wakiwa na tumaini kubwa la kushinda uchaguzi.

Wimbo unaokumbukwa na mtu yeyote aliyehudhuria mikutano ya kampeni za ACT-Wazalendo ni 'Tunataka Nchi Yetu'. Wimbo huu unawataka Wazanzibari wadai nchi yao. Unaanza kwa kunukuu Ibara ya 1 ya Katiba ya Zanzibar inayowapa madaraka na mamlaka. Unadai kwamba watu ni masikini kwa sababu viongozi wanajitajirisha wenyewe na kuyanufaisha masilahi ya wakubwa kutoka Bara kwa gharama ya watu wa kawaida. Pamoja na tuni na mitindo ya kuburudisha na kufuruhisha, jumbe zilizobebwa na nyimbo zilizopigwa kwenye kampeni za ACT-Wazalendo zilichochea watu, hususan watu masikini, kuiona CCM na Muungano kama chanzo cha matatizo yao na kwa hiyo watumie sanduku la kura kujikomboa.

20 Inafahamika kama Zenji Fleva kwa maana ya ladha ya Zanzibar, ni muziki wa Kiswahili unaochanganya muziki wa Taarab wa Wazanzibari na Bongo Fleva na unapambwa na ladha ya muziki wa Kiarabu na Kihindi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe wenye hisia uliojificha. Mchanganyiko huu unaibua hisia za wimbo kwa mwimbaji na msikilizaji na kwa hiyo unahawahamasisha watu wacheze kama kikundi kwa hisia za kina huku wakizunguka.

21 Umeanzia kwenye mitaa ya Tanzania, singeli ni muziki wa kuvuta hewa haraka na wa kichokozi unaojumuisha vifaa vya muziki vilivyopangiliwa na mara nyingi maneno yanyorudiwarudiwa ili kusisitiza jambo miongoni mwa wachezaji na kufanya watu watamani sana kucheza.

Ukiachilia mbali wasanii wa Bongo na Zenji Fleva ambao gharama yao inakadiriwa kuwa ni kubwa, CCM na ACT-Wazalendo walitumia aina zingine za sanaa za gharama nafuu au wasanii ambao ni miongoni mwa wafuasi wao. Aina hizo za sanaa zilijumuisha muziki wa taarab, *quaswida* na ngoma za asili kutoka Zanzibar kama mchikicho, msewe na kibati.[22]



*Vijana wakicheza sarakasi kwenye moja ya mikutano ya kampeni ya ACT-Wazalendo uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Mtambile.*

### 8.4.5 Kampeni za Wagombea Urais wa Vyama Vingine vya Siasa

Mikutano ya kampeni za vyama vya siasa ambavyo havikuwa na rasilimali za kutosha kama CUF ilikuwa na mambo machache na iliruhusu wagombea kuzumngumza muda mrefu kuhusu sera zao na ni kwa nini wachaguliwe. Lakini matokeo yake hayakuwa makubwa sana kwa sababu kampeni hizo hazikuvutia watu wengi ukilinganisha na zile za CCM na ACT-Wazalendo. Uwezo mdogo wa kufanya kampeni katika ngazi zote uliwafanya wagombea wa ngazi ya jimbo na kata kutegemea mikakati mingine kama vile kampeni za nyumba kwa nyumba ambazo haikuwa rahisi kuzitazama. Kauli mbiu kadhaa za kampeni zilitumiwa na vyama vya siasa kwa lengo la kuwaeleza wapiga kura sera zao kama Jedwali Namba 8.4 linavyoonesha.

22 Kibati ni ngoma laini ambapo mwanaume anaongoza wimbo kwa kutamka maneno kwa sauti na wanawake wanaocheza wanajibu. Ngoma hii ya taratibu inakiruhusu kikundi kutoa ujumbe kuhusu kazi iliyofanywa na chama cha siasa na kumsifia mgombea huku wakimueleza nini cha kufanya baada ya kumhakikishia kwamba wanamuunga mkono.

**Jedwali Na. 8.4: Kauli Mbiu Zilizotumiwa na Vyama vya Siasa Zanzibar**

| Chama cha Siasa | Kauli Mbiu Iliyotumika |
|---|---|
| ACT-Wazalendo | Ulipo tupo. Dira mpya; chaguo la watu wa Zanzibar; uchumi unaofanya vizuri na Zanzibar yenye furaha |
| ADC | Dira ya maendeleo |
| CCM | Zanzibar mpya, uchumi mpya, tumetekeleza na tunasonga mbele, yajayo ni mazuri na yajayo yanafurahisha |
| CHADEMA | Mabadiliko na uhuru wa kweli, nguvu ya umma, maendeleo ya watu, uhuru, haki na maendeleo |
| CUF | Haki sawa kwa wote, haki na furaha kwa wote |
| NRA | Maendeleo kwa wote, Zanzibar kwa ajili ya vijana |
| AAFP | Mabadiliko hayaepukiki; maendeleo ni kujiamini |

*Chanzo: Ripoti za LTO wa REDET, 2020*

**Jedwali Na. 8.5: Mikakati ya Uchaguzi ya Vyama vya Siasa Zanzibar**

| Na. | Mkakati wa Kampeni | Chama cha Siasa |
|---|---|---|
| 1. | Mikutano ya umma | CCM, ACT-Wazalendo, CHADEMA, NRA, CUF |
| 2. | Nyumba kwa nyumba | Vyama vyote |
| 3. | Mtaa kwa mtaa | Vyama vyote |
| 4. | Mabango na vipeperushi | CCM, ACT, CHADEMA, CUF, NRA |
| 5. | Kusafirisha watu kwenda kwenye mikutano ya kampeni | CCM, ACT-Wazalendo, NRA |
| 6. | Vikundi vya ngoma | CCM, ACT-Wazalendo, CHADEMA, NRA |
| 7. | Kuvaa fulana na nguo zenye rangi na bendera za vyama | CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo |
| 8. | Matumizi ya magari ya matangazo | CCM, ACT-Wazalendo, CUF, CHADEMA, CHAUMA. |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

### 8.4.6 Kampeni Hasi

REDET ilibaini kwamba kwa ujumla kampeni za uchaguzi zilikuwa za amani kama walivyosema wagombea. Hata hivyo, kwenye majimbo ambayo yalikuwa na ushindani mkali matukio ya kampeni hasi yalijitokeza. Mathalani, wafuasi wa CCM walimwita mgombea urais wa ACT-Wazalendo mtu aliyekuja na jahazi, wakimaanisha kwamba siyo Mzanzibar. Vyama vya upinzani, hususan ACT-Wazalendo, vilimwita mgombea urais wa CCM mtalii wa Mkuranga, wakimaanisha

kwamba Dkt. Hussein Mwinyi alikuwa mtalii kutoka Tanzania Bara kwenye jimbo la Mkuranga ambako aligombea ubunge mara ya kwanza.




*Gari la ACT-Wazalendo katika uwanja wa Kendwa huko Nungwi likionesha lugha hasi ya kampeni (bora UVIKO-19 kuliko CCM).*

Huko Malindi na Nungwi lugha ya matusi ilitumika dhidi ya wagombea kama "Tuache kumchagua mwanaume mzuri tumchague babu!" Kulikuwa na malalamiko kuhusu matumizi ya lugha ya matusi dhidi ya wanawake. Wagombea wa kike kutoka vyama vyote vya siasa na nafasi zote walishambuliwa zaidi kwa lugha ya matusi ili kuwashushia hadhi na nafasi yao kwenye uongozi, yakiwamo matamko kwamba walishindwa kusimamia ndoa zao na kwa hiyo wasingeweza kusimamia masuala ya kisiasa.



*ACT-Wazalendo ikisafirisha watu kwenda kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Mahonda.*

### 8.4.7 Usafirishaji Watu Kwenda kwenye Maeneo ya Kampeni

Vyama vyote vilivyokuwa vinashindana kama vile CCM, ACT-Wazalendo, CUF na AAFP vilisafirisha watu kwenda kwenye mikutano yao ya kampeni. Katika tukio moja, REDET ilibaini mtindo wa kijeshi ukitumika kusafirisha watu kwenda kwenye eneo ambalo mkutano wa kampeni wa CCM ulitarajiwa kufanyika.



*Wanachama wa CCM wakielekea kwenye mkutano wa kampeni wa mgombea urais uliofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja tarehe 3 Oktoba 2020.*



*Lori linalofanana na lori la kijeshi likisafirisha wafuasi wa CCM kuelekea kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Mnazi Mmoja.*

### 8.4.8 Mienendo Mibaya katika Kampeni za Uchaguzi na Vurugu

Tume ya Uchaguzi Zanzibar na kamati yake ya maadili ilichukua hatua kushughulikia mienendo mibaya ya wagombea wakati wa kampeni. Kampeni zilizohamasisha uvunjifu wa sheria na vurugu zilidhibitiwa. Katika tukio moja, kamati ya maadili ya kitaifa ya Zanzibar ilihairisha kampeni za Maalim Seif Sharrif Hamad, mgombea urais wa ACT-Wazalendo, kwa siku tano kwa sababu alichochea vurugu kwa kuwahamsisha wafuasi wake kupiga kura tarehe 27 Oktoba 2020, siku ya kupiga kura ya mapema kufuatia lalamiko la mgombea wa Demokrasia Makini.

REDET ilibaini matukio machache ya vurugu. Usiku wa tarehe 10 Oktoba 2020 majira ya saa 2.30 asubuhi huko Kwale Maburani kwenye jimbo la Ziwani, ofisi ya CCM iliyoko jirani na ofisi ya ACT-Wazalendo ilichomwa moto. Polisi waliwakamata na kuwaweka ndani watuhumiwa wengi. Wakati huohuo watu wengi waliondolewa na vyombo vya usalama na kupelekwa kwenye vijiji vingine. Watuhumiwa wote baadaye waliachiwa na hatimaye maisha yalirejea katika hali yake ya kawaida jimboni humo. Siku ya Ijumaa tarehe 16 Oktoba 2020 baada ya mkutano wa kampeni wa ACT-Wazalendo uliofanyika katika Tawi A la Kiuyu kwenye jimbo la Micheweni wafuasi wake waliondoka uwanjani hapo kwa makundi wakiimba kwa hisia kuhusu chama na wagombea wao. Kundi moja lilipita kwenye shamba la ndizi la mwanachama wa CCM. Mwenyeshamba alijaribu kuwazuia wafuasi hao wa ACT-Wazalendo lakini hawakumtii na kusababisha ugomvi kati ya mtu huyo na kundi hilo la wafuasi. Hatimaye, kundi hilo lilimshinda na kumpiga. Watu wengine waliokuwapo, hususan wafuasi wa CCM, waliingilia kwa kuwapiga wafuasi wa ACT-Wazalendo. Polisi waliwasili dakika chache baadaye. Hata hivyo, hasara ilikuwa imeshatokea, ikiwamo kujeruhiwa kwa baadhi ya watu na kupelekwa katika hospitali ya Micheweni ili wapatiwe matibabu.

Kama Jedwali Namba 8.6 linavyoonesha, kwa ujumla kampeni za uchaguzi Zanzibar zilikuwa huru na za usawa ingawa zilikuwa na dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) kama ambavyo watazamaji 33 (asilimia 86) kati ya watazamaji 50 wa muda mrefu walivyosema.

**Jedwali Na. 8.6: Tathmini ya Kampeni za Uchaguzi za Zanzibar**

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Kampeni za uchaguzi zilikuwa na dosari chache. Zilikuwa safi, huru na za haki. | 80-100 | A | 13 | 26.0 |
| Kwa ujumla, kampeni za uchaguzi zilikuwa huru na za haki, lakini zilikuwa na dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). | 60-69 | B | 30 | 60.0 |
| Kampeni za uchaguzi zilitoa fursa kwa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) kushiriki kwa uhuru lakini kulikuwa na matukio mengi ya uvunjaji wa taratibu na kanuni za kampeni na chama tawala bila adhabu yeyote kutolewa na kulikuwa na upendeleo ambao inawezekana uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | 50-59 | C | 7 | 14.0 |
| Kampeni za uchaguzi zilikuwa na dosari nyingi sana zilizohusiana na kutokuzingatia taratibu, kanuni na maadili ya uteuzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 0 | 0.0 |
| Kampeni za uchaguzi ziliharibiwa au kuendeshwa vibaya. Ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 0 | 0.0 |
| Mwenendo wa kampeni za uchaguzi ulikuwa mbovu. Kulikuwa na upendeleo mwingi, dosari nyingi na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijiondoa au walitoa malalamiko rasmi. Kampeni zilikuwa ni mchakato ulioharibika. | 0 | F | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | | | **50** | 100.00 |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 8.5 FUMBO/KIZUNGUMKUTI CHA UPIGAJI KURA WA MAPEMA

Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Namba 11 ya mwaka 1984 ilirekebishwa na Sheria Namba 4 ya mwaka 2018 ili watendaji wa uchaguzi (Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo cha Uchaguzi, askari polisi na wafanyakazi wa Tume) na wapiga kura wengine ambao walitarajiwa kutekeleza majukumu ya kiusalama siku ya uchaguzi waweze kupiga kura mapema.[23] Kifungu cha 82 (1)-(2) cha sheria mpya ya uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2018 inawaruhusu watu watakaosimamia uchaguzi na watu wa usalama kupiga kura mapema. Kifungu cha 82(2) kinasema kwamba upigaji kura wa mapema utahusisha uchaguzi wa Rais wa Zanzibar tu. Watu wanaoruhusiwa kupiga kura mapema ni watendaji wa uchaguzi, yaani Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Vituo Wasaidizi, askari polisi, Makamishna na wajiriwa wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Ingawa CCM, CUF na ADC hawakuwa na tatizo lolote kuhusiana na upigaji kura wa mapema, chama kikuu cha upinzani, yaani ACT-Wazalendo, hakikukubaliana na utaratibu huo na kwa hiyo kiliendesha kampeni kali dhidi yake. Kwa ujumla, ACT-Wazalendo ilikuwa na wasiwasi na mchakato huo na kudai kwamba ulikuwa ni mpango wa CCM wa kumuibia Ndugu Hamad kura zake. Walisema kwamba orodha haikuwa kama ilivyotarajiwa, kitu ambacho kiliashiria kwamba ilitengenezwa ili kuongeza kura za CCM. Wafuasi wa ACT-Wazalendo walihoji ni kwa nini mpango huo ulikuwa unatekelezwa Zanzibar tu na si katika uchaguzi wa Muungano pia.

Katika mikutano yao ya kampeni mingi wagombea wa ACT-Wazalendo waliwahamasisha wafuasi wao kupiga kura terehe 27 Oktoba 2020, tarehe ya upigaji kura wa mapema. Kwenye jimbo la Mtambile wafuasi wa vyama vikuu vya upinzani ambao walisadikika kuwa wa ACT-Wazalendo na CHADEMA walipinga vikali upigaji kura wa tarehe 27 Oktoba kiasi kwamba waliweka magogo na mawe barabarani kuzuia uingiaji wa magari ambayo yalikuwa yanasambaza karatasi za kura na vifaa vingine vya uchaguzi. Ugomvi ulitokea kati ya baadhi ya wakazi wa jimbo la Mtambile na vyombo vya ulinzi na usalama, hususan kwenye kata za Mtambile na Kengeja. Mapambano yalikuwa makali mno kiasi kwamba watu watano walijeruhiwa.

23 Ibara ya 82 (1) & (2) ya Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya mwaka 2018 ambayo ilisainiwa na kuwa sheria tarehe 16 Januari 2018. Ibara hiyo inahusu Uchaguzi Mkuu na Chaguzi Ndogondogo za Urais.



*Mawe na magogo yaliyowekwa barabarani kwenye kata ya Kengeja jimbo la Mtambile kuwazuia maafisa wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar wasisambaze vifaa vya kupigia kura tarehe 27 Oktoba 2020*

Kwenye jimbo la Ziwani, mtazamaji wa muda mrefu wa REDET alibaini kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilitumia magari ya jeshi kusambaza watendaji wa uchaguzi na vifaa vya uchaguzi usiku wa kuamkia siku ya kupiga kura mapema tarehe 27 Oktoba 2020. Mabomu ya machozi na silaha zingine zilitumika kuwatawanya wafuasi wa ACT-Wazalendo ambao walikuwa wamekusanyika katika vituo mbalimbali vya kupigia kura. Mgogoro uliendelea kwenye jimbo la Ziwani lote mpaka tarehe 30 Oktoba 2020 na ungeweza kuwazuia wapiga kura wasiende kwenye vituo vya kupigia kura tarehe 28 Oktoba 2020. Siku ya kupiga kura ya mapema baadhi ya watazamaji wa uchaguzi kutoka FAYCO walizuiliwa kwa muda na askari polisi huko Ziwani ambao walidai kwamba watazamaji hao hawakuwa na vitambulisho kwani vitambulisho vyao havikuwa na nembo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Ripoti ya LTO wa Ziwani, 2020). Kwenye jimbo la Ole huko Pemba, REDET ilishuhudia vurugu zilizosababisha vifo vya watu watano na wengine zaidi ya 10 wakijeruhiwa (Ripoti ya LTO wa REDET, Ole, 2020).

Viongozi wa juu wa ACT-Wazalendo Zanzibar, wakiwamo Ndugu Hamad na wafuasi wake ambao walidaiwa kuwahamasisha watu waende kupiga kura walikamatwa. Wakati wanakwamatwa, vyombo vya usalama vilitumia nguvu na kusababisha tafrani miongoni mwa watu katika mitaa mingi ya Unguja na Pemba. Huko Unguja REDET ilishuhudia upigaji kura wa mapema ukifanyika kwa amani

zaidi ya Pemba ingawa kulikuwa na milipuko michache ya mabomu ya machozi iliyosikika mitaani ili kutawanya aina zote za mikusanyiko.

Kwa ujumla, REDET ilibaini dosari zilizohusiana na zoezi la upigaji kura wa mapema. Kwanza, zoezi lilifanyika kwa usiri. Mathalani, kituo cha kupigia kura cha kwenye jimbo la Ole kilihamishiwa jimbo la Chake Chake (Shule ya Michakaeni) bila taarifa kutolewa. Pili, vyama vya siasa na watazamaji wa uchaguzi hawakuruhusiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura. Tatu, upigaji kura uliahirishwa kwa muda katika baadhi ya vituo vya kupigia kura bila taarifa yeyote kutolewa kwa vyama vya siasa. Nne, ingawa kulikuwa na kituo cha kupigia kura kimoja tu kwenye kila jimbo kituo hicho hakikutangazwa. Hadi saa 3:00 asubuhi baadhi ya vyama vya siasa na mawakala wao walikuwa hawajui vituo vya kupigia kura viko wapi.

## 8.6 KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

### 8.6.1 Upigaji Kura

Siku ya kupiga kura Zanzibar ilikuwa Jumatano tarehe 28 Oktoba 2020 ambayo ilitanguliwa na upigaji kura wa mapema siku moja iliyopita. Kama Jedwali Namba 8.7 linavyoonesha, upigaji kura ulianza mapema na ni kwenye majimbo matatu kati ya majimbo 50 yaliyotazamwa ambapo upigaji kura ulianza saa 2:00 asubuhi. Kabla upigaji kura haujaanza, masanduku ya kura yaliyofungwa kwa ajili ya uchaguzi wa rais wa Zanzibar yaliyobeba kura zilizopigwa tarehe 27 Oktoba yalioneshwa kwa mawakala wa vyama vya siasa ili waone kwamba hakuna mtu aliyeyachezea. Kura ziilizopigwa tarehe 27 Oktoba zilipaswa kuhesabiwa pamoja na kura zilizopigwa tarehe 28 Oktoba 2020. Masanduku ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani yenye karatasi ya kura za Rais wa Muungano na Mbunge pia yalioneshwa kwa watu waliokuwapo kwenye vituo vya kupigia kura ili waone kuwa yalikuwa yamefungwa kwa lakiri.

**Jedwali Na. 8.7: Kuanza kwa Upigaji Kura**

| Je, upigaji kura ulianza saa ngapi katika jimbo lako? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Saa 1:00 asubuhi hadi saa 7:30 asubuhi | **43** | **86.0** |
| Saa 7:31 asubuhi hadi saa 8:00 asubuhi | 4 | 8.0 |
| Kuanzia saa 8:01 na kuendelea | 3 | 6.0 |
| **Jumla** | **50** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 8.8 linaonesha kuwa REDET ilibaini kwamba vifaa vyote vya kupigia kura vilikuwapo bila upungufu mkubwa kuripotiwa. Iliripotiwa kwamba vifaa vingi vya kupigia kura vilisambazwa siku moja kabla na kwa hiyo kuruhusu upigaji kura kuanza kwa wakati.

**Jedwali Na. 8.8: Utoshelevu, Mipango na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, kuna vifaa vya kupigia kura vyovyote vilivyokosekana katika kituo chako cha kupigia kura? | 4 (8) | 46 (92) | **50 (100)** |
| Je, karatasi za kura zilikuwa hazijajazwa na kufungwa kabla ya upigaji kura kuanza? | 44 (88) | 6 (12) | **50 (100)** |
| Je, mpangilio wa kituo cha kupigia kura uliwezesha usiri katika kupiga kura? | 48 (96) | 2 (4) | **50 (100)** |
| Je, kulikuwa na polisi au maafisa usalama waliovaa sare? | 50 (100) | 0 (0) | **50 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

### 8.6.2 Kuhesabu Kura

Katika vituo vingi, zoezi la kuhesabu kura lilianza mara moja baada ya mpigaji kura wa mwisho kupiga kura yake. Kwa kuwa idadi ya wapiga kura kwa kituo haikuwa kubwa, watu wengi walikuwa wameshapiga kura ilipofika saa 10:00 jioni kama Jedwali Namba 8.9.

**Jedwali Na. 8.9: Kuanza Kuhesabu Kura**

| Je, uhesabuji kura ulianza saa ngapi katika kituo chako cha kupigia kura? | Kiwango | asilimia |
|---|---|---|
| Saa 10:00 jioni hadi saa 10.30 jioni | 21 | 42.0 |
| Saa 4:31 asubuhi hadi saa 11:00 jioni | 9 | 18.0 |
| Saa 5:01 asubuhi na kuendelea | 20 | 40.0 |
| **Jumla** | **50** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 8.10 linatoa muhtasari wa utazamaji wa zoezi la kuhesabu kura uliofanywa na REDET. Kwa ujumla, zoezi la kuhesabu kura lilifanywa na maafisa wenye mamlaka ya kufanya hivyo kisheria. Hakukwa na vitisho au kuingiliwa. Data zinaonesha kwamba kwa kiasi kikubwa migogoro kuhusiana na kura ambazo hazioneshi mtu alikusudia kumpigia kura nani haikutatuliwa.

**Jedwali Na. 8.10: Mipango na Taratibu kwenye Vituo vya Kuhesabu Kura**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, ni watu wanaoruhusiwa kisheria tu ndio waliokuwa ndani ya kituo cha kuhesabia kura? | 46 (92) | 4 (8) | **50 (100)** |
| Hakuna mtu yeyote aliyewatisha au kuwabughudhi Wasimamizi wa Vituo wakati wa kuhesabu kura? | 4 (8) | 46 (92) | **50 (100)** |
| Je, kuna wakala wa chama cha siasa chochote aliyepinga matokeo ya uchaguzi? | 11 (22) | 39 (78) | **50 (100)** |
| Je, migogoro kuhusu kura ambazo hazioneshi mtu alikusudia kumpigia kura nani ilitatuliwa kwa kiwango cha kuwaridhisha mawakala wa vyama wote? | 39 (78) | 11 (22) | **50 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Katika eneo la Kiungani kwenye jimbo la Nungwi lenye vituo vya kupigia kura 13 zoezi la kuhesabu kura halikufanyika kwa sababu ya vurugu zilizojitokeza mtaani hapo. Baada ya mchakato wa kupiga kura kumalizika ilidaiwa kwamba mawakala wa vyama vya siasa waliokuwa nje walituma jumbe kwa wafuasi wa vyama vya upinzani wakidai kwamba uchaguzi ulikuwa umeibiwa hata kabla zoezi la kuhesabu kura halijaanza na kusababisha vurugu. Matairi yalichomwa na mawe yaliwekwa katika barabara za kuelekea kwenye vituo vya kupigia kura. Kwa hiyo, wanamgambo wenye silaha waliovaa nguo za kiraia na kufunika nyuso zao wajulikanao kama mazombi au *janjaweed* walipambana na wafanya fujo hao mitaani kabla polisi na wanajeshi hawajaingilia kati. Polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya watu waliotaka kuvamia vituo vya kupigia kura. Watazamaji walitolewa na kupelekwa kwenye Wilaya ya Kaskazini A. Kwa hiyo, watazamaji walishindwa kutazama zoezi la kuhesabu na kujumlisha kura lililofanyika Gamba. Zoezi la kuhesabu kura katika vituo vingine vya jimbo la Nungwi liliendelea isipokuwa Kiungani na Bandakuu ambako vurugu zilitokea.



*Mawe ambayo wafanyafujo waliyaweka kuzuia uingiaji kwenye vituo vya kupigia kura eneo la Hamburu kwenye jimbo la Nungwi*

### 8.6.3 Kutangaza Matokeo

Kwa mujibu wa sheria, kura ni lazima zihesabiwe katika kituo cha kupigia kura na baada ya hapo matokeo yabandikwe nje ya kituo. Kwa kiasi kikubwa hili lilifanyika ingawa takribani nusu ya vituo vyote vya kupigia kura vilivyotazamwa matokeo ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani hayakubandikwa nje ya vituo kama sheria inavyotaka kama Jedwali Namba 8.11 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 8.11: Ubandikaji wa Matokeo ya Uchaguzi**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla(100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar yalibandikwa nje ya kituo cha kupigia kura? | 24 (48) | 25 (52) | **50 (100)** |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yalibandikwa nje ya kituo cha kupigia kura? | 29 (58) | 18 (36) | **47 (94)**[1] |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yalibandikwa nje ya kituo cha kupigia kura? | 32 (64) | 18 (36) | **50 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

REDET ilitaka kujua mtazamo wa watu kuhusu matokeo ya uchaguzi. Jedwali Namba 8.12 linaoonesha kwamba kwa ujumla watu hawakujali matokeo ya uchaguzi yalikuwaje ikiwa na maana kuwa hawakuonesha hisia zozote.

**Jedwali Na. 8.12: Kukubalika kwa Matokeo ya Uchaguzi**

| Jibu | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Watu waliyafurahia sana matokeo ya uchaguzi. | 6 | 12 |
| Watu walikasirishwa sana na matokeo ya uchaguzi. | 9 | 18 |
| Watu hawakujali kuhusiana na matokeo ya uchaguzi. | 35 | 70 |
| **Jumla** | **50** | **100** |

Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020

Matokeo ya uchaguzi yalipokelewa kwa hisia tofauti. Baadhi ya wagombea waliyakubali moja kwa moja lakini wengine waliyapinga. Kama Jedwali Namba 8.13 linavyoonesha, kiwango cha kukubalika kwa matokeo ya uchaguzi kilianzia asilimia 50 hadi asilimia 54 ya matokeo yote ya uchaguzi yaliyotazamwa.

**Jedwali Na. 8.13: Kama Wagombea Waliyakubali Matokeo ya Uchaguzi**

| Swali | Kiwango | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo (asilimia) | Hapana (asilimia) | Haihusiki (asilimia) | Jumla (asilimia) |
| Je, wagombea udiwani walioshindwa waliyakubali matokeo ya uchaguzi? | 27 (54) | 12 (24) | 11 (22) | 50 (100) |
| Je, wagombea ubunge walioshindwa waliyakubali matokeo ya uchaguzi? | 28 (56) | 15 (30) | 7 (14) | 50 (100) |
| Je, wagombea wa viti vya Baraza la Wawakilishi walioshindwa waliyakubali matokeo? | 27 (54) | 12 (24) | 11 (22) | 50 (100) |
| Je, kulikuwa na matukio yeyote ya vurugu baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa? | 5 (10) | 37 (74) | 8 (16) | 50 (100) |

***Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020***

Matokeo ya uchaguzi yalitangazwa katika ngazi tofauti. Matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yalitangazwa katika kata. Matokeo ya uchaguzi wa Wabunge na Baraza la Wawakilishi yalitangazwa katika ngazi ya jimbo. Matokeo ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa katika ngazi ya kitaifa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Matokeo yanaonesha kwamba ACT-Wazalendo ilishinda viti vinne vya ubunge na vinne vya Baraza la Wawakilishi. Kwa upande wa matokeo ya uchaguzi wa Rais, Dkt. Hussein Mwinyi wa CCM alishinda kwa kishindo kwa kupata kura 380,402 (asilimia 76.3 ya kura zote zilizopigwa) dhidi ya Maalim Seif Sharif Hamad wa ACT-Wazalendo aliyepata kura 99,103 (asilimia 19.9) ya kura zote zilizopigwa.

Tathmini iliyofanywa na REDET ya upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo iliyopo katika Jedwali Namba 8.14 inaonesha kwamba takribani asilimia 72 ya watazamaji wa muda mrefu waliamini kwamba zoezi liliendeshwa kwa amani lakini zilikuwapo dosari chache. Lakini watazamaji watano (asilimia 10) kati ya watazamaji wa muda mrefu 50 walisema kwamba zoezi liliingiliwa na kuendeshwa vibaya kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuelewa ni kitu gani kilitokea.

**Jedwali Na. 8.14: Tathmini ya Upigaji Kura, Uhesabuji Kura na Utangazaji Matokeo**

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulikuwa na dosari chache ambazo hazikuathiri matokeo ya uchaguzi ya jumla. Mchakato ulikuwa huru na wa haki. | 80-100 | A | 12 | 24.0 |
| Kwa ujumla, upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulikuwa huru na wa haki, lakini kulikuwa na baadhi ya dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). | 60-69 | B | 24 | 48.0 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulitoa fursa kwa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) kushiriki kwa uhuru lakini kulikuwa na matukio mengi ya uvunjifu wa taratibu na kanuni za kampeni yaliyofanywa na chama tawala bila adhabu yeyote kutolewa na kulikuwa na upendeleo ambao inawezekana uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | 50-59 | C | 5 | 10.0 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matoeko uligubikwa na dosari nyingi sana ambazo zilihusiana na kutokuzingatiwa kwa taratibu, kanuni na maadili ya uteuzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 4 | 8.0 |

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo uliingiliwa au kuendeshwa vibaya kiasi kwamba wadau hawakuelewa ni kitu gani kilikuwa kimetokea. Ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 5 | 10.0 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulikuwa mbovu. Kulikuwa na upendeleo mwingi, dosari nyingi na rushwa kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijiondoa au walichukua hatua zingine. Ulikuwa ni mchakato ulioharibika. | 0 | F | 0 | 0.0 |
| **Jumla** | | | **50** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 8.7 MATUKIO BAADA YA UCHAGUZI WA ZANZIBAR

Matokeo ya uchaguzi hayakupokelewa vizuri na ACT-Wazalendo na CHADEMA ingawa vyama vingine vya upinzani visiwani humo vilimpongeza mshindi, Dkt. Hussein Mwinyi. Viongozi wa kitaifa wa vyama viwili (ACT-Wazalendo na CHADEMA) waliitisha mkutano na waandishi wa habari ili kuelezea kutopendezwa kwao na namna uchaguzi ulivyoendeshwa na kusema kwamba hawautambui uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na matokeo yake. Kupitia mkutano huo waliwaomba wafuasi wao kufanya maandamano yasiyokuwa na ukomo kudai haki zao za kidemokrasia. Tarehe 29 Oktoba 2020 Ndugu Hamad na wenzake 27, pamoja na Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Ndugu Juma Duni Haji na Ismail Jussa Ladhu, walikamatwa na polisi. Akizungumza na vyombo vya habari, Ndugu Awadhi Juma, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, alisema waliwakamata kwa sababu walikuwa wanafanya maandamano kinyume na sheria ambayo yangeweza kuvunja amani. Waandamanaji hao, akiwamo Ndugu Hamad, waliachiwa takribani saa mbili usiku kwa dhamana yenye sharti kwamba lazima waripoti kituo cha polisi kila siku.

Wakati huohuo, Ibara ya 9 (3) ya Katiba ya Zanzibar inaruhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na Ibara ya 39(2) inamtaka Rais wa Zanzibar ateue Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais siku saba baada ya kula kiapo. Kama Makamu wa Pili wa Rais anatoka kwenye chama cha Rais, Ibara ndogo ya

39 (3) inasema kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais atoke chama ambacho ni cha pili kwenye uchaguzi wa Rais isipokuwa kama chama hicho kimepata chini ya asilimia 10 ya kura za urais. Kama Rais anachaguliwa bila kupingwa, Makamu wa Kwanza wa Rais atatoka kwenye chama chenye idadi ya pili ya viti vya Baraza la Wawakilishi. Wiki moja baada ya Dkt. Hussein Mwinyi kula kiapo, waandishi walimuuliza swali kuhusiana na nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Alisema kwamba alikuwa ameiandikia barua ACT-Wazalendo, chama ambacho kilistahili kupendekeza jina la Makamu wa Kwanza wa Rais.

Tarehe 10 Novemba 2020 gazeti la *Mwananchi* lilisema kwamba Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Ndugu Hamad, aliwaeleza kwamba chama kilikuwa kinafikiria kama wajiunge na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. ACT-Wazalendo ilijiunga na serikali hiyo tarehe 6 Desemba 2020 baada ya Rais Hussein Mwinyi kumteua Ndugu Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tarehe 7 Desemba 2020 Dkt. Mwinyi alimteu Nassor Ahmed Mazrui, Katibu Mkuu Msaidizi wa chama, na Omar Said Shaaban, Mwanasheria wa Chama, kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mahusiano ya vyama hivyo viwili visiwani Zanzibar yaliimarika baada ya Ndugu Hamad kuzungumza kwa njia chanya kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa maandalizi ya kusherehekea Mapinduzi tarehe 12 Januari 2021. Kulikuwa na programu zilizohusisha ushirikiano wa vyama hivyo viwili Zanzibar kipindi cha kuelekea sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Muhimu zaidi ni safari ya Ndugu Hamad na Dkt. Mwinyi Chato kwenda kuonanan na Dkt. John Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Januari 2021. Dkt. Magufuli aliwapongeza viongozi hao wa Zanzibar kwa kukubaliana kufanya kazi ya kuijenga Zanzibar bora na kuahidi kuwapa ushirikiano.

## 8.8 TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI WA ZANZIBAR

Kuhusiana na tathmini ya jumla ya uchaguzi wa Zanzibar, kama Jedwali Namba 8.15 linavyoonesha, watazamaji wa muda mrefu walio wengi (28 kati ya 50, au asilimia 56) walisema kwamba kwa ujumla uchaguzi ulikuwa huru na wa haki, lakini zilikuwapo dosari ambazo zingeweza kuwaathiri baadhi ya wadau. Kati ya watazamaji 50, 10 (asilimia 20) walidai kwamba mchakato wa uchaguzi uliwaruhusu wadau kushiriki kwa uhuru ingawa kulikuwa na uvunjifu mwingi wa kanuni uliofanywa na chama tawala bila kuchukuliwa hatua yeyote na kulikuwa na upendeleo ambao lazima uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vya

siasa. Uchaguzi wa Zanzibar ulionekana **kuwa huru lakini usiokuwa wa haki** kwa sababu ya kuondolewa kwa wagombea wengi wa upinzani bila sababu za msingi na bila kuheshimu sheria za uchaguzi zilizopo na vitendo vya watendaji wa uchaguzi ambao walifanya makosa bila kuchukuliwa hatua. Inawezekana mambo haya yaliviathiri baadhi ya vyama vya siasa na wagombea. Mchakato wa upigaji kura wa mapema haukuwa wa wazi ingawa kura hizo zilikuwa na athari kwenye uchaguzi wa Rais wa Zanzibar.

**Jedwali Na. 8.15: Tathmini ya Jumla ya Uchaguzi wa Zanzibar**

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Uchaguzi ulikuwa na dosari chache ambazo hazikuathiri matokeo ya uchaguzi ya jumla. Kwa ujumla, uchaguzi ulikuwa safi, huru na wa haki na uliashiria matakwa ya wapiga kura. | 80-100 | A | 10 | 20 |
| Uchaguzi ulikuwa huru na wa haki, lakini kulikuwa na dosari ambazo inawezekana ziliwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). | 60-69 | B | 28 | 56 |
| Uchaguzi ulitoa fursa kwa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura) kushiriki kwa uhuru lakini kulikuwa na matukio mengi ya uvunjifu wa taratibu na kanuni za kampeni yaliyofanywa na chama tawala bila adhabu yeyote kutolewa na kulikuwa na upendeleo ambao inawezekana uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | 50-59 | C | 8 | 16 |
| Uchaguzi uligubikwa na dosari nyingi sana zilizohusiana na kutokuzingatiwa kwa taratibu, kanuni na maadili ya uteuzi, matatizo ya kiusimamizi na matukio ya vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 3 | 6 |
| Uchaguzi uliharibiwa au kusimamiwa vibaya kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuelewa ni kitu gani kilitokea. Ni kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 1 | 2 |

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Uchaguzi ulikuwa mbovu. Kulikuwa na matukio mengi ya vurugu, rushwa na uchochezi kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijitoa au walichukua hatua zingine. Uchaguzi wote ulikuwa ni mchakato ulioharibika. | 0 | F | 0 | 0 |
| **Jumla** | | | **50** | 100 |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 8.9 HITIMISHO

Uchaguzi wa Zanzibar ulifanyika wakati vyama vya siasa vikijipanga upya na wakati kukiwa na wagombea wapya na wanasiasa wa siku nyingi. Kufuatia kujiunga na Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2010, CUF, ambacho kilikuwa chama kikuu cha siasa cha upinzani Zanzibar, ilijitoa kwenye serikali hiyo kwa kutokubaliana na matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 na kususia kwake kwa uchaguzi wa marudio. Matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 yalikiacha chama cha CUF kwenye mgogoro wa muda mrefu kufuatia kujitoa na kurudi tena kwa mwenyekiti wake, Profesa Ibrahim Lipumba. Kutambuliwa kwa Profesa Lipumba na Msajili wa Vyama vya Siasa na uamuzi wa mahakama wa kumpa ushindi mwenyekiti huyo ulimfanya Maalim Seif Sharif Hamad na wafuasi wake wahamie ACT-Wazalendo. Ingawa upigaji kura wa mapema ulisababisha utata na ulikuwa chanzo cha vurugu, hatimaye ACT-Wazalendo ilikubali kujiunga na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kwa hiyo kupunguza joto Zanzibar ambalo lilikuwa linapanda baada ya chama hicho kuyakataa matokeo ya uchaguzi na kukataa kuiunga mkono serikali.

# SURA YA TISA

# SIKU YA UCHAGUZI NA TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI WA MWAKA 2020

## 9.1. UTANGULIZI

Kwenye sura hii tunafanya tathmini ya siku ya kupiga kura iliyohusisha kupiga kura, na kuhesabu na kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Tathmini hiyo itafuatiwa na tathmini ya jumla ya uchaguzi wa mwaka 2020. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu 12, ikiwamo sehemu hii ya utangulizi. Sehemu zinazofuata zinatoa taarifa za kina kuhusu upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo; mipango ya kiusalama katika vituo vya kupigia kura; matukio yaliyotokea baada ya uchaguzi; tathmini ya jumla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wa Tanzania; na hatimaye hitimisho.

## 9.2. KUFUNGUA NA KUFUNGA VITUO VYA KUPIGIA KURA NA VIFAA VYA KUPIGIA KURA

### 2.9.1 Kuanza kwa Upigaji Kura

Uchaguzi ulifanyika Jumatano ya tarehe 28 Oktoba 2020, kitu ambacho hakijawahi kutokea Tanzania kwani ilikuwa ni mara ya kwanza uchaguzi unafanyika kati ya juma. Serikali ilisema siku ya kupiga kura ingekuwa siku ya mapumziko ili kuwaruhusu wapiga kura wengi kushiriki katika zoezi la kupiga kura bila kikwazo chochote kama vile kwenda kuabudu kama inavyojitokeza uchuguzi ukifanyika Jumapili. Hii ilikuwa hatua nzuri iliyochukuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwani moja ya malalamiko ya muda mrefu ni kwamba uchaguzi ukifanyika Jumapili baadhi ya watu wananyimwa haki yao ya kupiga kura kwa kuwa wanakwenda kwenye ibada.

Upigaji kura ulipangwa kuanza saa 1:00 asubuhi na kuendelea hadi saa 10:00 jioni ikiwa na maana kwamba vituo vya kupigia kura vilipaswa kuwa wazi na tayari kwa zoezi hilo. Utazamaji wa REDET unaonesha kwamba asilimia 90 ya vituo vyote vya kupigia kura vilifunguliwa kwa wakati ingawa asilimia tano ya vituo vilifunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kuendelea kama Jedwali Namba 9.1 linavyoonesha.

**Jedwali Na 9.1: Ufunguzi wa Vituo vya Kupigia Kura**

| Muda | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Saa 1.00 asubuhi hadi saa 1.30 asubuhi | 2,387 | 90.6 |
| Saa 1.31 asubuhi hadi saa 2.00 asubuhi | 116 | 4.4 |
| Saa 2.01 asubuhi na zaidi | 133 | 5.0 |
| **Jumla** | **2,636** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Kuchelewa kwa zoezi la kupiga kura kulitokana na sababu kadhaa. Mathalani, kituo cha kupigia kura namba 1984802 cha Seliani-2 katika kijiji cha Olevolos kata ya Kimnyaki jimbo la Arumeru Magharibi kilifunguliwa saa 1:20 asubuhi kwa sababu mawakala wa vyama vya siasa waliwasili kituoni hapo bila Fomu Namba 14. Kwenye maeneo mengine kama ilivyoonekana Kibamba vituo vya kupigia kura vya ofisi ya kata ya Mbezi Luis vilihamishwa dakika za mwisho kwenda sehemu nyingine yenye umbali wa takribani kilometa mbili na kuilazimisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutengeza vibanda vya muda. Hatua hii ilicheleweshа upigaji kura kwa takribani dakika 15.

Katika vituo vingi vya kupigia kura ilibainika kwamba hakukuwa na misururu mirefu ya wapiga kura na kwa ujumla upigaji kura ulienda vizuri. Kabla hawajapiga kura zao, wapiga kura walipewa msaada kwenye hatua zifuatazo: (a) wapiga kura walitafuta majina yao yaliyobandikwa nje ya kituo au kupitia simu zao za mkononi; (b) uhakiki wa vitambulisho vya wapiga kura; (c) kukabidhi karatasi za kura tatu ziligongwa muhuri na kukunjwa vizuri kwa wapiga kura baada ya kuzitoa kwenye vitabu vyake; (d) kupiga kura kwenye vituturi husika; (e) kuweka karatasi hizo tatu za kura kwenye masanduku ya kura husika (lenye mfuniko wa bluu kwa ajili ya wagombea urais, lenye mfuniko mweusi kwa ajili ya wagombea ubunge na lenye mfuniko mweupe kwa wajili ya wagombea udiwani); na (f) kupaka vidole vya wapiga kura wino usiofutika.

### 9.2.2 Utoshelevu na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura

Kama Jedwali Namba 9.2 linavyoonesha, vituo vingi vya kupigia kura vilikuwa na vifaa vya kutosha (2,495, asilimia 94.6), isipokuwa kwenye vituo vichache vya kupigia kura ambavyo vilikuwa na upungufu wa baadhi ya vifaa. Masanduku ya kura yalikuwa tupu wakati wa kupiga kura, ingawa kwenye vituo vya kupigia

kura vichache (52, asilimia 2) watendaji wa uchaguzi hawakuwaonesha wapiga kura masanduku hayo ili waone kuwa yalikuwa tupu. Mpangilio wa vituo vya kupigia kura ulihakikisha usiri unakuwapo katika upigaji kura kwenye vituo vingi vya kupigia kura.

**Jedwali Na. 9.2: Utoshelevu, Mpangilio wa Kituo cha Kupigia Kura na Usalama wa Vifaa vya Kupigia Kura**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Jumla |
| Je, kuna vifaa vya kupigia kura vyovyote vilivyokosekana kwenye kituo cha kupigia kura? | 141 (5.4) | 2,495 (94.6) | **2,636 (100)** |
| Je, masanduku ya kura yalikuwa tupu na yamefungwa kabla ya upigaji kura kuanza? | 2,584 (98.0) | 52 (2.0) | **2,636 (100)** |
| Je, mpangilio wa kituo cha kupigia kura ulizingatia usiri katika kupiga kura? | 2,559 (97.1) | 77 (2.9) | **2,636 (100)** |
| Je, walikuwapo polisi au vyombo vya usalama vilivyovaa sare kwenye kituo cha kupigia kura? | 2,578 (97.8) | 58 (2.2) | **2,636 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Kwa ujumla Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliweka mipango ya kiusalama ya kutosha kwenye vituo vya kupigia kura kama ilivyoonekana kwenye vituo vya kupigia kura asilimia 98 ambapo polisi na askari wa vyombo vingine vya usalama waliovaa sare walikuwapo.

### 9.2.3 Upangaji, Ufikikaji wa Vituo vya Kupigia Kura na Namna ya Kuwahudumia Wapiga Kura

REDET ilitaka kuona kama mchakato wa kupiga kura ulikwenda vizuri kadiri iwezekanavyo kwa mpangilio wa watendaji na vifaa. Hali kadhalika, ilitaka kuona kama vituo vya kupigia kura vilifikiwa na watu wenye ulemavu, kama kulikuwa na dalili zozote za ufanyaji kampeni nje ya vituo vya kupigia kura na kama kulikuwa na wapiga kura wowote wenye vitambulisho ambao hawakuruhusiwa kupiga kura. Matokeo yanaoneshwa katika Jedwali Namba 9.3.

**Jedwali Na. 9.3: Upangaji, Ufikikaji na Namna ya Kuwahudumia Wapiga Kura**

| Utazamaji | Kiwango (asilimia ) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, kituo cha kupigia kura kilifikiwa na watu wenye ulemavu? | 2,380 (93.2) | 173 (6.8) | **2,553 (100)** |
| Je, kulikuwa na viashiria vyovyote vya ufanyaji kampeni, pamoja na vifaa vya kampeni, karibu na kituo cha kupigia kura? | 86 (3.4) | 2,467 (96.6) | **2,553 (100)** |
| Je, majina ya wapiga kura yalikosekana kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura? | 897 (35.1) | 1,656 (64.9) | **2,553 (100)** |
| Je, kulikuwa na matukio yeyote ya vurugu, vitisho au unyanyasaji dhidi ya Wasimamizi wa Vituo vya kupigia kura? | 83 (2.3) | 2,470 (96.8) | **2,553 (100)** |
| Je, kulikuwa na matukio ya vurugu, vitisho au unyanyasaji dhidi ya wapiga kura? | 56 (2.2) | 2,497 (97.8) | **2,553 (100)** |
| Je, yalikuwapo makundi yeyote ya watu mita 200 kutoka kwenye vituo vya kupigia kura? | 389 (15.2) | 2,164 (84.8) | **2,553 (100)** |
| Je, upigaji kura ulisimamishwa au kusitishwa kwa sababu yeyote ile? | 74 (2.9) | 2,479 (97.1) | |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Ilielezwa kwamba wapiga kura waliokuwa wamepoteza vitambulisho vyao walitumia vitambulisho kama vile leseni ya udereva, pasi ya kusafiria au kitambulisho cha taifa kupiga kura. Kwa kiasi kikubwa, wapiga kura wenye ulemavu walisaidiwa na watu waliowachagua wao wenyewe ambao walikuwa wameongozana nao kwa lengo hilo. Kwa kiasi fulani, wapiga kura waliokuwa peke yao walisaidiwa na watu waliokuwa kwenye mstari ambao waliwachagua wao wenyewe. Isipokuwa kwa wapiga kura wenye ulemavu, wapiga kura wengine wote waliingia kwenye vitutturi mmoja mmoja. Mazingira ya nje ya vituo vya kupigia kura yalikuwa ya utulivu sana na hapakuwa na dalili za kuhonga/kutisha watu. Kwenye maeneo mengi hakukuwa na vurugu.

Taratibu za kupiga kura ziliwapa kipaumbele wazee, wanawake wajawazito na watu wenye ulemavu. Kulikuwa na mistari miwili: mmoja wa wapiga kura wa kiume na mwingine wa wapiga kura wa kike kama ilivyoonekana katika vituo vyote vya kupigia kura Zanzibar na baadhi ya vituo vilivyotazamwa Tanzania Bara.



***Mgombea urais wa CHAUMMA Ndugu Hashim Rungwe akipiga kura yake Kinondoni, Dar es Salaam. Picha kwa hisani ya Azam Tv.***



***Mgombea urais wa CCM, John Pombe Magufuli, akiwa ameambatana na Mkewe, Bi. Janeth Magufuli, akiwa kwenye mstari akisubiri zamu yake ya kupiga kura ifike kwenye jimbo la Chamwino, Dodoma.***

### 9.2.4 Ufungaji wa Vituo vya Kupigia Kura

Vituo vingi vya kupigia kura vilifungwa saa 10:00 jioni kama ilivyoelekezwa na Tume. Kulikuwa na watu wachache sana waliosubiri kupiga kura wakati wa kufunga vituo vya kupigia kura. Kama Jedwali Namba 9.4 linavyoonesha, watu wachache sana walikuwa kwenye mistari wakisubiri kupiga kura saa 10:00 jioni. Hivyo, Tume haikulazimika kuongeza muda wa kupiga kura kama ilivyokuwa kwenye chaguzi zilizotangulia.

**Jedwali Na. 9.4: Wapiga kura Wakisubiri Kupiga Kura Muda wa Kufunga Vituo vya Kupigia Kura**

| Ni watu wangapi walikuwa wanasubiri kupiga kura wakati wa kufunga vituo saa 10:00 jioni? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Hakuna watu | 1711 | 67.0 |
| 1-4 | 601 | 23.6 |
| 5-9 | 80 | 3.1 |
| 10 na zaidi | 161 | 6.3 |
| **Jumla** | **2553** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Kwa kiasi kikubwa, watu waliokuwa kwenye mistari wakati wa kufunga vituo vya kupigia kura walipiga kura bila bugudha yeyote. Kwa ujumla, ni watu wachache sana hawakuruhusiwa kupiga kura wakiwa kwenye vituo vya kupigia kura kama ilivyoonekana kwenye vituo vya kupigia kura 945 kati ya vituo 2,553 (asilimia 37).

**Jedwali Na. 9.5: Kama Wapiga Kura Waliokuwa kwenye Mstari Waliruhusiwa Kupiga Kura**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, wapiga kura waliokuwa kwenye mstari saa 10:00 jioni waliruhusiwa kupiga kura? | 1608 (62.9) | 945 (37.2) | **2553 (100)** |
| Je, alikuwapo mpiga kura yeyote katika mstari ambaye hakuruhusiwa kupiga kura baada ya saa 10:00 jioni? | 111 (4.4) | 2442 (95.7) | **2553 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 9.6 linaonesha kwamba kufikia saa 10:00 jioni asilimia 93 ya wapiga kura wote walikuwa wameshapiga kura. Ni asilimia tatu tu ya wapiga kura walikuwa vituoni baada ya saa 11:00 jioni na zaidi wakisubiri kupiga kura.

**Jedwali Na. 9.6: Muda ambao Mpiga Kura wa Mwisho Alipiga Kura**

| Muda | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Saa10:00 hadi saa10:30 jioni | 2,381 | 93.3 |
| Saa 10:31 hadi saa 11:00 jioni | 91 | 3.6 |
| Saa 11:00 jioni na zaidi | 81 | 3.2 |
| **Jumla** | **2,553** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Miongoni mwa dosari chache walizozielezea watazamaji wa REDET ni pamoja na tukio lililotokea kata ya Nyasa, jimbo la Masasi Mjini, ambapo mtu mmoja alikamatwa na kura saba za kughushi zikiwa tayari zimeshapigwa kwa ajili ya mgombea urais na ubunge wa CCM ambazo alikusudia kuziweka kwenye sanduku la kura. Kwenye kituo cha kupigia kura cha Mpekeso I cha kata ya Matawale mwanamke aliyesemekana kuwa katibu wa tawi wa CCM, Bi Asumini Ally, alikamatwa na kura za kughushi 16 takribani saa 7:00 mchana.

## 9.3. KUHESABU KURA, KUJUMLISHA KURA NA KUBANDIKA MATOKEO KWENYE VITUO VYA KUHESABIA KURA

Kura zilianza kuhesabiwa kwenye kila kituo cha kupigia kura mara tu baada ya mtu wa mwisho kupiga kura yake. Matokeo yote ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani yalipaswa kubandikwa nje ya kituo cha kupigia kura na nakala ya matokeo hayo kupatiwa mawakala wa vyama vya siasa. Kama Jedwali Namba 9.7 linavyoonesha, nusu ya vituo vyote vya kupigia kura vilivyotazamwa zoezi la kuhesabu kura lilianza saa 10:00 jioni mara baada ya muda wa kupiga kura kumalizika. Ni kwenye vituo 564 (asilimia 22) vilivyotazamwa tu ambapo zoezi la kuhesabu kura lilianza baada ya saa 11:00 jioni.

**Jedwali Na. 9.7: Muda wa Kuanza na Kukamilisha Uhesabuji Kura**

| Muda | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Saa 10:00 jioni hadi saa 10:30 jioni | 1,237 | 48.9 |
| Saa10:31 jioni hadi saa 11:00 jioni | 727 | 28.8 |
| Saa 11:.01 jioni na kuendelea | 564 | 22.3 |
| **Jumla** | **2,528** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 9.8 linavyoonesha kwamba kwa kiasi kikubwa uhesabuji kura

ulifanyika kwa mujibu wa sheria. Isipokuwa kwa kiasi kidogo, watu wote waliokuwapo kwenye vituo vya kupigia kura walikuwa ni watu wanaoruhusiwa kisheria. Kulikuwa na matukio machache ya vitisho na usumbufu. Malumbano juu ya kura zenye mgogoro yalitatuliwa kwa amani.

**Jedwali Na. 9.8: Mipangilio na Taratibu kwenye Vituo vya Kuhesabia Kura**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, ni watu ambao wanaruhusiwa kisheria tu waliokuwa kwenye kituo cha kuhesabia kura? | 2,501 (98.9) | 27 (1.1) | **2,528 (100)** |
| Je, alikuwapo mtu yeyote aliyewatisha au kuwasumbua Wasimamizi wa Vituo wakati wa kuhesabu kura? | 79 (3.1) | 2,449 (96.9) | **2,528 (100)** |
| Je, alikuwapo wakala yeyote wa chama cha siasa ambaye aliyakataa matokeo ya uchaguzi? | 100 (4.9) | 2,428 (96.1) | **2,528 (1000** |
| Je, migogoro kuhusu kura ambazo hazioneshi mtu alikusudia kumpigia kura nani ilitatuliwa kwa kiwango cha kuwaridhisha mawakala wote wa vyama vya siasa? | 2,380 (94.2) | 148 (5.9) | **2,528 (100)** |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Rais yalibandikwa nje ya kituo cha kuhesabia kura? | 2,208 (87.3) | 320 (12.7) | **2,528 (100)** |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Wabunge yalibandikwa nje ya kituo cha kuhesabia kura? | 2,201 (87.1) | 327 (12.9) | **2,528 (100)** |
| Je, matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yalibandikwa nje ya kituo cha kuhesabia kura? | 2,223 (87.9) | 305 (12.1) | **2,528 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

REDET ilitaka kujua zoezi la kuhesabu kura lilichukuwa muda gani kumalizika na matokeo ya uchaguzi kubandikwa nje ya kituo cha kuhesabia kura. Kama Jedwali Namba 9.9 linavyoonesha, asilimia 40 ya vituo vyote vya kuhesabia kura vilivyotazamwa matokeo ya uchaguzi yalibandikwa ndani ya dakika 40 baada ya muda wa kupiga kura kumalizika. Hata hivyo, kwa ujumla ndani ya saa moja baada ya zoezi la kupiga kura kumalizika matokeo ya uchaguzi yalibandikwa nje ya vituo

vya kupigia kura.

**Jedwali Na. 9.9: Muda wa Kuhesabu Kura na Kubandika Matokeo ya Uchaguzi**

| Je, ilichukua muda gani kwa matokeo ya uchaguzi kubandikwa nje ya kituo cha kuhesabia kura baada ya zoezi la kupiga kura kumalizika? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Mara moja (dakika 1-30) | 1007 | 39.8 |
| Dakika 30-60 | 670 | 26.5 |
| Zaidi ya saa moja | 851 | 33.7 |
| **Jumla** | **2528** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 9.10 linaonesha hisia za watu kuhusu matokeo ya uchaguzi. Kwa ujumla, kulikuwa na hisia tofatuti. Takribani nusu ya watu walifurahia na nusu nyingine haikujali. Kwenye baadhi ya maeneo baadhi ya watu walishangazwa na matokeo. Kulikuwa na kutokuamini kwa jumla kwani walitarajia ushindani mkubwa, hususan kati ya vyama vikuu. Badala yake CCM ilipata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa Rais na Wabunge

**Jedwali Na. 9.10: Hisia za Watu Kuhusu Uchaguzi Mkuu**

| Je, matokeo ya uchaguzi yaliyobandikwa nje ya vituo vya kuhesabia kura yalipokelewaje? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Watu walifurahi sana. | 1374 | 54.4 |
| Watu walikuwa na hasira sana. | 88 | 3.5 |
| Watu hawakujali. | 1066 | 42.2 |
| **Jumla** | **2528** | **100.00** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Rushwa na matumizi ya fedha kuwahonga watu waliohusika na uchaguzi vingeweza kutokea na kuhatarisha mchakato mzima wa kuhesabu kura. Lakini, kama Jedwali Namba 9.11 linavyoonesha REDET haikushuhudia matumizi ya fedha ya aina hiyo.

**Jedwali Na. 9.11: Kutumia Fedha Kushawishi Wapiga Kura, Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura au Mawakala wa Vyama**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, ulishuhudia fedha ikitumika kushawishi wapiga kura? | 20 (0.8) | 2508 (99.2) | **2528 (100)** |
| Je, ulishuhudia fedha ikitumika kushawishi Wasimamizi wa Vituo vya kupigia kura? | 9 (0.4) | 2519 (99.6) | **2528 (100)** |
| Je, ulishuhudia fedha ikitumika kushawishi mawakala wa vyama? | 13 (0.5) | 2515 (99.5) | **2528 (1000** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 9.4 MIPANGO YA KIUSALAMA

Uchaguzi unaweza kusababisha taharuki. Kwa hiyo, usalama unapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba watu wote wanaohusika wako salama. Vituo vingi vya kupigia kura vilikuwa na idadi ya kutosha ya maafisa usalama. Maafisa usalama walikua polisi kwa kiasi kikubwa, ingawa mgambo na walinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa walitumika pia. Wengi wao hawakuwa na silaha, walikuwa na mienendo mizuri lakini makini. Kwenye maeneo mengine maafisa usalama hawakuwa rafiki kiasi hicho. Mathalani, kuonekana kwa maafisa usalama wenye silaha nzito huko Wete kuliwatisha wapiga kura. REDET ilishuhudia wastani wa maafisa usalama 10 katika Shule za Jadida na Mitiulaya.

Huko Unguja Kaskazini maafisa usalama walifanya vitendo vilivyowapa watu wasiwasi. REDET ilishuhudia kwamba takribani saa 10:15 jioni maaafisa usalama waliovaa sare waliingia kwenye kituo cha kupigia kura ili wapige kura. Upigaji kura huo haukufuata taratibu kwani hawakuonesha vitambulisho vyao vya mpiga kura na inadhaniwa kwamba walipiga kura zaidi ya moja.

## 9.5 KUTANGAZA MATOKEO

Matokeo yalitangazwa katika ngazi tatu kama ilivyofanyika kwenye chaguzi zilizotangulia. Matokeo ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa kwenye ngazi ya taifa na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Matokeo ya uchaguzi wa Wabunge yalitangazwa kwenye ngazi ya jimbo na Wasimamizi wa Uchaguzi na matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yalitangazwa na Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi. Hadi matokeo ya uchaguzi wa Rais yanatangazwa tarehe 30 Oktoba 2020 majimbo yote na kata zote zilikuwa zimeshatangaza matokeo yake ya uchaguzi.

### 9.5.1 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais

Zoezi la kuhesabu kura lilifanyika haraka kiasi na matokeo ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa bila ucheleweshaji wowote siku ya kuamukia tarehe 30 Oktoba 2020 na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Semistocles Kaijage. Rais aliyekuwa anatetekea kiti chake, Dkt. John Pombe Magufuli wa CCM, alishinda kwa kupata kura 12,516,252, Ndugu Tundu Antipass Lissu wa CHADEMA alipata kura 1,933,271, Ndugu Bernard Camilius Membe wa ACT-Wazalendo alipata kura 81,129, Ndugu Leopold Mahona wa NRA alipata kura 80,787 na Profesa Ibrahimu Lipumba wa CUF alipata kura 72,885. Kwa ujumla, takribani watu milioni 14 walipiga kura. Idadi inayofanana na hiyo haikupiga kura ingawa walistahili kufanya hivyo.

Kwenye majimbo mengi ujumlishaji wa kura za uchaguzi wa Rais na Wabunge katika kituo cha kujumlishia kura cha wilaya ulifanyika kwa kutumia projekta. Huko Mbagala matokeo hayakuonyeshwa kwa kutumia projekta. Kila kitu kilifanyika mbali bila mawakala wa vyama vya siasa na wagombea waliokuwapo kujua ni kitu gani kilikuwa kinaendelea na kwa hiyo kusababisha uhalali na uwazi wa mchakato wa kujumlisha kura kutiliwa shaka. Kitu cha kufarahisha ni kwamba maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kituoni hapo walidai kwamba hawakupewa projekta na Tume.

ACT-Wazalendo, CHADEMA na CUF walikataa matokeo ya uchaguzi wakidai kwamba hayakuwa ya kweli. Mwenyekiti wa CUF Profesa Ibrahimu Lipumba aliahidi kwamba chama chake hakitashiriki tena uchaguzi utakaofanyika chini ya katiba ya sasa. Tarehe 31 Oktoba 2020 ACT-Wazalendo na CHADEMA walitoa Tamko la Pamoja Kuhusu Uchaguzi Mkuu Uliofanyika Oktoba 27 na 28 kuyakataa matokeo. Walisisitiza kwamba hata pale ambapo wagombea wao walishinda, hawakuyatambua matokeo hayo na kwa hiyo wasingewaruhusu kushiriki katika vyombo vya kufanya maamuzi. Katika tamko hilo, walitaka uchaguzi ufanyike upya, waliiomba jumuiya ya kimataifa kuwaunga mkono na kuwaomba wafuasi wao kushiriki katika maandamano ya nchi nzima wakidai uchaguzi urudiwe upya.

### 9.5.2 Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge

Majimbo yote yalitangaza matokeo ya uchaguzi wa Wabunge tarehe 30 Oktoba 2020 kabla ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais. CCM ilishinda viti 258, ACT-Wazalendo viti vinne, CUF kiti kimoja na CHADEMA kiti kimoja. Kama

Jedwali Namba 9.12 linavyoonesha mbili ya tatu ya wagombea wote wa ubunge waliyakubali matokeo ya uchaguzi na waliobaki waliyakataa. Kwenye maeneo mengi, waliokataa matokeo ya uchaguzi wa Wabunge walikwenda mahakamani na kufungua kesi.

**Jedwali Na. 9.12: Kukubali Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge**

| Je, wagombea waliyakubali matokeo ya uchaguzi wa wabunge? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndiyo | 122 | 61.0 |
| Hapana | 58 | 29.0 |
| Haihusiki | 20 | 10.0 |
| **Jumla** | **200** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Huku wakisisitiza kwamba hawayatambui matokeo ya uchaguzi, CHADEMA ilijaribu kumzuia mshindi wake pekee wa ubunge kutoka jimbo la Nkasi Kaskazini asihudhurie vikao vya Bunge. Suala hili lilisababisha mabishano kwani mbunge huyo mteule alidai kwamba isingekuwa haki baada ya yeye kutumia rasilimali nyingi na kushinda uchaguzi kwa jitihada zake binafsi asiruhusiwe kuhudhuria vikao vya Bunge. Hatimaye alihudhuria kikao cha kwanza cha Bunge na kuwafanya viongozi wa juu wa chama watishie kuchukua hatua za kinidhamu dhidi yake. Hali kama hiyo ilijitokeza kufuatia uteuzi wa Wabunge wanawake wa viti maalumu. Tume ilipeleka Bungeni orodha ya wabunge wa viti maalumu 19, orodha ambayo Katibu Mkuu wa CHADEMA aliikataa mara moja akidai kwamba majina hayo hayakupitishwa na vyombo husika vya chama. Baadaye ilibainika kwamba majina yalipitishwa na Baraza la Wanawake CHADEMA. Viongozi wa chama walisisitiza kwamba wanawake hao wasijiunge na Bunge. Kinyume na uamuzi huo, wabunge hao walikwenda kuapishwa Bungeni tarehe 24 Novemba 2020 baada ya kikao cha kwanza cha Bunge ambacho kwa kawaida hutumika kuapisha wabunge. Suala hili lilizua hasira kwa upande wa chama ambacho kwenye mkutano wake wa tarehe 27 Novemba 2020 kiliwafukuza wabunge hao 19 walioasi kikisema kwamba siyo wanachama wa CHADEMA na kwamba walikuwa wamevuliwa nafasi zote kwenye chama. Uamuzi huo ulipokelewa kwa hisia tofauti na wananchi. Baadhi ya vikundi vya wanaharakati walivitaka vyombo vya juu vya CHADEMA kubadilisha uamuzi huo, wakidai kwamba ulitokana na mfumo dume. Baadaye CHADEMA ilitoa tamko kwamba wabunge hao walikuwa na haki ya kukata rufaa kwenye vyombo vya chama.

Kwenye majimbo machache REDET ilishuhudia vurugu pale wapiga kura walipochoka kusubiri muda mrefu matokeo ya uchaguzi yatangazwe. Huko Dodoma shughuli za siku ya uchaguzi zilikwenda vizuri isipokuwa kwenye kata za Berege, Nghambi na Chitemo kwenye jimbo la Mpwapwa ambako vurugu zilitokea. Vurugu zilizotokea katika Shule ya Msingi Nghambi na zilisababisha watendaji wa uchaguzi wakimbie na kuviacha vifaa vya uchaguzi na nyaraka. Kwenye kata za Berege na Chitemo, pikipiki zilichomwa moto na maafisa usalama na watu wengine walijeruhiwa.



*Afisa usalama aliyejeruhiwa kwenye jimbo la Mpwapwa*



*Vifaa vya uchaguzi vilivyoachwa baada ya vurugu kutokea*



*Pikipiki zilizochomwa moto kufuatia vurugu zilizotokea Mpwapwa*



*Pikipiki zilizochomwa kwenye kata ya Berege, Mpwapwa*

Watazamaji wa REDET walitazama zoezi la kujumlisha kura kwenye majimbo mengi. Hali ilikuwa tofauti kwenye majimbo machache kama vile Micheweni ambako watazamaji hawakuruhusiwa kutazama zoezi la kujumlisha kura.




*Mbunge mteule, Abdallah Chaurembo, akipokea cheti cha ushindi kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo la Temeke, Lusubilo Mwakabibi, baada ya kushinda uchaguzi wa ubunge.*

### 9.5.3 Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani

Matokeo ya uchaguzi wa Madiwani yalitangazwa na Wasimamizi wa Uchaguzi Wasaidizi katika ngazi ya kata. Kwa kuwa kazi ya kuhesabu kura haikuwa kubwa kama ya ngazi zingine mbili zilizofuata, kata zilitangaza matokeo ya uchaguzi mapema zaidi ya majimbo.

Kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba 9.13, wagombea walio wengi (132 [asilimia 66] kati ya 200 waliotazamwa] waliyakubali matokeo ya uchaguzi wa Madiwani lakini wagombea 43 (asilimia 21) waliyakataa.

**Jedwali Na. 9.13: Kukubalika kwa Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani**

| Je, wagombea waliyakubali matokeo ya uchaguzi wa madiwani? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndiyo | 132 | 66.0 |
| Hapana | 43 | 21.5 |
| Haihusiki | 25 | 12.5 |
| **Jumla** | **200** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Ingawa kwenye majimbo mengi amani ilitawala wakati wa kuhesabu kura na kutangaza matokeo, kwenye baadhi ya majimbo hali ilikuwa tofauti. Kwenye kata ya Ugawaji jimbo la Nachingwea, kwa mfano, polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya wafuasi wa CHADEMA ili kumtangaza mgombea udiwani wa CCM mshindi wa kiti cha udiwani. Matokeo yake ni kwamba nyumba ya mgombea ubunge wa CCM Ndugu Makoroganya ilichomwa moto na watu wasiojulikana usiku wa tarehe 28 Oktoba 2020. Picha zifuatazo zinaonesha gari na nyumba ya Ndugu Makoroganya zikiwa zimechomwa moto.





*shoto) lililochomwa moto katika makazi ya Ndugu Makoroganya na nyumba (kulia) ambayo pia ilichomwa moto wakati wa vurugu zilizotokea usiku wa tarehe 28 Oktoba 2020 baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa*

## 9.6 MWITIKIO WA WAPIGA KURA

Moja ya vitu vya kushangaza kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ni mwitikio mdogo wa wapiga kura siku ya tarehe 28 Oktoba 2020. Mwitikio huo mdogo ulishangaza zaidi ukizingatia shauku kubwa iliyokuwapo kwenye uchaguzi na nia ya kuleta mabadiliko. Mikutano ya kampeni ya vyama vya siasa viwili vilivyoshindana, yaani CCM na CHADEMA, ilivutia watu wengi sana. Uwingi huo wa watu katika mikutano uliashiria kwamba idadi kubwa zaidi ya watu ingejitokeza siku ya kupiga kura. Matokeo ya uchaguzi wa Rais yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi yalionesha kwamba wapiga kura 14,684,324 (asilimia 50.3) walijitokeza kupiga kura kati ya watu 29,188,347 walioandikishwa. Kwa maneno mengine, watu 14,504,023 walioandikishwa hawakwenda vituoni kupiga kura.

Hali kadhalika, REDET ilibaini baadhi ya tofauti kwenye matokeo ya uchaguzi na kwa hiyo kuonesha mielekeo tofauti kati ya matokeo ya uchaguzi wa Rais na matokeo ya uchaguzi wa Wabunge. Kwenye jimbo la Mbagala, wagombea urais na ubunge wa CCM walishinda kwa kupata kura 299,811 na 280,003 kutoka kwa wapiga kura 432,326 walioandikishwa (sawa na asilimia 72 ya kura za urais). Kwenye kata sita kati ya kata 10 zilizotazamwa mwitikio wa wapiga kura kwenye uchaguzi wa Madiwani ulikuwa asilimia 20. Kama mwitikio wa wapiga kura kwenye uchaguzi wa Rais na Wabunge ulikuwa asilimia 72 kwenye jimbo basi kungekuwa na mwitikio sawa kwenye uchaguzi wa Madiwani.[24] Je, ni matokeo ya mchakato wa kujumlisha kura mbovu na usio wa wazi katika kituo cha kujumlishia kura cha wilaya? Vivyo hivyo, matokeo yanayokinzana yalionekana kwenye jimbo la Kinondoni ambako watu waliopiga kura za udiwani walikuwa 92,448 au asilimia 30 ya wapiga kura wote walioandikishwa na wale waliopiga kura za ubunge walikuwa 135,194 au asilimia 44 ya wapiga kura walioandikishwa.

## 9.7 MATUKIO YALIYOJITOKEZA BAADA YA UCHAGUZI

Matukio yanayojitokeza baada ya uchaguzi ni mjumuisho wa matukio yote yanayohusu uchaguzi yanayotokea baada ya matokeo ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kutangazwa. Kwa kiasi kikubwa matukio hayo yanahusu namna watu wanavyoyapokea matokeo ya uchaguzi. Pale ambapo kwa kiasi kikubwa uchaguzi unaonekena ulisimamiwa vibaya na kuna udanganyifu, kuna uwezekano mkubwa wa vurugu kutokea na kinyume chake ni kweli pia.

### 9.7.1 Mlipuko wa Vurugu

Jedwali Namba 9.14 linaonesha kwamba matukio machache ya vurugu yalitokeza baada ya uchaguzi kumalizika. Hali hii pia inadhihirishwa na ukweli kwamba ni wagombea wachache tu wa ubunge na udiwani walioonesha nia ya kutoa malalamiko kutokana na kutoridhika na matokeo ya uchaguzi.

24 Kwenye jimbo la Mbagala wapiga kura 314,355 kati ya 432,326 walioandikishwa walijitokeza. Imepakuliwa tarehe 7 Novemba kutoka http://temekemc.go.tz/new/matokeo-ya-uchaguzi-manispaa-ya-temeke-2020

**Jedwali Na. 9.14: Matukio ya Vurugu Yaliyotokea baada ya Uchaguzi**

| Swali | Kiwango (asilimia) | | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Haihusiki | |
| Je, matukio yeyote ya vurugu yalitokea baada ya matokeo ya uchaguzi wa Madiwani kutangazwa? | 13 (6.5) | 171 (85.5) | 16 (8) | **200 (100)** |
| Je, matukio yeyote ya vurugu yalitokea baada ya matokeo ya uchaguzi wa Wabunge kutangazwa? | 10 (5.0) | 183 (91.5) | 7 (3.5) | **200 (100)** |
| Je, kuna malalamiko yeyote yaliyotolewa kwa mamlaka husika baada ya matokeo ya uchaguzi wa Madiwani kutangazwa? | 14 (7) | 165 (82.5) | 21 (10.5) | **200 (100)** |
| Je, kuna malalamiko yeyote yaliyotolewa kwa mamlaka husika baada ya matokeo ya uchaguzi wa Wabunge kutangazwa? | 21 (10.5) | 164 (82) | 15 (7.5) | **200 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Baadhi ya matukio ya vurugu yaliyoshuhudiwa ni matukio yaliyotokea Liwale ambapo usiku wa tarehe 28 Oktoba 2020 watu walikusanyika katika ofisi za Halmashauri ya Liwale. Polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya watu hao. Vurugu ziliendela na tarehe 29 Oktoba 2020 kundi la watu wasiojulikana lilivamia na kuchoma moto makazi ya mgombea ubunge wa CCM Ndugu Zuberi Kuchauka na makazi ya mgombea udiwani Ndugu Mkoyage.



***Makazi ya mgombea ubunge wa CCM Ndugu Zuberi Mohamed Kuchauka ambayo yalichomwa moto usiku baada ya uchaguzi wa tarehe 28 Oktoba 2020 katika kata ya Nangado, Liwale***



***Mwonekano wa makazi ya mgombea udiwani wa kata ya Likongowele Ndugu Mkoyage baada ya kuchomwa moto usiku kabla matokeo hayajatangazwa katika kata ya Likongowele tarehe 28 Oktoba 2020.***

Huko Tunduma hali ilikuwa mbaya kwani mara baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika kwenye kata ya Makambini, makundi ya vijana yalivamia kituo

cha kupigia kura cha Shule ya Msingi Makambini wakidai kwamba kulikuwa na masanduku ya kura feki yaliyoletwa na CCM. Polisi walitumia mabomu ya machozi kurudisha utulivu. Katika kituo kimoja cha kupigia kura kwenye kata ya Muungano, watendaji wa uchaguzi walishambuliwa na kuumizwa na kundi la watu waliokuwa karibu na vituo vya kupigia kura. Baada ya matokeo kutangazwa katika kituo cha kupigia kura cha Tunduma Mjini vurugu zilitokea. Makundi ya watu wenye hasira waliokataa matokeo waliharibu mali, kuzuia barabara na kuchoma matairi barabarani. Watu wengi walijeruhiwa, akiwamo kiongozi wa CCM wa mtaa wa Mwakakati ambaye alichomwa kisu.



*Askari polisi wanarejesha amani katika kituo kikuu cha mabasi cha Tunduma tarehe 29 Oktoba 2020.*



*Uharibifu wa mali katika soko la Iboya Tunduma Mjini*

Vurugu zilitokea huko Ukerewe ambako ucheleweshaji wa kutangaza matokeo uliwafanya watu wakose uvumilivu na kuchoma moto ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata.

### 9.7.2 Kuingiliwa na Kufungwa kwa Mitandao ya Kijamiii

Tarehe 27 Oktoba 2020 mitandao ya kijamii kama Twitter, Instagram, Ving na Whatsapp ilizimwa. Suala hilo ambalo halikuwahi kutokea lilitangazwa na vyombo vya habari vingi vya mitandaoni vya kimataifa kama *BBC* na *DW*. *DW* ilisema kwamba WhatsApp na Twitter zilikuwa zimezimwa na Hamduni Marcell alisema kwamba kuzimwa kwa mitandao ulikuwa ni uamuzi wa serikali ili kudhibiti mawasiliano wakati na baada ya uchaguzi.[25] Ingawa serikali haikutoa maelezo yeyote au onyo kabla ya kuzima mitandao ya kijamii na majukwaa ya mitandaoni, mwandishi wa habari wa kujitegemea Maggid Mjengwa aliiambia *DW* kuwa lengo lilikuwa ni kudhibiti usambazaji wa taarifa za uongo kwenye mitandao ya kijamii  kwani kufanya hivyo kunaweza kusababisha kukosekana kwa usalama na utulivu. Hali hii ilisababisha usumbufu mwingi kwani ilikuwa vigumu kuwasiliana. Mitandao ya kijamii ilifunguliwa polepole kuanzia tarehe 30 Oktoba 2020 baada ya matokeo ya uchaguzi wa Rais kutangazwa.

### 9.7.3 Utafutaji Hifadhi na Madai ya Kutishiwa Uhai

Katika hali ambayo si ya kawaida, uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulishuhudia wanasiasa wakubwa kutoka vyama vya upinzani wakitafuta hifadhi nje ya nchi wakidai kwamba walikuwa wamepokea taarifa za uhakika kwamba kuna watu walitaka kuwadhuru. Ndugu Tundu Lissu ambaye alikamatwa tarehe 2 Novemba 2020 baada ya kuitisha maandamano ya nchi nzima na kuyakataa matokeo ya uchaguzi alitafuta hifadhi katika makazi ya Balozi wa Ujerumani mara baada ya kuachiwa huru kwa dhamana. Tarehe 10 Novemba 2020 liondoka nchini na kuelekea Ubeligiji ambako alikuwa anapatiwa matibabu baada ya kupigwa risasi nyingi kwenye tukio ambalo lilionekana kama la kutaka kumuua wakati anahudhuria vikao vya Bunge mwaka 2017. Alisindikizwa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na Mabalozi wa Ujerumani, Marekani na Uingereza.

Ndugu Godbless Lema, mbunge wa jimbo la Arusha Mjini aliyeshindwa, awali alikimbilia Nairobi, Kenya, akidai kwamba maisha yake yapo hatarini. Tarehe 10 Novemba vyombo vya habari vilisema kwamba Ndugu Lema na familia yake walikuwa wamepatiwa hifadhi nchini Canada na kwa hiyo walikuwa wanaondoka Kenya. Madai ya vitisho kama hayo yaliyotolewa na mgombea ubunge wa

25 Mchambuzi wa masuala ya kisiasa wa Dar es Salaam, Marcell Hamdun, iliiambia *DW* kwamba "Twitter, Instagram, Xing na hata WhatsApp zilikuwa hazifanyi kazi na hakukuwa na namna ya kuwafikia watu. Siyo udhibiti. Hakuna mawasiliano kabisa." Imepakuliwa kutoka https://www.dw.com/en/tanzania-restricts-social-media-during-election/a-55433057 tarehe 3 Novemba 2020.

CHADEMA Ndugu Lazaro Nyalandu yalififia na jaribio lake la kuondoka nchini lilishindikana.

## 9.8 UTENDAJI NA MWENENDO WA WATENDAJI WA UCHAGUZI

Kila kituo cha kupigia kura kilikuwa na watendaji wa uchaguzi waliotekeleza majukumu mbalimbali: Msimamizi wa Kituo, Msimamizi wa Kituo Msaidizi na Karani Mwongozaji. Karani Mwongozaji alikuwa na wajibu wa kuwaelekeza wapiga kura kwenye vituo vya kupigia kura husika na kuhakiki taarifa zao. Msimamizi wa Kituo aliwapokea wapiga kura na kuhakiki taarifa zao akisaidiwa na Msimamizi wa Kituo Msaidizi ambaye alimpatia mpiga kura karatasi za kura husika ziligongwa muhuri. Jedwali Namba 9.15 linaonesha kwamba vituo vingi vya kupigia kura vilikuwa na watendaji wa uchaguzi watano au chini ya watano.

**Jedwali Na. 9.15: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi katika Vituo vya Kupigia Kura**

| Idadi | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| 1-5 | 2,063 | 78.3 |
| 6-10 | 401 | 15.2 |
| 11 au zaidi | 172 | 6.5 |
| **Jumla** | **2636** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

REDET ilipima utendaji wa watendaji wa uchaguzi kwa kuangalia kama walilinganisha taarifa za wapiga kura na zile za kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, walikagua kidole cha mwisho ili kuona kama walishakwisha piga kura, waliruhuru watu wasiokuwa na sifa kupiga kura na walitoa upendeleo kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha, watu wenye ulemavu na wazee kupiga kura bila kucheleweshwa, hususan wakati ambapo kulikuwa na mistari mirefu. Muhtasari wa kwenye Jedwali Namba 9.16 unaonesha kwamba kwa ujumla watendaji wa uchaguzi walipatiwa mafunzo ya kutosha na walitekeleza majukunu yao kwa kiwango cha kuridhisha.

**Jedwali Na. 9.16: Utendaji wa Watendaji wa Uchaguzi**

| Kiashiria cha Utendaji | Kiwango (asilimia) | | Jumla (100) |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | |
| Je, watendaji wa uchaguzi walilinganisha vitambulisho vya wapiga kura na taarifa zilizomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura? | 2,543 (99.6) | 10 (0.4) | **2,553 (100)** |
| Je, watendaji wa uchaguzi walikagua vidole vya mwisho vya wapiga kura kuona kama vilikuwa na wino usiofutika? | 2,350 (92.1) | 203 (7.9) | **2,553 (100)** |
| Je, vidole vya mwisho vya wapiga kura vilipakwa wino usiofutika? | 2,550 (99.9) | 3 (0.1) | **2,553 (100)** |
| Je, watendaji wa uchaguzi waliwaruhusu watu wasiokuwa na sifa kupiga kura? | 53 (2.1) | 2500 (97.9) | **2,553 (100)** |
| Je, watu wasiostahili waliruhusiwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura? | 90 (3.5) | 2463 (96.5) | **2,553 (100)** |
| Je, wapiga kura wasioona walisaidiwa na kupewa majalada ya nukta nundu? | 1,697 (66.5) | 856 (33.5) | **2,553 (100)** |
| Je, wanawake wajawazito, wanaonyonyesha na watu wenye ulemavu walipewa kipaumbele katika kupiga kura? | 2,515 (98.5) | 38 (1.5) | **2,553 (100)** |
| Je, watendaji wa uchaguzi waliweka mazingira magumu kwa wapiga kura wanawake kupiga kura? | 57 (2.2) | 2496 (97.8) | **2,553 (100)** |
| Je, watendaji wa uchaguzi walifanya kazi yao kwa weledi na uhalisia? | 2,478 (97.1) | 75 (2.9) | **2,553 (100)** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

## 9.9 UTENDAJI NA MWENENDO WA MAWAKALA WA VYAMA VYA SIASA

Asilimia 95 ya watazamaji wetu walisema kwamba mawakala wa vyama vya siasa walikuwapo wakati wa kuhesabu kura. Ni asilimia tano tu ya watazamaji wetu ndiyo waliosema kwamba mawakala wa vyama vya siasa hawakushuhudia zoezi la kuhesabu kura. Asilimia 80 ya watazamaji wetu walisema kwamba matokeo ya uchaguzi yalibandikwa katika vituo vya kupigia kura, lakini asilimia 20 walisema matokeo hayakubandikwa.

### Jedwali Na. 9.17: Mawakala wa Vyama vya Siasa

| Je, mawakala wote wa vyama vya siasa waliokuwapo katika kituo cha kupigia kura waliruhusiwa kushuhudia zoezi la kuhesabu kura? | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndiyo | 2,442 | 96.6 |
| Hapana | 86 | 3.4 |
| **Jumla** | **2528** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Kwenye baadhi ya majimbo Mkoani Dar es Salaam, mawakala wa vyama vya siasa walikatazwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura kwa sababu hawakuwa na kitu chochote ambacho Wasimamizi wa Vituo vya uchaguzi wangetumia kuwatambua. Lakini mawakala wa CCM waliruhusiwa baada ya kuwasilisha barua kutoka kwenye chama chao ambayo ilikuwa inawatambulisha kwa Wasimaizi wa Vituo vya kupigia kura. Kwenye maeneo kama ya Segerea, askari polisi aliyekuwapo kituoni aliingilia kati na kusitisha kuanza kwa zoezi la kupiga kura hadi mawakala wote wa vyama wameruhusiwe kuingia. Katika kituo cha kupigia kura cha Mashujaa cha Sinza jimbo la Ubungo, mawakala wa CHADEMA waliruhusiwa kuingia saa 3.30 asubuhi baada ya kuwasilisha baarua kutoka kwenye chama chao. Kituo cha kupigia kura cha Shule ya Msingi Mlimani kwenye jimbo la Ubungo kilikuwa tofauti. Vituo vyote vilikuwa na mawakala wa vyama na waliruhusiwa kutokana na imani ya Wasimamizi wa Vituo vya uchaguzi juu yao na walijitambulisha kama mawakala wa vyama vya siasa tofautitofauti.

REDET ilibaini kwamba badhi ya mawakala wa vyama vya siasa hawakujua sheria, taratibu, majukumu na wajibu wao. Kwenye jimbo la Arumeru Magharibi, wakala wa CHADEMA alihoji ni kwa nini kituo cha kupigia kura cha Embalakai kiliwekwa kwenye ofisi za mifugo katika makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha badala ya kuweka sehemu ya wazi. Katika kituo cha kupigia kura namba 1983805 cha Shule ya Sekondari ya Ilkiding'a-5 kijiji cha Ilkiding'a kata ya Ilkinding'a, wakala wa CHADEMA alikagua vitambulisho vya wapiga kura na kulinganisha na taarifa zilizomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hali hii ilisababisha msimamizi wa uchaguzi kunyang'anya nakala zote za Daftari la Wapiga Kura kutoka kwa mawakala wa vyama vya siasa akidai kwamba kama wangeendelea kuwa nazo matatizo yangetokea.

Ingawa Tume ilitoa mwongozo uliokataza matumizi ya vifaa vya mawasiliano na vya kielektroniki kama simu za mkononi, katazo hilo alikuzingatiwa kwa kiwasi

kikubwa na Wasimamizi wa Vituo vya kupigia kura, Wasimamizi Wasaidizi, Makarani Waongozaji, mawakala wa vyama vya siasa na wapiga kura walilivunja.

## 9.10 TATHMINI YA MICHAKATO YA UPIGAJI NA UHESABUJI KURA

REDET ilitathmini michakato ya kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo kama sehemu ya tathmini ya jumla ya ubora wa uchaguzi. Matokeo ya michakato hiyo miwili yanaoneshwa katika Jedwali Namba 9.18 na Jedwali Namba 9.19.

### 9.9.1 Tathmini ya Mchakato wa Upigaji Kura

Kama Jedwali Namba 18 linavyoonesha, kwa kiasi kikubwa zoezi la upigaji kura lilifanyika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zinazosimamia uchaguzi Tanzania.

**Jedwali Na. 9.18: Tathmni ya Zoezi la Upigaji Kura**

| Tathmini ya Mchakato wa Upigaji Kura | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Zoezi la upigaji kura lilifanyika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. | 184 | 92.0 |
| Zoezi la upigaji kura liligubikwa na uvunjifu mkuwa wa sheria, taratibu na kanuni. | 16 | 8.0 |
| **Jumla** | **200** | **100.00** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

### 9.9.2 Tathmini ya Mchakato wa Kuhesabu Kura

Matokeo yaliyopo kwenye Jedwali Namba 9.19 yanaonesha kwamba mchakato wa kuhesabu kura ulifanyika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za nchi. Ulinganishaji wa matokeo yaliyopo kwenye Jedwali Namba 9.18 na Jedwali Namba 9.19 unaonesha kwamba kwa ujumla zoezi la kuhesabu kura lilifanyika kwa mujibu wa sheria.

**Jedwali Na. 9.19: Thathmini ya Mchakato wa Kuhesabu Kura**

| Tathmini ya mchakato wa kuhesabu kura | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|
| Machakato wa kuhesabu kura ulifanyika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. | 172 | 86.0 |
| Mchakato wa kuhesabu kura uligubikwa na uvunjifu wa sheria, taratibu na kanuni. | 28 | 14.0 |
| **Jumla** | **200** | **100.0** |

*Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020*

Jedwali Namba 9.20 linaonesha matokeo ya shughuli zilizofanyika siku ya uchaguzi, pamoja na upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo.

**Jedwali Na. 9.20: Tathmini ya Siku ya Kupiga Kura**

| Vigezo vya Tathmini | Alama (asilimia) | Daraja | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulikuwa na dosari chache ambazo hazikuathiri matokeo ya uchaguzi ya jumla. Uchaguzi ulikuwa safi, huru na wa haki. | 80-100 | A | 1702 | 77.6 |
| Kwa ujumla, upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo ulikuwa huru na wa haki, lakini kulikuwa na dosari ambazo zingeweza kuwaathiri baadhi ya wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). | 60-69 | B | 383 | 17.5 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo uliruhusu ushiriki huru wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). Lakini chama tawala kilivunja taratibu bila kuchukuliwa hatua na kulikuwa na upendeleo ambao uliwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | 50-59 | C | 64 | 2.9 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo uligubikwa na dosari nyingi mno zinazohusiana na kutofuata baadhi ya sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi, kutokana na usimamizi mbovu na vitisho na upendeleo. | 40-49 | D | 22 | 1.0 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo uliingiliwa au ulisimamiwa vibaya kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuelewa ni kitu gani kilitokea. Ni kama manafunzi aliyeshindwa mtihani. | 1-39 | E | 19 | 0.9 |
| Upigaji kura, uhesabuji kura na utangazaji matokeo ulikuwa mbovu. Kulikuwa na matukio mengi mno ya vurugu, rushwa na uchokozi kiasi kwamba baadhi ya wagombea walijitoa kwenye uchaguzi au walichukua hatua zingine. Ulikuwa ni mchakato ulioharibika. | 0 | F | 4 | 0.2 |
| **Jumla** | | | **2194** | **100.0** |

***Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020***

Kama Jedwali Namba 9.20 linavyoonesha, kati ya watazamaji wa muda mfupi na muda mrefu 2,194, watazamaji 1,702 (asilimia 77.6) walisema kwamba shughuli zilizofanyika siku ya uchaguzi zilikuwa safi, huru na za haki; watazamaji 383 (asilimia 17.5) walisema zilikuwa huru na za usawa kiasi, watazamaji 64 (asilimia 2.9) walisema ulikuwa uchaguzi huru lakini si wa haki; na watazamaji 22 (asilimia 1) walisema uchaguzi haukuwa huru na wa haki. Ni kwenye vituo vinne tu vya kupigia kura ambapo mchakato ulipewa alama ya chini kabisa kwa sababu ya vurugu.

## 9.11 TATHMINI YA JUMLA YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

Baada ya kutazama michakato ya kabla ya uchaguzi, siku ya uchaguzi na baada ya uchaguzi, REDET inapenda kutoa maoni ya wazi na ya uhalisia kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika Tanzania wa mwaka 2020. Jedwali Namba 9.21 linaonesha tathmini ya jumla iliyofanywa na watazamaji wa muda mrefu kuhusiana na uchaguzi mkuu.

**Jedwali Na. 9.21: Tathmini ya Jumla ya Michakato ya Uchaguzi**

| Tathmini ya jumla ya uchaguzi wa mwaka 2020 | Alama na daraja (asilimia) | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Uchaguzi ulikuwa na dosari chache sana ambazo hazikuathiri matokeo ya uchaguzi ya jumla. Kwa ujumla uchaguzi ulikuwa safi, huru na wa haki. | A (80-100) | 89 | 44.5 |
| Uchaguzi ulikuwa huru na wa haki lakini ulikuwa na dosari chache ambazo kwa ujumla wake hazikuathiri kwa kiasi kikubwa matokeo ya mwisho ya uchaguzi na hazikuwaathiri wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). | B (60-79) | 81 | 40.5 |
| Uchaguzi uliruhusu ushiriki huru wa wadau (vyama vya siasa, wagombea na wapiga kura). Lakini vyama vikubwa vilivunja taratibu bila kuchukuliwa hatua na kulikuwa na upendeleo ambao ualiwaathiri baadhi ya wagombea na vyama vyao. | C (50-59) | 20 | 10.0 |
| Uchaguzi uligubikwa na dosari nyingi sana juu ya kutokufata sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi, matatizo ya usimamizi na upendeleo. | D (40-49) | 7 | 3.5 |

| Tathmini ya jumla ya uchaguzi wa mwaka 2020 | Alama na daraja (asilimia) | Kiwango | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Uchaguzi uliingiliwa au kusimamiwa vibaya kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuelewa ni kitu gani kilitokea. Ilikuwa kama mwanafunzi aliyeshindwa mtihani. | E (1-39) | 3 | 1.5 |
| Uchaguzi uligubikwa na dosari nyingi mno. Kulikuwa na vurugu nyingi, rushwa na uchokozi kiasi kwamba baadhi ya wagombea waliamua kujitoa kwenye uchaguzi au kuchukua hatua zingine. Uchaguzi wote ulikuwa ni mchakato ulioharibika. | F (0) | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **200** | **100** |

***Chanzo: Ripoti za Watazamaji wa REDET, 2020***

Kama Jedwali Namba 9.21 linavyoonesha, kati ya watazamaji wa muda mrefu 200, watazamaji 89 (asilimia 44.5) waliamini kwamba uchaguzi ulikuwa "safi, huru na wa haki" lakini wenye dosari chache; watazamaji 81 (asilimia 40.5) walionesha kwamba ulikuwa "huru na wa haki kiasi"; na watazamaji 20 (asilimia 10) walieleza kwamba uchaguzi ulikuwa "huru lakini si wa haki".

## 9.12 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Katika sehemu hii, tunahitimisha taarifa hii kwa kutoa maoni juu ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wa Tanzania. Hitimisho hilo linafuatiwa na mapendekezo.

### 9.12.1 Hitimisho

Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibabr zilisimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa kiasi cha kuridhisha na kuufanya uwe wa kuaminika. Wapiga kura walipewa fursa ya kushiriki kwa uhuru kwenye michakato mbalimbali ya uchaguzi kuanzia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hadi kupiga kura siku ya uchaguzi, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. REDET inavipongeza vyombo vya kusimamia uchaguzi, vyama vya siasa na wagombea wao, wadau wote wa uchaguzi na Watanzania kwa ujumla kwa mafanikio hayo makubwa. Kulingana na utazamaji ilioufanyika REDET inaupatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wa Tanzania cheti kinachoonesha kwamba uchaguzi ulikuwa "**huru na wa haki kiasi**".

### 9.12.2 Mapendekezo

Kulingana na utazamaji wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 uliofanywa na REDET, mapendekezo yafuatayo yanatolewa kwa wadau mbalimbali nchini Tanzania, yaani serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, vyama vya siasa na vyombo vya habari.

#### 9.12.2.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kuangalia namna ya kuboresha chaguzi na matokeo yake kwa:

i. kuepuka majaribio yeyote ya kuminya uhuru wa vyombo vya habari, ikiwamo mitandao ya kijamii;
ii. kuwezesha utafiti na majadiliano juu ya sababu za mwitikio mdogo wa wapiga kura na kushuka kwa ufahamu wa uraia;
iii. kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili itekeleze vizuri Sheria ya Gharama za Uchaguzi;
iv. kuanzisha mfuko wa fedha za uchaguzi ili kuimarisha mafanikio yaliyopatikana kwa kutumia fedha za ndani kwa mara ya kwanza kugharimia uchaguzi;
v. kuimarisha TAKUKURU ili ishughulikie tuhuma za rushwa wakati wa uteuzi wa wagombea katika vyama;
vi. kupitia ufanisi wa njia zilizopo kwa ajili ya kukadiria gharama za majimbo na kata, na
vii. kuhakikisha kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa weledi na linajizuia kutoa kauli za kisiasa dhidi ya wagombea na vyama vya siasa.

#### 9.12.2.2 Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar

Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zifikirie kufanya mambo yafuatayo ili kuboresha uendeshaji uchaguzi:

i. kupitia vifungu vinavyohusu upigaji kura wa mapema kwani vimekuwa chanzo cha vurugu badala ya kuwezesha uendeshaji uchaguzi kama ilivyokusudiwa;
ii. kupitia fomu za uteuzi ili kupunguza uwezekano wa wagombea kuondolewa kwa sababu za kiufundi na si uwezo wa kisiasa na ukubalikaji wao kwa wapiga kura;
iii. kukwepa ucheleweshaji usio wa lazima kwenye kutangaza matokeo ya uchaguzi ambao unaweza kusababisha vurugu pindi uvumilivu ukiisha kwa upande wa watu wanaosubiri matokeo;

iv. kupanga vituo vya kupigia kura mapema ili kupunguza uwezekano wa mabadiliko ya dakika ya mwisho ya vituo vya kupigia kura ambayo yanawachaganya wapiga kura;

v. kutumia njia nyingi za mawasiliano kuwapa taarifa waombaji walioteuliwa kwenda kwenye usaili;

vi. kuhakikisha kwamba vyama vya siasa na wagombea wanaweza kushindana katika chaguzi kwa usawa mbele ya sheria. Mfumo wa kisheria wa uchaguzi utumike bila upendeleo au ubaguzi;

vii. kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi zote za kusimamia uchaguzi;

viii. wananchi wapewe data juu ya jinsia, ulemavu na umri pamoja na mambo mengine ili wafanye uchambuzi na kuangalia ushirikishwaji kwenye mchakato wa uchaguzi;

ix. kuongeza uwazi kwa kutangaza taarifa juu ya pingamizi zote na uamuzi uliochukuliwa;

x. kuwafanya wagombea waliopita bila kupingwa wapigiwe kura ili kuondoa uwezekano wa wagombea kujipitisha wenyewe kwa kutumia njia zisizokubalika;

xi. kuwa na msimamo mgumu kuhusu uvunjaji wa maadili ya uchaguzi, ikiwamo kuingilia mapema ili kuzuia matumizi ya lugha za asili wakati wa kampeni za uchaguzi na kuzuia ufanyikaji wa kampeni za uchaguzi ambazo hazipo kwenye ratiba kama vile mikutano inayofanyika pembezoni mwa barabara;

xii. kutoa elimu ya uraia na ya mpiga kura wakati wote ili kujenga utamaduni wa kufanya kampeni za uchaguzi zinazoheshimu jinsia za watu na mahitaji ya makundi maalumu;

xiii. kuvishirikisha vyombo vya habari katika ngazi ya kitaifa na kijamii ili kuyafikia makundi ya wapiga kura mbalimbali nchi nzima;

xiv. kuhakikisha kwamba vituo vya kupigia kura na vya kuandikisha wapiga kura vinafikika na watu wenye ulemavu ili kuongeza ushiriki wao; na

xv. kufanya marekebisho ya lazima kwenye mwongozo wa watazamaji wa uchaguzi wa ndani na wa kimataifa wa mwaka 2020 ili kutoa nafasi ya kukata rufaa dhidi ya kunyimwa kusajiliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

#### 9.12.2.3 Mapendekezo kwa Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa vinaweza kufanya mambo yafuatayo ili kuongeza thamani kwenye mwenendo na ushiriki wao katika mchakato wa uchaguzi:

i. kuweka mawakala wengi wa uchaguzi ili kuongeza imani kwenye mchakato wa uchaguzi na kupunguza hisia kwamba vitendo vya ovyo vinafanyika;

ii. kushiriki kwa vitendo katika kampeni za uchaguzi kama njia ya kuwafanya wapiga kura wajitokeze kupiga kura;

iii. kuhakikisha ushiriki sawa kwenye uchaguzi wa wanaume na wanawake;

iv. kuheshimu sheria za uchaguzi na ratiba ya kampeni iliyoratibiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar;

v. kutofanya kampeni hasi.

vi. kutokutumia vikundi vya usalama saidizi kwani kufanya hivyo kunatishia amani na utulivu; na

vii. kutowatumia viongozi wa dini na majukwaa ya kidini ili kuungwa mkono.

#### 9.12.2.4 Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari

Kama ni mhimili wa nne wa demokrasia (baada ya Bunge, Mahakama na Dola), vyombo vya habari vinaweza kuboresha nafasi yao ya kutangaza habari zinazohusiana na uchaguzi kwa kufanya mambo yafuatayo:

i. kuwaangazia watu wa kawaida zaidi, masuala ya watu wa kawaida na maoni ya watu wa kawaida ili wafanye maamuzi sahihi;

ii. kufanya tathmini na mijadala kuhusu masuala yanayowahusu na wanayohitaji kuyafahamu ili wafanye maamuzi sahihi siku ya uchaguzi;

iii. kutoa muda na nafasi sawa na kutangaza bila upendeleo vyama vya siasa na wagombea urais, ubunge na udiwani;

iv. kufuata maadili ya siku zote na ya vyombo vya habari katika kutangaza habari ili kutotangaza masuala hasi kama taharuki, lugha ya chuki, mashambulizi ya watu, kuchafuana na vitendo vingine vinavyovunja maadili kama kupokea rushwa, hususan kwa kuficha rushwa hizo katika bahasha ya kaki; na

v. kufanya jitihada na kuwekeza katika kutoa taarifa bora na kwa weledi kama vile kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa, kuhakikisha ukamilifu na uhalisia, kufanya jitihada kutoa habari zisizo za upendeleo au kutoa taarifa kama mlinzi au mfuatiliaji na kutekeleza jukumu la kuhudumia umma vizuri.

## MAREJEO


Africa Centre for Strategic Studies (2020) Once a Beacon of Hope, Tanzanians Now Resist Growing Authoritarianism: 2020)https://africacenter.org/spotlight/once-a-beacon-of-hope-tanzanians-now-resist-growing-authoritarianis

Almond, A. and Sydney Verba (1963) The Civic Culture Political Attitudes and Democracy in Five Nationals Princeton: N.J, Princeton University Press.

CRC Report (2020) Tanzania recent Governance trend and 2020 Elections in Brief: https://fas.org/sgp/crs/row/R46579.pdf.

*Daily News* (2020) NEC extends deadline for agents swearing in; 22nd October

*Daily News* (2020) *JPM Much Successes Recorded in Judiciary* 18th June.

*Daily News* (Tanzania) (2019) Tanzania Government Wins Online Content Case. Retrieved from http://dailynews.co.tz on 3rd March 2021.

*Daily News* (2020) Forgiveness *a Vital Magufuli's Attribute* 20th August .

*Daily News* (2020) *Kinana Prays for JPM Forgiveness* 5th June.

*Habari Leo* (2020) Vyama Vyasaini Maadili ya Uchaguzi; Alhamisi 28 Mei.

Huntington, Samuel (1991), *The Third Wave: Democratisation in the Late Twentieth Century*. Norman: University of Oklahoma Press.

Linz, Juan, "(1990) "Transition to Democracy" *The Washington Quarterly*, 13 No. 3, 143-164

Mkapa, Benjamin W. (2019) *My Life My Purpose: A Tanzanian President Remembers*. Dar es Salaam; Mkuki na Nyota.

Wazambi, F. and Komanya, J. (2014), *State of Human Rights in Tanzania Mainland: Key Issues and Highlights for the Year 2019:* retrieved: https://www.humanrights.or.tz/assets/images/upload/files/Tanzania, 20th March 2021.

Mushi, S (2001) "Background to the Survey and the Civic Culture Method", in Mushi, S, Mukandala R, Baregu, M (2001) *Tanzania's Political Culture. A Baseline Survey*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University.

National Election Commission (2016) The Report of the National Electoral Commission on the 2015 Presidential, Parliamentary and Councilors' Elections, Dar es Salaam; Government Printer.

Przeworski, Adam (1991) *Democracy and the Market*, Cambridge; Cambridge University Press.

Rustow, D. (1970) "Transition to Democracy: Toward a Dynamic Model" *Comparative Politics*, 2(3): 337-363

Said, Khalifa (2019) "Tanzania: Maalim Seif Joins ACT-Wazalendo"; *The Citizen* Newspaper, 19th March.

SMZ (2018) *Kanuni za Uchaguzi: Chini ya Kifungu cha 144(1) cha Sheria ya Uchaguzi*, Zanzibar: Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

SMZ (2018) *Sheria ya Uchaguzi NAM. 4. 2018*, Zanzibar: Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

SMZ (2020) *Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984; Toleo la 2020*, Zanzibar: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Taylor, Ben (2019) "Oppositional Musical Chairs", *Tanzanian Affairs*, retrieved from: https://www.tzaffairs.org/ 20th March 2021.

TEMCO (2016) *Report of the Tanzania Election Monitoring Committee on the 2015 General Elections in Tanzania,* Dar es Salaam: TEMCO.

*The Citizen* (2020) NEC extends swearing-in of agents after hiccups; 22nd October

*The Citizen* (2020) Tanzania opposition parties cooperation controversy prompts debate; 24 September

*The East African* (2018) What Next for Tanzania Opposition in Wave of Defections to CCM, 11th August.

*The Guardian* (2020) Swearing-in of poll agents rescheduled; 22nd October.

Twaweza (2016) almost one year into the fifth phase government: citizens approve of the removal of ghost workers, free primary education and the dismissal of public servant: Press Release: https://www.twaweza.org/uploads/files/GovernmentPerformancePressReleaseENGLISH-FINAL.pdf; retrieved on 20th March 2021

United Republic of Tanzania (1977) The Constitution of the United Republic of Tanzania, Dar es Salaam: Government Printer.

United Republic of Tanzania (1985) The National Elections Act, Dar es Salaam, Government Printer

United Republic of Tanzania (2020) The National Elections (Presidential and

Parliamentary Elections) Regulations. Dar es Salaam, Government Printer.

Valenzuela, Samuel J. (1992) "Democratic Consolidation in Post-transitional Settings: Nations, Processes and Facilitating Conditions", in Mainwaring et al. (eds) *Issues in Democratic Consolidation,* Notre Dame, University of Notre Dame Press.

World Bank (2019) Tanzania Path to Poverty Reduction and Pro-poor Growth: https://www.worldbank.org/en/country/tanzania/publication/tanzanias-path-to-poverty-reduction-and-pro-poor-growth.

World Bank (2020) Tanzania Mainland Poverty Assessment: Part 2-Structural Transformation and Firms Performance. World Bank, Washington: Retrieved from https://openknowledge.worldbank.org/handle/10986/33543 License: CC BY 3.0 IGO" on 3rd March 2021

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Watazamaji wa Muda Mrefu Waliosambazwa

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 1 | ARUSHA | ARUSHA MJINI | **DKT. AUDAX KWEYAMBA** |
| | | ARUMERU MAGHARIBI | SUDI AHMED MINJA |
| | | KARATU | LIGHTNESS KAALE |
| | | ARUMERU MASHARIKI | WANDE V. MAKWAIA |
| | | MONDULI | MICHAEL MWAMBANGA |
| | | | |
| 2 | DAR ES SALAAM | ILALA | AHIMIDIWE MUNUO |
| | | SEGEREA | HENRY RODRICK |
| | | UKONGA | FELIX NYELLA |
| | | KIGAMBONI | AMBILISIA MOSHA |
| | | KAWE | JOSEPHINE BESHA |
| | | KINONDONI | DKT. RASUL MINJA |
| | | MBAGALA | OMAR ISSA |
| | | TEMEKE | FORTUNATA THOMAS |
| | | KIBAMBA | DKT. LUPA RAMADHANI |
| | | UBUNGO | **DKT. NG'WANZA KAMATA** |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 3 | DODOMA | DODOMA MJINI | **ZABIBU SWIMA** |
| | | KONDOA MJINI | SALOME KUNDI KITINYA |
| | | CHAMWINO (zamani lilikuwa Chilonwa) | DKT. NANDERA MHANDO |
| | | MVUMI ( zamani lilikuwa MTERA) | DELSON NELSON |
| | | CHEMBA | ANITA MASAKI |
| | | KIBAKWE | DKT. NOVETHA KIGOMBE |
| | | MPWAPWA | ISHENGOMA GOSBERT |
| | | | |
| 4 | GEITA | GEITA MJINI | **EDWARD SIMON** |
| | | NYANG'HWALE | MIKA WANENE MIKA |
| | | BUKOMBE | DKT. STEPHEN MABAGALA |
| | | CHATO | BERNADETHA CHOMA |
| | | GEITA | DKT. EMMANUEL ELIA |
| | | MBOGWE | JULITA SERV KESSY |
| | | | |
| 5 | IRINGA | IRINGA MJINI | **PROFESA ESTER DUNGUMARO** |
| | | MAFINGA MJINI | CHARLES CHARLES KANYUSI |
| | | KALENGA | PATRICIA MAKWAIA |
| | | KILOLO | CANDIDA P. MYOVELA |
| | | MUFINDI KASKAZINI | TITUS GINDO |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 6 | KAGERA | BUKOBA MJINI | **DKT. DEOGRATIUS RUGAIMUKAMU** |
| | | BIHARAMULO MAGHARIBI | JOYCE CYRIL MWACHA |
| | | KARAGWE | ADALBERT BAGERA |
| | | NKENGE | NDAMLANI GOSBERT |
| | | MULEBA KUSINI | PETER MSIGULA |
| | | NGARA | MARY KALIKAWE |
| | | BUKOBA RURAL | NORA NYAKWAE |
| | | | |
| 7 | KATAVI | MPANDA MJINI | **DR. JESPER KATOMERO** |
| | | MPANDA VIJIJINI | HELLEN MMASI |
| | | NSIMBO | EZRA ELIA MBANGWA |
| | | | |
| 8 | KIGOMA | KIGOMA MJINI | **IRENE MUSOKWA** |
| | | KASULU MJINI | CHRISTA KOMBA |
| | | BUHIGWE | KELLEN SYLVESTER MNGOYA |
| | | MUHAMBWE | CREDIUS NESTORY MWESIGA |
| | | KIGOMA KASKAZINI | DKT. MATHEW SENGA |
| | | KIGOMA KUSINI | PRISCA P. MATOWO |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 9 | KILIMANJARO | MOSHI MJINI | **DKT. MATRONA KABYEMELA** |
| | | HAI | MELZEDECK KAIJAGE |
| | | VUNJO | GLORY MAREALLE |
| | | MWANGA | MUTAZAA RICHARD |
| | | ROMBO | HELLEN FESTO URIO |
| | | SAME MASHARIKI | PROFESA ESTHER ISHENGOMA |
| | | SIHA | CAROLYN SHUBIS |
| | | | |
| 10 | LINDI | LINDI MJINI | **PROFESA BERNADETA KILLIAN** |
| | | MCHINGA | DEBORAH ALEXANDER MBAKILAKI |
| | | KILWA KUSINI | DKT. ELEVATUS NKEBUKWA |
| | | LIWALE | JOSEPHINE NZUMBI |
| | | NACHINGWEA | STANSLAUS P. SHABANGI |
| | | | |
| 11 | MANYARA | BABATI MJINI | **DKT. CONSOLATA SULLEY** |
| | | MBULU MJINI | FRANCIS KOU |
| | | HANANG | NELSON S NCHOBE |
| | | KITETO | INGRAM BUTIKU |
| | | SIMANJIRO | HILDA MASHAURI |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 12 | MARA | MUSOMA MJINI | **DKT. KELVIN MUNISI** |
| | | BUNDA MJINI | DINI SHAFII |
| | | TARIME MJINI | FURAHA JULIUS |
| | | MWIBARA | GRAYSON MGONJA |
| | | MUSOMA VIJIJINI | LILIAN MLAGWA |
| | | RORYA | LUCY RINGO |
| | | SERENGETI | DENNIS SANCHAWA |
| | | TARIME VIJIJINI | ISAYA MPIRI |
| | | | |
| 13 | MBEYA | MBEYA MJINI | **DKT. PASTORY PARESTICO** |
| | | LUPA | DKT. PAUL ONDIEK |
| | | KYELA | THADEI PALME |
| | | MBEYA VIJIJINI | ANNE HENRY KITONA |
| | | RUNGWE | AKLAN M. MAJALIWA |
| | | | |
| 14 | MOROGORO | MOROGORO MJINI | **DKT. DENNIS GATAMBWA** |
| | | KILOMBERO | JACKLINE MCHAPWAYA |
| | | MIKUMI | ELISA KIIZA PROSPER |
| | | MALINYI | HOTI RAMADHANI |
| | | ULANGA | PENINA NKINGA |
| | | | |
| 15 | MTWARA | MTWARA MJINI | **DKT. LUCY KIOWI** |
| | | MASASI MJINI | ZUBEDA NASIBU SWEYA |
| | | NANYAMBA | MUGOLOZI BAITANI |
| | | NEWALA MJINI | TUNU RITTE |
| | | NDANDA | ICE BAHAME |
| | | MTWARA VIJIJINI | VERONICA KIMELA |
| | | TANDAHIMBA | DERICK FELICIAN JOHN |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 16 | MWANZA | NYAMAGANA | **PROFESA ERNEST MALLYA** |
| | | ILEMELA | JASPER HARRY SABUNI |
| | | BUCHOSA | ADROFINA SALVATORY |
| | | KWIMBA | DOROTHY KALOLI |
| | | MAGU | RAMADHANI KINGI |
| | | SENGEREMA | DKT. GODFREY SANSA |
| | | UKEREWE | DKT. ABDULLAH HAMZA |
| | | | |
| 17 | NJOMBE | MAKAMBAKO | LENIN FELICIAN |
| | | NJOMBE MJINI | **PETRO MSELEWA** |
| | | LUDEWA | LILIAN MWABULAMBO |
| | | MAKETE | GEORGIA BARONGO |
| | | | |
| 18 | PWANI | KIBAHA MJINI | **PROFESA AMON CHALIGHA** |
| | | BAGAMOYO | STELLA EMANUEL RUNYORO |
| | | KISARAWE | RAMLA IDRISA HAYESHI |
| | | MKURANGA | STANSLAUS NKALANGA |
| | | RUFIJI | ABDALLAH RASHID |
| | | | |
| 19 | RUKWA | SUMBAWANGA MJINI | **DKT. FLORENCE RUTECHURA** |
| | | KALAMBO | MERCY MACHANGE |
| | | NKASI KASKAZINI | HAPPY SHEM PAYOWELA |
| | | KWELA | SELEMANI MWALIKI |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 20 | RUVUMA | SONGEA MJINI | **DKT. HADIJA MWENDA** |
| | | MBINGA MJINI | FRIDOLIN HENJEWELE |
| | | PERAMIHO | JACQUELINE F. MWANDA |
| | | TUNDURU KASKAZINI | WILFRED KAHUMUZA |
| | | | |
| 21 | SHINYANGA | SHINYANGA MJINI | **DKT. JACKLINE MGUMIA** |
| | | KAHAMA MJINI | VERENA KAGALI |
| | | KISHAPU | ISMAIL KASSIGAYE |
| | | MSALALA | FREDRICK SINTAU |
| | | | |
| 22 | SIMIYU | BARIADI | **DKT. THOMAS NDALUKA** |
| | | BUSEGA | DKT. THERESIA MUGOBI |
| | | MASWA MASHARIKI | DKT. STEPHEN KILASI |
| | | KISESA | TUMAINI MSHANA |
| | | MEATU | MARY GABRIEL MOSHI |
| | | | |
| 23 | SINGIDA | SINGIDA MJINI | **PROFESA PENDO MALANGWA** |
| | | SINGIDA MASHARIKI | GABRIEL KIIZA |
| | | IRAMBA MAGHARIBI | ELIZABETH VALENTINO LEMA |
| | | MANYONI MASHARIKI | BONIFACE MULISA |
| | | IRAMBA MASHARIKI | ESTHER SABAS KAVISHE |
| | | | |
| 24 | SONGWE | TUNDUMA | **DKT. FARAJA NDUMBARO** |
| | | VWAWA | LADISLAUS TUMBU |
| | | MBOZI | IRENE MASSAWE |
| | | MOMBA | JERRY SAIWELLO |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 25 | TABORA | TABORA MJINI | **DKT. MUHIDIN SHANGWE** |
| | | NZEGA MJI | JESCA MUGANDA |
| | | BUKENE | JOCYLENE MKILIMA |
| | | IGUNGA | IRENE MAKUMBA |
| | | KALIUA | ALLAN MKOPOKA |
| | | SIKONGE | VICKY I MOSHI |
| | | URAMBO | SYLVESTER RWEYEMAMU |
| | | IGALULA | DKT. ANETH P. BYABATO |
| | | TABORA KASKAZINI | CLEMENTINA KABENGULA |
| | | | |
| 26 | TANGA | TANGA MJINI | **DKT. EUGENIA KAFANABO** |
| | | HANDENI MJINI | ISSA DUNIA |
| | | KOROGWE MJINI | LIZBERT ASSEY |
| | | KILINDI | ALI MBAROUK OMAR |
| | | LUSHOTO | EMMANUEL ALOYCE SULEIMAN |
| | | MKINGA | NOELLA R. KISSASSI |
| | | MUHEZA | RWEYEMAMU RAPHAEL |
| | | PANGANI | ANGELINA SALEWA |
| | | | |
| 27 | KASKAZINI PEMBA | KONDE | HASSAN K. JUMA |
| | | MICHEWENI | ILLUMINATA HENRY MASAAKA |
| | | TUMBE | PASCAL SULLE |
| | | WINGWI | SAMSON MWALUSAMBA |
| | | GANDO | DKT. BENJAMIN MBUGHI |
| | | KOJANI | MNZAVA NAMVITA |
| | | MTAMBWE | JACKSON COY |
| | | PANDANI | FATUMA NIYOPA SAID |
| | | WETE | **DKT. HAMZA KONDO** |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 28 | KASKAZINI UNGUJA | CHAANI | **ASHA ABOUD** |
| | | KIJINI | SAID MBAROUK |
| | | MKWAJUNI | DKT. PATRICK MASANJA |
| | | NUNGWI | DKT. MASOUD DAUDA |
| | | TUMBATU | NYIGU BONIFACE SABAS |
| | | BUMBWINI | DKT. ZABRON KENGERA |
| | | DONGE | WALTER LUANDA |
| | | MAHONDA | AMINA JUMA ABBAS |
| | | | |
| 29 | KUSINI PEMBA | CHAKECHAKE | **AHMAD ALI HAJI** |
| | | CHONYA | THOMAS PAUL |
| | | OLE | MWASONGWE HEBRON |
| | | WAWI | NEHANDA ANENO |
| | | ZIWANI | OMAR YUSUF |
| | | CHAMBANI | PRINCE ANTONIO |
| | | KIWANI | DKT. ELIZABETH BITEGERA |
| | | MKOANI | SIMON SIRIKALE |
| | | MTAMBILE | DKT. MAKARIUS ITAMBU |
| | | | |
| 30 | KUSINI UNGUJA | CHWAKA | **TAINA KIKOTI** |
| | | TUNGUU | ISLAM SALUM |
| | | UZINI | KANDI SAID |
| | | MAKUNDUCHI | ELIZABETH MATIKO |
| | | PAJE | JABIR SAID |
| | | | |

| NA. | MKOA | JIMBO | MTAZAMAJI WA MUDA MREFU |
|---|---|---|---|
| 31 | MJINI MAGHARIBI | BUBUBU | ABEID TWALI |
| | | MFENESINI | ROSE PASCAL |
| | | MTONI | DKT. JACOB LISAKAFU |
| | | MWERA | PRISCILLA EMMANUEL |
| | | WELEZO | MANSULA TWAHIL SHEMERA |
| | | DIMANI | ALLY DUNIA |
| | | FUONI | MARIAM HAMISI |
| | | KIEMBE SAMAKI | **DKT. DAMIAN SHUMBUSHO** |
| | | MWANAKWEREKWE | NYAGABONA MALIMA |
| | | PANGAWE ( zamani lilikuwa Kijitoupele) | RAUHIA ALI HAJI |
| | | AMANI | SALMA ALLY KATABAZI |
| | | CHUMBUNI | JACKLINE NDOMBELE |
| | | JANG'OMBE | OMARY THABIT |
| | | KIKWAJUNI | SIMON KILAWA |
| | | KWAHANI | LULU AMEIR |
| | | MAGOMENI | KAIJUKO JERMAINE |
| | | MALINDI | ROSE KABYEMELA |
| | | MPENDAE | EMMANUEL YOHANA LICHAGULA |
| | | SHAURIMOYO | TWAHIL H. SHAKIRU |
| | | | |

## Kiambatisho 2: Barua ya Usajili kutoka Tume

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

*Anwani ya Simu "UCHAGUZI".*

*Nambari ya Simu: +255 22-2114963 / 2114963*

*Nambari ya Faksi +255 22 2116740*

*Barua Pepe: uchaguzi@nec.go.tz*

*Tovuti: www.nec.go.tz*

*(Barua zote za kiofisi ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi)*

Jengo la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Mtaa wa Shaban Robert/ Garden Avenue,

S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. BA 71/74/01H

Tarehe: 29 Juni, 2020

University of Dar es Salaam,
Research and Education for Democracy in Tanzania (REDET),
S.L.P 35039,
DAR ES SALAAM.

**YAH: MAOMBI YA KUWA WATAZAMAJI KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia kanuni ya 18(5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, na kanuni ya 16(5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 inapenda kukutaarifu kwamba, imekubali ombi lenu la kuwa watazamaji katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kabla ya kuanza zoezi hilo la utazamaji Taasisi yako pamoja na watu wote itakaowatumia katika zoezi hilo la utazamaji watatakiwa kusajiliwa rasmi kama watazamaji. Kwa sasa Tume ipo katika mchakato wa maandalizi ya zoezi hilo la usajili, hivyo baada ya muda mfupi Tume itawapatia taarifa juu ya utaratibu mzima wa zoezi la usajili pamoja na mambo mengine yanayohusiana na jambo hilo.

Nakutakia kazi njema

Dkt. Wilson Mahera Charles
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

## Appendix 3: Photo Gallery



*Mwenyekiti wa REDET, Prof. Rwekaza Mukandala akiwasilisha Taarifa ya Awali ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 tarehe 3 Novemba, 2020.*



*Mwenyekiti wa REDET na Kiongozi Mkuu wa Timu ya Watazamaji wa Uchaguzi akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa mafunzo ya watazamaji wa muda mrefu tarehe 25 Septemba 2020.*



*Picha ya pamoja wakat wa mafunzo ya watazamaji wa muda mrefu tarehe 25 Septemba 2020.*



*Msajili wa Vyama vya Siasa Msaidizi, Sisty Nyahoza, akiwasilisha mada yake.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Emmanuel Kawishe, akiwasilisha mada yake.*



*Kamishina Mstaafu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Profesa Amon Chaligha, akiwaelezea washiriki wa mafunzo ya watazamaji wa muda mrefu uzoefu wake kuhusu usimamizi wa mchakato wa uchaguzi.*



*Mchambuzi wa masuala ya jinsia, Profesa Bernadeta Killian, akiwasilisha mada yake kuhusu namna ya kufuatilia na kurekodi ushiriki wa makundi maalum wakati wa zoezi la utazamaji wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.*



*Wapiga kura wakisubiri kupiga kura.*



*Mafunzo kwa vitendo kwa maafisa wasimamizi wa uchaguzi yakiendelea.*



*10. Pikipiki iliyopambwa mabango ya mgombea urais Zanziba wa ADA-TADEA, Bw. Juma Ali Khatib.*




*Bango lenye ujumbe kuhusu elimu ya mpiga kura kama linavyoonekana kwenye dashibodi ya moja ya gari la abiria mjini Unguja.*




*Kampeni ya pamoja ya ACT-Wazalendo, CUF, TLP, NCCR-Mageuzi na CHADEMA katika kata ya Kibara, jimbo la Mwibara.*



*Mwangalizi wa muda mrefu wa REDET akielekea kwenye shughuli za kampeni Kisiwa cha Fundo, Zanzibar.*



*Bango la kampeni la mgombea ubunge wa CUF kwa jimbo la Mbozi, Bw. Nkunyuntila Siwale, wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.*




*Bango la kampeni la mgombea ubunge kwa tiketi ya TLP wa jimbo la Singida Mashariki, Bw. Morris Thomas Nkongolo, likiwa na picha ndogo ya mgombea wa CCM wa kiti cha urais, John Pombe Joseph Magufuli, wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.*



***Gari likiwa na kibao chenye herufi "JPM" ambazo ni kifupi cha majina ya mgombea urais wa CCM, John Pombe Magufuli, kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Babati Mjini tarehe 25 Oktoba 2020.***




*Wafuasi wa CCM wakibeba mfano wa jeneza lililovikwa bendera ya CHADEMA wakipita moja ya mitaa ya manispaa ya Songea baada ya kutangazwa matokeo ya kiti cha ubunge tarehe 29 Oktoba 2020.*



*Rais John Magufuli akiwa ameambatana na Mufti Mkuu wa Tanzania, Aboubakar Zubery Bin Ally, Balozi wa Moroko nchini Tanzania, Abdelilah Benryane, Shehe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhadi Mussa Salim, na viongozi wengine wa BAKWATA, akitembelea msikiti uliojengwa kwa ufadhili wa Mfalme Mohamed VI wa Moroko, wakati akielekea kwenye mkutano wa kampeni viwanja vya Mburahati tarehe 13 Oktoba 2020 (Picha kwa hisani ya Blogu Rasmi ya Rais, Ofisi ya Rais).*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiombewa Dua iliyokuwa ikiongozwa na Mufti Mkuu wa Tanzania Sheikh Aboubakar Zubeir Bin Ally mara baada ya kutembelea Msikiti Mkuu wa Bakwata uliokamilika kujengwa kwa ufadhili wa Mfalme Mohamed VI wa Morocco.*

# Temco Election Reports 1990-2020



## Sekretarieti ya Programu ya TEPO



**Prof. Rwekaza S. Mukandala**

*Mwenyekiti wa REDET na Kiongozi Mkuu wa Timu ya Watazamaj wa Uchaguzi.*



**Dr. Rasul A. Minja**

*Mkurugenzi wa Programu*



**Prof. Bernadeta Killian**

*Mchambuzi wa Masuala ya Jinsia*



**Dr. Lupa Ramadhani**

*Mchambuzi wa Masuala ya Kisiasa*



**Dr. Dotto P. Kuhenga**

*Mchambuzi wa Vyombo vya Habari*



**Mr. Dunia Nassoro**

*Mhasibu*



**Ms. Anney Yamungu**
*Afisa Tawala na Vifaa*



**Ms. Hellen Nyukuri**
*Katibu Muhtasi*



**Mr. Captain Kikwaya**
*Mtaalam wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano*



**Ms. Mwati Kisesa**
*Mhudumu wa Ofisi*



**Ms. Matilda Mrosso**
*Mhudumu wa Ofisi*